**3 MEI, 2024**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 3 Mei, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tuketi.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tutaanza na maswali kwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Namwita Mheshimiwa Esther Lukago Midimu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 227

**Wodi ya Kulaza Wagonjwa Kituo cha Afya Zagayu – Itilima**

**MHE. LUCY J. SABU K.n.y. MHE. ESTHER L. MIDIMU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Wodi za Kulaza Wagonjwa katika Kituo cha Afya Zagayu Wilayani Itilima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kituo cha afya hufanyika kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza inahusisha majengo ya *OPD*, maabara, upasuaji wa dharura, wodi ya wazazi, upasuaji, jengo la kufulia na kichomea taka; na awamu ya pili inahusisha ujenzi wa wodi za kulaza wagonjwa. Hivyo, Kituo cha Afya Zagayu kitatengewa bajeti ya ujenzi wa wodi katika awamu ya pili ya ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Kwa niaba yake, Mheshimiwa Lucy Sabu.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza: Je, ni lini awamu ya pili ya ujenzi wa wodi za Kituo cha Afya Zagayu utaanza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mtaalamu wa mionzi katika Hospitali ya Wilaya ya Itilima? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Lucy John Sabu kwa namna ambavyo ameendelea kuwasemea wananchi wa Mkoa wa Simiyu, pia kufuatilia huduma za afya katika vituo vya huduma za afya katika Mkoa wa Simiyu. Nimhakikishie tu kwamba, tulianza na ukarabati na upanuzi wa hospitali za halmashauri kongwe zile 50 na baada ya hapo tutakwenda sasa kuongeza majengo yanayopungua katika vituo vya afya ambayo itakuwa ni awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mara tu baada ya kukamilisha ukarabati na upanuzi wa hospitali kongwe za halmashauri, tutakwenda kuanza upanuzi na ujenzi kwenye vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nafahamu kwamba Kituo cha Afya cha Zagayu na vituo vingine kote nchini vina upungufu wa wataalam hususan wa mionzi *X-Ray* pamoja na *Ultra-sound*. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshaanza mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam ili kuondoa *gap* ya upungufu wa watumishi uliopo na tutapeleka mtaalamu katika Kituo cha Afya cha Zagayu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anna Lupembe, swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini zitaletwa fedha awamu ya pili katika Kituo cha Afya cha Itenka?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijamsikia vizuri.

**MWENYEKITI:** Naomba urudie swali lako.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini awamu ya pili ya fedha za Kituo cha Afya cha Itenka zitakuja?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafahamu kwamba Kituo cha Afya cha Itenka ambacho kipo katika Jimbo la Nsimbo ni kituo ambacho pia kinahitaji fedha kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshaweka mkakati, baada ya ukamilishaji wa hospitali za halmashauri, tutakwenda kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga, swali la nyongeza.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali. Lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Matamba kinachotegemewa na zaidi ya kata sita na tuliweka katika kipaumbele kwenye ujenzi wa vituo vya afya?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Mheshimiwa Festo Sanga alishawasilisha kipaumbele cha Kata ya Matamba kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha afya na tayari Serikali imeshakiweka kwenye vituo vya kimkakati kinatafutiwa fedha kwa ajili ya kwenda kuanza ujenzi. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hiyo itafanyika, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tendega, swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Pawaga kinaendelea vizuri, lakini gari lake ni bovu, lini Serikali mtapeleka gari zima? Ahsante sana

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu Daktari Samia Suluhu Hassan ameshanunua magari ya wagonjwa zaidi ya 326 na tayari tumeshayagawa katika halmashauri zote kote nchini. Pia amenunua magari kwa ajili ya usimamizi wa huduma za afya magari 222.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie tu kwamba nina uhakika halmashauri hiyo pia imeshapata magari, ni suala la maamuzi ya Mkurugenzi kuona wapi ni kipaumbele ili aweze kupeleka Pawaga au maeneo mengine wananchi wapate huduma nzuri zaidi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Lyabukande katika Jimbo la Solwa? Ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tulishafanya *mapping* ya maeneo yote ya kata za kimkakati, kata zenye wananchi wengi zaidi, na ambazo ziko mbali zaidi na kituo cha karibu cha huduma. Kama kata hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge inakidhi vigezo vya kujengewa kituo cha afya, naomba nilichukue jambo hilo, nitawasiliana na wataalamu, pia na menejimenti ya wilaya na mkoa tuweze kuweka utaratibu wa kuanza ujenzi, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Lini Serikali itatimiza ahadi ya kupeleka fedha, shilingi milioni 200 kwenye Kituo cha Afya cha Bungu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtoe hofu Mheshimiwa Mpembenwe kwamba tunafahamu Serikali ilishaahidi kupeleka hiyo shilingi milioni 200 kwa ajili ya ukamilishaji wa kituo hicho cha afya, na hivi sasa tuko kwenye taratibu za ukamilishaji tu wa kupeleka hizo fedha ili tuweze kuendelea na kazi za ujenzi zilizobaki.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyonyeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Wananchi wa Kata ya Upendo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Mji wa Mafinga, tumeanzisha ujenzi wa kituo cha afya. Je, lini Serikali itaongeza nguvu ili wananchi wakamilishe ujenzi wa kituo hicho cha afya cha Kata ya Upendo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeze sana wananchi wa Kata ya Upendo katika Mji wa Mafinga kwa namna ambavyo wamejitolea kuchangia nguvu zao kuanza ujenzi wa kituo cha afya. Pia nampongeza Mheshimiwa Mbunge, na nimhakikishie tu kwamba siku zote Serikali hii sikivu ya Awamu wa Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tutakwenda kuunga mkono juhudi za wananchi kuhakikisha kwamba kituo hicho kinakamilika, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda kwa kifupi.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Tunashukuru sana kwa Kituo cha Afya cha Ikuti katika Jimbo la Rungwe, na vingine vyote vimeenda vizuri, lakini tunaomba mtupatie jengo la kuweka *X-Ray*. Ni lini mtatusaidia Mheshimiwa Naibu Waziri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe kwamba ujenzi wa jengo la *X-Ray* uko ndani ya uwezo wa mapato ya Halmashauri ya Rungwe. Kwa hiyo, waanze ujenzi na Serikali itapeleka *X-Ray* kwa ajili ya wananchi kuanza kupata huduma hizo.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na maswali, namwita sasa Mheshimiwa Flatei Gregory Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini, sasa aulize swali lake.

Na. 228

**Kugawa Vijiji na Kata katika Jimbo la Mbulu Vijijini**

**MHE. FLATEI G. MASSAY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itagawa vijiji vya Sidgi, Hayderer juu, Umbur pamoja na Kata za Hayderer, Haydom, Maghangw, Dongobesh na Maretadu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa uanzishwaji wa maeneo ya kiutawala ili kusogeza huduma karibu na wananchi. Aidha, uanzishaji wa maeneo mapya ya utawala huzingatia Sheria ya Serikali za Mitaa Mamlaka za Wilaya Sura 287 na Mamlaka za Miji Sura 288 pamoja na Mwongozo wa uanzishwaji wa Maeneo ya Utawala wa Mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua uhitaji wa kugawa baadhi ya maeneo mapya ya utawala ikiwemo vijiji vya Sidgi, Hayderer Juu, Umbur pamoja na Kata za Hayderer, Haydom, Maghangw, Dongobesh na Maretadu, lakini kwa sasa, Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu kwenye maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma kwa ufanisi zaidi na baadaye kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Flatei.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vijiji alivyovitaja vyote vina shule mbili mbili za msingi, wamejenga ofisi katika vijiji, na karibu mambo mengi yamekuwa tayari; na kwa sababu idadi ya watu ni kubwa: Kwa nini usiruhusu sisi wenyewe wananchi tukaanzisha vijiji hivyo mpaka Serikali itakapopata uwezo wa kuvianzisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa sababu kata anazotaja, kwa mfano Kata hii ya Hayderer inapakana na majimbo ya uchaguzi; Hanang, Babati na Singida na ni kubwa sana; kama Kata ya Haydom ina watu 30,000; na kwa kuwa hali imekuwa mbaya na haitawaliki: Kwa nini usiruhusu basi chini ya halmashauri tukawa na kata ndogo ili walau patawalike?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba Mheshimiwa Mbunge mara kwa

mara ameleta hoja ya kuanzisha vijiji hivi kutokana na ukubwa wake, pia kuanzisha kata hizi kutokana na ukubwa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua. Tumepanga kwanza kukamilisha maeneo ya utawala yaliyopo, na ninyi Waheshimiwa Wabunge ni mashuhuda kwamba tumekuwa kila siku tukiomba kujenga majengo ya utawala, ofisi za kata, majengo ya halmashauri, kwa Wakuu wa Wilaya, na Wakuu wa Mikoa. Bado tuna kazi ya kukamilisha miundombinu katika mamlaka zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimhakikishie kwamba tunatambua kwamba vijiji hivi ni vikubwa, lakini kwa mujibu wa sheria, halmashauri haina mamlaka ya kuanzisha Kijiji. Kwa hiyo, hatuwezi tukasema halmashauri iende ikaanzishe vijiji yenyewe au ianzishe kata yenyewe, lazima tuzingatie sheria na ni suala tu la muda. Nimhakikishie Mheshimiwa Flatei kwamba muda ukifika, tutahakikisha kwamba tunafanyia kazi kata hizi pamoja na vijiji hivi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara Kata ya Mwaya ni kata kubwa sana na tayari tumeshaleta maombi kwa Serikali kuhusu kuigawa kata hiyo na kwa kuzingatia majibu ya Serikali: Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anatuhakikishiaje kwamba mchakato wa kuanza kugawa maeneo utakapoanza na Kata ya Mwaya wataigawa? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Asenga kwamba Kata hiyo ya Mwaya katika Halmashauri ya Mji wa Ifakara itapewa kipaumbele mara tutakapoanza kugawa maeneo mapya ya utawala, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali linalofuata. Nimwite sasa Mheshimiwa Francis Koka, kwa niaba yake Mheshimiwa Mtemvu atauliza hilo swali.

Na. 229

**Ujenzi wa Daraja la Mto Mpiji**

**MHE. ISSA J. MTEMVU K.n.y. MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Daraja la Mto Mpiji ili kuunganisha Kibaha na Kibwegere Wilaya ya Ubungo?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Katimba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa Daraja la Mto Mpiji linalounganisha Halmashauri ya Mji wa Kibaha na Kibwegere katika Wilaya ya Ubungo. *TARURA* kwa kushirikiana na Mhandisi Mshauri Smarcon imefanya usanifu wa kina *(detailed design)* wa daraja hilo lenye urefu wa mita 60. Kazi hiyo imekamilika na inakadiriwa gharama za ujenzi kuwa ni shilingi bilioni tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo, na pindi zitakapopatikana, ujenzi utaanza mara moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtemvu kwa niaba, swali la nyongeza.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, naomba niulize maswali mawili yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2021/2022 ilishawahi kutengwa shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili la kivuko hiki, lakini haijatekelezwa. Leo majibu ya msingi yanaonesha kwamba wanaendelea au wamekamilisha tathmini na gharama wamezipata upya, sasa wanatafuta fedha. Nini *commitment* ya Serikali kujenga daraja hili ili kuokoa vifo vya watoto ambapo hata jana tu mtoto mmoja amekufa kwenye kivuko hiki?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Jimbo la Kibamba kuna Mto Mpiji wenyewe na Mto Mbezi ambapo kuna vivuko vingi sana hatarishi kwa watoto wetu na watu wanaotumia. Je, ni ipi ahadi ya Serikali kuleta fedha maalum kujenga vivuko hivi ili tuokoe maisha ya watu wetu? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu kwenye majibu yangu ya msingi, tayari Serikali imefanya tathmini na imebaini kwamba zinahitajika shilingi bilioni tatu kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ya Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ipo kazini na ndiyo maana kuna ongezeko kubwa la bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka muda huu Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia imeridhia kuongeza bajeti maalum ya shilingi bilioni 350 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu hii. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepokea na itaweka kipaumbele kikubwa sana kuhakikisha kwamba inaanza ujenzi wa miundombinu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, vivyo hivyo nirejee maelezo yangu ya awali kwamba Serikali inaona umuhimu mkubwa sana wa miundombinu hii muhimu kwa maslahi ya wananchi, na tayari bajeti ya dharura ya *TARURA* imeongezeka. Vile vile kuna bajeti maalum kwa ajili ya ukarabati na marekebisho na ujenzi wa miundombinu hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inalichukulia suala hili la ujenzi wa miundombinu hii kwa umakini mkubwa na itakuja kujenga miundombinu hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba kwenye Wilaya ya Kilindi kipo Kijiji cha Mgera ambacho kina daraja limekatika takribani miaka mitatu sasa na Serikali haijarekebisha hali hiyo na upande wa pili ndipo ambapo taasisi zote za Serikali zipo huko. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kutoa maelekezo kwa *TARURA* kwenda kurekebisha daraja hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vipaumbele vya *TARURA* ni pamoja na kuhakikisha kwamba inahakikisha miundombinu ya barabara hizi haikatiki kimawasiliano. Kwa hoja ya Mheshimiwa Mbunge naomba baada ya kipindi hiki cha maswali na majibu tukutane, tukae, tuweze kufanya mawasiliano na kama ni kweli eneo hili limekata mawasiliano, kuna umuhimu na kipaumbele kikubwa sana ambacho inabidi kitolewe kwa ajili ya kuhakikisha tunarudisha mawasiliano katika eneo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Monni, swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Mpendo na Kijiji cha Amia kinatenganishwa na mto mkubwa

ambao unaitwa Mto Bubu. Ni lini sasa Serikali itajenga daraja ili kuunganisha vijiji hivi viwili?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama nilivyotangulia kusema kwamba ni muhimu sana kuwe kuna mawasiliano na ndiyo kipaumbele katika mipango kazi au utekelezaji wa majukumu ya *TARURA* kuhakikisha kwamba mawasiliano hayakatiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kadiri alivyoleta maombi yake na kwa kuzingatia vipaumbele na upatikanaji wa fedha, Serikali itamsaidia kwenda kurekebisha miundombinu hii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Alfred Kimea, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Korogwe Mjini kuna madaraja mawili ambayo yana changamoto kubwa. Moja lipo katikati ya mji ambalo vivuko vyake vimekatika pembeni, watoto wanapata ajali ya kuanguka; daraja lingine la Kitifu, limekatika kabisa, hakuna mawasiliano kati ya kata mbili; Kata ya Mgombezi pamoja na Mtonga: Je, Waziri haoni sababu ya kuwaelekeza *TARURA* kurekebisha madaraja hayo mawili muhimu kwenye Jimbo la Korogwe Mjini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba nitafanya mawasiliano na Meneja wa *TARURA* ili kufahamu changamoto iliyopo katika eneo hilo na kama ni dhahiri kwamba mawasiliano yamekatika, basi kama ulivyo utaratibu wa *TARURA* ni kuweka kipaumbele katika kuhakikisha inaunganisha na kuna mawasiliano katika barabara zetu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili tumelipokea na tutalifanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Bado nina swali la 234. Namwita sasa Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, aulize swali lake.

Na. 230

**Ujenzi wa Barabara ya Mbinga Mpepai hadi Mtua**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Mbinga Mpepai hadi Mtua kwa kiwango cha changarawe?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Mbinga Mpepai – Mtua ambayo inatambulika kwa jina la Mbinga – Liparamba yenye urefu wa kilometa 41.87 ipo kwenye utekelezaji kwa mwaka huu wa fedha 2023/2024, na wakandarasi wapo eneo la kazi. Serikali kupitia *TARURA* imetenga shilingi milioni 947.2 ambazo zitatumika kutengeneza kilometa 31 kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mradi wa *TACTIC* itatekeleza ujenzi wa barabara hii kilomita mbili kwa kiwango cha tabaka la lami. Serikali itaendelea kuhudumia mtandao wa barabara katika Mji wa Mbinga ikiwemo barabara hii kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwanza

naishukuru Serikali kwa kutenga shilingi milioni 947.2 kujenga kilometa 31. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Katika majibu ya Serikali ni kwamba, kilometa mbili zitajengwa kwa kiwango cha lami kupitia Mradi wa *TACTIC*. Nataka nifahamu, ni lini mradi huo utaanza kutekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Ni lini Serikali itajenga Barabara ya Mbinga – Kikolo – Kihungu na barabara ya Mbinga – Kitanda hadi Miembeni?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tayari hatua zote za muhimu zimekamilika kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, mradi huu sasa utaanza kutekeleza ujenzi wa barabara hiyo ya lami ya kilomita mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili ambalo ameuliza juu ya ujenzi wa Barabara ya Mbinga Mjini – Kikolo mpaka Kihungu yenye urefu wa kilometa 30, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika mwaka wa fedha 2024/2025 zimetengwa shilingi milioni 60 kwa ajili ya kufanya marekebisho ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kitanda ambayo yenyewe ina kilometa 28, kwenye mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilitenga kwenye bajeti shilingi milioni 80, lakini katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imetenga shilingi milioni 47.18 kwa ajili ya marekebisho. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali imelichukua suala hili la ujenzi wa barabara hizi kwa umakini mkubwa na itaendelea kutekeleza ujenzi huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako mazuri kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Wizara ya Nishati. Namwita sasa Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 231

**Kupeleka Umeme katika Shule na Taasisi za Dini Kigoma**

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha zoezi la kupeleka umeme katika Shule zote na Taasisi za Dini katika Mkoa wa Kigoma?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Kigoma una vijiji 307 ambapo vijiji 257 vimepatiwa umeme na kazi ya kupeleka umeme katika vijiji 50 vilivyosalia inaendelea kupitia Mkandarasi aitwaye *State Grid Electrical and Technical Works Limited* anayetekeleza Mradi wa Kusambaza Umeme Vijijini, Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili. Wakati wa uunganishaji wa wateja katika miradi, wakala hutoa kipaumbele kwa taasisi za umma zikiwemo shule na taasisi za dini. Serikali kupitia Wakala, inaendelea kuratibu upatikanaji wa umeme katika taasisi za umma vijijini, hususan Shule na Taasisi za Dini kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Genzabuke, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, zipo shule za sekondari ambazo bado hazijapata umeme. Pamoja na shule hizo, mwaka jana, 2023 niliomba Shule ya Sekondari Kimenyi ipatiwe umeme, lakini mpaka sasa shule hiyo iliyopo Kata ya

Kagera Nkanda haijaweza kupatiwa umeme. Ni lini sasa sekondari hiyo ya Kimenye itapelekewa umeme? (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Mkoa wa Kigoma una wilaya saba. Kati ya wilaya hizo, ni wilaya nne tu ambazo zimepatiwa umeme wa gridi ya Taifa. Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika wilaya zilizosalia kwa maana ya Kigoma Vijijini, Kigoma Mjini na Uvinza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kupeleka umeme katika Shule ya Kimenyi iliyopo katika Kijiji cha Kagera Nkanda, tayari mkandarasi ambaye anatekeleza mradi wa kupeleka umeme katika Kijiji cha Kagera Nkanda yupo *site*. Sasa nimwelekeze Meneja wa Mkoa wa Kigoma ahakikishe anatenga fungu la ziada kwa sababu shule hii ipo mita 900 kutoka kwenye njia ya umeme anayojenga mkandarasi. Kwa hiyo, pale ambapo njia hii itakamilika, basi watenge fungu la nyongeza kwa ajili ya kuunganisha umeme kwenda kwenye shule hii ya sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kupeleka umeme wa gridi katika hizi wilaya tatu, Serikali inatekeleza mradi wa kupeleka umeme wa gridi katika Mkoa wa Kigoma ambapo mradi huu kwa sasa umefikia asilimia 94. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa mradi unaendelea vizuri sana na tunajenga njia ya umeme ya kilovoti 400 kutoka Nyakanazi hadi Kidahwe. Umeme ukifika Kidahwe utaenda Kigoma Mjini pamoja na Uvinza kwa kadiri ya utekelezaji wa mradi ambao upo kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie wananchi wa Kigoma kuwa mradi wa kupeleka gridi ya umeme Kigoma unaendelea vizuri sana na utamalizika kwa wakati. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Pathan, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA A. PATHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itakamilisha zoezi la kupeleka umeme katika shule na taasisi zote zikiwepo za dini katika Mkoa wa Lindi?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miradi ambayo inaendelea, ni maelekezo ya Serikali kwamba shule na taasisi ambazo zipo mita chache katika maeneo ambayo tunapitisha njia za umeme, basi taasisi hizi ziweze kuunganishwa. Zile ambazo zipo umbali wa zaidi ya mita 900 kwenda nyuma, ni maelekezo kwamba Ofisi zetu za Mikoa na Ofisi za *TANESCO* za kimkoa zihakikishe zinatenga bajeti ya ziada na nyongeza kuhakikisha zinapeleka umeme katika taasisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maelekezo ya Serikali kuhakikisha taasisi zote za msingi zinapata umeme kwa ajili ya ustawi wa watu wetu na shughuli za maendeleo za wanajamii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dorothy Kilave, swali la nyongeza.

**MHE. DOROTHY G. KILAVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini umeme unaopita eneo la Uhasibu utakamilika ili Jimbo la Temeke tuweze kupata umeme usiokatikakatika tena?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Kurasini ni kweli limekuwa lina changamoto ya umeme, lakini tuna ujenzi wa laini ya chini ya umeme kwa ajili ya kuboresha umeme katika Wilaya ya Ilala. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi unaendelea vizuri sana na upo katika hatua za mwisho za umaliziaji. Pindi utakapokamilika, wananchi wa jimbo lako watapata umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuhakikishia tunasimamia mradi huu kwa weledi mkubwa sana kuhakikisha unakamilika kwa wakati.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itapeleka umeme kwenye vijiji vilivyobakia kwenye Wilaya ya Kilosa pamoja na Morogoro Vijijini? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kilosa na Morogoro Vijijini wakandarasi wapo *site*. Tunaendelea kuwahimiza wakandarasi kutekeleza miradi hii kwa weledi kuhakikisha wananchi wanapata umeme kwa wakati na kuhakikisha wanakamilisha majukumu yao kulingana na mikataba yao, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Jimbo la Muleba Kusini ina vijiji vitatu ambavyo havijapata umeme; Kijiji cha Kiholele, Burungura na Bihanga. Ni lini Serikali itapeleka umeme katika vijiji hivyo?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hivi vijiji vitatu kwenye Jimbo la Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mkandarasi yupo *site*. Tutaendelea kumsimamia ili aongeze kasi kuhakikisha vijiji hivi vinawaka umeme.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Kapinga kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, namwita sasa Mheshimiwa Bakar Hamad Bakar, aweze kuuliza swali lake.

Na. 232

**Vyombo vya Usafiri Vilivyosajiliwa Zanzibar Kutambuliwa Tanzania Bara**

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR** aliuliza: -

Je, lini vyombo vya usafiri vilivyosajiliwa Zanzibar vitatambuliwa Tanzania Bara?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ipo katika hatua ya Marekebisho ya kifungu cha nane cha Sheria ya Usalama Barabarani, Sura ya 168, ambacho kinazungumzia usajili wa vyombo vya moto hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupokea maoni ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, mapendekezo haya yatawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa hatua zaidi.

**MWENYEKITI:** Swali la nyongeza, Mheshimiwa Bakar.

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mchakato wa mabadiliko ya sheria hii ili kuweza kufanya vyombo vya usafiri kutambulika hapa Tanzania Bara umeonekana umechukua muda mrefu sana, sasa ni kwa nini Serikali haioni haja ya kuweka mwongozo maalumu kipindi hiki wakati tunasubiria mabadiliko ya sheria hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Bakar, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya

Zanzibar zipo katika mazungumzo, naomba tuwe na subira na utaratibu uliopo kwa sasa uendelee kutumika. Pale mazungumzo yatakapokamilika, basi marekebisho yatafanyika ili kuhakikisha kwamba vyombo vinasajiliwa kwa pamoja.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Namwita sasa Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, aulize swali lake.

Na. 233

**Kufunga Shughuli za Uvuvi katika Ziwa Tanganyika**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE** aliuliza:-

Je, kuna utafiti wa kisayansi unaoonyesha kufunga shughuli za uvuvi Ziwa Tanganyika kuruhusu kuzaliana kwa Samaki kutakuwa na tija?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika Ziwa Tanganyika unafanyika kwa njia endelevu, Wizara kwa kushirikiana na nchi zinazounda Mamlaka ya Ziwa Tanganyika inatekeleza Mkataba wa Kikanda wa Nchi Wanachama wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika unaoweka hatua za usimamizi wa uvuvi endelevu katika Ziwa Tanganyika na Bonde lake. Aidha, miongoni mwa hatua za usimamizi ni kuanzishwa kwa utaratibu wa kupumzisha shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kila ifikapo tarehe 15 Mei hadi 15 Agosti ya kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upumzishaji wa Ziwa Tanganyika katika kipindi cha miezi mitatu, unatarajiwa kuwa na tija ya muda mrefu kwa kuwa tafiti katika nchi zinazozunguka ziwa zinaonesha

kuwa kipindi hicho kunakuwepo na samaki wengi wachanga aina ya migebuka na dagaa. Samaki hawa wanahitaji kipindi cha miezi mitatu mpaka minne kufikia kiwango cha kuvuliwa. Aidha, kupumzisha ziwa katika kipindi hicho kutaruhusu samaki kukua na mavuno kuongeza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kandege, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa kuwa kwa kiasi kikubwa upungufu wa samaki unachangiwa na uvuvi haramu: Je, Serikali imejipangaje katika kuhakikisha inapambana na uvuvi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, mwitikio wa umuhimu wa ufugaji kwa kutumia vizimba katika Ziwa Tanganyika upo chini sana: Je, Serikali ipo tayari kwa kushirikiana na Wabunge wanaotoka ukanda wa Ziwa Tanganyika kutoa elimu kwa wananchi ili waweze kuchangamkia fursa hii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza na hili swali la kwanza. Ni kweli, uvuvi haramu unachangia kwa kiasi kikubwa sana kupungua kwa samaki katika maziwa yetu, siyo tu Ziwa Tanganyika, bali maziwa yote yanayozunguka nchi yetu. Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi tayari imeshaweka mikakati madhubuti kuhakikisha uvuvi haramu unakwenda kukomeshwa katika maziwa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati ipo mingi na nisingependa sana kuisema kwa sababu mingi inahusisha masuala ya kiintelijensia. Tayari vijana wetu wa kijeshi wameshaanza kufanya *operation* katika maeneo mbalimbali kuhakikisha tunadhibiti uvuvi haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni kule Bahari ya Hindi. Wale Wabunge wanaotoka katika maeneo hayo, tayari wameona jitihada za Serikali kukomesha uvuvi kwa njia ya

mabomu kama ambavyo Serikali imechukuwa hatua stahiki zinazotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusiana na vizimba. Ni kweli, tumeshaanza kutoa elimu, na elimu haina mwisho, tunaendelea kutoa elimu kupitia wataalamu wetu. Mimi na Mheshimiwa Waziri tayari tumeshafika katika maeneo hayo kuendelea kutoa elimu kwa wavuvi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo tayari kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge tunapopata nafasi, siku za *weekend* tunakwenda kutoa elimu. Hata baada ya Bunge, tupo tayari kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge kwenda kutoa elimu kwa wavuvi wetu ili waweze kuelewa namna sahihi ya kuchukua vizimba na boti kwa ajili ya mikopo ya riba nafuu ambayo Wizara imekuwa ikiendelea kuitoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ipo tayari kushirikiana na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha tunakwenda kutoa elimu kwa kusaidiana na Serikali, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri anajua kwamba Ziwa Tanganyika sisi tunaotoka maeneo yale ndiyo shamba letu na ndiyo duka letu, hivyo unapopumzisha hilo ziwa kwa miezi mitatu, ningependa kufahamu, Serikali mmetenga kiasi gani kwa ajili ya kuwapatia wavuvi kwa kipindi hicho cha mpito?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki cha miezi mitatu ni kweli, kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kuwa Ziwa Tanganyika kwa asilimia kubwa wanaozunguka eneo hilo, ndiyo shamba lao. Kwa kutambua hilo, Wizara imekuja na mkakati wa kuwakopesha wavuvi hao vizimba.

Vizimba hivi vitasaidia kuongeza uzalishaji ambao umekuwa ukifanyika katika hilo Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli wavuvi wa Ziwa Tanganyika wamepokea jambo hili kwa mikono miwili na wapo tayari. Pia tayari tumeshapokea maombi mengi na tarehe 5/5/2024 Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi anakwenda kukabidhi vizimba kwa wale wote walioomba katika eneo la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo tayari kuendelea kutoa vizimba kwa wale watakaoomba na milango ipo wazi waendelee kuomba. Huu ndiyo utakuwa mbadala pekee wa kuwasaidia wavuvi katika eneo hilo la Ziwa Tanganyika.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Alexander Mnyeti, kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Wizara ya Maji, namwita sasa Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, aulize swali lake.

Na. 234

**Malipo ya Fidia kwa Wananchi Waliopitiwa na Bomba la Maji la Mto Ruvuma**

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA** aliuliza:-

Je, lini Serikali italipa fidia kwa Wananchi waliopitiwa na bomba la maji la Mto Ruvuma – Mtwara Vijijini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Mto Ruvuma hadi Manispaa ya Mtwara – Mikindani na baadhi ya maeneo ya Lindi na Mtwara, vikiwemo vijiji vilivyopo pembezoni mwa bomba kuu. Kwa sasa Serikali inaendelea na mapitio ya usanifu wa mradi huo ili kujiridhisha na mawanda yake. Kazi hiyo ikikamilika, maeneo yote yanayopitiwa na miundombinu ya maji yataainishwa na kisha daftari la tathmini litaandaliwa kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi wote ambao maeneo yao yatapitiwa na miundombinu hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtamba, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza. Ikiwa Serikali imefanya tathmini na maandalizi ya mchakato wa fidia ulishafanyika, maana yake ni kwamba, fedha ilitengwa kwa ajili ya mradi huo. Sasa nataka kujua, mradi huu umekwama wapi na fedha iliyotengwa tokea mwaka 2015 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu imepelekwa wapi?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Shamsia kwa namna ambavyo anaendelea kupambana na kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilika. Mradi huu haujakwama kwa sababu, kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, fedha zilitengwa mwaka 2015. Katika upande wa *engineering*, unapofanya usanifu na baada ya usanifu mradi ukakaa kwa muda mrefu kabla ya kutekelezwa, maana yake ni kwamba inawezekana kuna mabadiliko ya mahitaji ya eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachofanya sasa kama Serikali ni kufanya mapitio ya usanifu ili tujiridhishe kama mahitaji ambayo yalikuwepo 2015 ni sawa na mahitaji ya sasa au

tunapobadilisha ule usanifu maana yake ni kwamba, maeneo ambayo mradi utapita inawezekana kukawa na mabadiliko, ili tujiridhishe kwamba watakaolipwa watalipwa fedha kulingana na njia kuu ya bomba ambapo litapita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu haujakwama na tumeshaanza tayari kuhakikisha kwamba wananchi wa Mtwara wanapata maji, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza. *(Makofi)*

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa maji wa kujenga mtambo wa kusafisha maji chanzo cha Mbukwa, Wilaya wa Wanging'ombe wenye thamani ya shilingi bilioni 3.5 mkandarasi alikabidhiwa tangu Oktoba, 2023. Wananchi wa Wanging'ombe wanataka kujua, ni lini mradi huu utaanza kufanya kazi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya, kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Njombe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa mradi huu upo kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata maji. Serikali imetoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 154 kwa ajili ya kuhakikisha kwamba upatikanaji wa maji vijijini unaendelea kutekelezwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea juzi hapa kwamba wakandarasi wamekuwa wakijifichia kwenye kivuli cha kwamba Serikali haijalipa. Serikali imetoa shilingi bilioni 154 kwa ajili ya maji vijijini na shilingi bilioni 69 kwa ajili ya Mamlaka ya Maji Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana na kupeana taarifa,

nasi kama Serikali tuweze kuchukua hatua dhidi ya wakandarasi ambao wameonekana wanasuasua katika miradi ya Serikali, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ndaki, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naipongeza Serikali kwa Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria kwenda Kata ya Seng'wa, Jimbo la Maswa Magharibi. Nataka kuuliza, je, ni lini sasa vijiji viwili vilivyobaki vya Mwanundi na Manawa, navyo vitapata maji hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mbunge wa Maswa Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwa kazi kubwa anayoifanya kwa ajili ya wananchi wake wa Maswa. Vilevile tunaipongeza sana Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba mradi ambao ulikwama kwa takribani miaka 10 na kitu, kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kuja mpaka Busega, Bariadi hadi Itilima na awamu ya pili Maswa, Meatu, tayari mkandarasi ameshasaini mkataba na tayari yuko *site* ameshaanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge tuendelee kushirikiana kuhakikisha kwamba wananchi wetu wa Mkoa wa Simiyu wanaendelea kupata maji safi na salama, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge, swali la nyongeza.

**MHE. ALLY M. KASSINGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kutoa maji katika Mji wa Kilwa Masoko kupeleka Kilwa Kisiwani ambao ulitengewa shilingi bilioni 1.6, kwa zaidi ya miaka mitatu sasa umekwama. Nini maelezo ya Serikali kuhakikisha kwamba

wanatatua tatizo la mradi huu na hatimaye wananchi wa Kilwa Kisiwani wanapata maji kama ilivyotarajiwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kassinge, Mbunge wa Kilwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri, jana tulikuwa wote na Mheshimiwa Mbunge na tulijadili sana kuhusu huu mradi. Baada ya kukaa naye na kujadili kwa kina kuhusu mradi huu, nikachukua hatua ya kuwashirikisha wataalam, na hivi tunavyoongea, tayari *RM* ameshaanza kuchukua hatua dhidi ya mkandarasi ambaye bado hajatekeleza mradi huu kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunajiridhisha kama anadai ili tuone kama ameshaleta hati ya madai ili aweze kulipwa na mradi uweze kuendelea bila kuwa na changamoto yoyote, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itarekebisha Bwawa la Maliwanda ambalo maji yake wanatiririka tu saa hizi kwa sababu ya mafuriko? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Getere, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua changamoto iliyopo Bunda, na changamoto hii Mheshimiwa Getere ameshanitaarifu na kuna wananchi ambao wamepata changamoto kule. Nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya kutoka hapa tutaonana ili tukaangalie namna ya kuchukua hatua za dharura ili kuanza kutatua changamoto iliyojitokeza katika jimbo lake, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cherehani, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Maji wa Kata ya Igunda umekuwa wa kusuasua kwa muda mrefu. Ni nini kauli ya Serikali ili kuweza kukamilisha mradi huu ili kuondoa adha kwa wananchi wa Kata ya Igunda? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cherehani, Mbunge wa Ushetu, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba wilaya zilizoko katika Mkoa wa Shinyanga, zote zinapata maji kutoka Ziwa Victoria isipokuwa tu Ushetu. Tayari tumeshakaa na Mheshimiwa Mbunge na bahati nzuri jana tulijadili sana hili suala na hivyo vijiji tayari nimeshaviripoti kwa wataalamu wetu ili wakajiridhishe tuvute maji kutoka Kahama Mjini au tuvute maji kutoka Shinyanga ilimradi tu wananchi wa vijiji hivyo waweze kupata maji, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, sasa namwita Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, aulize swali lake.

Na. 235

**Ujenzi wa Barabara ya Tabora – Mambali – Bukene hadi Itobo**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Tabora – Mambali – Bukene hadi Itobo kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Tabora – Mambali – Bukene hadi Itobo kilometa 114, unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi sasa jumla ya kilometa nane kuanzia Tabora Mjini hadi Nyuzi *Round-about* zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ujenzi wa kilometa moja kuanzia Kijiji cha Uduka kuelekea Kabanga unaendelea na umefikia 60%. Kwa sehemu iliyobaki, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea na kazi za ujenzi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zedi, swali la nyongeza.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba barabara hii inajengwa kwa awamu na awamu, maana yake ni mwaka wa fedha, kwamba ni kidogo kidogo. Swali langu ni kwamba, je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuongeza idadi ya kilometa kwa hii awamu kwa mwaka wa fedha, kwa sababu tukiendelea na kilometa moja moja kwa kila mwaka wa fedha na barabara hii imebakiza kilometa 104, haoni kwamba itatuchukua miaka 104 kumaliza barabara hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali siyo kuijenga hii barabara kwa awamu kwa kipindi chote, lakini mpango wa Serikali ni kuijenga barabara hii yote kwa kiwango cha lami na ndiyo maana imesanifiwa yote. Kwa kadiri tunavyopata fedha Serikali imeona ni bora tuanze kujenga kwa awamu kadiri fedha zinavyopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna uhakika kwamba kadiri tutakavyokuwa tunaendelea, na bajeti itakavyoruhusu, mpango

ni kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami kama anavyoomba Mheshimiwa Mbunge, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mko wengi sana mnaotaka kuuliza maswali ya nyongeza hapa. Kwa hiyo, nawaomba watakaopata nafasi, waende moja kwa moja kwenye swali na swali liwe fupi. Tuanze na Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ni miezi sita sasa Barabara ya Mbulu – Garbabi mkandarasi ameondoka *site*. Je, ni lini mkandarasi atarudi *site* kumalizia kazi iliyobaki?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi ambaye anamsema, najua anajenga Mbulu hadi Garbabi, lakini huyu mkandarasi tumesaini naye mkataba wa kuanzia Labay kwenda Haydom na Dareda kwenda Dongobesh na Mheshimiwa Mbunge ni shahidi. Baada ya mvua kukatika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mkandarasi ataendelea na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichokuwa kinafanyika ni kujenga makaravati ambayo yalikuwa hayaathiriki na mvua inayoendelea. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba mkandarasi yupo, anaendelea kuzijenga barabara ila tu alikuwa amepunguza kasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Rose Busiga, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE V. BUSIGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itakamilisha Barabara ya Geita – Bukoli – Kakola mpaka Kahama kwa kiwango cha lami ili kusaidia kuunganisha Mkoa wa Geita na Shinyanga? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Rose ni moja ya barabara ambayo Serikali imeipa kipaumbele kikubwa sana. Ni kweli kwamba Mkoa wa Geita na Mkoa wa Shinyanga ulikuwa haujaunganishwa kwa kiwango cha lami na hii ndiyo ajenda kubwa ya Mkoa wa Geita. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kuanzia Kahama hadi Ilogi – Kakola, kwa kushirikiana na wenzetu wa bajeti, tayari tumeshasaini mkataba, kwa hiyo, hiyo barabara itajengwa. Tunavyoongea sasa hivi barabara ya kutoka Ilogi – Bukoli – Nyaluyeya hadi Geita, ipo kwenye mpango wa manunuzi ambayo muda wowote itatangazwa ili tuweze kuunganisha Geita na Kahama kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha Barabara ya Chalinze – Segera hadi Himo ambayo imeanza kupoteza ubora wake? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja ya Chalinze – Segera hadi Himo ni kati ya barabara ambazo zimejengwa siku nyingi na ni finyu. Sasa hivi tuko tunaifanyia usanifu ili kuweza kuifanyia *rehabilitation* kwa maana kwanza, ni kuifanya matengenezo makubwa kwa maana ya marekebisho kwa maeneo ambayo ni finyu na pia kule kwenye miinuko kuweza kuipanua na kufanya barabara tatu. Kwa hiyo, huo ndiyo mpango ambao sasa hivi mhandisi mshauri anafanya ili kuibadilisha kabisa hiyo barabara, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya Manyoni – Sanza – Chali hadi Dodoma kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyotaja Mheshimiwa Mbunge sasa hivi tunakamilisha usanifu na baada ya hapo tutaanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini Serikali isitoe kipaumbele kwa barabara za kiusalama ambazo zinapakana na nchi jirani na wilaya mbalimbali za Tanzania, mathalan ile ambayo inapakana na nchi jirani ya Kenya na Wilaya ya Tarime na Rorya kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vigezo vya kujenga Barabara. Kigezo kimojawapo ni pamoja na barabara za ulinzi. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tunapochagua barabara za kuzijenga, ulinzi ni moja ya kigezo kikubwa sana. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ipo mipango ya kuzijenga hizo Barabara, lakini barabara ziko nyingi, kwa hiyo, tunakwenda kwa awamu kuzijenga hizo barabara, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maimuna Mtanda, swali la nyongeza.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, zoezi la ku-*mobilize resource* katika Barabara ya Mnivata – Newala – Masasi limechukua muda mrefu na barabara haipitiki. Je, ni lini ujenzi rasmi wa lami utaanza ili wananchi wapite vizuri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza uzuri wa hiyo barabara inafadhiliwa na wenzetu wa *African Development Bank* na tunafanya ufuatiliaji. Kitu ambacho nawahakikishia

Waheshimiwa Wabunge ni kwamba katika kipindi hiki cha mvua na hasa mvua ambayo imezidi, imekuwa zaidi ya wastani, kwa hiyo, kwenye miundombinu ya barabara imekuwa ni ngumu sana kufanya kazi za barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama kuna changamoto yoyote ya *mobilization* kwenye hiyo barabara, tutafuatilia tuone kama kuna changamoto yoyote, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, imetokea taharuki kubwa kule Iringa baada ya kusikia Miradi ya *REGROW* imesimama, wakafikiri kwamba na Mradi wa Ruaha umesimama. Je, Mheshimiwa Waziri atatuambia nini kinaendelea juu ya hii Barabara ya Ruaha? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Barabara ya Iringa kwenda *Ruaha National Park* kilometa 103 haina uhusiano na *Program* ya *REGROW*. Hii inafadhiliwa na *World Bank* na hivi tunavyoongea sasa hivi tuna miradi zaidi ya sita ambayo iko kwenye hiyo *package*. Sasa hivi tuko kwenye *tender evaluation* na kilometa zote 103 zinajengwa kutoka Iringa hadi Msembe, *Ruaha National Park*, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kibiti – Lindi imeathiriwa sana na mafuriko yanayoendelea katika maeneo hayo. Je, Serikali ina mpango gani wa matengenezo ya dharura hasa kwenye Daraja la Somanga na Daraja la Mbwemkuru? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba moja ya barabara ambazo zimeathirika sana ni barabara ya Kusini na ndiyo barabara kuu. Tunamshukuru Mungu tu kwamba mpaka sasa hivi walau watu wanaweza kupita, lakini tumeshaainisha maeneo yote ambayo yamepata changamoto kubwa na hasa kutokana na hii changamoto ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba bado maji yanaendelea kupita, kwa hiyo, baada ya kukauka Serikali imejipanga kuhakikisha kwamba tunarejesha mawasiliano. Hiyo ndiyo itakuwa kazi ya kwanza kurejesha mawasiliano na kuimarisha barabara zile zilizoharibika ili ziweze kurudi katika hali yake ya kawaida ikiwa ni pamoja na barabara muhimu sana ya kwenda Kusini aliyoitaja Mheshimiwa Chikota, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaenda kwenye swali linalofuata. Nimwite sasa Mheshimiwa Tumaini Magessa, kwa niaba yake Mheshimiwa Enosy Swalle, aulize swali.

Na. 236

**Ujenzi wa Barabara ya Katoro hadi Ushirombo**

**MHE. EDWIN E. SWALLE K.n.y. MHE. TUMAINI B. MAGESSA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Katoro hadi Ushirombo hususani kipande cha Katoro hadi Luhembero utaanza?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Katoro hadi Ushirombo yenye urefu wa kilometa 58.2 unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Kwa sasa maandalizi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya Nyikonga hadi Kashelo kilometa 10.5 yanaendelea chini ya ufadhili wa Benki ya Dunia ambapo mkataba kwa ajili ya kuanza ujenzi unatagemewa kusainiwa mwezi Agosti, 2024. Kwa sehemu zilizobaki za Katoro – Nyikonga kilometa 26.2 na Kashelo – Ushirombo kilometa 21.5, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Swalle, swali la nyongeza.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naishukuru sana Serikali na Wizara hii ya Ujenzi, wanafanya kazi nzuri sana nchini kwa ajili ya ujenzi wa barabara. Sasa ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Wananchi wa Jimbo la Lupembe nao wanahitaji barabara. Kumekuwa na ahadi ya muda mrefu ya Barabara ya Kibena – Lupembe mpaka Madeke. Ni lini barabara hii itaanza ujenzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, mwaka 2022 tuliomba barabara ya wananchi wa Mtwango – Kichiwa kwenda Ikuna, ipandishwe hadhi kuwa barabara ya *TANROADS*, iweze kujengwa kwa lami. Je, ni upi mpango wa Serikali kujenga barabara hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na swali la kwanza, barabara ya Kibena *Junction* - Lupembe – Madeke – Mlimba hadi Ifakara tayari tumeshaanza utekelezaji kwa kuijenga kwa kiwango cha lami. Kwa upande wa Morogoro tayari tuna kilometa 100 ambazo tumeshaanza kuzijenga na Wakandarasi wako *site* kwenye *lot* ya kwanza na nyingine tumeshasaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuanzia Mkoa wa Njombe kwenye Jimbo la Mheshimiwa Swalle, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza yalikuwa ni

maelekezo ya Rais na alitoa ahadi kwamba barabara hiyo ianze kujengwa kwa kiwango cha lami na tunavyoongea tuko kwenye hatua za mwisho za manunuzi tukianza na kilometa 42 kuanzia Kibena *junction*. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa mradi huo upo na tupo kwenye hatua za mwisho za manunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu kupandisha hadhi kwa maana ya barabara kutoka *TARURA* kwenda *TANROADS*, nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba ziko taratibu ambazo kama Wilaya na Mkoa wakishakamilisha taratibu zote wanaleta taarifa kwa Mheshimiwa Waziri ambaye baadaye anatuma timu ambayo inaenda kufanya tathmini ya ile barabara. Kwa hiyo, kama hatua zote zimekamilika nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa tutakupa majibu ya kuipandisha hadhi hiyo barabara kama itakidhi vigezo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, lini ahadi ya siku nyingi ya Serikali ya ujenzi wa barabara ya Kilolo – Kisinga – Wotalisoli – Mlafu hadi Ilula, itakamilika? Barabara hii ikikamilika watu watakuwa hawaendi mpaka mjini. Naomba Serikali itoe majibu ili wananchi wa Kilolo wasipate matatizo makubwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara aliyoitaja Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati amekuwa anaifuatilia sana. Nimhahakishie kwamba tayari tumeshalichukua, tulishawaelekeza wenzetu wa *TANROADS* na *TARURA* Mkoa wa Iringa waweze kutoa tathmini ya awali ili tuweze kuingiza kwenye mpango wa kuifanyia usanifu wa kina, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu, swali la nyongeza.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Barabara ya Kasamwa kupitia Nyaseke kwenda Nyang'hwale inaunganisha Wilaya mbili, lakini sasa hivi madaraja yote yamekatika na iko chini ya *TARURA* ambao hawana uwezo wa kuijenga. Ni lini *TANROADS* wanaweza kukubali kuihamishia huko ili iweze kutengezwa?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijampata vizuri huku mwishoni ili niweze kumjibu vizuri.

**MWENYEKITI:** Mwishoni pale ulikuwa unauliza nini Mheshimiwa?

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Kasamwa kupitia Nyaseke kwenda Wilaya ya Nyang'hwale, inaunganisha Wilaya mbili za Geita na Nyang'hwale lakini iko chini ya *TARURA*. Sasa hivi kuna madaraja makubwa matatu yamekatika na haipitiki kabisa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kanyasu, Waziri ameshakuelewa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba, sasa tunavyoongea *TARURA* imeimarika sana. Ina wataalam na hata bajeti yake imeongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama kutakuwa na changamoto ya kitaalamu *TANROADS* mara nyingi tumekuwa tukisaidiana na wenzetu wa *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumelipokea na hii nadhani inaenda kwa miundombinu yote ikiwa ni pamoja na madaraja yote Tanzania ambayo yameharibika iwe ya *TARURA* ama ya *TANROADS*. Hivyo, tumelipokea, namwagiza Meneja wa *TANROADS,* Geita waweze kuwasiliana na mwenzake wa *TARURA* Mkoa wa Geita waone namna watakavyoshirikiana, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini ujenzi wa Daraja la Godegode linalounganisha majimbo mawili, Jimbo la Kibakwe na Jimbo la Mpwapwa utaanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Daraja la Godegode lilikuwa limeshapata Mkandarasi lakini alijitoa likatangazwa upya. Tunavyoongea sasa hivi, tumeshapata Mkandarasi mwingine, tuko kwenye majadiliano ya mwisho ili aweze kuanza kazi ya kulijenga hilo Daraja la Godegode, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Manyanya, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani nyingi kutoka kwa wananchi wa Nyasa, kwa kuwa barabara ya kutoka Rwanda mpaka Ndumbi kipande hiko kimeshasainiwa tayari, je, Serikali haioni kwamba ni vema sasa ikaanza kujenga kutokea Ndumbi – Lituhi na kuelekea Rwanda badala ya utaratibu wa kutokea Rwanda kuja Ndumbi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hilo ni ombi na pendekezo la Mheshimiwa Mbunge. Sisi tunaomba tulipokee na tutaliangalia, kama kitaalam na kiutekelezaji litatufaa hatutokuwa na shida kwa sababu cha msingi ni kuijenga hiyo barabara yote kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, tumelipokea Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tumalizie swali la mwisho kwenye Wizara hii. Namwita sasa Mheshimiwa Hassan Zidadu Kungu, Mbunge wa Tunduru Kaskazini aulize swali lake.

Na. 237

**Ujenzi wa Barabara ya Pacha ya Mindu hadi Nachingwea**

**MHE. HASSAN Z. KUNGU** aliuliza: -

Je, lini Barabara ya Pacha ya Mindu – Ngapa hadi Nachingwea itajengwa kwa Kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya kutoka Pacha ya Mindu – Ngapa hadi Nachingwea yenye urefu wa kilomita 153 yameanza, ambapo zabuni kwa ajili ya kumpata Mhandisi Mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ipo katika hatua ya tathmini *(evaluation)*. Kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina zinatarajiwa kuchukua kipindi cha mwaka mmoja, hivyo zitakamilika mwezi Juni, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kungu.

**MHE. HASSAN Z. KUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali na yenye kuleta matumaini. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, barabara ile ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kwamba mwaka 2025 itakuwa imekamilika kwa kiwango cha lami na kwa kuwa, barabara ile ni muhimu sana kwa uchumi wa Wilaya ya Tunduru kutokana na madini yanayochimbwa katika Kijiji cha Ngapa, Ngapa B ama Ngapa Mtoni na kwa upande wa Nachingwea kule Kitowelo. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutuhakikishia kwamba ifikapo 2025 barabara ile itakuwa imekamilika kwa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazo barabara ambazo zimeahidiwa kwenye Ilani na zipo ambazo Ilani imetuelekeza tukamilishe usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kuzijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba barabara hii iko kwenye Ilani kwa maana ya kukamilishwa usanifu suala ambalo nataka nimhahakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalikamilisha mwezi Juni kama tulivyoahidi. Baada ya hapo sasa tutaingiza kwenye mpango wa kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami ili wananchi hawa ambao amewataja na shughuli zao za kibiashara waweze kufanya kwa unafuu na kwa uharaka, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nashon, swali la nyongeza.

**MHE. NASHON W. BIDYANGUZE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itajenga daraja katika Mto Malagarasi pale Ilagala? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, daraja la Malagarasi Chini najua sasa hivi halipitiki kutokana na maji kujaa. Tumeshakamilisha ama tuko mwishoni kukamilisha usanifu wa daraja hilo. Nataka nimhahakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pale lilipo tunalihamisha linakwenda juu kwa sababu lipo karibu sana na Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea pengine katika bajeti kwa sababu hatujapitisha, kama usanifu utakuwa umekamilika, basi litakuwa lipo kwenye mipango ya maandalizi ya kuanza kulijenga hilo daraja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu maswali ya kutosha kwa leo, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Angelina Sylvester Mabula, Mbunge wa Ilemela, naye aulize swali lake.

Na. 238

**Mgogoro wa Ardhi kati ya Wananchi na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege**

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA** aliuliza: -

Je, lini mgogoro kati ya wananchi wa Kiwanja cha Ndege Mwanza na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege – Mwanza utatatuliwa?

**MWENYEKITI:** Majibu Naibu Waziri, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali Kuu kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa ina nia ya dhati na imeendelea na jitihada mbalimbali katika kushughulikia mgogoro huu ili kuhakikisha unaisha. Aidha, taratibu za utwaaji ardhi zinaendelea kwa kufanya uthamini wa mali za wananchi, pindi uthamini utakapokamilika taratibu nyingine zitaendelea kulingana na Sheria ya Ardhi pamoja na Sheria ya Uthamini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Serikali. Napenda kuiuliza Serikali, ni sababu zipi ambazo zimefanya wabadili uamuzi wa awali ambapo ilikuwa wanatoa eneo la meta 700 kutoka kwenye njia ya kurukia ndege na sasa wanachukua eneo lote mpaka nje ya milima upande wa pili ambapo hapahitajiki kwa upanuzi wa Uwanja wa Ndege? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, naishukuru pia Serikali kwamba zoezi la uthamini limeanza na lilipangwa kufanyika kwa

siku 55, mpaka sasa hivi siku 38 zimekamilika, ni mitaa miwili tu ambayo imefikiwa ambayo ni Mtaa wa Bulyanhulu na Shibula bado mitaa mitatu; mtaa wa Kihili, Monze na Nyamwilolelwa. Je, ni lini kazi hiyo itakamilika kwa mitaa yote mitano ili wananchi waweze kupata haki yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na eneo ambalo awali lilikuwa limepangwa, lakini baada ya tathmini ya kina na tukiangalia kwamba Serikali ina mpango mkubwa wa kufanya Uwanja wa Ndege wa Mwanza kuwa wa Kimataifa, vipo vigezo mbalimbali, kimojawapo ni usalama. Tathmini ya kiusalama ilipofanyika, ilidhihirika kwamba ni muhimu na ni lazima wananchi wa eneo lote lile wapishe ili tuweze kuwa na uwanja ambao siyo tu ni mkubwa, lakini pia unakidhi takwa la kisheria pamoja na la ukubwa kwa maana ya kiusalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, kuhusiana na muda. Pendekezo la Mkoa kupitia Mkuu wa Mkoa la kuwatoa wananchi katika eneo lile kwa sababu za kiusalama lilipokamilika lilibidi liwasilishwe Serikalini na baada ya kupata idhini, tayari uongozi wa Mkoa pamoja na Kamishna wa Ardhi wa Mkoa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wameshaanza mchakato kwa ajili ya uthamini. Mara tu tutakapokamilisha, tutaanza zoezi la kulipa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Priscus Tarimo, swali la nyongeza.

**MHE. PRISCUS J. TARIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshaanza mchakato wa kuwalipa fidia wananchi wanaopisha upanuzi wa uwanja wa Moshi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wale wanaostahili tumeshaanza kuwalipa na wengine tumeshawalipa,

lakini kuna wananchi waliovamia ambao hawatastahili kulipwa katika eneo hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso, kwa kifupi.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Fidia imekuwa ikicheleweshwa sana kwa muda mrefu kwa hawa wanaopisha upanuzi wa viwanja na mmekuwa mkiahidi mtalipa riba, mfano pale Uwanja wa Manyara - Karatu. Je, ni lini mtalipa hizo riba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya fidia katika viwanja vyote nchini ikiwemo Kiwanja cha Manyara yatalipwa kwa kuzingatia sheria na taratibu za ulipaji fidia Serikalini.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, namwita sasa Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, aulize swali lake.

Na. 239

**Kufufua Usafiri wa Reli kutoka Dodoma kwenda Singida**

**MHE. MARTHA N. GWAU** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufufua usafiri wa Reli kutoka Dodoma kwenda Singida?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* ina mpango wa ufufuaji na ukarabati wa miundombinu ya Reli ya Kati yenye kiwango cha *Meter Gauge*. Aidha, *TRC* inaendelea na ukarabati na uboreshaji wa Njia Kuu

kutoka Dar es Salaam - Isaka ambapo kwa awamu ya kwanza uboreshaji umefanyika kutoka Dar es Salaam hadi Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa awamu ya pili, Serikali ina mpango wa kuboresha kipande cha Tabora – Isaka ikiwemo kukarabati kipande cha Dodoma – Manyoni kwa maeneo yaliyobaki wakati wa utekelezaji wa awamu ya kwanza. Vilevile, Serikali inafanya tathmini ya ukarabati wa njia ya reli ya Manyoni – Singida ili kuimarisha shughuli za kiuchumi kupitia usafiri wa reli kwa kuunganisha ukanda huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Gwau.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza: Je, ni lini Serikali italipa fidia kwa wananchi waliopisha maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa *SGR*, ambao ni wananchi wa Halmashauri ya Itigi na wananchi wa Halmashauri ya Manyoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Ni lini Serikali italipa *Service Levy* kutokana na ujenzi wa reli ya *SGR* kwa hizi Halmashauri ambazo zimepitiwa na reli hii; Halmashauri ya Itigi na Halmashauri ya Manyoni? Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia malipo hayo, nataka nimjulishe kwamba mfumo wa utoaji wa ardhi katika eneo hilo umekuwa ukienda sambamba na kulipa fidia. Maeneo ambayo hayajalipwa fidia kwa sasa ni yale maeneo ambayo tuna uchimbaji wa malighafi ya ujenzi ikiwa ni pamoja na Tambukareli, *Centre* pamoja na Milembela. Maeneo hayo yataendelea kulipwa kulingana na hatua za uthamini zitakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusiana na *Service Levy* kwa Halmashauri zote mbili kwa maana ya Itigi pamoja na hiyo nyingine ya Manyoni, tulifanya vikao mwaka jana, 2021 kati ya *TRC* pamoja na Halmashauri zote mbili, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake baada ya kukubaliana ikaonekana kwamba pengine inatakiwa waanze kulipwa shilingi 1,500,000,000 kwa kila Halmashauri moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza, tayari wameshalipwa shilingi 214,000,000 kila mmoja na malipo mengine yataendelea kufanyika kulingana na jinsi tutakavyokuwa tumechimba zile *material*. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge. Namwita sasa Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya aulize swali lake.

Na. 240

**Mabaraza ya Ardhi kuwa chini ya Mahakama**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itahamisha Mabaraza ya Ardhi kwenda kwenye Mfumo wa Mahakama?

**MWENYEKITI:** Namwita Mheshimiwa Waziri mwenyewe, Mheshimiwa Jerry Silaa, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuboresha mfumo uliopo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imeandaa mapendekezo ya kuhamisha shughuli zinazofanywa na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenda katika mhimili wa Mahakama. Pindi taratibu zitakapokamilika, Serikali italifahamisha Bunge lako Tukufu, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chege, swali la nyongeza.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Rorya haina Baraza la Ardhi la Wilaya jambo linalosababisha wananchi kusafiri umbali mrefu zaidi ya kilomita 60 mpaka 100 kwenda Tarime kufuata huduma hii, ambapo kwa umbali huo wakati mwingine wananchi hukata tamaa kushughulikia haki zao za kimsingi na za kisheria za utatuzi wa migogoro ya ardhi. Je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa kuna umuhimu wa kuanzishwa Baraza la Ardhi la Wilaya ya Rorya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kumekuwa na minong'ono mingi ya wananchi kuhusu kukithiri kwa vitendo vya rushwa kwenye utatuzi wa migogoro kwenye Mabaraza ya Ardhi ya Wilaya. Nataka kujua mpango mkakati milionao kama Serikali kuhakikisha kwamba vitendo hivi vya rushwa ambavyo vinanyima haki kwa wananchi, Serikali mmejipanga vipi kushughulika navyo ili angalau wananchi waweze kupata haki zao za kimsingi katika maeneo haya? Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nia hasa ya kuanzisha mabaraza haya yalikuja wakati wa ripoti ya Profesa Issa Shivji katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma za kutatua

migogoro ya kisheria katika kipindi ambacho Mahakama zilikuwa hazina ufanisi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali langu la msingi, kwa sasa Mahakama zetu zimeboreshwa sana, zina mifumo ya kisasa na zimesambaa nchi nzima na ndiyo nia ya Serikali kuondoa Mabaraza haya kwenye Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kupeleka kwenye Wizara ya Katiba na Sheria chini ya Mhimili wa Mahakama. Katika kufanya hivyo, moja itatatua tatizo ambalo sasa wanalipata wananchi wa Rorya la kusafiri umbali mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiri kwamba kumekuwa na malalamiko mengi hata kwa Waheshimiwa Wabunge humu ndani kuhusu tuhuma za rushwa kwenye Mabaraza haya. Wizara ilishatoa taarifa kwenye Kamati ya Bunge na ninaomba nitoe taarifa mbele ya Bunge lako Tukufu, pale tutakapopata taarifa mahsusi za Baraza ambalo limefanya shauri kwa kutumia maamuzi ambayo yanaonekana yameshawishiwa na rushwa, tutachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa nimekubaliana na Mheshimiwa Chege, Wizara inaendelea na taratibu za kuongeza Wenyeviti wa Mabaraza. Mpaka sasa tuna wilaya 36 ambazo zina mabaraza ikiwepo Wilaya ya Rorya, na pale tutakapopata Mwenyekiti wa Baraza, nimwahidi kwamba tutampeleka Mwenyekiti na Baraza litaanzishwa kwenye Wilaya ya Rorya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. DAVID M. DAVID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mwaka huu 2024, Januari Mheshimiwa Waziri wa Ardhi alikuja Same kushughulikia matatizo ya ardhi na mipaka katika Kata za Ruvu, Makanya na Bangalala na alituma wataalam wakaangalia matatizo yalivyo. Je, Mheshimiwa Waziri atarudi lini tena Same kwenye Kata za Bangalala, Makanya na Ruvu ili kushughulikia matatizo hayo?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba tarehe 26 Januari, 2024 nilifika Wilaya ya Same kwenye Jimbo la Mheshimiwa Dkt. David Mathayo. Kweli timu imeshakwenda na taarifa wameshaniwasilishia, na ninamwomba subira Mheshimiwa Dkt. David Mathayo, amekuwa akifuatilia kwa karibu sana, na pia nawaomba subira wananchi wa Jimbo la Same Magharibi, pindi nitakapomaliza bajeti yangu mwisho wa mwezi huu, Juni mwanzoni nitaongozana na Mheshimiwa Mathayo, tutaenda kutoa taarifa hiyo kwa wananchi, naomba wawe wavumilivu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa, kwa kifupi.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mabaraza haya ndiyo yamekuwa chanzo cha kurefusha migogoro ya ardhi nchini. Ni lini sasa mtaleta sheria ili mabaraza haya yaweze kuondolewa na kesi hizi ziweze kuendelea kwenye Mahakama zetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, Mbunge kwamba, ni kweli kuna mlolongo mrefu kama alivyosema Mheshimiwa Chege. Mabaraza hayapo wilaya zote, wapo Wenyeviti wanaolazimika kufanya mabaraza zaidi ya wilaya moja na hii inachelewesha haki kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inamalizia mikakati ya hatua za mwisho za kuhamishia mabaraza haya kwenye mhimili wa Mahakama na pindi itakapokuwa tayari tutaleta sheria Bungeni kwa ajili ya kutekeleza utaratibu huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana kwa majibu. Tunakwenda kwenye swali letu la mwisho. Namwita sasa Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, aulize swali lake.

Na. 241

**Kurejeshwa Nchini Kimondo cha Ivuna**

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE** aliuliza: -

Je, lini Kimondo cha Ivuna kitarejeshwa nchini na kutumika kama kivutio cha utalii?

**MWENYEKITI:** Naibu Waziri, Mheshimiwa Dunstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua kuwepo kwa kimondo kilichoanguka Kijiji cha Ivuna, Mkoa wa Songwe mwaka 1938 kikiwa na ujazo wa tani 0.0077 sawa na asilimia 0.0044% ya kimondo cha Mbozi kilichopo katika Kijiji cha Isele Mkoani Songwe chenye tani 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Kimondo cha Ivuna kinahifadhiwa kwenye Makumbusho ya Historia ya Asili iliyo katika Mji wa London Nchini Uingereza. Aidha, Wizara kwa kutambua umuhimu wa malikale zilizochukuliwa nchini kabla na baada ya uhuru kwa sababu mbalimbali kikiwemo Kimondo cha Ivuna, imeunda Kamati ya Kitaifa inayoratibu namna bora ya kurudisha au kunufaika na malikale hizo zilizopo nje ya nchi. Kamati inafuatilia taarifa zake ili kuweza kuishauri Serikali njia sahihi za kukirudisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Sichalwe swali la nyongeza.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni miaka 86 toka kimondo hiki kichukuliwe kule Ivuna

Jimbo la Momba, kimekuwa kikihifadhiwa kwenye hiyo *museum* iliyopo huko London. Je, sisi kama Wana-Momba tutanufaika vipi na kile ambacho wanakipata kwenye *museum* yao na Taifa kwa ujumla, baada ya miaka 86?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mahali hapo ambapo kilichukuliwa kimondo kwenye Kijiji cha Itumbula Kata ya Ivuna zipo taarifa nyingi ambazo zinazunguka eneo hilo ambazo zinavutia kwa ajili ya mambo ya utalii. Je, ni lini Wizara ya Maliasili na Utalii mtafika eneo hilo la Itumbula, Ivuna ili mweze kukutana na wazee wa mahali hapo tuweze kuwasimulia historia nzuri ya kupendeza katika eneo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba Serikali imeunda timu ya Kitaifa ya kuishauri namna bora ya kunufaika na uwepo wa malikale katika nchi za wenzetu ambazo zimetokea katika nchi yetu. Namwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, Kamati hii au timu hii inafanyia kazi mambo haya na itaishauri Serikali namna nzuri ya sisi kunufaika na malikale hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili kwamba ni lini tutakwenda kwenye eneo lile, nataka kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara tayari imeshafika kwenye eneo lile na imeanzisha tamasha ambalo hufanyika kila mwezi Juni. Tamasha hilo linaibua fursa za kiutalii kwenye eneo hilo na wataalamu wetu wanakamilisha michakato ya kujumuisha eneo hili liwe sehemu ya tamasha linalofanyika katika mkoa ule.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nicodemas Maganga, swali la nyongeza.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa kupitia Ilani ya Chama chetu tuliwaahidi wananchi kwamba kwenye mapori yetu tutatenga maeneo ya kuishi watu, lipo pori la Kigosi ambalo limepakana na Kata ya Iponya na Kata ya Bukandwe: Ni lini Serikali itatenga maeneo ya kuishi watu ili waweze kufanya shughuli zao na kuishi kwa uhuru na amani kwenye hiyo hifadhi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili lililoulizwa ni tofauti sana na swali la msingi. Naomba kumshauri Mheshimiwa Mbunge alilete swali hili kama swali mahsusi ili niweze kulijibu kikamilifu.

**MWENYEKITI:** Nakubaliana na Mheshimiwa Naibu Waziri, lije kama swali la msingi. Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu kwa Waheshimiwa Wabunge. Kama mnavyoona, najaribu sana kuchukua wengi kadri inavyowezekana. Kwa wale ambao hawakupata nafasi, Jumatatu nayo ni siku.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni ambao wametutembelea Bungeni leo, tuanze na wageni ambao wamekaa Jukwaa la Spika na hawa ni wageni tisa wa Mheshimiwa Spika ambao ni wadau wa *Mbeya Tulia Marathon,* wapo safarini kuelekea Mbeya kwenye kushiriki mbio hizo zitakazofanyika terehe 11 Mei, 2024. *(Makofi)*

Pia tunaye Jimmy Jamal, Mkurugenzi wa Vipindi *Classic FM Radio,* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Zaria Kweka, ni Mkurugenzi Mkuu wa *Dodoma Media Group*, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Mike Mushi, Mshauri wa Bodi ya Betika; pia wapo Ndugu Selemani Kodima, Ndugu Mariam Kasawa, Ndugu Abdallah Twaha, Ndugu Emmanuel Ndahani, Ndugu Veronica Komba na Ndugu Baraka Mgeyekwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Mheshimiwa Hussein Bashe, Waziri wetu wa Kilimo, huyu ni Ndugu Godfrey Malekono, Afisa Mtendaji Mkuu wa Soko la Bidhaa mbalimbali, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wageni kutoka *CRDB* ambao ni Ndugu Fredrick Nshekanabo ambaye ni Afisa Mkuu wa Fedha, yupo Ndugu Chabu Mishwaro, ni Meneja wa Kanda ya Kati na pia yupo Ndugu Richard Tarimo, ni Meneja Mahusiano Kilimo na Biashara, Wateja Wakubwa Makao Makuu. *(Makofi)*

Kundi la pili ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni wawili wa Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mbunge Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu ambao wanatoka hapa Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni wa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Vijana Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Mwanza. *(Makofi)*

Mwingine ni mgeni wa Mheshimiwa Maryam Omar Said ambaye ni mdau wa mazingira na pia ni rafiki yake kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni mwingine aliyepo ni mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Pius Chaya ambaye ni mpigakura wake kutoka Manyoni, Mkoa wa Singida. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Vita Kawawa ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Maimuna Pathan ambao ni familia yake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Vilevile wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Mwita Getere ambao ni Wajumbe wa *Scheme* ya Karamwe Mariwanda kutoka Bunda Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 25 wa Mheshimiwa Noah Lemburis ambao ni wapigakura wake na wanachama wa Kikundi cha *UPEFA* kutoka Jimbo la Arumeru Magharibi Mjini Arusha. *(Makofi)*

Wengine waliopo ni wageni 12 wa Mheshimiwa Edward Olelekaita ambao ni wapigakura wake kutoka Jimbo la Kiteto Mkoa wa Manyara, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Pia wapo wageni 10 wa Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Jimbo la Madaba Mkoa wa Ruvuma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 69 wa Mheshimiwa Rose Busiga ambao ni Umoja wa Wanawake Tanzania Jimbo la Geita Mjini na Geita Vijijini, karibuni sana kwenye Bunge. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 11 wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, hii ni Kwaya ya Safina kutoka Jijini Dodoma. Naona hawajaingia bado.

Tunao wageni tisa wa Mheshimiwa Fatma Toufiq, hawa ni Kikundi cha *Tanzanite Fashion Show* wakiongozwa na Eva Raphael - *Miss Tourism Africa 2022* na Balozi wa *Miss Tourism Africa 2024* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. Huyo *Miss* atunyooshee mkono hapa kama yupo, karibu sana. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 19 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambao ni viongozi wa dini kutoka Mpanda, Mkoa wa Katavi, karibuni sana viongozi wetu wa dini. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 39 wa Mheshimiwa Agness Marwa ambao ni Wachungaji wa *Bunda Bible College* kutoka Mkoa wa Mara, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi waliotutembelea kwa ajili ya mafunzo, kwanza ni wanafunzi 48 na walimu watatu wa Shule ya Sekondari

Bwawani kutoka Chalinze, Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 39 wa Umoja wa Wanachuo kutoka Musoma wanaosoma Jijini Dodoma, karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hayo ndiyo majina ya wageni. Sasa tunaendelea na hatua inayofuata.

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na michango yenu kwenye Bajeti hii ya Kilimo. Ninayo majina ya wachangiaji hapa. Tutaanza na Mheshimiwa Profesa Patrick Alois Ndakidemi atafuatiwa na Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, halafu Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, ajiandae.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Nikiwa kama Mjumbe wa Kamati, nianze moja kwa moja kwa kuiunga mkono hoja na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo pamoja na msaidizi wake na Watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na taasisi zilizopo chini ya Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri wanayoifanya kwenye kukiendeleza kilimo chetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa ushuhuda. Kwenye utoto wangu ilikuwa ni miaka ya 1960, lakini kuanzia miaka ya 1970 nilikuwa kijana. Kuanzia miaka hiyo ya 1970 nimekuwa natoa huduma katika Wizara ya Kilimo hadi leo hii. Kwa

hiyo, kuna ushuhuda nataka niseme kwamba, kwa miaka hii ambayo tumeingia huku Bungeni, Bajeti ya Kilimo kwa nia njema ya Mheshimiwa Rais wetu imeongezeka kutoka shilingi bilioni 294 na mpaka sasa hivi tuna bajeti hii ambayo Mheshimiwa Waziri anatuomba pesa ni shilingi trilioni 1.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, natoa ushuhuda hapa kwamba mara hii maendeleo na mwenendo wa Wizara ya Kilimo ni mzuri sana. Tumejionea wenyewe kwamba kilimo kinachangia vizuri kwenye Pato la Taifa na kilimo cha sasa hivi kimeleta tija. Mheshimiwa Waziri anapeleka mbolea kule na tija inaonekana ikiwemo kujitosheleza kwa chakula ndani ya nchi yetu na kuna ajira, na vijana wa *BBT* wapo pale. Pia taasisi zote maendeleo yao ni mazuri sana na zinafanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Umwagiliaji pia inafanya kazi nzuri sana, tunaona miradi mingi ya umwagiliaji. Hapa namshukuru sana Mheshimiwa Waziri, kwenye Jimbo langu nimeshapata miradi ya umwagiliaji kiasi. Ukanda wa tambarare kule Mandaka Mnono kuna mradi unajengwa. Pale Mabogini kuna mradi ambao ulikuwa ni wa Wajapani, lakini ukanda wa Arusha Chini tunahitaji mradi pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni mengi, ni ya kuua mtu kabisa na sasa hivi wananchi wa Arusha Chini, kwenye vijiji vya Chemchem na Mikocheni kuna mafuriko, watu wapo kambini. Namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba twende tukawekeze mradi wa umwagiliaji pale Mikocheni na Chemchem maji ni mengi. Haya maji sasa badala ya kutusaidia kuzalisha chakula yanaumiza wananchi na wapo makambini kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utahusu zao la kahawa. Nikiwa kama mtu niliyetoka kwenye eneo linalolima kahawa nitachangia kwenye hili eneo na ndicho kitu ambacho wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro wale wanaolima kahawa watapenda wakisikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa ni zao muhimu sana, tunaliita ni dhahabu ya kijani. Zao hili ni bidhaa ya pili kwa

umaarufu hapa duniani. Baada ya mafuta ya *petrol* na *diesel* kahawa ndiyo zao la pili maarufu hapa duniani. Pia ni kinywaji cha pili kinachotumika duniani baada ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi kama Mwanakilimanjaro naringa sana kwamba tunazalisha kinywaji cha pili kwa matumizi duniani. Inakadiriwa kwamba watu wanaokunywa kahawa duniani wanatumia kama vikombe bilioni 2.6 kwa siku. Wanywaji hawa wa kahawa wanaipenda kahawa kwa sababu ina mambo mengi mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, wataalamu wanasema kwamba kahawa inaondoa msongo wa mawazo, kahawa inaweza ikazuia usipate kisukari *(type two diabetes),* inaweza ikazuia ugonjwa wa moyo, inaweza ikapunguza maumivu na pia inaweza ikarefusha Maisha. Watafiti wameshaona haya mambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaringa kwamba mikoa inayozalisha kahawa hapa duniani inachangia kwenye haya mambo kwenye dunia yetu hii. Mikoa hii ni mingi, ipo zaidi ya 12 ikiwepo Mkoa wa Kilimanjaro, Arusha, Ruvuma, Lushoto na kule kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa katika maeneo yetu hapa nchini inazalishwa na wakulima wadogo wadogo ambapo duniani kuna wakulima milioni 25 wanaoshiriki kwenye kuzalisha kahawa. Pia sisi Tanzania ni sehemu ya hawa wakulima wadogo wadogo wanaozalisha 80% ya kahawa hapa duniani. Kwa hiyo, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa kama mzawa wa eneo linalozalisha kahawa, niseme hapa kwamba wakulima wa kahawa kwa ujumla wake wana maisha magumu, siyo jinsi tunavyofikiria ilivyokuwa kule nyuma. Bei wanazopata ni ndogo, hazitoshelezi ukilinganisha na kazi kubwa ambayo ipo kwenye uzalishaji wa kahawa. Zao la kahawa lina kazi ngumu sana na zina gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kahawa ya *Arabica,* kuna kukata matawi, kuna kufanyia palizi, kuna kuweka mbolea, kuna kupiga dawa, kuna kupukuchua kahawa, kuna kuvuna kahawa, kuna kuchagua na kuondoa zile kahawa mbovu, kuna kukausha na kuisafirisha kuipeleka sokoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ugumu wa uzalishaji wa hii kahawa kutokana na hivyo vitu ambavyo nimesema wanavifanya wakulima wetu, bei ya kahawa ni ndogo. Kwa mfano, taarifa tulizozipata kutoka kwenye Bodi ya Kahawa kwa mwaka 2022/2023 zimeonyesha kwamba bei ya kahawa ilikuwa shilingi 3,000 kwa kilo kwa kahawa aina ya *Arabica* na shilingi 2,000 kwa kahawa aina ya *Robusta. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii kilo ya kahawa ambayo tumeuza kwa shilingi 2,000 mpaka shilingi 3,000 huwa ikienda kule nje huzalisha vikombe 120 hadi 140 vya kahawa. Kahawa kilo moja ya kwetu hapa huzalisha vikombe 120 mpaka vikombe 140 vya kahawa na bei ya kikombe kimoja cha kahawa huko wanakoitumia ni sawa na dola 3.5 mpaka dola 3.7. Tukija kwenye pesa za Kitanzania, hiki kikombe kimoja cha kahawa kinauzwa shilingi 8,750 mpaka shilingi 9,300. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkulima kama nilivyoeleza hapo awali, hupata shilingi 2,000 mpaka shilingi 3,000 kwa kilo moja ambapo hawa wanaokwenda kuinywa kule, mtu anayeuza yule wa mwisho ukizidisha hivyo vikombe 120 mpaka 140 anapata kati ya shilingi 1,050,000 mpaka shilingi 1,300,000. Kwa hiyo, hebu linganisha shilingi 2,000 na shilingi 3,000 mpaka shilingi 1,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kinachoonekana hapa ni kwamba mwananchi anayezalisha kahawa anapata chini ya bei ya nusu kikombe cha kahawa. Kwa hiyo, pamoja na hii bei kuwa ndogo, wananchi hawa wamechangia kwa kiasi kikubwa kwenye pato la Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2023/2024, Bodi ya Kahawa imeonyesha kwamba tumeuza tani 81,000 na kuiingizia

nchi yetu kiasi cha shilingi bilioni 440.4. Hii inaonyesha kwamba tumevunja rekodi ya mauzo ya kahawa kwenda nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ambayo tunayo, naomba niishauri Serikali kitu kimoja, ili kahawa iweze kuleta tija na wananchi wafurahie hii kazi ya kuzalisha hili zao la kahawa, cha kwanza ambacho ninaishauri Serikali, kwa mfano kwenye Mkoa wa Kilimanjaro, sisi ni wazalishaji wakubwa wa kahawa ya *Arabica* ambayo ndiyo inapendwa duniani kote. Sasa, shida moja kubwa tuliyonayo kule ni maji. Kahawa inahitaji maji ya kutosha. Muda wote kahawa inahitaji ipate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya nyuma tulikuwa na miradi kama ya *traditional irrigation project,* ilikuwa inahudumia ile mifereji ya asili. Watu wanapata maji wanazalisha kahawa na mazao mengine. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, mimi fedha za Mfuko wa Jimbo nilipeleka kusaidia mifereji ya asili, naomba nao waje waniunge mkono ili turekebishe ile mifereji tupate maji ya kutosha ili wananchi wapate kahawa ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili, tumeona *disparity* iliyopo kati ya bei wanayopata wananchi na kule duniani watu wanavyopata faida kutokana na hii kahawa. Naomba Serikali isaidie wananchi kupata masoko ya uhakika, na tusiwe na ukiritimba ili yule mlaji wa mwisho apate fedha ya kutosha na aweze kunufaika na hili zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitashauri, ninajua Mheshimiwa Bashe ni mtu makini sana, apambane na wale wanaozalisha *end products* za kahawa, tusindike kahawa yetu hapa hapa nchini. Wakamate wale ma-*tycoon* wakubwa watano wanaotengeneza *products* za kahawa, waje waweke viwanda hapa ili tusindike kahawa yetu hapa na tuiuzie hapa hapa ili zile fedha ziweze kubaki hapa nchini na wananchi wetu watapata bei nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa mwingine ni kuhusu usambazaji wa miche bora ya kahawa. Tumeona

kwamba mwaka huu wanategemea kusambaza miche milioni 20. Namwomba Mheshimiwa Waziri, bado tunahitaji miche. Watu wamehamasika, kwa hiyo, miche iongezwe, kwani miche milioni 20 haitoshi. Mikoa inayolima kahawa ni mingi na kwa hiyo, ikiwezekana tushirikishe wadau wengine ili tuweze kuzalisha miche ya kutosha.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Profesa, hitimisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, cha mwisho ni kuboresha huduma za ugani kwa wakulima ili wapate pembejeo kama dawa, kama ilivyokuwa zamani, ili waweze kushiriki kikamilifu kwenye uzalishaji wa hili zao la kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Profesa Patrick Alois Ndakidemi. Sasa namwita Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri, atafuatiwa na Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda ajiandae.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa hii. Leo naomba mchango wangu ujikite kwa pongezi, kwa sababu kwa kipindi chote niko Bungeni tangu mwaka 2015 sijawahi kuacha kuchangia hotuba ya kilimo. Natangulia kwa kusema kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wabunge siku zote kilio chetu kilikuwa ni kwamba Serikali imfuate mkulima shambani. Serikali hii ilikuwa inamwacha mkulima anateseka, wanakuja kukutana naye kwenye mavuno wakitafuta soko kwa tozo, sijui kwenye mageti, lakini leo hii tuseme ukweli, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo inamfuata mkulima shambani na kipima udongo na kumpa ushauri wa kitaalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii inamfuata mkulima kwa kumuuzia mbegu kwa ruzuku, Serikali hii inamfuata mkulima mdogo kwa kumpa mbolea ya ruzuku, Serikali hii pale mkulima ambapo anakwama kwamba bei ya soko imeshuka, kupitia Wizarani, *NFRA* inakwenda kununua hayo mazao ili kumnusuru mkulima asipate hasara, vilevile hali ya mavuno ikiwa mbaya Serikali hii inaleta chakula cha msaada. Jamani Serikali hii kupitia Wizara ya Kilimo inaupiga mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii haijarudi nyuma, leo inaandaa mpango wa miaka 25 kwa ajili ya kwenda kufanya mapinduzi makubwa kwenye kilimo. Naomba kuwaambia, waweke mfumo mzuri wa kupokea ushauri ili wapate ushauri hadi wa wakulima ambao hawajui kusoma na kuandika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema kwamba, hizi *documents* za Mpango huu ziwepo kwenye lugha zote mbili; Kiswahili pamoja na Kiingereza. Serikali hii imebuni kuanzisha ajira mpya milioni tatu ambazo wamejikita kwa wanawake na vijana na leo hii wameanzisha mashamba makubwa ya pamoja, yaani Miradi ya *BBT*, na vilevile ni wasikivu na wanapokea ushauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili liliwashauri kwamba pamoja na hizi mpya, wawafuate wakulima kule *site* walipo. Leo hii kupitia bajeti ya mwaka huu tunaona wanaenda kupeleka miradi ya *BBT* kwenye halmashauri 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, kuna hizi halmashauri zenye maneno kama mji au jiji, watukumbuke, kwa sababu siyo zote ni ya mjini, wengine tuna mashamba. Pale kwangu mimi ni Diwani wa Halmashauri ya Kondoa Mji, tunayo Skimu ya Umwagiliaji ya King'ang'a Mtaa wa Iyoli Kata ya Kingale, pale tuna ekari 30,000. Tunaomba watuletee ili vijana na akina mama wa Halmashauri ya Kondoa Mji waweze kujiajiri na waweze kunyanyua uchumi wa mtu mmoja mmoja.

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. KHADIJA S. TAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa kwa mzungumzaji. Anazungumza vizuri sana, lakini ningeomba amwombe pia Mheshimiwa Waziri kujumuisha siyo wanawake na vijana peke yake, iwe ni pamoja na watu wenye ulemavu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam, unapokea hiyo Taarifa.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea Taarifa, lakini pia niongezee hapo kwenye jiji, Mheshimiwa Spika ndiye kiongozi wa Bunge letu, tusimsahau. Halmashauri ya Jiji la Mbeya haina mradi wa umwagiliaji. Naomba kwenye hitimisho naye useme neno ili kiongozi wetu wa mhimili naye apone.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BBT* hii leo kwa ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na Wizara imepitisha, inakwenda kutoa mikopo kwa vijana na wanawake ambao tayari wamejiajiri katika kilimo. Jamani Serikali hii pamoja na miradi mikubwa ya umwagiliaji, bado inakwenda kuchimba kisima kule kwa mkulima wa chini kabisa. Jamani naomba mmwage makofi mengi na mumpatie maua yake Mheshimiwa Waziri Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na kilio kikubwa kuhusiana na tafiti. Tumeona ana mpango wa kuanzisha *Genebank*. Mimi nimekuwa ni muumini wa kuitaka Serikali isiache teknolojia. Dunia sasa hivi inaongelea *GMO,* kwa hiyo, tuanze tafiti tujue kibaya ni kipi na kizuri ni kipi ili sisi wenyewe tujiamulie kuliko kusikia tu makelele. Kwa hiyo, suala la uanzishwaji wa *Genebank* naona sasa ile hoja yangu niliyokuwa naisema muda mrefu sasa inafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Waziri hapa aliwahi kufunga mipaka wakati watu wamezalisha mahindi ya kutosha, hakurudi Bungeni, lakini tumeona kwa Mheshimiwa Bashe, Mungu atampa baraka kwa kufungua masoko na kumruhusu mkulima. Basi Wana-

Nzega watamrudisha kwa kishindo na tunamwomba Mheshimiwa Rais amwache akamilishe Ajenda 10 - 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niongee kama Mbunge wa Mkoa wa Dodoma. Dodoma tumekuwa tukilima kinyonge miaka yote kwa sababu ya hali yetu ya hewa tuliyokuwa nayo. Ni hali ya nusu ukame na mvua zinakuwa finyu; lakini ardhi yetu sisi ina rutuba na inakubali mazao yote ya chakula pamoja na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilifikia hatua tukaambiwa Dodoma tusilime mahindi. Kwa mara ya kwanza tangu uhuru wa hii nchi ni Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na uongozi wa Wizara ya Kilimo chini ya Mheshimiwa Bashe, leo hii tunayo miradi 29 kwenye wilaya zote saba za mkoa wetu, ambapo miradi hii ikishakamilika tutakuwa na hekta za umwagiliaji zaidi ya 70,579 ndani ya mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na wakulima wa Mkoa wa Dodoma na kwa vile dira ya nchi ni kujilisha, sisi pamoja na Afrika na dunia, Mkoa wa Dodoma unaenda kujilisha wenyewe na unaenda kulisha nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye *BBT* sisi ndio *pioneers,* tunayo miradi mikubwa ya kwanza ya *BBT* pale Chinangali pamoja na Ndogowe ambako kuna zaidi ya ekari 11,000; na kwenye ekari hizo, ekari 1,000 Wizara imewapa wananchi wangu wa pale. Pokea salaam kutoka kwa Mwenyekiti wa Mlazo, na anasema Jumatatu atakuwepo hapa ili tuweze kuongea kwa ajili ya maendeleo ya mradi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo naomba nichomekee kwamba halmashauri zote zimepata miradi ya hizi skimu za umwagiliaji na mabwawa isipokuwa Halmashauri ya Mji wa Kondoa ambayo mimi ni Makamu Mwenyekiti wake, na jana ameshuhudia nilivyommiminia sifa kwa niaba ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, 2023 nilimwomba na akanipa mradi kwenye *Mwongoroma Irrigation Scheme,* lakini

sijaiona kwenye karatasi zake. Naomba Mheshimiwa Waziri akija kuhitimisha aseme neno ili mimi, vijana wangu na wanawake wa Halmashauri ya Mji wa Kondoa tupone kupitia mradi huu wa *Mwongoroma Irrigation Scheme* wenye zaidi ya ekari 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naomba niipongeze sana Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, inafanya kazi kubwa. Bila upendeleo nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu, Ndugu Raymond Mndolwa. Sisi kama Kamati tumetembelea miradi yake, anajua kila *detail,* hadi rangi ya kupaka, halafu huyu ni mwana CCM mzuri ndiyo maana majengo ya pale Chinangali ni ya kijani, na huo ndiyo utekelezaji wa ilani. Achape kazi, kwani Mheshimiwa Rais amemwamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mti wenye matunda ndiyo unaopigwa mawe. Vilevile huyu ni muumini wa jinsia "ke," zaidi ya 80% ya watendaji wake pale kwenye Tume ni akina mama na ndiyo maana mambo yanaenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali watoe fedha za kutosha na kwa wakati ili kurahisisha kazi ya Tume ya Umwagiliaji kwa sababu upelekaji wa fedha siyo mzuri. Kwa hiyo naomba warekebishe, kwa sababu tunasema kilimo cha umwagiliaji ndicho kilimo cha uhakika. Nawapongeza kwa kutenga fedha kwa ajili ya *feasibility study* pamoja na *detailed design.* Sasa wasije wakapotoka, wasifanye miradi bila ya *feasibility study* na *detailed design*. Huo ndiyo uwe msimamo wao. Miradi mingi imekufa kwa kukosa *feasibility study* na *detailed design*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi, tunalalamika kwamba maduhuli siyo mazuri kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, nashauri kwamba hebu sasa wakae na Wizara ya Kilimo, wateue maeneo na wayarasimishe ili sasa hii Tume iende kuingia *PPP* na hivyo iweze kujiendesha na kutuletea vyanzo kwa sababu uwekezaji unaofanyika na Serikali ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusiana na zao la zabibu. Nakumbuka jitihada za aliyekuwa Naibu Waziri

wake ambaye sasa hivi ni Waziri wa Madini, na alishirikiana naye sana katika kuanzisha Ajenda 10 - 30; alikuwa ni *pioneer* sana wa zao hili. Hili ndilo zao letu la asili Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliomba hata tuwe na bodi ndogo ya zao hili. Leo hii tuna zabibu kavu tunaingiza kutoka nje, tuna zabibu za meza wakati tunaweza kuzalisha, lakini watu wanakamua michuzi hawana sehemu ya kuweka. Naomba Mheshimiwa Waziri akija kuhitimisha, aseme neno ili wakulima wa zabibu wa Dodoma wapone. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kumalizia. Ninao ujumbe wa kutoka kwa wanawake wa Mkoa wa Dodoma. Kwa kweli tumeona namna gani Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ilivyompa kipaumbele mwanamke. Kwenye uzalishaji wa kilimo mwanamke utamkuta shambani, utamkuta sokoni akiuza mboga mpaka pamoja na nafaka. Mwanamke huyo alikuwa hapewi kipaumbele, lakini leo miradi yote, mipango yote mikubwa ya Wizara ya Kilimo mwana mama anawekwa, mwanamke anathaminiwa, na kwa kweli hiyo ni heshima kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia na wanasema hivi, hawayumbishwi na maneno ya wakosaji. Ukishawashinda kwa hoja, watakuja na viroja. Haya ninayoyasema ni msimamo thabiti. Kule Kondoa wananiita Kivaravumba, kundi liko nyuma. Nikisema akina mama wamenituma, namaanisha kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wanachokiomba, Mwenyezi Mungu ampe afya Mheshimiwa Rais, uzima, na utimamu wa kila kitu. Mwaka 2025 wanasema Samia wanaye na wanatamba naye. Wao wanachosema watamuunga mkono kwa wao kugombea nafasi za kuchaguliwa kuanzia Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji pamoja na Uchaguzi Mkuu, kwa maana ya Udiwani na Ubunge. Mimi mwenyewe binafsi wameniomba nikajaribu jimboni, na nimekubali nitamuunga mkono Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, naomba hitimisha.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wanawake wa Mkoa wa Dodoma wanasema wanaunga mkono kauli ya Katibu Mkuu wetu, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi aliyesema mwakani fomu ni moja na fomu ni ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wapo watu wenye viroja ambao wanatumwa tumwa kwenye mitandao kusema eti Katibu Mkuu amevunja demokrasia…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uhitimishe, muda umekwisha.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama chetu kinaongozwa na Katiba na Kanuni…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** …lakini tuna utamaduni wetu na heshima tulishajipangia, Rais aliyekuwepo madarakani,…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba uhitimishe hoja yako.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** …Rais aliyepo madarakani habughudhiwi, hafananishwi na yeyote. Tunamwongezea muda wake kwa mujibu wa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Naomba umalize Mheshimiwa.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** …tunamwongezea muda Mheshimiwa Rais amalizie, leo kilimo tuna Ajenda ya 10-30 chini ya maono ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, mwingine wa nini? Fomu ni moja, na ni ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, naomba kuunga mkono hoja, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Kulikuwa na Taarifa, lakini Taarifa haitolewi baada ya mchango kwisha. Tunakwenda kwa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda na Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami nitoe mchango wangu kwenye bajeti hii muhimu kwa maendeleo na ustawi wa nchi yetu. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema ambaye yeye kwa uwezo na neema yake ndiye ametuwezesha leo tuko hapa tukijadili mambo kwa ajili ya mustakabali wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza kwa dhati kabisa mbeba maono namba moja wa nchi hii, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya. Ukiangalia Wizara ya Kilimo ilivyo sasa hivi, fedha inazotengewa na kupelekewa ni ishara kwamba Mheshimiwa Rais yuko kazini na ana nia ya dhati ya kuwatumikia Watanzania. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jambo hili kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Bashe, yeye na Naibu Waziri na watendaji Wizarani. Kwa kweli Wizara ya Kilimo wanatutendea haki, wanafanya kazi nzuri. Hatuna deni na ninyi zaidi ya ushauri kwenye maeneo machache na kukumbushana vitu vichache ili kuboresha na kuendeleza kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo naomba nichangie kwenye maeno matatu. Eneo la kwanza nitachangia kuhusu kilimo cha umwagiliaji, eneo la pili ni zao la chai na eneo la tatu ni zao la mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2019/2020 eneo lililokuwa linafaa kwa shughuli za umwagiliaji na lililokuwa linatumika kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji lilikuwa ni hekta 475,052. Leo kupitia taarifa ya Mheshimiwa Waziri, nasi wenyewe tunajionea, eneo

linalofanya kazi kwa shughuli za umwagiliaji limefika hekta 727,280.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama miradi ikikamilika, kwa mujibu wa taarifa na maelezo na hotuba ya Mheshimiwa Waziri, tutafika hekta 983,466 sawa na 81.9% ya malengo tuliyowekewa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni kubwa sana, Tume ya Umwagiliaji na Wizara ya Kilimo wanastahili pongezi kwa kazi hii kubwa na nzuri wanayoifanya. Tunawaomba waendelee na kazi hii, na tuongeze eneo linalofaa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa sababu umwagiliaji ndiyo maisha na ndiko kufanikiwa kwenye kilimo chetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mambo machache kuhusiana na eneo hilo hilo la umwagiliaji. Moja, namshukuru Mheshimiwa Waziri, yeye ni mtu wa vitendo na anatimiza ahadi zake. Tumekaa naye katika vikao vingi tangu akiwa Naibu Waziri tukihangaika na Bwawa la Mkomazi na Skimu zake ambazo alituahidi. Leo tunapozungumza, kazi iko zaidi ya asilimia saba kule kwenye Bwawa la Mkomazi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 18 kwa ajili ya mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto ndogo na pengine Wizarani wanapata hofu. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Waziri kwamba, najua mimi siyo mtakatifu, lakini nina hofu ya Mungu na ninajua kuna Mungu. Namhakikishia, kama Mungu aishivyo, Mradi wa Mkomazi utatekelezwa kwa sababu ndiyo dhamira yetu, ndiyo nia yetu, ndiyo maisha yetu, ndiyo uhai wetu na ndiyo uchumi wetu, aondoe wasiwasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa alikuwa kwenye lile eneo, amezungumza na wananchi, wako wananchi wamepata hofu. Niwatoe hofu wananchi wenzangu wa Kata za Mkomazi, Mkumbara, Mazinde na Mombo kwamba mradi huu hatutakubali hata siku moja ukashindwa kutekelezwa. Kama Mungu aishivyo, mradi huu utatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri, tulikubaliana kuhusu Chekelei, tumeona wameshatangaza, tunamshukuru sana. Ninao ushauri kwenye maeneo machache kwenye eneo hilo la umwagiliaji. Moja, miradi ya umwagiliaji inatumia fedha nyingi sana. Naomba Wizarani waweke utaratibu thabiti kabisa wa kufanya miradi hii iwe endelevu na isiwe kwamba baada ya kujenga na kumaliza, baada ya miaka mitatu minne tunaingia kwenye changamoto, miradi inakuwa ni changamoto na mingine haifanyi kazi vizuri. Tuweke utaratibu endelevu, wananchi waelimishwe ili miradi hii iwe endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Tume inapewa fedha nyingi sana na Serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi hii. Ushauri wangu, huko tunakokwenda tuangalie, pamoja na kwamba hii ni huduma kwa wananchi wetu, tuangalie namna ya kuijengea uwezo Tume, isikae kwa asilimia mia moja kusubiri kupewa fedha na Serikali, kuwe na namna mbalimbali za kuifanya Tume kutengeneza mapato ili mambo yake yaweze kuwa mazuri na hivyo waendelee kukarabati skimu hizi na mambo yaendelee kuwa endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana, 2023 tulizungumza na tukaenda ofisini kwa Mheshimiwa Waziri, tukakaa tukazungumza kuhusu ukarabati kwenye Skimu za Mombo, Mafreta na Kwemazandu. Ninamshukuru nimeiona kwenye kitabu cha hotuba. Ombi langu ni moja, kwamba Skimu ya Mombo mwaka 2021 tulikwenda na Mheshimiwa Waziri Mkuu yeye akiwa Naibu Waziri, tukazungumza kuhusu Skimu ya Mombo, pembeni kuna eneo la Kwamkumbo ambapo mto ule umejaa udongo, maji yanapoteza mwelekeo yanaingia kwenye mashamba ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023 tulizungumza na Mheshimiwa Waziri, tulienda ofisini kwake tukakaa na tukazungumza kuhusu ukarabati kwenye *scheme* za Mombo, *scheme* ya Mafreta, kwenye *scheme* ya Kwemazandu, ninakushukuru nimeiona kwenye kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni moja, *scheme* ya Mombo mwaka 2021 tulikwenda na Mheshimiwa Waziri wewe ukiwa Naibu Waziri, tukazungumza kuhusu *scheme* ya Mombo pembeni kuna eneo la Kwamkumbo, ambao mto ule umejaa udongo, maji yanapoteza mwelekeo yanaingia kwenye mashamba ya wananchi. Sasa unapokwenda kukarabati *scheme* hii ya Mombo, tuhakikishe kwamba tunaweka *package* kwa ajili ya kutengeneza eneo la Kwamkumbo ili wananchi wetu wafanye kilimo vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mheshimiwa Waziri, kama tulivyokubaliana ameweka kwenye bajeti yake kwenda kufanya upembuzi kwenye *scheme* za Magoma na Kwakunda. Ombi langu, tulitembea naye kule Korogwe; ukipita pale kwa Mdole kule kwa Mufti upande wa kulia mpaka unafika Magoma, ni bonde na maji, yanapotea. Pamoja na Kufanya upembuzi kwa ajili ya ukarabati katika *Scheme* ya Magoma, tunaomba tuweke mpango wa kujenga bwawa ili mambo ya watu wa Magoma yawe mazuri na mazao yao yasiondoke wakati wa mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nataka kuchangia ni kwenye eneo la zao la chai. Mheshimiwa Waziri, sina mashaka na Bodi ya Chai, wanajitahidi na wanafanya vizuri. Nilisoma kwenye *website* ya Wizara, taarifa ya tarehe 15 Februari, 2022, karibu nusu ya wakulima wa chai tulionao ni wakulima wadogo, lakini zao la chai linakabiliwa na changamoto kubwa mbili; changamoto ya kwanza ni bei ya chai kwamba ni ndogo na inaumiza sana wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba natambua changamoto hii ya bei ya chai inachangiwa sana na bei ya soko la dunia, naiomba sana Wizara, Bodi ya Chai na taasisi nyingine, tuweke mkazo kwenye kuongeza ubora wa chai yetu ili iweze kwenda kushindana vizuri kwenye masoko, tuweke mkazo, tuweke uwekezaji kwenye mnyororo wa thamani ili tunapozalisha chai na kuipeleka kwenye soko, iweze kufanya vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, kama nilivyosema zaidi ya nusu ya wakulima wa chai ni wakulima wadogo, lakini sehemu

kubwa ya wakulima wadogo wanategemea viwanda vya wakulima wakubwa ambao wanawekeza kwenye mashamba makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni kule Korogwe, Mheshimiwa Waziri ni shahidi. Mheshimiwa Waziri, wiki iliyopita tulizungumza na alifanya mawasiliano, nampongeza kwa juhudi alizozifanya kwenye Kampuni ya *Mohammed Enterprises,* jana wamefungua kiwanda na wameanza kuchakata chai ya kwao wenyewe na wanajiandaa kwenda kununua chai ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii changamoto imekuwa ikijirudia mara kwa mara. Ushauri wangu kwa Mheshimiwa Waziri, ombi na ushauri wangu, hebu Serikali ione namna ya kukaa na hao wawekezaji. Kama hakuna uwezekano na hawawezi kuendelea na kazi ya uzalishaji, tutafute namna ya kuongeza nguvu tuwape wakulima wadogo hivi viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Kenya 75% ya viwanda vilivyopo Kenya vinasimamiwa na wakulima wadogo (ni viwanda vya wakulima wadogo). Tuone namna ya kuwapa nguvu wakulima wadogo wawe na viwanda vyao na wasitegemee viwanda vya wawekezaji ili mwekezaji akiyumba mambo yao yasiyumbe na biashara ya chai iendelee kuwa nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la mwisho nichangie kwenye eno la Katani (Mkonge). Nampongeza Mheshimiwa Waziri, na tunaishukuru Serikali hasa sisi watu wa Mkoa wa Tanga kwa kufufua na kurejesha zao la mkonge kwenye ramani ya mazao ya nchi yetu, mmefanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nawapongeza, tumeongeza uzalishaji, tulikuwa tani na 36,000, leo tunazungumza mkonge, tuko kwenye uzalishaji wa nyuzi zaidi ya tani 56,000 sasa. Pia kuna changamoto na nimewahi kuisema na nitaendelea kuisema siku zote mpaka tutakapoelewana vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hizi tani 56,000 tunazozalisha za nyuzi za mkonge, 70% tunapeleka nje. Tafsiri yake rahisi ni nini? Tunakwenda kuuza ajira za watu wetu, tunakwenda kuuza kodi za kwetu na pia tunakwenda kuishi kwa kutegemea soko la wenzetu. Zikitokea changamoto kama ilivyotokea kwenye *COVID,* wakulima wetu wanaingia kwenye matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri, najua anaweza, aongeze nguvu kwenye kuimarisha soko la ndani la mkonge hasa kwenye kuimarisha viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema humu ndani mara nyingi, bado tuna changamoto ya nyuzi za *plastic*, bado tuna changamoto ya uingizaji mkubwa wa magunia ya *duty*, tukiweka vizuri maeneo hayo, tutafanya vizuri. Leo kwenye nchi hii, mahitaji ya gunia kwa mwaka ni zaidi ya *piece* milioni 15…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Naomba uhitimishe.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wamepewa viwanda. Namshauri Mheshimiwa Waziri, hebu akae na watu waliopewa viwanda vya kamba na viwanda vya magunia ili tusiuze ajira za watu wetu. Tuhakikishe usalama wa soko la watu wetu kwenye eneo la Mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Keneth Nollo na Mheshimiwa Bupe Nelson Mwakang'ata, ajiandae.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kwenye Wizara muhimu sana katika Taifa letu. Tunafahamu kabisa, bado

sijaamini kama tumeacha ule msemo uliokuwa unasema, Kilimo ni Uti wa Mgongo. Ninaamini bado tunaendelea nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu, tunampongeza Mheshimiwa Waziri, kwani ni mtu unayeweza. Sasa naomba katika kuweza kwake, kuna shida kubwa sana na anafahamu mimi na yeye tunaongea mara nyingi kuhusu suala la wakulima wa chai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri achukue juhudi za makusudi, kwanza kufika katika Wilaya ya Rungwe na kuonana na wakulima bila kupitia njia nyingine yoyote. Kwa nini nasema hivyo? Tunapozungumzia chai, ni zao ambalo limewapa fedha wazazi wetu miaka na miaka. Nimeona juhudi unazozizungumzia, pia tulikuwa na kikao cha wadau ambao watu waliokuwepo, na Waziri kama kiongozi wetu, alitoa tamko kwamba, kiwanda cha *MO* cha Rungwe kisifungwe, kwa sababu kikifungwa wale wakulima wanaolima chai watauza wapi, wakati muda waliokuwa wameutoa siyo muda ambao wale wakulima wamejiandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwambia Mheshimiwa Waziri kwamba kiwanda kimefungwa, wafanyakazi wamesimamishwa bila taratibu za kazi tunazozijua, watu wako nyumbani wameondoka na hawajui hatima zao zikoje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu Mheshimiwa Waziri aliniambia ametuma timu yake. Bado nina mashaka na timu. Naomba yeye kama Waziri, najua Waziri ni taasisi, ana watu wake, lakini kuna maeneo kama Taifa yanayosumbua, tunaomba Mheshimiwa Bashe afike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo mwanzo, chai ni zao muhimu sana. Tuna Kiwanda cha Busokelo na Kiwanda cha Katumba. Leo hii viwanda hivi vyote havieleweki. Unafahamu kabisa Katumba imeanza kuuza baadhi ya majengo, inawapa shaka sana wakulima. Leo hii wanakwambia kwamba wanarudisha vile viwanda kwa wakulima. Mheshimiwa Waziri, wakulima hao ni akina nani? Kuna watu wanajiita *AMCOS*.

*AMCOS* ni familia zinajiunga, zinajisajili na kuwaacha wakulima kwa zaidi ya 2,000 ambao ndio wenye mali na ndio wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana ya umuhimu wa kuunda Tume. Natambua Mheshimiwa Waziri Mkuu aliwahi kuunda tume, lakini hatukuwahi kupata majibu. Sasa basi, kwa sababu tunaingia mwaka mpya wa Serikali, naomba uunde tume iende chini ikasimamie ugawaji wa vile viwanda hasa Busokelo na Katumba virudi kwa wakulima wa Wilaya ya Rungwe ili uchumi wa Rungwe uendelee na wakulima wasiyumbishwe kabisa katika uuzaji wa chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la parachichi limezungumzwa na wenzangu wa Njombe na sisi Rungwe tumeshasema kwamba, hii ni dhahabu ya kijani, lakini leo hii mizani inayotumika na wauzaji na madalali imekuwa ni feki na inawadhulumu wakulima haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii madalali, kwa sababu nafahamu kuna hawa *Herb Africa*, wananunua kwetu kwa 80%; nilikuwa naongea na yule kiongozi ambaye Waziri amemleta hapa kwenye maonesho kwamba, kwa nini msiende moja kwa moja kwa wakulima kuliko kutumia madalali? Leo hii dalali ananunua parachichi anakwambia 50% ni *reject*. Hiyo *reject* kwa macho ya nani? Kwa sababu yeye ni mnunuzi, ameshashusha chini ya mti, anasema haya maparachichi ni *reject*? Naomba tuwasimamie wakulima wetu. Mwisho wa siku tunataka tuwajenge Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Mheshimiwa Rais ameongeza bajeti ya kilimo. Nafahamu hizo ni jitihada kubwa sana. Basi ikawasaidie, na kama ni keki ya Taifa, wakulima wote tukapate sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu masoko. Leo hii masoko ni shida. Nafahamu yananunuliwa, sawa. Hata hivyo, kwa nini tusiweke *AMCOS* ambazo ni za kweli, siyo zile za kwanza nilizozisema? Kama wakulima waliopo katika vikundi,

tupeleke moja kwa moja Uswisi, Dubai, na kadhalika badala ya kutegemea makampuni binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunalalamika, hakuna ajira, lakini tuna uwezo wa kukusanya vijana wetu kwa kutumia ile mikopo ya asilimia 4.4.2, kwa maana ya asilimia nne wanawake, asilimia nne vijana na asilimia mbili za watu wenye ulemavu; tukawaunganisha huko, tukawasaidia kama Taifa, wakauza nje badala ya kupita katikati kama madalali hapa katikati. Mheshimiwa ninafahamu unaweza na ukiamua unaweza, ninaomba usimamie hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Rungwe ndizi ni zao kubwa sana. Leo hii nchi za Jamaica zinanunua silaha kwa kuuza ndizi. Kwa nini sisi tunashindwa? Kwa nini tusihakikishe kwamba ndizi ni zao la kibiashara, wawe wanakuja watu binafsi kutoka Malawi na Zambia kununua ndizi ya Rungwe? Kwa nini tusisimamie tukaweka mkazo hapo na kusaidia vilevile kuuza huko nje? Viwanda vidogo vidogo ndilo suluhisho la mkulima wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalifahamu kabisa zao la kahawa kwamba ni zao zuri sana na wakulima wamejitahidi sana kuendeleza zao hili, lakini malipo yao yanachukua mwezi mpaka miezi mitatu mkulima hajalipwa kahawa yake. Leo hii utakuta msimu mwingine anataka kununua mbolea, pesa ziko kwenye vyama vya ushirika, hawajalipwa. Tunaomba Mheshimiwa Waziri asimamie hilo. Ninajua kuna Bodi za Kahawa na Bodi za chai, naomba tusimamie wananchi wetu waweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye zana za kilimo. Rais wa Awamu ya kwanza aliweka viwanda kwa makusudi kabisa. Kule Mbeya tulikuwa tuna *ZZK* kwa ajili ya kusaidia vifaa hivi. Naomba sana tuwekeze na bajeti yetu ijikite zaidi kwenye zana za kilimo ili kuwasaidia wakulima. Suala la mbolea amekwenda nalo vizuri, lakini bado tunaomba nguvu iongezeke ili tuweze kufanikisha wakulima hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, naomba kurudia tena, kwa sababu ni la muhimu sana, kwamba viwanda vinavyofungwa vizuiwe. Hakuna haja ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri kwa sababu jitihada anazozifanya tunaziona. Tukianza kugombana kwa kushika shilingi, nafikiri wakati mwingine tutamkatisha tamaa. Naomba alisimamie hilo, tusifike mahali pa kuleta hoja binafsi kwa sababu tu ya wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wawekezaji hawa wengi wanatoka nchi za jirani, isije ikawa wanafanya hivyo kwa makusudi, wanatuharibia huku Tanzania, lakini kwenye nchi zao kahawa inaendelea na chai inaendelea. Kwa sababu wengi wanatoka nchi jirani, sitaki kuitaja kwa sababu ya mambo ya kiusalama na mambo ya kiurafiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana watu wetu wa *TISS* na wengine wafuatilie hawa wawekezaji kwamba wanakuja kuwekeza, kutuharibia au kutusaidia! Kwa sababu anakaa miaka mitano, halafu baadaye kiwanda kinakufa, lakini kwake ana kiwanda hicho hicho na kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, majibu ya Mheshimiwa Waziri yatatufanya tufurahi au tunyang'anyane mshahara ili kuhakikisha kwamba haki za Wanarungwe na Wanajombe wote zinakuwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naomba kuunga mkono hoja. Kipindi Mheshimiwa Waziri atakapojibu swali langu vizuri ndiyo hoja itaungwa mkono na vinginevyo haitawezekana. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. Namwita sasa Mheshimiwa Keneth Ernest Nollo, atafuatiwa na Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata na Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, ajiandae.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Moja ya jukumu la Wizara ya

Kilimo ni kuhakikisha usalama wa chakula. Hilo ni moja ya jukumu la Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mnavyofahamu, Serikali imehamia Dodoma. Jiji la Dodoma sasa ni kioo kwa maana ya kwamba ndipo Makao Makuu ya Serikali. Idadi ya watu wameongezeka na watu wengi wameendelea kuingia katika mji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, Serikali ni lazima iangalie hali ya maisha ya wananchi katika Jiji la Dodoma na wilaya zinazozunguka. Nataka niseme, bado Serikali haijaonesha mkakati wa kuweka umadhubuti kwamba, pamoja na maendeleo makubwa tunayoyaona ndani ya Jiji la Dodoma, lakini ukitoka ndani ya wilaya zake, hakuna mkakati wa kilimo unaoonekana. Nnataka niliseme hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba, kwa mfano ukija Wilaya ya Bahi, tunalima mpunga na tuna *scheme* kubwa sana na ile *scheme* ilijengwa mwaka 1984, lakini haijawahi kufanyiwa ukarabati, na ni *scheme* kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Bahi ilipo, *scheme* ile inapitika na ndipo lami inapopita kutoka Singida, ipo karibu na mji lakini *productivity* yake iko chini kwa sababu haijakarabatiwa. Sasa huu ni mwaka wa nne Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amekuwa ananiweka kwenye upembuzi yakinifu. Pia, safari hii tena ameniweka kwenye upembuzi yakinifu. Kwa hiyo, hii ninaiona pia imetoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka niseme, alikuja Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi, Ndugu Chongolo na akaahidi akasema tunaanza ukarabati na wananchi walisikia. Mimi nikasema kweli kwamba sasa ukarabati unaanza, lakini hakuna ukarabati na leo niko kwenye upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nataka niseme, Serikali na kwa Mkoa wa Dodoma, bado hakuna mipango ya

kuondoa umasikini kupitia kilimo. Mbegu za uwele tunazozitumia ni zile zile na *productivity* yake iko chini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona kwa ruzuku kwa mwaka 2023 ni shilingi bilioni 136. Njoo Dodoma uone kama tumepata ruzuku hata shilingi milioni 300, tena kwa mkoa mzima! Sisi ruzuku hatupati. Kama hatupati ruzuku, basi hata mbegu si mtufanyie utafiti. Kwa hiyo, mbegu tunalima zilezile, hela ya ruzuku kwetu sisi hatuioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Bashe, yeye ni zao la Kanda ya Kati, hawezi kuitofautisha Nzega na Dodoma, kwani hali ya hewa ni ile ile. Hata hivyo, hakuna programu za utafiti wa mbegu na mbegu hatupati. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri hilo aliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu matumizi bora ya ardhi. Nchi yetu akija mwekezaji anayetaka ekari 5,000 au 6,000 kwa Pamoja, hawezi kuzipata. Ndiyo maana hata uwekezaji kipindi kile Zimbabwe wale Wazungu walipopata shida pale, walishindwa kuja kwetu. Kidogo walibahatisha Zambia, sisi hatuna ardhi. Tuna ardhi kubwa ya maneno, lakini ardhi ya kilimo hatuna, na hatuna kwa sababu ya sera zetu kwamba hatuzidhibiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda vijijini, kuna uholela. Mtu anakuja anaweka *beacon* tayari ameshategesha pale. Akija mwekezaji, ina maana yule mtu wa kawaida ametangulia kuliko Serikali. Kwa hiyo, ardhi yetu katika kilimo kumekuwa na uholela mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Mheshimiwa Bashe sisi alitupatia na akatuomba tutenge eneo kwa ajili ya *BBT*. Tumetenga ekari 3,500, sasa zile ekari watu wanazinyemelea kwa sababu ule mkakati hauonekani. Sisi kule tumetenga lile eneo na bahati nzuri barabara inatengenezwa, tumepeleka maji pale katika Kijiji cha Ikumbulu, tumejenga zahanati na tunawaambia kwa sababu unakuja mradi mkubwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Mheshimiwa Bashe hilo nalo aliangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu Serikali katika vipaumbele vyake kwenye kupunguza kuagiza ngano na mafuta ya chakula. Tumekuwa na matamanio hayo, lakini mkakati madhubuti hauonekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija kwenye alizeti ambayo ndiyo inaleta mafuta ya chakula, bado hatujawa na *strategic plan* kuhusu zao la alizeti; ipo kwenye vile vipaumbele vikubwa, lakini mkakati wa alizeti hauonekani. Kutokuwa na mkakati ndiyo maana hata mbegu bora za alizeti sisi hatupati. Mmewahi kutuletea mbegu pale Bahi, ilirefuka kama mita tatu, mvua inaisha na yenyewe bado inarefuka. Kwa hiyo, tunaomba mbegu ya uhakika kwenye alizeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la ngano kama nilivyosema, nchi hii hatujaamua, tatizo lililopo ni kwamba ardhi tunayo, lakini ni uthubutu, bado tunaendelea kuagiza ngano hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilitaka niseme kwenye suala zima la ardhi ambalo nimesema, akija mwekezaji hapa, *Tanzania Investment Center* wanafanya kazi kubwa sana katika maeneo mengine. Nilikuwa naomba kwenye suala la ardhi washirikisheni na mwapatie baadhi ya maeneo makubwa *TIC* waweze kushikilia. Wamefanya vizuri kwenye suala zima la kuleta wawekezaji kwenye viwanda, lakini kwenye suala zima la ardhi bado kuna shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nataka niseme kwa dhati, Taifa lolote duniani ni lazima kwanza lipate udhibiti mkubwa wa maendeleo ya kilimo na kilimo sisi tunasema kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa letu. Naona mawazo ya Mheshimiwa Waziri ni ya ku-*transform* nchi hii. Tunaomba Serikali imuunge mkono, falsafa hizi ambazo anazo za kutaka ku-*transform* nchi katika kilimo, basi Serikali itoe fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli fedha zinakuja nyingi, lakini njoo katika utekelezaji, haijafika zaidi ya 50%. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Serikali iangalie, bado tunahitaji fedha katika kilimo,

lakini bado kilimo chetu hakijawa na tija cha kuleta wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Nollo. Namwita sasa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alfred Kimea na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, ajiandae.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye bajeti hii muhimu iliyoko mbele yetu, Bajeti ya Kilimo ya 2024/2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na kuweza kuchangia katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kazi yake ni njema na nzuri hasa kwenye suala zima la kilimo. Mama amefanya mapinduzi makubwa sana. Tukiangalia 80% ya Watanzania ni wakulima. Mama amefikiria, ameweza kuweka ruzuku kwenye suala zima la pembejeo za kilimo. Hongera sana Mama, umeupiga mwingi, tumpe mama maua yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kumpongeza kaka yangu Mheshimiwa Bashe na Naibu wake, kaka yangu Mheshimiwa Silinde kwa kazi nzuri na ubunifu mkubwa kwenye sekta hii ya kilimo. Hongereni sana, nami namwomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa kibali mama na aendelee kuwapa nafasi ili muweze kuwatumikia Watanzania kama mlivyowatumikia kwenye suala zima la sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Katibu Mkuu na Wakurugenzi Watendaji wote wa Taasisi za Wizara ya Kilimo,

tukianza na *TFC, NFRA, CPB, ASA*, Kahawa, Korosho, Tumbaku, *TOSCI* na Tume ya Umwagiliaji. Kwa pamoja wameweza kufanya kazi nzuri na ndiyo maana Wizara ya Kilimo na sekta ya kilimo sasa hivi imekuwa ni nzuri sana na ni kimbilio la Watanzania. Wakulima wengi zamani walikuwa wanaonekana ni maskini, lakini kwa sasa mkulima ni tajiri na tunakwenda kupata mabilionea kwenye sekta ya kilimo. Yote hii inatokana na uongozi mzuri kuanzia kwa Rais, Waziri na Watendaji wote wa sekta hii, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naingia kwenye hoja yangu ya msingi, kwanza ni suala la *BBT*. Nimesoma ukurasa wa 10, kwanza kabisa naipongeza Wizara, nampongeza Waziri kwa mawazo mazuri ya kuleta wazo hili la *BBT,* ni wazo zuri sana. Mwanzoni watu walibeza, lakini hili wazo linakwenda kumkomboa Mtanzania, hasa vijana, wanawake na Watanzania kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusoma hapa, nimeona mpango wa *program* ya *BBT* umelenga kwenye mikoa ya Dodoma, Kigoma, Mbeya, Singida, Pwani, Tanga, Njombe na Kagera, lakini sijaona Mkoa wa Rukwa. Mkoa wa Rukwa ni miongoni mwa mikoa ambayo inalima sana na inaweza kulisha Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe mwenyewe na Mheshimiwa Waziri ni mashahidi kwamba Mkoa wa Rukwa tunalima sana, lakini kwenye suala la *BBT,* hapa sijaona jina la Mkoa wa Rukwa. Naomba sana Mkoa wa Rukwa tuna vijana wengi wakulima wanaoweza kulima vizuri, lakini hawana pa kulima. Tunaomba hii *BBT* na Mkoa wa Rukwa pia tuwemo kwenye mikoa hii ambayo mmeitaja hapa. Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapo naomba arekebishe na Rukwa iwemo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naingia kwenye suala la pembejeo. Naipongeza sana Serikali kwamba katika Mkoa wangu wa Rukwa tumepata pembejeo za kutosha, pembejeo zenye ruzuku. Wakulima wanamshukuru sana Rais na Mhesimiwa Waziri kwa kuwa tumeona na tumeshuhudia tumepata pembejeo na mbolea ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua unapomaliza msimu, msimu mwingine unaanza. Basi mwaka huu mbolea ziwahi kufika na kwa kiwango cha kutosha. Mbolea inapokuja kwa mfano, kwa mwaka huu mbolea ya *CAN* imekuja nyingi, lakini mbolea ya *UREA* imekuja kidogo. Muda wa kuweka mbolea ya *UREA* ulipofika ikawa kidogo, kwa hiyo, tunaomba msimu huu mbolea zote zije kwa kiwango sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mtovu wa shukrani nisipompongeza Mkurugenzi wa Taasisi ya *TFC,* kaka yangu Samwel Mshote na Watendaji wote wa *TFC,* wamefanya kazi nzuri. Pia wameweza kuleta mbolea na pembejeo kwa wingi katika Mkoa wa Rukwa. Mkoa wetu wa Rukwa tunakwenda kuvuna mahindi kwa wingi na changamoto yetu itakuwa ni soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara izingatie sana, mmehamasisha wakulima wameweza kulima kwa wingi, sasa tatizo litakuja kwenye suala zima la soko, nasi mnajua kabisa tumepakana na nchi jirani ambazo tayari zina majanga ya njaa. Tunaomba mtakapojiridhisha kwamba sasa *NFRA* imenunua mahindi ya kutosha, basi mtupe kibali cha kufungua zizi, ili tuweze kuuza kwenye nchi jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la *NFRA*. *NFRA* pia wamefanya kazi nzuri sana, wamenunua mazao yetu kwa wingi, lakini changamoto ilikuwa ni kidogo tu, marekebisho kwenye suala zima la mizani. Mizani ilikuwa ni changamoto kubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba safari hii mrekebishe mizani iweze kutenda haki, mkulima atakapokwenda pale amepima kilo zake 100 kutoka huko nyumbani kwake, lakini akifika pale akipima, kilo tano au kumi zinapungua. Kwa hiyo, muweze kurekebisha suala zima la mizani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niongelee suala la mbegu. Tumeshuhudia kabisa wakulima wengi wanapenda sana mbegu za wenzetu wa Zambia, sijajua za kwetu tatizo ni nini? Ninachoomba ni kwamba, mfanye utafiti ili mbegu zetu ziweze kuingia kwenye ushindani wa masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee pia suala la kuleta mbolea. Mbolea isiishie tu wilayani, iende mpaka vijijini, lakini pia mbolea hiyo iweze kuuzwa kwenye viroba vya kilo tano tano, kilo 50 na kilo 25 kwa sababu, kwenye Mikoa na wilaya zetu kuna wakulima wadogo na wakubwa ambao wana uwezo wa kununua kilo tano wanunue kilo tano, wenye uwezo wa kununua kilo 25, wanunue kilo 25. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niongelee suala la ushuru. Suala la ushuru limekuwa ni changamoto huko, kwa sababu mkulima anapotoa mahindi yake shambani, tayari wataalamu wanafika pale kumtoza ushuru. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bupe, muda wako umeisha.

**MHE. BUPE N. MWAKANG'ATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita sasa Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, ajiandae.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie kwenye Wizara ya Kilimo. Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kuendelea kutupa nguvu, afya na uhai ambao unatuwezesha kuendelea kulitumikia Taifa la Tanzania, lakini hasa wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo kwa Mwenyezi Mungu, niruhusu nimpongeze Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mwenyekiti wa chama changu cha CCM kwa namna ambavyo anawajali wananchi wa Tanzania. Tunaona namna Serikali ambayo inaongozwa na Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, inavyoendelea kuongeza fedha kwenye sekta hii ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo inaajiri Watanzania zaidi ya 85%. Kwa hiyo, namna Rais wetu anavyoongeza fedha kwenye sekta hii, inaonesha ni namna gani anavyowajali Watanzania, hasa Watanzania wanyonge ambao wengi wamejikita kwenye sekta hii ya kilimo. Kwa hiyo, nampongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anavyoendelea kutekeleza ilani ya chama chetu ya mwaka 2020/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, kwa kazi hii kubwa ambayo anaifanya Mheshimiwa Rais, ni dhahiri kwamba, Watanzania wanamwelewa na Watanzania mwakani wako tayari kumlipa kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwa hiki kipindi kifupi ambacho yuko madarakani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumshukuru na kumpongeza Mwenyekiti wangu wa CCM na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, natumia fursa hii kwa kifupi sana kuwapongeza Watendaji Wakuu kwenye Wizara hii; Mheshimiwa Waziri Bashe na Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Silinde, kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kuongoza Wizara hii na ku-*transform* Sekta hii ya Kilimo kwa vitendo. Ndugu zetu hawa ni mahodari sana na wamekuwa na ushirikiano mkubwa na Waheshimiwa Wabunge pale tunapokuwa na changamoto zetu. Kwa hiyo, tuwashukuru sana na kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache sana leo ya kuchangia. Jambo la kwanza, nitachangia kwenye *issue* ya masoko na la pili ni kwenye sekta ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa kwenye sekta ya kilimo ni upatikanaji wa masoko. Tumeona wakulima wetu wengi wakikata tamaa kuendelea na sekta ya kilimo kwa ajili ya uhaba wa masoko, lakini natumia fursa hii kuipongeza Wizara kwa namna wanavyopambana kuhakikisha Wakulima wa Tanzania wanapata masoko ya mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi sana, nawapongeza *NFRA* ambayo inaongozwa na Ndugu yangu Dkt. Andrew Komba.

Ndugu huyu namfahamu, nilifanya naye kazi kwenye Kamati ya Viwanda na Biashara kipindi kilichopita kabla sijahamia Kamati nyingine. Ndugu huyu ni mchapakazi, mwadilifu na ni mtu ambaye anashirikisha sana Waheshimiwa Wabunge. Tuendelee kumwamini na kumpa ushirikiano aweze kuongoza sekta hii ili aendelee kutoa masoko kwa wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Rais kwa anavyoendelea kuongeza fedha kwenye eneo la *NFRA* ili kuongeza uwezo wao wa kuhifadhi mazao. Ukiangalia kwenye hotuba ya Waziri, sekta hii, *I mean NFRA,* inaenda kuongezewa uwezo wa kuhifadhi kutoka tani 400,000 mpaka tani 500,000, na pia Serikali ina mpango wa kuongeza mpaka zifike tani 3,000,000 Mwaka 2030. Kwa hiyo, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri Bashe, na pia tunampongeza kwa namna ambavyo anawajali Watanzania kwa kuwaongezea sehemu ya kuuza mazao yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoiomba Serikali ni kuendelea kupunguza *restrictions* kwa wananchi wetu kuuza mazao yao nje. Serikali ikishanunua kiwango ambacho inahisi inakihitaji kuhifadhi, basi ziada inayobaki, wananchi waruhusiwe kwenda kuuza nje, ili wapate bei nzuri wanufaike na kilimo chao, hasa kilimo cha mahindi ambayo kule kwetu Tanga tunalima sana. Hiyo ilikuwa ni hoja yangu ya kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya pili ni kwenye kilimo cha umwagiliaji. Wananchi wengi wa Tanzania wanakuwa *discouraged* kuingia kwenye kilimo, kwa sababu hakitabiriki, kwa sababu kuna asilimia kubwa ya *risk*. Tulikuwa tunategemea mvua, lakini kutokana na mabadiliko ya tabianchi hali imebadilika sana na mvua hazitabiriki au zinakuja nyingi kiasi kwamba wananchi wanapata hasara kwa sababu ya mafuriko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna inavyoendelea kuongeza fedha kwenye Taasisi yetu ya Umwagiliaji na kila mwaka wanavyozidi kuongeza ekari ambazo wananchi watakuwa wanalima zaidi ya mara moja wakitumia

umwagiliaji pasipokutegemea mvua. Haya ni mapinduzi makubwa kwenye nchi yetu ya Tanzania. Ninaamini watu wengi watakuwa wanakimbilia kilimo, lakini pia hata taasisi za kifedha sasa zitafungua mioyo yao na kukopesha wakulima kwa kuwa wana uhakika wakulima watakuwa wanaenda kuvuna kwa sababu miundombinu ya umwagiliaji ipo ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nampongeza sana Rais wetu kwa namna ambavyo anaendelea kuongeza fedha kwenye Tume yetu ya Umwagiliaji. Ukiangalia kwenye bajeti, zaidi ya shilingi bilioni 400 zimetengwa mwaka huu kupelekwa kwenye sekta ya umwagiliaji ambayo ni zaidi ya 30% ya bajeti nzima. Hii ni kazi kubwa ambayo Serikali yetu inaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu nimpongeze kaka yangu na ndugu yangu Raymond Mndolwa kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kuisimamia Tume hii ya Umwagiliaji. Mwanzo nilihisi anapendelea tu Skimu za Tanga kwa sababu ndiko anakotokea, lakini siyo hivyo, kila Mbunge kila mahali anampongeza na kumsifu jamaa huyu kwa namna anavyosimamia skimu nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama ndugu yake ambaye tumeishi pamoja, namfahamu vizuri, natumia fursa hii kumpongeza. Pia namshukuru Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Mama Samia Suluhu Hassan kwa namna alivyomwamini. Naamini ataleta mapinduzi makubwa kwenye Sekta ya Umwagiliaji, tunamwomba Rais aendelee kumwacha pale, na tunamwomba Waziri Bashe aendelee kumwamini ndugu yetu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo langu la Korogwe Mjini nina skimu tatu kubwa za umwagiliaji, moja inaitwa Mahenge, nyingine inaitwa Kwa Mngumi, na nyingine Kwa Msisi. Mwaka 2023 tulisaini kandarasi ya kutengeneza Skimu ya Mahenge, lakini mwaka mzima hakuna kitu kilichofanyika na mkandarasi yule ameonekana hana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru Waziri, lakini kupitia Ndugu yetu Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji walimtoa mkandarasi yule na sasa hivi skimu ile inaenda kutengenezwa kwa njia ya *force account*. Ninaiomba Wizara iiangalie Skimu ile ya Mahenge kwa jicho la kipekee kabisa ili ipate kukamilika kwa sababu ilikuwa ina matumaini makubwa. Wananchi waliamini msimu huu wanaenda kuingia kwenye kilimo, skimu ikiwa imekamilika, lakini mwaka mzima hakuna kilichofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, chonde chonde ndugu yangu asimamie kwa kutumia ile *force account* ambayo wamepanga ili kutengeneza ile skimu ipate kukamilika. Pia nashukuru kwa skimu zangu mbili zilizobaki, Skimu ya kwa Mngumi na Skimu ya Kwa Msisi kwamba, ziko kwenye mpango wa mwaka huu na wanasema wanaenda kutangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023 walisema Skimu ya Kwa Msisi inatangazwa, lakini mpaka kufikia wakati huu hawajatangaza kusaini mkataba kwenye skimu ile. Sasa ninachoomba, Mheshimiwa Waziri mwaka huu kwa sababu wananchi wa Kata ya Kwa Msisi wamekuwa wanasumbua sana, wanahitaji mkandarasi apatikane ili waweze kutengenezewa ile skimu yao ya Kwa Msisi, kwa kuwa, ni sehemu ambayo wanaihitaji kwa ajili ya maisha yao kwa sababu hawana shughuli nyingine zaidi ya kilimo. Kwa hiyo, naomba skimu ile itangazwe ili iweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja na Mungu akubariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, na Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, ajiandae.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nami kupata fursa kuwa miongoni mwa wachangiaji katika bajeti ya Wizara ambayo ni muhimu sana kwa ustawi wa Taifa letu. Naomba nianze kumshukuru Mwenyezi

Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia afya ili niweze kusimama leo nikiwa na afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niungane na wenzangu ambao wamempongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya hasa katika sekta hii ya kilimo. Tunabaki na hadithi kuwa, katika nchi ambazo zina uhakika wa kujitosheleza kwa chakula ni pamoja na nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujitosheleza kwa chakula siyo kama ni jambo ambalo limekuja kama vile ni mtu unalala unaamka, linatokana na mipango thabiti ambayo imewekwa, mipango thabiti katika kuhakikisha kwamba kila mwananchi mkulima anafikiwa na mbolea. Inawezekana kwamba, kuna baadhi ya maeneo ya vijijini ambayo mbolea haikufika, lakini sisi wananchi wa Kalambo tuna kila sababu ya kusema ahsante kwa sababu mbolea hii imefika kwa walengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa marekebisho. La kwanza, ni suala zima la mbolea kufika kwa wakati, lakini mbolea ambayo ndiyo hitaji la wananchi ifike. Kama wenzangu walivyokuwa wamesema, ni vizuri pia Mheshimiwa Waziri akaendelea kufikiria juu ya *packaging* ya mbolea. Siyo lazima wote wakanunua kilo 25 na kilo 50. Ifike wakati kwamba anayehitaji kilo tano apate, kilo 10 apate na kilo 20 apate, lakini na hao wanaohitaji kilo 25 waweze kupata na wapate kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijikite katika suala zima la ubora katika kilimo. Ili uweze kupata mahindi yaliyo bora na ili uweze kuwa *competitive* kwa maana ya uzalishaji unaoleta tija na kilimo kile ambacho kila mkulima akifurahie, ni pale ambapo tunakuwa na uhakika wa shamba ambalo limeandaliwa vizuri, lakini tuwe na uhakika wa mbegu zilizo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa katika mbegu ndiyo naomba nitumie muda mwingi kuelezea jinsi ambavyo tuna kazi kubwa ya kuhakikisha kwamba tunajitosheleza katika suala zima la uzalishaji wa mbegu. Mheshimiwa Waziri unajua, kama Taifa

tumekuwa tukitumia mbegu ambazo zinatoka kwa majirani zetu. Kwa sisi ambao tuko mpakani, tunategemea mbegu kutoka Malawi na Zambia. Kwa kuwa Mwenyezi Mungu ametaka Taifa la Tanzania twende kwa kasi, hayo Mataifa yote ambayo nimeyataja sasa hivi, yana ukame mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? Ni wakati mwafaka tuhakikishe kwamba tunazalisha mbegu za kutosha kwa ajili ya kuwasaidia Watanzani na kwa ajili ya kuuza katika mataifa hayo ambayo sisi tumekuwa tukinunua kutoka kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba tukiwa na uhakika na mbegu iliyo bora ambayo inakubali, itakuwa ni chanzo cha mapato na katika mchango wa kilimo kwa kuingiza *forex*. Hili ni eneo mojawapo ambalo tunaweza tukafanya vizuri na tukazalisha mbegu za kutosha. Kwa uwekezaji ambao unawekwa katika bajeti ya kilimo, hatuna sababu ya kutokuzalisha mbegu za kutosha kwa ajili ya watu wetu na kwa ajili ya kuuza kwa majirani zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba niikumbushe Wizara, kuwa tunazo mbegu bora na nzuri, ni jambo moja, lakini siyo busara tukaamua kwamba kwa sababu tunazalisha hizi mbegu, basi tukasahau mbegu zetu za asili. Tusije tukafanya kosa hilo kubwa. Ukienda kwa wananchi ambao wanakuwa wanalima mahindi, wanajua mbegu zao za asili ambazo zina uvumilivu mkubwa sana katika kupambana na maradhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ukiwa na la kwako unajivuna. Isije ikafikia mahali kwamba lazima tutoe mbegu kwa hao ambao wametuletea, halafu tukaua kabisa mbegu zetu za asili. Hii iende kwenye mazao yote, kwa maana ya mahindi, ulezi, ngano na mtama. Ni vizuri kitengo hiki ambacho kinahakikisha kwamba tunakuwa na mbegu zetu za asili, tuzilinde kwa wivu mkubwa sana. Wajibu wetu ni kuhakikisha kwamba katika hizi mbegu zetu za asili tunafanya maboresho ili ziweze kuwa zinazalisha kwa wingi na kwa ubora ambao unatakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongelea habari ya kuwa na shamba lililoandaliwa vizuri na mbegu iliyo bora na mbolea ambayo inatakiwa. Hili naomba niipongeze Wizara, wameanzisha jitihada za kuhakikisha kwamba udongo unapimwa. Ukishakuwa unajua afya ya udongo, kiasi cha mbolea ambayo inatakiwa kuwekwa utakuwa unajua, kwa sababu siyo kila udongo unahitaji *Urea* na siyo kila udongo unahitaji *DAP*. Ifike mahali ambapo sisi kama Taifa tujivunie kwamba maeneo yote yamepimwa kwa maana ya kujua afya ya udongo, na pia tuwe na uhakika kiasi gani cha mbolea na aina gani ambayo inatakiwa kutumika katika ardhi yetu. Hii itakuwa tunawasaidia wakulima wetu. Siyo busara unaambiwa kwamba ekari moja utumie mifuko mitatu ya *Urea*. Wakati mwingine unakuwa unazidisha udongo tayari hauhitaji *Urea* lakini kwa sababu tumeshakariri kwamba *Urea* ndiyo inatakiwa, inakuwa haitusaidii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishakuwa na uhakika wa mazao yaliyo bora, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha kwamba mwananchi huyu aliye Kalambo anahakikishiwa soko la uhakika la mazao yake kama ni mahindi, ulezi na mtama. Siyo kazi yake alime halafu ahangaike kutafuta soko. Suala la kutafuta soko bado libaki mikononi mwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa kupitia kitengo chake cha *NFRA*, kulikuwa na kitengo kinahangaikia suala zima la kutafuta masoko na masoko twende kuyatafuta huko duniani. Serikali ndiyo mna uwezo wa kuongea kwa misuli yenu kwa mawasiliano mliyonayo na mahusiano mliyonayo kuhakikisha kwamba kama ni mahindi tunapeleka *South Sudan*, *Congo*, Kenya, Malawi na Zambia. Siyo kazi ya Mwananchi wa Kalambo kwenda kutafuta soko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtusaidie ili tuwe na uhakika wa kwamba tukiwa tunalima tuna uhakika wa soko, tunapata hamu ya kwenda kulima mwaka unaofuata, lakini kama mwaka huu tunakuwa na bei nzuri halafu mwakani bei ikawa siyo nzuri, hakika kilimo hakitakuwa kivutio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanzo ambao tumeuanza na mwendo huu ambao Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wake wanaenda, wakaze buti, inawezekana ndani ya muda mfupi mchango kutoka kwenye sekta ya kilimo ambayo inaajiri zaidi ya Watanzania 75% ukaonekana kwa wazi kabisa. Ifike mahali kuwe na malengo ya kwamba itafika mahali ambapo badala ya kwamba Wizara iwe inapata pesa kutoka Serikali Kuu, kilimo ndicho ambacho kiwe kinatoa pesa kupeleka Serikali Kuu na wakati mwingine hata ruzuku tusitarajie kwamba itakuwepo miaka yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala zima la mazao ya chakula kwa maana ya mafuta. Kumekuwa na *notion* kwamba ukitaka michikichi, maana yake ni Kigoma peke yake, *la hasha!* Narudia tena michikichi inakubali mwambao wote wa Ziwa Tanganyika na inakubali hata ukienda Kyela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kandege. Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni ndani ya ukumbi wetu ambao ni vizuri tukawatambua.

Tunao wageni sita wa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe, hawa ni Chama cha Wakulima wa Parachichi Tanzania wakiongozwa na Mwenyekiti wao, Ndugu Rebecca Andrew, karibuni sana. Chama hiki Makao Makuu yake yako Njombe, Tanzania. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ambaye ni rafiki yake kutoka Jijini Dar es Salaam, karibu sana Bungeni, yuko pale kwenye kona. *(Makofi)*

Wapo wageni 122 wa Mheshimiwa Elibariki Kingu na hawa ni SMAUJATA kutoka Mkoa wa Singida, karibuni sana kwenye Bunge letu. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao wametutembelea kwa ajili ya mfunzo, hawa ni wanafunzi 46 kutoka Chuo Kikuu cha Tumaini *(KCMC)*

Makumira kutoka Mkoa wa Kilimanjaro, karibuni sana wanafunzi wa chuo. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 70 na watumishi wawili kutoka Taasisi ya Uhasibu na Fedha kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Bungeni kwa ziara ya mafunzo. *(Makofi)*

Baada ya utambulisho huo, sasa namwita mchangiaji anayefuata ambaye atakuwa ni Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, atafuatiwa na Mheshimiwa Suma Ikenda halafu Mheshimiwa Dkt. Medard Ntara, ajiandae.

**MHE. DENNIS L. LONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia niungane na wenzangu ambao wamenitangulia kuipongeza Serikali yetu kwa kuonesha *seriousness* kwenye suala zima la kilimo ambapo tumezoea kusema kwamba ni uti wa mgongo. Tunasema kilimo ni uti wa mgongo kwa sababu ndiyo eneo ambalo linatuhakikishia ajira za watu wengi wa Tanzania. Katika hili, ongezeko la bajeti kwenye Wizara hii ni jambo ambalo linatuonesha na linatufariji sana sisi wawakilishi wa wananchi kuona kwamba kuna mkazo ambao unawekwa kwenye eneo la kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya kuhakikisha kwamba Taifa liko salama kwa sababu ya usalama wa chakula. Nawapongeza wasaidizi wake wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Bashe; Naibu Waziri Mheshimiwa Silinde; Katibu Mkuu, ndugu yetu Gerald Mweli na watendaji wengine wa taasisi mbalimbali ambazo ziko chini ya Wizara ya Kilimo, ambao wamepewa jukumu la kuhakikisha kwamba Taifa letu liko salama katika sekta nzima ya chakula, lakini ajira kwa maana ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirejea mpango wa bajeti ambao uliwasilishwa mbele ya Bunge lako miezi mitatu iliyopita, ulijikita sana kwenye sekta ya kilimo kama eneo muhimu la kutuhakikishia ongezeko la pato la Taifa, ajira na chanzo cha ku-*stabilise* thamani ya pesa yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *projection* ya kilimo ni kwamba tunategemea ongezeko kubwa la kilimo. Ni matumaini yangu kwamba tutafikia malengo hayo iwapo baadhi mambo tutayazingatia, kwa sababu mchango wa sekta ya kilimo ni mkubwa kwenye uchumi wa nchi yetu. Tunaweza kuona kwamba pato la Taifa kwenye ajira peke yake, 26% inatokana na kilimo kwa Watanzania, na 65% mpaka 70% ya Watanzania wameajiriwa katika sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona mchango wa kilimo ni zaidi ya 65% kwa maana nzima ya uchumi wa viwanda kwa maana ya malighafi, na tunaweza kuona kwamba zaidi ya kaya milioni nane za Watanzania wameajiriwa aidha moja kwa moja ama *indirectly* katika sekta ya kilimo, wakati kaya milioni nne zinategemea mauzo ya chakula kama chanzo kikuu cha mapato. Kwa hiyo, siyo eneo la kulifanyia mzaha kwa sababu limebeba hatma na *stability* ya nchi yetu na usalama wa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza kuona kwamba hapa kuna ongezeko kubwa la bajeti. Ndani ya mwaka 2021/2022 tulikuwa na shilingi bilioni 294 lakini mwaka 2022/2023 ikapanda mpaka shilingi bilioni 751; na mwaka 2023/2024 Bajeti ya Kilimo imepanda mpaka shilingi bilioni 970 ambayo ni zaidi ya ongezeko la 29%, na leo hii tunazungumzia *over one trillion*. Siyo jambo dogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko yote ambayo tunaweza kuzungumzia, upandishaji wa bajeti hii, tunategemea kwamba uende ukaongeze uzalishaji. Ongezeko la uzalishaji tunategemea kwamba utaweka ziada kubwa zaidi katika eneo la chakula ambalo linaenda kupunguza gharama ya uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kuna mfumuko wa bei katika mazao hasa ya chakula. Kwa hiyo, ziada ambayo tunazalisha kupitia kilimo haijampa nafuu mkulima au mwananchi mmoja mmoja kwa sababu bado tuna *experience* mfumuko wa bei ya vyakula. Kwa hiyo, maeneo ambayo nitajielekeza katika mchango wangu ni nini tufanye ili tupunguze mfumuko wa bei ya

vyakula ili ongezeko la mavuno liwe na tija kwa Mtanzania mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo nina ombi, huu mfumuko wa bei kwa mfano mwaka 2023, tulikuwa na zaidi ya asilimia tisa ukilinganisha na mwaka juzi ambayo tulikuwa na asilimia sita, inayotokana na gharama za uzalishaji. Gharama kubwa ya uzalishaji inasababisha mkulima akose uwezo wa kuweka akiba. Kwa hiyo, jitihada za kujiondoa kwenye umaskini kupitia kilimo bado zinakwazwa na ongezeko la bei katika uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nategemea bajeti ya kilimo mwaka huu ije kitofauti kabisa na bajeti zilizotangulia. Kivipi? Kwa sababu mwaka huu tuna-*experience* hali ambayo siyo ya kawaida katika nchi yetu; uharibifu mkubwa wa barabara, madaraja na vivuko ni ndwele ambazo zinaashiria hali ngumu zaidi huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunazungumzia 70% ya Watanzania waliojiajiri kupitia kilimo, maana yake wako vijijini. Kama tunazungumzia kwamba barabara za *TARURA* hazipitiki huko vijijini, maana yake tunazungumza kwamba hatuwezi kusafirisha pembejeo kwa bei ile ile ambayo tumeizoea. Kama hatuwezi kusafirisha pembejeo kwa bei ambayo tumezoea, maana yake inaenda kuongeza gharama ya uzalishaji kwa mkulima. Maana yake inaenda ku-*compromise* ongezeko la chakula na usalama wa chakula kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitegemea bajeti hii ijikite kwenye suala zima la *restoration* ya miundombinu. Wakati wa majumuisho, napenda kuona Serikali kwa pamoja; Wizara ya Kilimo, *TARURA, TANROADS* na Viwanda na Biashara, wanakuja na mkakati wa kuokoa kilimo na mkulima katika maeneo ya vijijini na pembezoni, kwa sababu bajeti hii bado naona ni ya kawaida ukilinganisha na ya mwaka 2024. Ni bajeti ya kawaida katika kipindi ambacho siyo cha kawaida. Hivyo, tunategemea Serikali ichukue maamuzi yasiyokuwa ya kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maamuzi yasiyokuwa ya kawaida sasa hivi ni kumhakikishia mkulima anakuwa na uhakika wa kupata mbegu na pembejeo zote kwa wakati na uhakika wa kusafirisha mazao yake kwa wakati. Hivi ninavyozungumza, pale jimboni kwangu kuna shamba la *ASA* Kilangali, wameshindwa kusafirisha mbegu kwa sababu barabara haipitiki. Kama hatuwezi kusafirisha mbegu kwa sababu barabara haipitiki hatima ya uzalishaji katika kilimo ni nini? Ni maeneo ambayo tunapaswa tuyaangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna hali mbaya ya barabara. Wananchi wangu 90% ni wakulima, lakini Kata ya Ulaya kwenda Kisanga mpaka Malolo hapapitiki; kutoka Malolo mpaka Uleling'ombe ambapo wanategemea kilimo haipitiki; kutoka Kidodi – Ruhembe – Kidogobasi - Kihelezo mpaka Ilundo hakupitiki, na hilo lote ni bonde la mpunga na bonde la kilimo cha miwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Masanze kwenda Kilangali, Mbamba mpaka Kiduhi hakupitiki na kuna Shamba la *ASA* ambalo linazalisha mbegu, lakini Zombo, Nyali na Nyameni hakupitiki kwa barabara. Mikumi - Kisanga kwenda Msolwa-Madizini ambao ndiyo wazalishaji wakubwa wa mboga mboga hapapitiki. Mabwerebwere - Tindiga ni sehemu ambazo zina tija kubwa ya kilimo, barabara hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapozungumzia hatima ya wakulima katika jimbo ambalo 90% ni wakulima, haliwezi kufikika katika barabara zake zote kwa sababu ya kukatika kwa miundombinu. Tunaweka wapi kilimo cha nchi yetu? Hilo tunapaswa tuli-*discuss* kama suala la dharura na pia tunapaswa tuli-*discuss* kama mpango maalum wa Bunge lako kuokoa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia hotuba ya Wizara ya Kilimo, tunazungumzia uharibifu wa miundombinu yote ya barabara na nini, lakini hatujazungumzia uharibifu wa skimu za umwagiliaji. Tunazungumzia skimu mpya, hatuzungumzii uharibifu wa skimu za kienyeji za wananchi. Tuna mpango gani kwanza wa

kuokoa skimu za kienyeji za wananchi? Tuna mpango gani wa kuokoa skimu ambazo zimeharibika ambazo tumeshawekeza fedha? Tuna mpango gani wa kuanzisha skimu mpya ambazo zinaenda kutuhakikishia ongezeko la uzalishaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, zao la miwa limesahaulika. Tunazungumzia ruzuku ya mbegu kwenye maeneo mengine lakini mkulima wa miwa amesahaulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo. Namwita sasa Mheshimiwa Suma Ikenda Fyandomo atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara na Mheshimiwa Asha Abdullah Juma ajiandae.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo. Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu wa Mbinguni kwa kunipa uzima na afya njema hatimaye imempendeza siku hii ya leo kusimama kwenye Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan na Amirijeshi Mkuu. Ninampongeza kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya kwa kuwaona wakulima. Wakulima walikuwa katika kipindi kigumu sana ambapo mbolea ilikuwa na bei kubwa sana, lakini aliweza kutoa fedha za ruzuku kutoka Mfuko wa Mbolea wa kilo 50 ambao ulikuwa unauzwa kwa shilingi 150,000, umeshuka bei mpaka shilingi 60,000 na shilingi 70,000. Pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Bashe ambaye ndiye Waziri wa Kilimo. Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Bashe kuwa Waziri wa Kilimo, naona kabisa jinsi ambavyo Mwenyezi Mungu anamwongoza kumpa macho ya rohoni kwa kumwona Mheshimiwa Bashe anafaa na anastahili

sana kwenye Wizara hii ya Kilimo, kwa bajeti hiyo ambayo ameisoma Mheshimiwa Bashe hapa ya shilingi trilioni 1,200 kuomba ipitishwe. Naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa kwenye ziara kule Kanda ya Ziwa mwezi wa tatu, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Bashe, aliweza kufanya jambo kubwa sana kwenye Taifa hili la Tanzania mara baada ya kusikia kuna mchele umeingia kutoka Marekani, kwamba mchele ule unakwenda kupelekwa kwenye shule za watoto wetu ambao ni wadogo, ambao ni malaika wa Mungu, mchele ule bila kujua una virutubisho gani na utakwenda kuathiri nini kwenye afya za watoto wetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Bashe kwa kusimamia afya za watoto wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili la Tanzania tuna maeneo mengi sana. Mikoa mingi inalima mpunga na mpunga huo ambao ndiyo unasababisha mchele, kule Mbeya, Kyela tunalima mpunga, Mbarali mpaka kuna *Kapunga Rice,* ni mpunga upo kule. Pia kule Kanda ya Ziwa nilipokuwa, kila mkoa ninakopita, ninaona barabarani mchele, ninaona mpunga umeshamiri sana ambapo ndani huko kwenye mashamba yamkini ndiko umeshamiri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo ndani ya Taifa letu hili la Tanzania, kama mpunga mwingi kiasi hicho, kule Rukwa na mahali pengine unalimwa mpunga wa kutosha sana, iweje mchele ukatoka Marekani uje kwenye Taifa letu hili la Tanzania? Wizara ya Kilimo ikiongozwa na Mheshimiwa Waziri Bashe ninawapongeza sana kwa kusimamia hili. Sisi kama viongozi, watetezi na wasimamizi wa wananchi wa Taifa hili la Tanzania, tunampongeza zaidi Mheshimiwa Bashe kwa nafasi hii kwa kuwa anatambua majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la kuleta mchele kutoka kwenye nchi ya Marekani, mwaka 2023 pia tuliletewa dawa za meno kwa ajili ya watoto wetu wapelekewe kule mashuleni. Lazima tuogope na tushtuke kwamba hiki kitu kinalenga nini? Sisi kama viongozi ndiyo wasimamizi wa Taifa hili la Tanzania, hasa kwa vizazi vyetu ambavyo ndiyo Taifa la kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Mheshimiwa Waziri Bashe anisikilize, Wilaya ya Rungwe wananchi wale wanategemea sana kilimo, wanalima mazao mengi sana, lakini wazazi wengi wanategemea sana chai. Kuna Kiwanda cha Chai cha Chivanje, kile kiwanda kimefungwa. Kuna wananchi wa Kayuki, Nsekela, Katonya, Ruwalisi, Ndende na Kiganga wale wote wamelima chai za kutosha. Wao wanajihimu kuchuma chai wakitegemea watapata fedha mwisho wa mwezi ili waendeleze maisha yao na ndiyo maisha yao siku zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufungwa kiwanda kile, namwomba Mheshimiwa Waziri Bashe akawatazame wananchi hawa wa Wilaya ya Rungwe aone namna ambavyo watafanya na kilimo kile cha chai watakifanya nini? Maana kiwanda kimefungwa, wakichuma chai wanaipeleka wapi? Naomba sana Mheshimiwa Waziri Bashe alitazame hili na kuwasimamia hawa wakulima wa chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kuna wakulima wa chai ambao wako kwenye Wilaya hiyo hiyo ya Rungwe, wakulima hawa wanapeleka chai kwenye Kiwanda cha Chai cha Katumba, ambao wako maeneo ya Rungwe, Kapugi, Masege, Segera, Mwakaleli, Mano, Lupa, Itete, Kimo, Suma na Nditi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hao wanafanya vizuri, lakini hawapati fedha kwa wakati. Wanazidishiwa sana muda. Sijajua kwenye hili hawa wakulima wa Mheshimiwa Bashe anawasimamia kwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba muda ni mchache sana, naongea kwa sehemu. Mheshimiwa Waziri, kule Mufindi, Mkoa wa Iringa, Serikali iliahidi mwaka 2022 kujenga kiwanda cha kuchakata maparachichi. Eneo lile ambalo mlikuwa mmeomba lipatikane ndipo mjenge kiwanda cha kuchakata maparachichi, limepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hicho cha kuchakata maparachichi ni cha kusaidia wananchi wa Nyanda za Juu Kusini ikiwemo Njombe, Mbeya, Iringa, Songwe na maeneo mengine.

Kule Tukuyu Wilaya ya Rungwe, Mkoa wa Songwe wamejitahidi sana kupanda maparachichi baada ya kusikia kauli hii ya Serikali. Hivyo basi, tunaomba sana wakati wa kuja kuwasilisha hapa, Mheshimiwa Waziri atuambie ni lini kiwanda hicho kitaanza kujengwa ili wananchi waweze kupona kwa ajili ya kuendeleza ulimaji huu wa parachichi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ambavyo anaendesha Wizara zote. Katika kumpongeza huko, kule Mbarali na Kyela zilitolewa fedha kiasi cha shilingi bilioni 79 kwa ajili ya skimu za umwagiliaji. Namwomba sana Mheshimiwa Bashe, kule Mkoa wa Mbeya bado kuna Wilaya nyingine ambazo zina uhitaji wa skimu hizo ikiwa ni pamoja na Mbeya *DC*, Busokelo, Chunya, Mbeya Mjini na pia kuna maeneo pamoja na Rungwe yenyewe, wana uhitaji wa skimu hiyo sana. Wanawake wale pamoja na vijana wanajituma sana kwenye mambo ya mashamba na ndiyo kazi yao kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo la *BBT* ambalo limeanzishwa ni jambo jema na zuri. Tumeona hapo jinsi ambavyo linafanikiwa. Pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri kwa namna ambavyo unayaona haya yote kwa ajili ya ajira ya kujiajiri wanawake na vijana. Kwenye hili, Mwenyezi Mungu aendelee kukusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakwenda kumalizia kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Naomba uhitimishe.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namtia moyo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa, nzuri anayoifanya. Narudia kwamba, Mwenyezi Mungu anamwongoza, anampa macho ya rohoni hatimaye akamteua Naibu Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko ambaye ana hofu ya Mungu, aendeshe mambo vizuri. Kila

kitu kinakwenda sawa, Mawaziri wake wako vizuri, Makatibu Wakuu, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa pamoja na Wakurugenzi wako vizuri. Mwenyezi Mungu ambariki sana Mheshimiwa Rais na ninaomba Mwenyezi Mungu aendelee kumpa macho ya rohoni

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Kilimo kwa juhudi. Kwa kweli anachakarika. Baada ya kusema hayo, mimi nitatoa maoni na ushauri na ninaomba Mheshimiwa Bashe, haya ninayoyasema hapa sasa hivi, leo ayaandike hapo. Namwambia hivi, mimi lazima shilingi nitaishika na anajua nakwenda kuzungumza nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na suala la hiki kilimo cha jembe la mkono. Mheshimiwa Waziri amekuja na programu kibao, mimi nikafikiria, hizi programu ni kwa ajili ya wakulima wadogo hawa wa Mdundualo au anawalenga wakulima hawa wakubwa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa jembe la mkono, nasema haya mambo anayoyapanga itakuwa ni ngumu. Hebu sasa tuamue, wakati CAG akija hapa akisema fedha zimeliwa nyingi, inasikitisha. Hebu tuamue hizi fedha sasa kila kijiji kipate matrekta. Kazi kubwa ya kilimo ni kulima. Ule ukulima ndiyo unaowatesa wakulima. Umefanya vizuri kwenye suala la mbolea, lakini sasa wanalima kiasi gani hawa wakulima wadogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta mtu anaweza kulima ekari mbili tu amechoka, akiweza sana ekari tatu, lakini tungekuwa na matrekta kama enzi zile za Mwalimu Nyerere, wakulima hawa wangeweza kulima ekari za kutosha. Pia hata miili yao na afya zao ziwe nzuri, hebu tujielekeze huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili linakwenda sambamba na mikopo wanayoitoa kwenye hizo benki za Mheshimiwa Bashe. Hivi, hiyo mikopo wanayoitoa ni mikopo kwa ajili wakulima wadogo au ni mikopo kwa wakulima wakubwa? Benki zinaweza kumkopesha mkulima huyu mdogo ambaye fedha zake wakati mwingine unakuta wanahitaji shilingi 500,000 au shilingi milioni moja, lakini benki zinawakopesha wakulima gani? Ndiyo maana wakulima wetu wanaingia kwenye hiyo mikopo ya kukausha damu kwa sababu benki zimeshindwa kuwasaidia wakulima wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku moja nilijaribu kuwaomba waende wakapate mkopo, shilingi 500,000 sijui shilingi 200,000 kwenye benki, hawapati. Sasa hii *TADB* ni kwa ajili ya wakulima gani Mheshimiwa Bashe? Tuliangalie hilo. Ukulima wa jembe la mkono hauwasaidii kabisa wakulima wadogo. Hii mipango yote, umesema hapa vipaumbele mazao 20 yale ya umwagiliaji, hivi watalima wakulima wadogo kweli kwa jembe la mkono! Mheshimiwa Bashe umejitahidi ukapeleka pikipiki, ingawa hizo pikipiki nikwambie zimekaa ofisini pale Halmashauri, ukiwapigia simu wanakwambia weka mafuta. Mimi nitaweza, kwani mimi ni Mbunge, hivi mkulima yule wa Mdundualo ataweza kuweka mafuta? Kwenye wale wataalam wako, sasa nikwambie zile pikipiki haziwasaidii wakulima wadogo, zinakwenda kwa wakulima wenye uwezo tu, hawa wakulima wakubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili liangaliwe. Wapeleke *power tiller* na matrekta kwa wakulima vijijini. Kila kijiji kiwe na matrekta angalau mawili au matatu, tutafanikiwa kwa hilo, lakini hivi hivi tutakuwa kila siku tunasema wakulima na tunawasifia wanatulisha, lakini wanatulisha kwa mateso makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoke hapo sasa niende huko kwenye zao analolipenda Mheshimiwa Bashe, alikuwa anazungumza wakati ule nilikuwa nafurahi, anawatetea wakulima sana. Sasa nije kwenye kilimo cha tumbaku. Hili zao Mheshimiwa Bashe naomba aendelee nalo kwa sababu anasema linaleta

fedha za kigeni. Likileta fedha za kigeni haziwasaidii wakulima wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, hii tumbaku aende nayo kwa wakulima wakubwa tu kama akina Mheshimiwa Cherehani, hao wanalipenda, lakini wakulima wadogo wa tumbaku wanateseka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi mvua imenyesha, mabani yote yameanguka kwa sababu hawana mabani bora. Kwa hiyo wanateseka, afya zao ni mgogoro. Wakulima wa tumbaku, kama Mheshimiwa Waziri anasema lina faida, twende tuongozane, kwenye *block farm,* twende Namtumbo akaone makazi yao. Bado wanakaa kwenye zile nyumba tunaziita mbavu za mbwa. Afya zao, wanaumwa vifua. Hebu hili zao la tumbaku kwa wakulima wadogo tuliondoe, siyo taratibu, tuliondoe mapema sana. Kuna mazao ambayo wanaweza wakalima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Manyanya, kule kwake Nyasa mlitaka kumpelekea tumbaku. Nyasa ni Wilaya ambayo ni maskini kwa kweli, yeye akajikita kwenye kahawa na mpunga kwa umwagiliaji. Hayo ni mazao ambayo wakulima wadogo wanaweza wakayalima. Mheshimiwa Bashe angalia, leo nenda Mbinga, Magugu kule Babati, wakulima wadogo wanalima mpunga na maisha yao ni mazuri, angalia nyumba zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda Mbinga leo, wakulima wadogo wa kahawa watasema hili zao safi, ukienda Mbinga tena Mheshimiwa Spika angekuwepo ningemwambia, hebu mtembeze, mpeleke Mheshimiwa Spika Mbinga mkaangalie kule nyumba za wakulima wadogo, hapo ndiyo utasema zao la kahawa lina faida kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye tumbaku Mheshimiwa Bashe, ahangaike na wakulima wakubwa tu, na hawa wanunuzi kwanza. Kwa tumbaku nikwambie ukweli, kwanza mkulima mdogo hawezi kupata *grade one* wala *grade two* wanapo-*classify* tumbaku zao. Hao wakulima wadogo kulipwa inakuwa ni

balaa. Anafanya kazi miezi nane au tisa hajalipwa, wanaishia tena kukopwa. Kwa hiyo, wale wakulima wakubwa na wanunuzi wanawatumia wakulima wadogo ili wapate tumbaku na wapate pesa, lakini huyu mkulima mdogo ananyanyasika mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliwahi kulima tumbaku wakati huo siyo Mbunge, nafanya kazi nyingine, sijawahi kupata *grade one* wala *grade two*, mpaka uzungumze na ma-*classifier*. Kwani hilo Mheshimiwa Bashe wewe hulijui! Hulijui hilo! Hebu tuwasaidie wakulima wadogo, ondoa zao la tumbaku kwa wakulima wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwambia Mheshimiwa Waziri, aende akaangalie kule, wale wakulima wa *block farm* ni majirani zangu, nyumba zao kwanza hazina adabu, kwa sababu wanatumia mbavu za mbwa, matundu kila mahali, watoto wanalala chumba hiki, wazazi wanalala chumba hiki, hakuna heshima kabisa. Halafu bado mnasema tumbaku inaleta *foreign currencies*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *foreign currency* haimsaidii mkulima mdogo. Niambie wamefaidika kwa kitu gani? Hapo nakwambia usiponiambia leo umejipangaje kuliondoa hili zao la tumbaku, nitakushangaa. Namtumbo ni Wilaya ya mwisho kabisa kule, umaskini umejaa, wanalima tumbaku hawapati chochote. Hapana, lazima tuwaonee huruma watu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu hii miradi ya umwagiliaji, mmejinasibu toka mwaka 2023 naisikia. Sasa naomba kwanza Waziri atuambie, miradi mingapi ya umwagiliaji imefanikiwa mpaka sasa? Pia huko Litui kwetu kuna vijiji vinaitwa Kimbande, Lundo na Chiulu, hiyo miradi ya umwagilijai imefikia wapi? Akinijibu hayo, yeye na mimi hapo tutapatana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niendelee kusema, Mheshimiwa Waziri azungumze na wanunuzi wako wakubwa, wajielekeze kwa wanunuzi wakubwa waache kwenda kuwanyanyasa wakulima wadogo wa tumbaku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Dkt. Thea Ntara. Nilimwita Mheshimiwa Asha Abdullah Juma atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Theonest Lwehikila na Mheshimiwa Rehema Juma Migilla ajiandae.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii uliyonipa sasa kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Naomba radhi leo sauti yangu imekuwa ya mahaba zaidi, kwa hivyo mtanistahimili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa roho safi na kwa sauti kubwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu, Jemedari Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa jinsi anavyosimamia kazi yake ya kuiongoza nchi yetu, mpaka hapa tulipo tunaenda vizuri. Mheshimiwa Dkt. Samia anaweza, tena anaweza sana na tungependa kusema asijali, madebe matupu hayaachi kutika, ndiyo dunia, lakini yeye anawaka na anaweza vizuri, na Mungu atamsimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu za pili naomba ziende tena kwa Mheshimiwa Dkt. Samia kwa kuchagua hii timu ambayo Mheshimiwa Waziri Hussein Mohamed Bashe, Naibu Waziri Mheshimiwa David Silinde na Katibu Mkuu Mweli na timu nzima. Hii timu ni kabambe na safi kwa mapambano, nafikiri itaipeleka nchi yetu tunakokufikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia ameweza kututoa kule tulikokuwa, na sasa kuna ongozeko la bajeti kutoka shilingi bilioni 294 mwaka 2021 kufikia shilingi trilioni 1.248 mwaka 2024/2025. Nani kama Mama Samia? Hii ni bajeti kubwa kwa kilimo kwa kujua kwamba bila mapinduzi ya kijani, hatuwezi kufika popote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya mauzo nje yameongezeka kutoka dola milioni 1.2, trilioni 2.5, mpaka dola bilioni 2.3 sawasawa na fedha za Tanzania shilingi trilioni sita.

Vilevile mapato yanayotokana na mazao ya malighafi ya kilimo yamefikia shilingi za Tanzania trilioni sita. Hii ni kazi kubwa sana iliyofanyika kwa umahiri wa Mheshimiwa Waziri wetu. Vijana hawa ambao nami pia nina mkono, kwa sababu Mheshimiwa Hussein Bashe nimemlea, Mheshimiwa David Silinde nimemlea na kama mtu anapinga apinge hapa mbele ya Bunge hili. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, nataka kuzungumza kuhusu mbegu asilia. Nashukuru sana Wizara kwa jitihada inazochukua kwa uhifadhi na utafiti wa mbegu hizi. Bajeti hii kwa kweli pia imetenga fedha za kuimarisha jengo la uhifadhi wa mbegu. Sasa Wizara isaidie kuharakisha mchakato wa kupitia sera ya mbegu ili kuwezesha hizi mbegu kutambulika kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naiomba Wizara kutenga bajeti kwa wakati ili kusimamia mbegu za wakulima pamoja na utafiti, hasa kwa vile ukitilia maanani kwamba mbegu hizi zinapotea kwa kasi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbegu za asili ni urithi wetu wa asili, kwa hiyo, lazima tuhakikishe zinaendelea kuweko na kustawi. Pengine zitakapokua vizuri zaidi na sisi tutauza huko na zitatuongezea kupata fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili ninalotaka kuzungumzia ni kilimo ikolojia hai. Nawapongeza sana Wizara kwa ushirikiano na asasi zisizo za Serikali kwa kuhakikisha kwamba tumekuwa wa kwanza katika Afrika Mashariki na Afrika chini ya Sahara, kuwa na Mkakati wa Kilimo Ikolojia Hai. Naomba tufahamu kwamba mfumo wa kilimo duniani umeanza kuelekea kwenye kilimo ikolojia hai. Tujue hata hao Ujerumani, ndiyo kwanza wamepitisha mkakati sambamba na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapongeza juhudi zinazoendelea kwa ushirikiano kuhakikisha kwamba kilimo hiki kinaeleweka na mpango kazi mkakati unaendelea kufanyiwa kazi. Tunategemea katika bajeti hii kutatengwa pesa kwa ajili ya

utekelezaji kwenye maeneo ya uhamasishaji, *(sensitisation)* hasa kwa sisi Waheshimiwa Wabunge kufahamu zaidi nini kilimo ikolojia hai ili tuweze kufanya maamuzi kwa namna gani mtu atumie kilimo kipi, kwa sababu tumeona pia katika kilimo hiki tunaweza kutumia samadi zetu wenyewe. Kwa hiyo, zitapunguza gharama ya kununua mbolea, au kupigania mbolea au kuomba mbolea iuzwe robo, kilo au nusu kilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tutakuwa tunakwenda zaidi kwenye mfumo ule ambao pia kwa mazao hayo imefahamika duniani kwamba yanapata soko zaidi. Tunaomba Wizara pia katika kupitia bajeti hii, itoe ruzuku kwa sababu wako vijana ambao wamejitolea kutengeneza viuatilifu kwa kutumia hayo hayo mambo ya kilimo hai. Kwa hiyo, Wizara iwaone na kuwapa *support* vijana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili nataka kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Hussein Mohamed Bashe kwa jinsi alivyosimamia hizi Bodi za Mazao. Napongeza kwa sababu bodi hizi zimeweza kufanya kazi kwa manufaa ya wakulima. Kwa mfano, bei ya *cocoa* imeweza kufika kutoka kilo 3,000 mpaka kilo 34,000 katika soko la dunia. Huu ni msingi mkubwa, kwa hiyo tukikazania hizi bodi hata kwenye mazao mengine, basi wakulima wetu wataendelea kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sioni kama kuna mtu anabisha hapa kama kilimo siyo muhimu kwa sababu naamini wote hapa tunakula ndiyo maana tuko hivi. Bila kula huwezi. Kwa hiyo, kilimo ni uti wa mgongo kama alivyosema. Kwa hiyo, kila namna tutakayoweza nchi hii tujitahidi kilimo chetu kiwe mbele tuweze kupata mazao zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naweza kushauri Serikali iweze kushirikiana, yaani Wizara hii ya Kilimo ishirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara kuongeza thamani katika mazao. Kwa mfano, kuna watengenezaji wa *chocolate* kule Kyela wanaita *Mababu Chocolate* wamejiongeza na wanauza *chocolate* zinauzwa dunia nzima. Kwa hiyo, tunaweza kupata zaidi. Wizara hizi zishirikiane ili kuwapa wananchi wale ambao wanajitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, nataka kuzungumzia hii dhahabu ya kijani (parachichi) ambayo kwa kweli *sometimes* imeshatokea habari kwamba parachichi zinarudishwa kwani zimeonekana zina viuatilifu sumu. Kwa hiyo, tuwe makini zaidi. Vilevile kama tungeweza kutenga eneo maalum kama vile Njombe, tukasema huku tutalima parachichi za kilimo ikolojia hai ili kuepusha na kukuza thamani kwa sababu parachichi zinahitajika sana na parachichi zetu zina thamani kubwa. Kwa hiyo, naomba ushauri huo utiliwe maanani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hayo, mimi naridhika kabisa na utendaji wa Waheshimiwa Mawaziri hawa. Nasema tu tuendelee kuwapa ushirikiano na nchi yetu itapanda kutokana na kwamba tumeweza kuongezewa bajeti kubwa kama hii. Kwa hiyo, mwakani tutapata zaidi ya hapo. Wote nataka mniombee dua nirudi tena humu Bungeni mie. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asha Abdullah *a.k.a* Mshua. Namwita sasa Mheshimiwa Anatropia Theonest na Mheshimiwa Rehema Juma Migilla ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia Wizara ambayo kama nyingine ni *catalyst*, basi hii ndiyo msingi na ndiyo mustakabali. Kwa sababu ukiangalia katika nchi zinazoendelea au nchi kama za kwetu, kilimo ndiyo uti wa mgongo, kilimo ndiyo kinaajiri watu wengi na kilimo ndiyo kinagusa. Ukiweza kuchechemua na kukuza kilimo kama inavyostahili, utakuwa umegusa watu wengi tofauti na Wizara nyingine pengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujiulize ni kwa kiwango gani tumeweza kulima? Ni kwa kiwango gani tumeweza kusimamia dira, dhima, mienendo na matarajio? Mheshimiwa Bashe ameeleza vizuri sana, napitia dira yake amesema, "Tujilishe sisi na tuwalishe wengine" ambayo ndiyo Dira ya Wizara. Nataka

kumwuliza ni kwa kiwango gani tumejilisha sisi na tumewalisha wengine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu ziko wazi, ameeleza kwamba kilimo kimeongezeka. Hizo ni takwimu ambazo zipo ambazo kilimo kimetoka 3.3% kwa mwaka 2020, kuja 4.2. mwaka 2022. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika uchangiaji wa Pato la Taifa tunaona kwamba kuna *slight change* kutoka 26.2% kuja 26.5%, lakini pia na ajira na vitu kadha wa kadha pamoja na namna ambavyo kimekua au fedha zinavyoongezeka katika kuuza nje: Sasa swali, je, tumefika tulikotaka kwenda? Tumefika kwa kasi tunayoenda nayo? Kuna kitu hakiko sawa? Ni wapi tunapaswa kuongeza nguvu? Haya ni maswali ambayo nayauliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, amesema tumeongeza kilimo, leo tumezalisha kutoka tani 17,000 kuja zaidi ya tani 20,000, mkaonyesha kwamba ongezeko ni *slight change,* lakini katika hilo ongezeko ni asilimia ngapi? Akaeleza kwamba ni asilimia mia moja na nimeandika hapa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaenda kwa takwimu ambapo asilimia inayoongezeka unaona kwamba haijawa tofauti sana na mwaka 2023 ambayo ilikuwa ni 114%. Leo tunaenda asilimia kama 120% ambayo unaona kwamba siyo ongezeko kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi *concern* yangu imekuwa tusiishi kwa kula tu, kwamba mmesema tunazalisha kwa ajili ya kulisha nchi tu, lakini *surplus* ikiwa ni tani 4,000,000 na kadhaa, unaona kwamba ni kiwango kidogo sana kutoka tani 16,390 mwaka 2023/2024 na ziada ya tani 4,000,000 na kuendelea. Takwimu zinaeleza kwenye hotuba yake, lakini unaona kwamba ni mchango mdogo sana ambao unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika huo mchango mdogo, ni juhudi gani zimejitokeza? Nimepitia hotuba ya Mheshimiwa Waziri nimeona akieleza matarajio ambayo amekuwa nayo, ni

matarajio makubwa tu ya kuongeza kilimo, akieleza kwamba kipaumbele chake cha kwanza ni kuongeza *productivity*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia wakaonyesha *productivity* imekuwa ni ndogo kwa miaka iliyopita na hasa ukilinganisha tunavyozalisha na tunavyovuna ni vitu viwili tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona kwamba nguvu kubwa wakulima wanaitumia kwenye kuzalisha, wanaitumia kwenye kulima eneo kubwa, lakini *output* yake inakuwa ndogo. Nimechukua mifano hapa kadha wa kadha, na mfano mdogo katika mpunga, katika ekari moja tulikuwa tunapata tani 1.25, lakini kumbe *estimate* tungeweza kupata tani nne na hapo hatujafika. Ukiangalia korosho ambayo sasa katika ekari moja unapata tani 0.5, lakini matarajio ni kwamba tunaweza kupata katika ekari moja zaidi ya tani mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, kahawa katika ekari moja leo tunachokipata ni 0.3 wakati unaweza kupata mpaka 1.5 *per acre*. Unaona kwamba nguvu bado ipo, lakini sasa ni kwa nini hatuwezi kuzalisha vya kutosha? Jitihada zinaonyesha zitapatikana kwenye mbegu kwamba tukipata mbegu bora tunaweza kuzalisha kwa ubora, lakini sasa unaona mbegu bora bado zinazalishwa kidogo. Ameonyesha kwamba, sasa mbegu ambazo leo zinapatikana ni tani zaidi ya 68,000 lakini *estimate* tunapaswa kupata tani zaidi ya 127,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua shida yetu ni nini? Ni kwa nini hatuzalishi zaidi? Tunaweza kuwa tunalima eneo kubwa, lakini kama tuna mbegu ambazo hazina tija, matokeo yake yanakuwa ni madogo. Kwa hiyo, sasa tunajua tukiwekeza zaidi kwenye kuzalisha mbegu zilizo bora, hata *output* itakuwa ni kubwa. Kwa hiyo, kile ambacho mnalenga kukifanya kitakuwa kimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini wakati mwingine vipaumbele havikamiliki? Ni kwa sababu wakati mwingine bajeti inayokuwa imetengwa haiendi. Sasa ukiangalia bajeti, tukija

kwenye ku-*scrutinise* bajeti, tunaona imeenda kwa 53% *point something* takribani 54%. Tumekuja hapa tukapanga kwamba mnapeleka zaidi ya shilingi bilioni 900 na kadhaa lakini zilizoenda hazijatimia. Unaona bajeti ya maendeleo, bajeti ya matumizi *(OC)* bado ni hela ambazo haziendi kule chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama bajeti haitoshi, tunategemea *output* au *productivity*, au mazao yenye kuwa na tija! Bila shaka hatuwezi kupata kwa wakati. Moja kati ya kipaumbele kingine, mkasema ni ajira zenye staha. Ameeleza vizuri Mheshimiwa Mbunge aliyemaliza sasa hivi. Kusema ukweli jembe la mkono siyo ajira yenye staha. Jembe la mkono ni ajira inayomtesa mkulima, anatumia muda mwingi, nguvu nyingi, kazi nyingi, akili nyingi lakini *productivity* na anapata nini kwa kweli hairidhishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunahitaji kuweka hela ya kutosha, tunahitaji kuweka nguvu ya kutosha ili kuona tunapata hiyo *output* pamoja na kuimarisha upatikanaji wa masoko. Hili hususan niliongelee mfano kwenye suala la kilimo cha *vanilla*. Wakazi wa Mkoa wa Kagera waliingia kwenye kilimo cha *vanilla* kwa nguvu kubwa sana, lakini wameishia kutapeliwa na bado matumaini hayakuwepo ya kutosha ya kuhakikisha tunapata soko la *vanilla* yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii naomba wakati wa kumalizia Mheshimiwa Waziri atoe kauli, ni nini hatima ya wakulima wa Mkoa wa Kagera kuhakikisha wanapata soko la hilo zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuongelee Mkoa wa Kagera na mikoa mingine ya pembezoni, walianzisha masoko ya kimkakati na hapa nataka Mheshimiwa Waziri aeleze, nami nitashikia shilingi. Nini hatma ya masoko ya Murongo, Tarime na Mutukula pamoja na maeneo mengine ambako kuna fedha ya Serikali. Fedha iliwekwa na masoko yametelekezwa. Nitashika shilingi hususan kujua hatima ya masoko hayo ambayo yangeweza kuchechemua upatikanaji wa masoko ambayo leo ndiyo tunayaongelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulima ni kazi ya wakulima, lakini upatikanaji wa masoko sasa ni kazi ya Serikali kwa sababu ninyi mna *network,* mna uwezo, mnaweza kuwasaidia wakulima kufikia hiyo azma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuimarisha matumizi ya TEHAMA. Ni kwa kiwango gani wananchi wanaweza kupata taarifa ya soko? Ni kwa kiwango gani wananchi wanaweza kuuza kutoka kwenye maeneo yaliyopo na pia kulima kidigitali? Tumeona juhudi kadha wa kadha ambayo ni pamoja na kuboresha mbegu na Maafisa Ugani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine wameeleza hapa, nami nataka niliongelee kuhusu uhaba wa Maafisa Ugani. Unawezaje kuboresha kilimo bila kuwa na watu *on the ground* ambao wanaweza kusimamia kuhakikisha wakulima wanazalisha na kupata tija tunayoitaka? Wameeleza kwamba upungufu ni zaidi ya 30% na zaidi, upatikanaji wake ni 35%. Unaweza uka-*equate* ukajua upungufu ni kiasi gani. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, lakini bado tuna kazi kubwa hasa *post-harvest loss,* mazao mengi yanapotea wakati wa kuvuna. Pia kutenga 10% ya *National Budget* kwenda kwenye kilimo. Hiyo ndiyo *Maputo Protocol* walivyoongelea. Ni kwa kiwango gani tunaenda kufikia hapo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia. Namwita sasa Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, atafuatiwa na Mheshimiwa Katani Ahmadi Katani. Hayupo Mheshimiwa Rehema Juma Migilla, basi Mheshimiwa Katani tuendelee.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa sisi wakulima wa korosho, mimi nimezaliwa kwenye korosho. *Transformation* ya zao la korosho nimeanza kukua nayo nikianza kutambaa mpaka natembea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumza, Mheshimiwa Rais ameendelea kutoa pembejeo za korosho bure. Leo tunapozungumza, Mheshimiwa Rais amekubali kurejesha fedha ya *export levy,* yote irudi kwenye Tasnia ya Korosho. Leo tunapozungumza, Mheshimiwa Rais ametoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 10 kwenda kutengeneza kongamano ya viwanda pale Maranje, Nanyamba. Kwa sisi wakulima wa korosho hakuna tunachoweza kumwahidi Mheshimiwa Rais zaidi ya kuendelea kumtafutia kura za mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya sekta ya kilimo, lakini napata mashaka makubwa sana tunaposema leo bajeti ya Wizara ya Kilimo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 970, kwenda shilingi trilioni 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunapozungumza, ukisoma taarifa ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, wamepokea 53.8% ya bajeti ya msimu uliopita mwaka 2023/2024. Tumebakiza mwezi mmoja tu tunakwenda mwaka mpya wa fedha. Maana yake ni kwamba 46.2% hawajapata fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutashindwa kuwapima watu hawa kwa *mission* na *vision* walizokuwanazo kwa sababu fedha wanayoiomba na kinachokwenda ni tofauti. Tutakapofika tarehe 13 Juni, hii bajeti tuliyoizungumza mwaka 2023/2024 inakwenda ukingoni. Leo tunapozungumza, wamepata shilingi bilioni 522. Sioni uwezekano wa kupata shilingi bilioni 448 kwa kipindi kilichobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Kilimo kwenye Taifa hili, ndiyo inaajiri watu wengi. Sekta ya Kilimo kwenye Taifa hili ndiyo inayofanya, leo wanafunzi wana shida ya vyoo, kwa sababu uzalishaji unaongezeka, watu wanazaliana ndiyo maana shuleni

kunatakiwa vyoo. Kunatakiwa watoto wapate chakula. Leo kama kuna shilingi bilioni 448, haijaenda na tumebakiza mwezi mmoja, tutashindwa kuwapima Waheshimiwa Mawaziri hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukiitazama Bajeti ya Wizara ya Maji, fedha zilizokwenda na kilichopangwa, havilingani. Tutapata shida ya kuwapima watu hawa. Dhamira ya Mheshimiwa Waziri ni njema sana, lakini kwa uendeshaji huu wa fedha ya upatikanaji wa fedha huu, tutashindwa kukaa sehemu salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakulima wa korosho, tunampongeza Mheshimiwa Waziri kwanza, kwa kutoa ule ulazaji wa *box* kwenda kwenye *TMX* na kwenye jambo hili awe na *comfort*. Nimesema mimi nimezaliwa kwenye korosho, *transformation* hii aliyoifanya, mwaka 1998/1999 mimi nilikuwa mpimaji wa korosho *godown*. Hiki alichokifanya Mheshimiwa Waziri cha kwenda kwenye *TMX*, tulikuwa tunafanya nyuma kwa namna nyingine. Wahindi wanakuja kwenye Chama cha Msingi, huyu anaweka bei yake na mwingine anaweka bei yake, anayeweka bei ya juu ndiyo tunamuuzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amefanya *transformation* ya kisasa. Tunakwenda kwenye *computerization* huko lakini kilishafanyika nyuma. Usipate shida na maneno ya kwenye mitandao, ukiona umerusha jiwe msituni ukasikia mtu analia, ameshatandikwa huyo. Haya yanayozungumzwa kwenye mitandao, kuna wadau wa korosho nimewaona kwenye mitandao. Impe *comfort* Mheshimiwa Waziri, sisi wawakilishi wa wananchi tunajua anachokifanya. Tunajua dhamira yake ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Fanya kazi yako vizuri Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maneno kwamba unaingilia Tasnia ya Korosho, unaingilia vyama vya ushirika. Wewe ni Waziri mwenye dhamana ya Kilimo, usipate hofu na maneno. Usipomsaidia mlaji, au usipomsaidia mkulima, hali itakuwa mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo pembejeo hizi ambazo Wizara inatoa bure ni zaidi ya shilingi 66,000 mfuko mmoja, lakini

pembejeo hizo ukisema Serikali msiingie, zinaweza kuuzwa bei yoyote. Mwaka 2023 tumeona wakati Mheshimiwa Waziri anarudisha bei ya mbolea, zilishafika shilingi 100,000 na kidogo, akajaribu kusimama, akahakikisha mkulima anapata mbolea kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo akitokea mdau akasema yeye ni mdau, akaandika huko; "Ogopa Waziri ku-*intervene*", wakulima wa Taifa hili wataumia. Ipo shida kwenye Sheria zenu za Ushirika, kuna wakati mnasema wanasiasa wasiingie kwenye ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hii ndiyo wanapokosea bila kufahamu ushirika wenyewe ni Sera na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambayo Waziri wake ni wewe. Sasa usikae ukawa na uoga uoga. Fanya *intervention* kwenye Sekta ya Kilimo, popote unapoona hapa mlaji, mkulima anakwenda kuathirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wanaolima ufuta na mbaazi, Serikali mmefanya *intervention*. Wameshaingia makubaliano ya mikataba na nchi zinazonunua mbaazi na ufuta. Mimi nashauri sana, tunapokwenda kwenye msimu wa korosho wa mwaka huu, tuweke bei dira, wakulima wajue bei dira ya korosho ili mnunuzi yeyote anayekuja, asinunue korosho chini ya bei dira ambayo Serikali mtaitangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutakapokwenda kwenye minada, kama mnunuzi hafiki bei hiyo, tusiuze korosho, na jambo hili mnaliweza. Kama leo mnaweza kununua mahindi *NFRA* mnayahifadhi, sidhani kama kuna mahali mtashindwa ikitokea kwamba bei dira ambayo mtaiweka *indicative price* kuna watu wanaweza kuchezesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwahi kukaa kwenye kikao cha tathmini ya korosho. Tukiwa kwenye kikao kile miongoni mwa mambo makubwa aliyoyafanya ni kuunda Tume ambayo ilikuwa huru na 98% ya maoni yaliyotolewa na Tume ni maoni sahihi yanayotoka kwa wananchi. Bodi yake ya Korosho ina madudu, ameyaona, watumishi wa Bodi ya Korosho amesikia madudu wanayoyafanya. Kama mtumishi mmoja anaweza kusaini

*documents* za vibali akiwa meneja tu wa sehemu fulani na bado wakawa naye, maana yake Serikali iko kimya, wanashiriki wizi na hujuma hizo, yaani Mheshimiwa Waziri na Bodi yake wanashiriki hujuma hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti iko wazi, mtu anasaini *document,* siyo afisa masoko wa bodi tena akiwa sehemu nyingine na wamekaa kimya mpaka leo na siyo kwamba hawajui. Ripoti inaeleza, mtu amechukua fedha za wakulima huko Katavi ili aagize mabomba sijui vitu gani; ilhali wakulima hawajapewa na ni mtumishi wa Serikali. Ripoti inaeleza mtu kuwa amechukua korosho bila vibali, korosho zinakamatwa, kuna ushahidi, kuna *voice note* wakitaka tutawapa, hizo *document* tunazo kama hawana ushahidi; lakini bado wanaendelea kukaa na mtu huyo kwenye tasnia ya korosho. Itakuwa ni Serikali ya ajabu sana, itakuwa ni Bodi ya Korosho ya ajabu sana; hujuma zinafanywa, *conflict of interests* inaonekana na bado wanakaa bila kuchukua hatua, ni Serikali ya aina gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu yuko kwenye tasnia, wakulima wanaumia. Ukisoma sheria waliyoitengeneza wenyewe Bodi ya Korosho, kwamba, kama unakamata korosho ambazo hazina *documents* zimepelekwa mahali kinyume na utaratibu faini ni kati ya milioni tano mpaka milioni 500

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Katani, muda wako umekwisha kabisa…

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite sasa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia bajeti hii muhimu na ya kihistoria ya shilingi trilioni 1.2. Awali ya yote

nimshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na uzima, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya kwa Taifa letu na miradi kedekede aliyotuletea ndani ya Jimbo la Hai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kweli nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Bashe, kwa kweli kiti kimepata mwenyewe kwa namna ambavyo anakimbizana na miradi na kwa namna ambavyo anasimamia sekta hii pamoja na wasaidizi wake, Mheshimiwa Naibu Waziri, kule kwetu tunamwita Mzee wa Makeresho, sasa amalize na lile Bwawa la Makeresho ili kazi iende vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia kaka yangu Naibu Katibu Mkuu, ndugu yangu Gerald kwa kazi kubwa anayoifanya. Nimpongeze pia Mkurugenzi wa Umwagiliaji, ndugu yangu Ray kwa kazi nzuri pia anayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza tangu nimekuwa Mbunge leo ndiyo namsikia Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Taifa, kwa kazi aliyoifanya, nitaeleza baadaye. Kwa mara ya kwanza nilikataa humu humu kwamba sitampongeza mpaka atakapokuwa amemaliza matatizo ya ushirika. Sasa kwa kuwa ameanza kazi hiyo vizuri na yeye nampongeza pamoja na watumishi wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna sababu ya kuipongeza taasisi hii na wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Mwaka jana walinipa miradi mingi sana Mheshimiwa Waziri kule Hai na watu wa Hai wakashukuru sana, lakini bado haijakamilika na haijakamilika kwa sababu pia hawajaletewa fedha. Fedha walizoombwa zimekuja kwa 53%, sasa hizo nyingine ziko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe tu Mheshimiwa Waziri, miradi ile ime-*troam*, walitwambia inafanyiwa *feasibility* nimeiona. Bwawa la Borutu nimeliona hapa, Makeresho nimeona, Kikafu chini angalau wameitangaza jana, nampongeza sana na namshukuru sana kwenye hili. Mwera na Kalali wameyatangaza. Bwawa la Bwana Mganga bado, Bwawa la Mtambo kule kwenye

Skimu ya Mtambo wameitangaza, nawashukuru sana; Ismaili bado hawajatangaza, lakini ilikuwa kwenye bajeti na Longoi Mapacha bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara aliyoniahidi mwaka jana ya kutoka Kwa Sadala kwenda Longoi ambayo inakuja kwenye Soko la kwa Sadala na ikizingatiwa Soko la kwa Sadala tayari Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan ameshatupatia shilingi bilioni 11.2. Sasa nimshauri Mheshimiwa hii miradi viporo aitangaze, nitamsaidia kwenda kudai. Mimi nakodisha tu mabasi matatu ya hao wananchi wa Hai, tunakwenda pale Hazina tunaimba nyimbo za ukombozi na Mheshimiwa Mwigulu atatoka tu ili atupe hizi fedha. Kwa hiyo yeye atangaze, asiogope, kazi ya kwenda kuzidai nitamsaidia, kwa sababu yeye jukumu lake ameshalifanya? Asipoitangaza hii miradi maana yake hana *justification* ya kuidai. Yeye atangaze halafu aone namna nitakavyomsaidia kwenda kuidai hii miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nimshukuru sana kwa jambo la kihistoria ambalo amelifanya kuhusiana na mradi wetu wa lile Soko la Mula. Sasa na hili lisiwe tena akaweka huku likavuka mwaka, hili likiwezekana tukishapitisha bajeti yake hapa, na tunapitisha hii bajeti; atangaze kujenga hili soko la kisasa, namna ya kudai nitamsaidia, nitamsaidia vizuri kwenda kudai kule Hazina, tutakwenda kushinda pale siku tatu tunaimba nyimbo za ukombozi mpaka watoe hela. Kwa hiyo nimtie moyo na nimwombe aendelee kufanya kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nililosema hapa ni kuhusu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Tanzania. Nimepiga kelele sana na ushirika na lengo nililokuwa nataka twende kwenye ushirika ni hapa tulipofika. Leo Wilaya ya Hai na nachukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wa Ushirika wa Wilaya ya Hai pamoja na Afisa Ushirika wa Mkoa wetu, hongereni sana, wamenielewa Mheshimiwa Waziri. Kwa mara ya kwanza tumesaini mkataba hadharani tena umeandikwa kwa Kiswahili. Tukachukua ule mkataba tukawapa vijana wetu walioko Dar es Salaam, tukawapa wananchi na ukatangazwa kwa uwazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaenda kufanya ziara na Mrajisi wa Vyama vya Ushirika Taifa kwenye chama kimoja baada ya kingine na mwisho tukaenda kusaini mkataba mchana kweupe, vyombo vya habari vikiwepo, wananchi wakiwepo. Hiki ndicho tunakitaka siyo ile biashara eti Mrajisi wa Ushirika anakwenda peke yake na watu wake wawili kusaini mikataba ya hovyo. Sasa niombe, najua shamba la *Silver Bay* mkataba unakaribia kwisha, najua kule Makoa bado, najua na maeneo mengine yanakuja, utaratibu uwe ni huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mashamba ni ya kwetu watushirikishe. Ndugu yangu amesema hapa kwamba sheria inatubana, sheria inasema tusiwaingilie, lakini tusinyimwe haki yetu sisi kama viongozi kujua. Nashukuru sana Wilaya ya Hai sasa hivi Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji wanakwenda kwenye vikao. Huo ndio ushirika tunaoutaka, wa uwazi na ukweli ili turudi kule tulipotoka ambapo ushirika uliweza kusomesha watoto wetu, ushirika ukajenga Chuo cha Ushirika Moshi, ushirika ukajenga barabara ya kwenda Kyalia kwa lami na kwamba fedha ya ushirika ndiyo imetunyanyua sisi. Kwa hiyo tunapolilia ushirika watuelewe na lengo letu lilikuwa ni hapo. Hongera sana kwa Mrajisi wa Ushirika kwa kazi kubwa aliyoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kushauri kwa ujumla. Mheshimiwa Waziri amefanya kazi nzuri sana, kwenye *indicator* zote za kupima *performance* amevuka. Nilikuwa naangalia upatikanaji wa chakula, nimeona amevuka, ameweza, chakula kwa ajili ya kula kipo, sasa aanze kuwaza kuhusu chakula kwa ajili ya biashara. Tutoke huko sasa tuanze kufanya biashara ya kilimo ya uhakika na siyo hii tunayoifanya. Kwenye hili anaweza kutengeneza *zones,* kwamba kama ukanda huu wanakuwa ni wataalam wa kulima zao fulani awape *indicator* za *performance* watu wake, awape vigezo, bwana wewe kwenye wilaya fulani, Wilaya ya Hai wewe ni mtaalam wa mbogamboga, wewe ni mtaalam wa kilimo cha kahawa, tunataka tani kadhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mkuu wa wilaya akimegemewa kipande chake na kwa bahati nzuri wako hapa, na Mkuu wangu wa Wilaya Amiri Mkalipa yuko hapa na sisi Hai

tupe. Malengo yawe kwamba nenda kazalishe kwa tani kadhaa, mambo ya umwagiliaji, hili eneo hili la umwagiliaji lilipo hapa la hekta 727,000 ni ndogo sana kwake. Amekwishapewa mashine za kuchimba visima huko, akipambana kwenye hili tukawa na eneo lote la umwagaliaji ambalo limepata maji, ana uwezo wa kuwaambia wataalam walioko kule kwamba nendeni mkatuzalishie. Kama ni mahindi kwa tani kadhaa, kama ni maharage tani kadhaa ili tuwe na chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *precautions* mwaka jana hapa nililizungumzia tena eneo hili. Hivi wanaposema kwamba tuna chakula tani kadhaa huwa wanaweka na chakula cha mifugo? Kwa sababu leo Mheshimiwa Waziri wanapozalisha wanasema wana mahindi yanayotosheleza mahitaji ya chakula, lakini hawaweki kwamba mahindi hayo hayo ndiyo yanayokwenda kutumika kutengeneza chakula cha kuku, ndiyo yanayotumika chakula cha mifugo. Sasa lazima waweke wakijua kabisa mahitaji halisi ya Watanzania ni yapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa haraka haraka kwa sababu kengele imegonga, naomba sana habari ya mbolea tafadhali ije kwa wakati…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha, naomba uhitimishe…

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** …pamoja na mbegu, nimeona wameweka hapa, watusaidie, kwenye hizi mbegu kuna mbegu nyingine feki, zimeanza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja, mengine nitaandika kwa maandishi, nitawasilisha na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu atakuwa Mheshimiwa Benaya Kapinga.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Nianze kwa kuunga mkono bajeti hii nzuri sana na ya kihistoria katika nchi yetu. Nitachangia kwenye maeneo matatu, eneo la ushirika, eneo la soko la mazao na eneo la ongezeko la bajeti yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni muumini wa ushirika. Nchi yetu hii imepitia katika historia ndefu sana kuhusiana na suala hili la ushirika. Kuna mahali ushirika ulifanya vizuri sana, lakini kuna mahali ushirika ulipoteana kweli kweli. Leo hii nafurahi kwa uwepo wa Waziri, Mheshimiwa Bashe angalau sasa kama nchi, wote kwa pamoja tunazungumza vizuri kuhusu ushirika. Nakumbuka wakati tunaanza Bunge hili baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walikuwa hawataki kusikia kuhusu suala la ushirika, lakini leo hii wote tunakwenda kwa pamoja kuhusiana na suala la ushirika. Niseme kiukweli kabisa upele umepata mkunaji na mkunaji mwenyewe ni Mheshimiwa Bashe. Hapa niungane na usemi ule wa Kiswahili wanasema mzigo mzito mkabidhi nani? Mnyamwezi, yule pale. Amekabidhiwa mzigo na ameufanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna hii Tume yetu ya Maendeleo ya Ushirika na jukumu mojawapo la hii Wizara ya Kilimo ni kusimamia maendeleo ya ushirika. Sasa katika utaratibu wa uratibu na utekelezaji wa ushirika hivi karibuni pametokea na maelekezo kwamba hawa wana ushirika wajibu wao ni moja kwa moja kwenye Tume ya Ushirika. Ni jambo zuri japo kwa mtazamo wangu tulikuwa na Sera hii ya Ugatuaji, kwamba haya mambo sasa yafanyike kule chini. Sasa unaposema watu hawa wa ushirika wajibu wao uwe moja kwa moja kwenye Tume naona unaenda tofauti na suala hili la ugatuaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale kwenye ushirika, kwenye kilimo tuna Maafisa Kilimo Wilayani, tuna Mkurugenzi pale Wilayani lakini tuna Wakuu wa Wilaya kule wilayani. Kwa bahati mbaya sana kupitia hili neno la kusema huyu afisa ushirika wajibu wake uko moja kwa moja kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika, wako baadhi ya hawa maafisa ushirika hawatoi heshima, wanatoa kiburi na maneno ya dharau kwa hizi taasisi ambazo ziko pale chini zinazosimamia kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako maafisa ushirika wanasema mimi siwajibiki kwa mkurugenzi, ataniambia nini? Mimi siwajibiki kwa mkuu wa wilaya, Mbunge ataniambia nini? Maneno haya si mazuri na kama kweli na sidhani kama ni nia ya Wizara ya Kilimo kuwafanya hawa maafisa ushirika kuongea lugha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeona kuna marekebisho ya sheria. Kama eneo mojawapo tunapaswa kuliangalia ni eneo la lugha hizi, lugha hizi zinawapa jeuri hawa maafisa ushirika, hawana nia nzuri ilhali ushirika unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikwambie kwamba ushirika ndiyo fimbo ya mnyonge, ushirika ndiyo fimbo ya sisi wanyonge, hivyo tuunganishe nguvu ili twende mbele, lakini tukiuharibu kwa maneno ya hawa maafisa ushirika hatimaye tutapoteana na hatutaona tija kwenye ushirika. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Bashe, hizi lugha zinakwaza wale ambao tumewapa jukumu la kusimamia hiki kilimo kule chini. Huwezi kuniambia mimi siwajibiki kwa mkuu wa wilaya, sasa unawajibika kwa nani? Huwezi kuniambia mimi siwajibiki kwa mkurugenzi na nikwambie kwenye maeneo mengine wana nguvu kweli kweli hawa maafisa ushirika, wana nguvu kweli kweli kiasi cha kumfanya mkurugenzi asifanye chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri atoe maelekezo, ikionekana kwenye sheria kuna namna yoyote basi waje na kanuni ili hawa watu wawajibike. Mbona tuna *TARURA* pale ambao wana heshima nzuri sana kwa mkuu wa wilaya pamoja na halmashauri na wengine ambao wamegatuliwa haya madaraka na wanafanya vizuri? Kwa nini maafisa ushirika waoneshe kiburi cha namna hiyo? Hilo lilikuwa eneo mojawapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni eneo soko. Nimeona jitihada nzuri ya wizara kama jukumu lao la kuratibu na kutafuta masoko wanalifanya vizuri. Sasa iko shida na hofu kwenye baadhi ya mazao likiwemo zao hili la mahindi. Sisi wakulima wa Mbinga tumelima vizuri sana, tumelima vizuri mwaka jana, tumelima vizuri mwaka juzi na tumelima vizuri mwaka huu.

Tuishukuru Serikali kwa miaka hii miwili nyuma mazao yetu yaliuzika vizuri sana, lakini hivi ninavyoongea bado wakulima wana mazao ya mwaka jana, hayajamalizika kuuzwa; lakini bado mazao ya mwaka huu yameshakomaa na baadhi ya wakulima wameanza kuvuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo iko hofu, kwamba masoko ya nje ya nchi yetu yamezuiwa. Sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa aondoe hii hofu kwa wakulima, kwamba ni kweli yamezuiwa? Kwa nini mazao haya hayauziki? Nimeambiwa sijui kuna *procedure, procedure* nyingi. Kwa hiyo niombe, kama ni kweli shida ni *procedures,* basi tuziondoe hizo *procedures* au tuzirahisishe ili mkulima huyu aliyelima apate tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema hapa kwamba, wakulima wetu hawa wanakimbilia kulima mazao wakiona yananunulika, yasiponunulika hawalimi na wasipolima nchi yetu itaingia kwenye shida zaidi maana njaa itatupata. Niombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hapa awaambie wakulima wa Mbinga kwamba hajazuia mpaka wowote. Wakulima hawa wawe huru kuuza mazao yao; eneo la pili hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini eneo lingine ni kuhusu hili ongezeko la bajeti. Naishukuru sana Serikali kwa nia njema kabisa hii ya kuongeza bajeti. Tumeshuhudia hapa kwamba huu ni mwaka wa tatu mfululizo bajeti inaongezeka. Tulitoka kwenye bilioni 200 tukaja kwenye bilioni 900 na leo hii tupo kwenye trilioni 1.2. Hongera sana kwa Serikali ya Awamu ya Sita, hongera sana kwa Mheshimiwa Rais kwa nia hii njema ya kumkomboa mkulima, lakini hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri. Najua hizi fedha haziji hivi hivi, zinakuja baada ya yeye kuonyesha mipango ya namna gani anakwenda kuzitumia, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa shida hii taarifa inafurahisha sana kusikia kwamba bajeti imeongezeka, lakini inasikitisha kusikia fedha zilizoenda huko kwenye Wizara hadi leo tumeambiwa kuwa ni 53% tu, hii ndiyo ilikwenda Wizara ya Kilimo. Mimi ni shuhuda mzuri sana nimeona mipango mizuri ya Mheshimiwa Waziri hapa,

ni mizuri mno, hata wenzangu wamesema. Tunampimaje Mheshimiwa Waziri ikiwa amekuja na mipango mizuri ya kuisaidia nchi hii, ikiwa amekuja na mipango mizuri ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, kwamba akitoe kilimo kutoka hatua tuliyokuwanayo kwenda hatua nzuri zaidi halafu fedha haiendi? Jambo hili siyo zuri, siyo zuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaitaka Serikali itoe fedha kwa namna tulivyyopitisha hapa Bungeni. Haiwezekani mipango hii ikaenda kutekelezeka? Hapa ningeomba waziri anapokuja kuhitimisha aniambie Mradi wangu wa Umwagiliaji Litumbandyosi unakamilika lini? Nimepekua pekua hapa siuoni sasa sijui ndiyo huu umeondoshwa kwa sababu ya hii ya kibajeti ama la…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya, muda wako umekwisha.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni ambao wapo humu ndani na tuwatambue.

Kwanza ni wageni 19 wa Mheshimiwa Mhandisi Samweli Hhayuma, wanafunzi kutoka *UDOM,* karibuni sana Bungeni. (Makofi)

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, rafiki zake kutoka Dar es Salaam, *Network of Special Needs*, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wageni ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo, wapo wanafunzi wanne kutoka Chuo cha Mipango Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 100 wa Chuo Kikuu cha Sokoine kutoka Mkoa wa Morogoro, karibuni sana kwenye ziara ya mafunzo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo nimkaribishe Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, ana jambo, ana taarifa ya kutoa, karibu. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na kwa heshima ya Bunge lako naomba nitoe Taarifa kwa Bunge lako Tukufu na kwa umma kuhusu Mwenendo wa Kimbunga cha Hidaya katika Bahari ya Hindi Mashariki mwa Pwani ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania leo tarehe 3 Mei, Saa tatu asubuhi, Mjini Dar es Salaam imetoa Taarifa ya Mwenendo wa Kimbunga cha Hidaya kilichopo katika Bahari ya Hindi Mashariki ya Pwani ya Nchi yetu. Kimbunga Hidaya kimeendelea kuimarika na kusogea kuelekea maeneo ya pwani ya nchi yetu ambapo hadi kufikia saa tisa usiku wa tarehe 3 Mei, 2024 kilikuwa kimeimarika zaidi na kuifikia hadhi ya kimbunga kamili kikiwa umbali wa takribani kilometa 401 Mashariki mwa Pwani ya Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki Kimbunga Hidaya kimeendelea kuimarika zaidi huku kasi ya upepo ikiongezeka hadi kufika kilometa 130 kwa saa. Mwenendo wa Mifumo ya Hali ya Hewa Baharini bado inaonesha uwezekano mkubwa wa Kimbunga Hidaya kusalia katika hadhi ya kimbunga kamili kwa saa kumi na mbili zijazo huku kikiimarika na kuendelea kusogea karibu kabisa na pwani ya Tanzania. Kimbunga hiki kinatarajiwa kuendelea kuwepo hadi tarehe 6 Mei, 2024 na kupungua nguvu baada ya tarehe 6 Mei, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwepo wa Kimbunga Hidaya karibu na pwani ya nchi yetu unatarajia kutawaliwa na kuathiri mifumo ya hali ya hewa hapa nchini. Ikiwa ni pamoja na kusababisha vipindi vya mvua kubwa na upepo mkali katika baadhi ya maeneo ya Mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani ikijumuisha Visiwa vya Mafia, Dar es Salaam, Tanga, Morogoro na

upande wa pili wa Muungano kwa maana ya Unguja na Pemba, na maeneo ya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipindi vya mvua nyepesi na upepo wa wastani tayari limeanza kujitokeza katika maeneo ya Mtwara. Ongezeko la mvua na upepo mkali unaoambatana na mawimbi makubwa baharini vinaratajiwa kusambaa katika maeneo mengi ya ukanda wa pwani kuelekea tarehe 4 - 6 Mei, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Idara ya Maafa tunaendelea kuwashauri wananchi katika maeneo tajwa na wote wanaojihusisha hasa na shughuli mbalimbali baharini wanashauriwa kuchukua tahadhari kubwa na pia kuendelea kufuatilia na kuzingatia taarifa za utabiri na tahadhari kutoka Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini Tanzania, pamoja na kupata ushauri wa kina na miongozo ya kitaalamu katika sekta husika ili kuweza kujikinga na athari zinazoweza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupitia Bunge lako Tukufu nizielekeze mamlaka za mikoa iliyotajwa kuendelea kuchukua tahadhari ya kiasi cha kutosha na kuendelea pia kutoa taarifa zinazohusiana na mwenendo wa kimbunga hiki ili kuchukua hatua stahiki pale dalili zinazoashiriwa na kuelezwa na Mamlaka ya Hewa zitakapoendelea kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai pia kwa taasisi mbalimbali nchini ikiwemo Kamati za Usimamizi wa Maafa katika Ngazi za Mikoa, Wilaya, Kata na mpaka maeneo ya Mitaa na Vijiji kuendelea kuchukua tahadhari na kufuatilia kwa karibu sana taarifa hizi za Mamlaka ya Hali ya Hewa Nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa tunaendelea kuziomba taasisi za dini na Watanzania wote, kuomba kwa Mwenyezi Mungu ili kwa mapenzi yake ikimpendeza jambo hili liweze kutuepuka katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania inaendelea kufuatilia kwa karibu sana mwenendo wa Kimbunga

Hidaya na athari zake kwa mifumo ya hali ya hewa hapa nchini na itaendelea kutoa taarifa kila baada ya masaa matatu mara kwa mara kila itakapobidi. Nitoe wito kwa Watanzania wote na hasa mikoa ambayo imetajwa katika taarifa hii ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania kuendelea kufuatilia taarifa hizi kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, naomba kutoa taarifa hiyo na kuiwasilisha. *((Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa taarifa hiyo na tunashukuru Mamlaka yetu ya Hali ya Hewa Tanzania imekuwa sahihi katika miaka ya karibuni siku zote, kwa hiyo tuzingatie jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, tutakaporejea tutaanza na Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo atafutiwa na Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe na baadaye atakuja Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maneno hayo nasitisha Bunge mpaka saa kumi na moja kamili.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Tutaanza na Mheshimiwa Bahati Keneth Ndingo, atafuatiwa na Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, ajiandae.

**MHE. BAHATI K. NDINGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kupata fursa hii na nianze kwa kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Wizara hii, kwa kazi kubwa na nzuri ambazo wametufanyia Wanambarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati jana kaka yangu Mheshimiwa Hussein Bashe anasoma bajeti yake yenye kurasa 307, neno Mbarali limetamkwa mara 27. Ukiachilia miradi ambayo iko kwenye *table* zile mbalimbali. Hii ni namna gani inaonesha Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetutendea haki Wana-Mbarali. Ilikuwa ni kiu ya miaka mingi kwa Wanambarali, kuona Serikali yao inawasaidia kuhakikisha inatengeneza miundombinu ya umwagiliaji ili bonde hili sasa tuwe na kilimo kilicho na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiangalia mambo ambayo Mheshimiwa Rais ameyafanya kwa Wilaya yetu ya Mbarali kwenye Sekta hii ya Kilimo, Wanambarali tutaandika historia ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wino wa dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti inayoenda kuisha sisi Wana-Mbarali tumepata miradi nane ya umwagiliaji. Mheshimiwa Rais ametutengenezea miradi nane ya umwagiliaji ambayo mpaka sasa wakandarasi wako *site*, shilingi 98,200,000,000 zimeshuka pale Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hivi ninavyozungumza mabwawa nane wanatafuta mkandarasi mshauri ili aende kuchimba Mbarali. Kubwa zaidi jana baada ya kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, wanakwenda kuongea na mwekezaji ili shamba moja la mwekezaji lirudi kwa wananchi, wakulima wadogo wa Mbarali ambao wamekuwa wakifanya kazi ya vibarua kwa muda mrefu, waende kupata maeneo ya kufanyia shughuli zao. Kwa kweli, tunayo haja ya kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu baada ya kukamilisha miradi hii, tunaamini kabisa Mbarali itakwenda kutulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wewe ni shahidi. Wana-Mbarali 90% ni wakulima, kikubwa tulichokuwa tunataka Wanambarali kuwa na kilimo chenye tija. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia ameonesha kuithamini na kuijali Mbarali kwa muda mfupi aliopokea kijiti. Leo kuna wazee wa Mbarali wamenipigia wanasema Dkt. Samia Suluhu Hassan, *vahongije* sana. Kwa lugha hii ya Kisangu tafsiri yake ni kwamba Wana-Mbarali tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kaka yangu Mheshimiwa Bashe na timu yake, Mheshimiwa Rais hakukosea kuiteua hiyo timu. Wanafanya kazi njema, wamekuwa wanakipenda kilimo na wanapenda wakulima wa Taifa hili, kwa kweli nawapongeza sana, wanafanya kazi njema sana. Kipekee nimpongeze kaka yangu Mndolwa amekuwa ni msaada mkubwa kwenye mambo ya umwagiliaji Mbarali, nimpongeze sana na tunaendelea kumpa ushirikiano wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kikubwa ninachoomba Mheshimiwa Bashe, pindi mazungumzo na mwekezaji yatakapokamilika, tunaomba mashamba haya yakagawiwe kwa walengwa, wakulima wadogo wa Mbarali, isitokee tena ma-*giant* wachache wakajimilikisha. Ili tija ile ambayo Mheshimiwa Rais anayo kwa wakulima wale wadogo ambao hawana uwezo wa kukodi mashamba, kwa muda mrefu wamekuwa wakifanya vibarua, leo wakapate ardhi, wakafanye shughuli yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, tunatambua kazi kubwa ambayo wanaendelea kufanya, ni muhimu sana kaka yangu afungamanishe sekta yake na sekta zingine ambazo zinaingiliana na wakulima. Kwa mfano, sasa hivi kilio kikubwa cha wakulima nchini ni ushuru, lazima awalinde wakulima hawa kwa wivu mkubwa, ashirikiane na TAMISEMI kutoa mwongozo wa namna ya upatikanaji wa ushuru kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano sasa hivi pale Mbarali, wakulima kilio chao simu zinazoingia sasa hivi ni mkulima anatoka shambani, kwenda kupeleka mazao yake nyumbani anatakiwa alipe ushuru. Hapo hapo akitoka nyumbani, anakwenda kulipa mashineni ushuru, akiwa anataka kuuza ushuru, hii ni kinyume na sheria iliyopo ya ushuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kwa sababu hata Mheshimiwa Naibu Waziri alitoa ufafanuzi hapa Bungeni, lakini bado huko hali inaendelea kuwa mbaya. Kwa hiyo, nimwombe Waziri alichukue hili kwa uzito unaostahili kwa sababu wakulima wanatumia gharama kubwa, wakati wa ushuru tusiende tukawakata ushuru mara mbili mbili, siyo sawa na Mheshimiwa Rais alitamka anataka kodi ambayo itakuwa ya amani na ukweli ili tuendelee kubarikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine hata wakulima wa Mbarali wanakumbwa sana na mikopo ya kausha damu, tena kule kinachofanyika kwa sababu taratibu za kupata mikopo kwenye benki bado ni changamoto, mkulima mdogo hawezi kupata mkopo na akipata mkopo hauwezi kumtosheleza. *Maximum* heka moja ya mpunga mpaka imalize kila kitu, siyo chini ya milioni moja mpaka milioni moja na nusu. Leo hii mkulima mwenye heka tano hata akipewa milioni mbili haiwezi kumsaidia, Wanachofanya, wanakwenda kukopeshwa pesa ili wakivuna wapeleke mpunga, kitu ambacho kinawaua wakulima wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe Waziri aendelee kuboresha maslahi ya upatikanaji wa fedha kwa wakulima, hasa wale ambao hawana dhamana. Benki hizi wakulima wanaoweza kupata mikopo ni wale ambao tayari wanazo dhamana na wana

uwezo mkubwa kidogo, lakini kwa wakulima wadogo bado tuna changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, vilevile kwenye suala la kufungamanisha na maeneo mengine, sisi Mbarali kwa safari hii, mbolea zilifika lakini wakulima walipata shida sana kuzifikisha mashambani, barabara zetu za vijijini hazipitiki. Kwa hiyo, tunaomba wanapokuwa kwenye mipango lazima aangalie sekta nyingine ambazo zitachangamsha vilevile kilimo. Leo una mipango mizuri, Dkt. Samia, alikuwa na mpango mzuri sana mbolea zifike kwa gharama nafuu, lakini kutoa mbolea pale walipoziacha mpaka kufika huko mashambani ile nafuu ambayo Mheshimiwa Rais anaiweka inapoteza tija kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuombe ndani ya Serikali, Wizara na Wizara nyingine waone namna maeneo haya ambayo, kilimo kinaendelea waweze kuangalia vichocheo vyote na sekta zote ambazo tutaweza kumrahisishia huyu mkulima aweze kuwa na kilimo chenye tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimwombe Waziri kwamba, natambua pamoja na miradi inayoendelea, tuna miradi mingine na *scheme* nyingine kama 11 ambazo zipo kwenye Mpango wa Serikali. Tayari mshauri mkandarasi ndio wanamtafuta. Niombe sana zoezi hilo lifanyike haraka ili mwaka ujao wa fedha tuone miradi hii ikiwa kwenye bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nishukuru sana kwa kazi kubwa ambayo Wizara hii imeifanyia Mbarali na Wana-Mbarali tunashukuru sana, kwa kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ametufanyia. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Geoffrey Idelphonce Mwambe, atafuatiwa na Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi na Mheshimiwa George Natany Malima, ajiandae.

**MHE. GEOFFREY I. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kusema machache kwenye bajeti yetu hii ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kutupa kheri na afya njema ya kuweza kuwatumikia Watanzania. Kipekee kuwatumikia Wanamasasi. Pia ningependa kuwashukuru sana ndugu zangu za Masasi kwa kuendelea kuniamini, kuniunga mkono, kushikamana na mimi kuhakikisha kwamba, tunaijenga Masasi mpya kulingana na kauli mbiu yetu.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake ya Chama Cha Mapinduzi, kwa juhudi kubwa ambazo wanazifanya kuweza kushirikiana na mimi pale Masasi, kuijenga Masasi mpya na Wanamasasi wanaona. Tumekubaliana na Wanamasasi kwamba mwakani mimi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tuna jambo letu, kwa hiyo wanatuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, ningependa kuchangia sasa kwenye Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Kwanza kwenye bajeti hii, tunaona ni bajeti ambayo inajielekeza kwenye kutatua changamoto ambazo tumekuwa sisi Wabunge tunazisema kila wakati. Kwa hiyo, napenda kuwapongeza sana Mheshimiwa Bashe na msaidizi wake Mheshimiwa Silinde, kwa kusikiliza hoja za Wabunge na hasa sisi Wabunge wa Mikoa ya Lindi na Mtwara na wenzetu wa Ruvuma, hasa kwenye maeneo yanayogusa tasnia ya korosho.

Mheshimiwa Spika, kwenye tasnia ya korosho tumekuwa tukisema siku zote hapa kwamba, bei ya mkulima anayopata kule wakati wa ununuzi siyo bei halisi, haiakisi bei halisi ya dunia. Bahati nzuri miaka 21 iliyopita wakati namaliza *degree* yangu ya pili *(masters)*. Nilifanya utafiti wangu ulikuwa ni kwenye mapato ya mkulima wa korosho, kwa sababu natokea kwenye mikorosho nimezaliwa huko na mimi mwenyewe nalima pia na kwamba kuna changamoto mbalimbali ambazo Serikali ikizirekebisha, basi bei ya mkulima inapanda. Tunafahamu pia kitaalam mapato ya

mkulima huwa tunasema ni mapato ya mara moja kwa mwaka. Wale *ni fixed income earners* (mara moja tu kwa mwaka), ni mtu ambaye unatakiwa kumwonea huruma.

Mheshimiwa Spika, ni sawasawa na sisi au watumishi wa umma, tungekuwa tunapewa mshahara mara moja tu, tarehe 1 Januari unapewa kwa ajili ya mwaka mzima, sijui kama tungeweza kuishi vizuri. Kwa hiyo, tuwaangalie wakulima kwa tafsiri hiyo hiyo ni watu ambao wanapokea pesa yao mara moja tu kwa mwaka. Hivyo basi, tunatakiwa tufanye juhudi zote zinazowezekana kuhakikisha kwamba, bei yao inakua na ikiwezekana iwasaidie kwenye kutatua changamoto za maisha yao.

Mheshimiwa Spika, hili nataka niliseme wazi kabisa, naunga mkono Hotuba yote ya Bajeti na hasa uamuzi wa Wizara ya Kilimo kuja na mfumo mpya wa uuzaji wa korosho na kuachana kabisa na mfumo wa zamani ambao ulikuwa unanufaisha wachache, wajanja na ambao hawahusiki kabisa na kilimo. Matumizi ya *TMX* ndiyo itakuwa suluhisho, tunaamnini itakuwa suluhisho hata kama itatokea changamoto kama Mheshimiwa Waziri alivyozungumza ni majaribio, lazima tujaribu. Naamini kabisa tukiitengeneza vizuri, tukatangeneza kupitia *financial modeling* namshauri Mheshimiwa Waziri kwa korosho pia na mazao mengine, ile bei elekezi tusiitaje kwa kuifikiria kukaa kichwani tu, tutumie *module* ya kiuchumi na kifedha tuweze ku-*calculate* kabisa gharama halisi za uandaaji wa shamba. Nafikiri Mheshimiwa Bahati amezungumza hapa kuhusu gharama za kuzalisha mpunga.

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *opportunity cost, k*wa yeye kuacha kutengeneza *income* sehemu nyingine ameenda kulima kule, pia lazima tumwekee kitu chake kama *incentives*. Pia kuna *profit margin* ambayo anatakiwa aipate yeye kama ilivyo kwenye biashara 15% au 20% ya bei, ile *base price,* pia tunataka huyu mkulima aweze kutanua uzalishaji wake *whether vertically* kwa kuongeza *productivity* au *horizontally* kwa kuongeza *area of production.*

Mheshimiwa Spika, lazima tuwe na *future investment,* tuifuate hii, kwenye gesi na maeneo mengine tunafanya hivyo, hata hizi *computer* tunaletewa huku, wanafanya hivyo hivyo kwenye *pricing system* yao. Mwisho *risk profile,* hawa wakulima wana-*risks* nyingi, *risk* ya kutokuvuna, hali ya hewa kubadilika, mavuno kuharibika njiani, unyaufu, kutolipwa kwa wakati, zote hizo unazi-*compile* unatengenezea sasa *base price,* ambayo tukiichukua ile tukaingiza kwenye *TMX* halafu tukashindanisha kwenye mnada, naamini kabisa wakulima wa korosho watapata fedha za kutosha na kupunguza umaskini kule nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka hata iliwahi kuzungumzwa mara nyingi tu na akiwemo aliyekuwa Waziri wa Fedha wakati ule ambaye kwa sasa ni Mheshimiwa Makamu wa Rais. Alikuwa anahoji Mkoa wa Mtwara kwa mfano, unapata karibu bilioni 600 mpaka 750 za korosho kwa kila mwaka, lakini hali ya wananchi hatuioni? Ni kwa nini hatuoni mabadiliko makubwa kwa wananchi? Ni kwa sababu kuna watu hapo katikati ambao siyo wakulima, wamejitokeza wanapata 40% mpaka 65% ya bilioni 700 zote, ambao siyo watu wa Mtwara. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, sisi Wabunge wote wa Mkoa wa Mtwara, Lindi na Ruvuma ambao tunalima korosho tumekubaliana kwa dhati kwamba amejibu hoja zote za kila siku, twende kwenye *TMX*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri kuhusu suala la *value chain* ya mazao ikiwemo korosho, tuliangalie *holistically* kutoka kwenye kulima, kuvuna, kusafirisha, kutunza *(storage),* kwenda kwenye *processing* ambayo ni ubanguaji na uongezaji wa thamani na mwisho kwenda kwenye soko. Humo kote kuna watu ambao kupitia hata *BBT* na programu nyingine wanatakiwa waingie humo katikati. Kila sehemu tuwe tunajua kwamba, ni watu gani tunahitaji waingie kwenye eneo gani ili tuchachue mnyororo mzima wa thamani na hatimaye kuongeza uwezo mkubwa wa wananchi wetu kupata mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kumshauri Mheshimiwa Waziri, huu Mfumo mpya wa *TMX* lazima tuu-

*promote*. Tengeneza *trade mission,* kwenda kwenye maeneo makuu ambayo yana wanunuzi wakubwa wa korosho, tuweze ku-*introduce* na kupata *pre-contract agreements* za *commitment* yao na namna gani tunaweza tukawasajili wakaingia kwenye mfumo wa ununuzi ili kuwe na *buy in* ili tuepuke *jeopard* ambayo inaweza ikatokea hapo katikati kutokana na mabadiliko ya mfumo.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ningependa kushauri ni elimu kwa Maafisa Ugani, kuna mmoja amezungumza hapa, Maafisa Ugani wengi wamesoma *agronomy,* sijui ni kawaida tu, wamesoma masomo *more general.* Ukimpeleka kwenye korosho hajui chochote ndio kwanza inabidi wewe mkulima uanze kumwambia. Kwa mfano, katika pembejeo za korosho viuatilifu hawajui kwamba, ni wakati gani sasa uweze kupulizia sumu inayoitwa sumu, halafu baada ya siku ngapi upulizie ile inayofuatia, halafu baada ya siku ngapi upulizie *sulphur,* au inaanza *sulphur* halafu inamalizia nyingine, hawajui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ni vitu ambavyo tunatakiwa tuwatengeneze Maafisa Ugani wetu tuwa-*customize* ikiwezekana hizi *TARI institutes* zitumike tu-*train* wawe na *specialization* kwenye maeneo kama Mlingano Tanga, wawe na *specialization* ya mazao yanayopatikana kule. *TARI* Naliendele Mtwara, wawe na *specialization* ya kule, tuwa-*train on the job training* ili waweze kufanya kazi vizuri ya kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho ambalo ningetamani niliseme kwenye Wizara hii ya Kilimo, namna ambavyo Wizara ya Kilimo inaweza kuchachua viwanda, huwa kawaida viwanda ni zao la kilimo. Kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri ashirikiane na Waziri wa Uwekezaji, Waziri wa Viwanda na Biashara ili kuhakikisha kwamba Wizara ya Kilimo ina-*feed* kwenye viwanda vilivyopo tuongeze ajira na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi, atafuatiwa na Mheshimiwa George Natany Malima, Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, ajiaandae.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hoja hii ya Wizara ya Kilimo. Kwa sababu ya muda naomba kusema kwamba naunga mkono hoja ya Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja kwa moja naomba tu nimpongeze Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuwashika mkono wakulima wa Tanzania kwa hiki anachokifanya kuendelea kuongeza bajeti ya kilimo. Tulianza na bajeti ya shilingi bilioni 294, msimu uliofuata ika-*shoot* mpaka 751 na hii tunayoendelea nayo bilioni 970 na sasa, tunamwomba aridhie kutoa trilioni 1.4 ili watu wa kilimo wakafanye kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwekezaji mkubwa kwenye kilimo maana yake ni nini? Maana yake ni tutarajie kuona matokeo makubwa sasa kutokana na uwekezaji huu. Matokeo haya makubwa tuangalie kuwasaidia wakulima wadogo, lakini sasa pia, tuelekee kwenye mashamba makubwa. Kwa wakulima wadogo bajeti ijibu changamoto zao, ikiwemo upatikanaji wa pembejeo. Wenzangu wamesema na mimi bado nasema, mbegu ni changamoto kwa wakulima, ni bei ghali na hata upatikanaji wake ni mgumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, nchi yetu inahitaji takribani tani 126,650,000 za mbegu bora, lakini kwa msimu uliopita upatikanaji ulikuwa ni tani 64,000 sawasawa na 54%. Kati ya hizo tani 40,000 zilikuwa za mahindi na tani 15 zilitoka nje ya nchi, lakini pamoja na hayo ndiyo tunasema, hizi mbegu ni za wenzetu. Wenzangu wamesema zinatoka Zambia, zinatoka Malawi, ndiyo akina *SEEDCO, DK, PANA, PIONEER, ZAMSEED,* ambapo pakti la kilo mbili linauzwa mpaka shilingi 17,000 au shilingi 18,000.

Mheshimiwa Spika, mkulima katika eka moja anahitaji pakiti tano ambapo hii inagharimu shilingi 85,000 mpaka shilingi 100,000 kwa ekari moja ambayo ni ghali sana kwa wakulima. Naomba

kutoa ushauri kwa Wizara, tunayo taasisi yetu ya utafiti, ina mbegu nyingi za msingi, mbegu mama, ni kwa nini wasipate mbegu zinazoweza kushindana? Tuzalishe mbegu zetu wenyewe ndani ya nchi kwa ruzuku, ili angalau gharama hii ya pakti moja la kilo mbili ishuke kutoka shilingi 17,000 au shilingi 18,000 na ifike shilingi 10,000 na hata chini zaidi ikiwezekana ili kutoa unafuu kwa mkulima.

Mheshimiwa Spika, niseme pia kuhusu mbolea. Naipongeza Serikali kuendelea kutoa ruzuku kwenye mbolea. Kweli, kumekuwa na ongezeko kubwa sana la matumizi ya mbolea ya viwandani baada ya Serikali kutoa ruzuku. Kabla ya Serikali kutoa ruzuku, matumizi ya mbolea yalikuwa ni kati ya tani 400,000 mpaka 600,000. Baada ya Serikali kuendelea kutoa ruzuku, makadirio yalikuwa ni tani 848,884 kwa mwaka, lakini kwa msimu huu hadi kufikia Aprili, tayari matumizi ya mbolea yameshaenda kwenye tani 1,052,000 na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni nini, kama tuna matumizi makubwa ya mbolea ya viwandani bila kupima udongo wa wananchi hiki kitu ni hatari sana. Kwanza ni hatari kwa gharama, lakini vilevile *on future* ni lazima itakuja kuwa haina usalama kwa udongo wa wananchi. Hivi kwa mfano, mkulima ardhi yake ina chumvichumvi ya kutosha *(salinity)* anaendelea kuongeza hii mbolea, mwisho wa siku ile ardhi hataweza kuitumia. Hakuna mmea ambao utaweza kuota hata kidogo. Mbolea ya chumvichumvi ni hatari kwa *microorganism* walioko kwenye ardhi, ni hatari kwa *soil texture* na ni hatari kwa kila kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuishauri Serikali, kwanza kwa sababu, Maafisa Kilimo wamepewa *soil tester*, hebu iwe ni lazima mkulima apime udongo wake kabla ya kutumia mbolea hii ili aweze kuelekezwa ni *nutrients* zipi zinakosekana. Pamoja na hayo, Serikali itoe pesa za kutosha kwa *TARI* Mlingano ambao wao wanapima udongo watupatie *soil map* ya Tanzania nzima, kwamba, ukanda huu kuna upungufu wa *nutrients* fulani, upande huu kuna upungufu wa *nutrients* fulani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba Serikali iendelee kuwekeza kwenye Kiwanda cha *Intracom* kilichoko hapa kwetu.

Kiwanda hiki uzuri wake, kinachanganya mbolea ya samadi ambayo nafikiri ni salama na ina *nutrients.* Kiwanda kina uwezo kwa kuzalisha tani 800,000 mpaka 1,000,000 kwa mwaka. Kwa sasa hivi kiwanda hiki kinazalisha tani 40. Ni kwa nini tusiwashauri wakulima? Hata kama matokeo yake yanaenda taratibu, pamoja na Kiwanda chetu cha Minjingu, hii ndiyo mbolea ya kuwashauri wakulima kuendelea kuitumia pamoja na samadi na kuendelea kutengeneza mboji. Vinginevyo tunavyokazana kuendelea kutumia mbolea ya viwandani, siku mmoja tutapata changamoto kubwa kwenye ardhi ya wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni hili suala la viuatilifu. Tumesema tunapunguza upotevu wa mazao *(post-harvest)* kwa kuanzia 35% mpaka asilimia tano. Kuna upotevu mkubwa sana wa mazao ya wakulima, hususan mahindi. Mahindi yakiwa stoo upotevu unaweza kufika mpaka 100% kwa sababu, wananchi wanahifadhi kwa kutumia hivi viuatilifu. Pengine kiuatilifu cha kifungashio cha gramu 200 labda mkulima anaambiwa anaweka kwenye magunia manne, lakini wadudu walioko kule hawafi na wengine wanakwepa, hii maana yake ni nini? Badala yake mkulima anatumia sumu kali sana, hizi wanazoita *high hazard pesticides,* ndiyo zinachanganywa kwenye mahindi, kwenye mazao yaliyoko pale na ambapo athari ya ile sumu ni mbaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba na pia naishauri Serikali, hebu kupitia *TPHA* hawa Wakala wanaoangalia hizi *pesticides* pamoja na afya ya mimea wavipitie hivi viuatilifu vinavyotumiwa na wakulima kwa sababu, kwa kweli ni hasara kabisa. Ukiweka mahindi yako stoo yakagongwa na wadudu, huwezi kuyauza wala huwezi kufanya kitu kingine na inakuwa ni hasara kubwa sana kwa wakulima. Waendelee kuliangalia hilo.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara waendelee kukarabati maghala yaliyoko kule kwenye ngazi ya kata kwa sababu, mkulima akishahangaika anatumia dawa fulani ya vidonge. Ile dawa ina *conditions* zake, lakini wakulima mle nyumbani yanakolala kwenye stoo zao ndiyo wanatumia hivi vidonge ambavyo ni hatari kabisa. Kwa hiyo, basi maghala yakarabatiwe wapeleke mazao kwenye maghala.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna teknolojia ambayo ilikuwa inaenda vizuri. Hii teknolojia ya kutumia mifuko yenye tabaka tatu ni ghali, ule mfuko mmoja ni shilingi 5,000. Mkulima mwenye mahindi yake magunia kadhaa, 20 mpaka 100 hawezi kuendelea kununua hii mifuko. Tunaomba ikiwezekana Serikali kwenye viwanda vinavyozalisha mifuko hii, waweke ruzuku ili angalau hii mifuko iuzwe kwa shilingi 2,000 na kurudi nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine ni kwenye soko. Naomba niwasemee wakulima wa Manyara ambao ni wakulima wazuri wa mahindi na maharage. Kusema ukweli kwa soko la mazao ya mahindi tunazidi kumrudisha mkulima kwenye umaskini. Kama sasa hivi gunia bado linauzwa shilingi 30,000 mpaka shilingi 40,000, huyu mkulima tunamrudisha kwenye umaskini. Sasa, kama Serikali au Wizara inatoa bei elekezi ya pembejeo ya mbolea, kwa nini isifikie mahali ikasema kwamba, mazao ya mkulima kwa mfano, mahindi kilo isiuzwe chini ya shilingi 800? Wakulima wanahangaika, vinginevyo basi *NFRA* inunue mazao ya wakulima, itafute masoko ili angalau wakulima waachane na adha ya kuhangaika na mazao huku wakiendelea kuchanganya dawa wakati wakiendelea kusubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine ni kwenye mashamba makubwa. Kama tunataka *transformation* kwenye kilimo, hatuna namna bila kwenda kwenye mashamba makubwa. Tuna *potential* kubwa katika nchi yetu. Tuna ardhi inayofaa kwa kilimo zaidi ya hekta milioni 44 ambapo tunatumia chini ya 40%.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kwa nini sasa hivi pengine Serikali, kupitia Wizara yake, isifahamu kabisa maeneo ya kilimo, hata ikaya-*acquire* kutoka kwa wananchi, ika-*treat* afya ya udongo, ikaweka miundombinu ya umwagiliaji ili iwe rahisi kwa wawekezaji? Waje wa-*invite* wawekezaji watuzalishie hilo *gap* la mazao muhimu? Kwa mfano, ngano, mbegu za mafuta na hata sukari? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukishaweka mazingira mazuri ni lazima tutapata wawekezaji. Hata hivyo, mashamba haya ya *BBT farm*

*blocks,* kutokana na *economy for scale* nafikiri kwamba, waelekezwe kabisa mazao ya kuzalisha ili nchi yetu tutoke kwenye *gap* la hayo mazao ambayo ni muhimu kwetu sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu mwingine na pengine wa mwisho, ni kuhusu kilimo cha umwagiliaji. Kilimo cha umwagiliaji ni kilimo cha uhakika na kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji ni gharama kubwa sana, hasa kuchimba mabwawa. Sasa, naiomba Serikali, haya mabwawa kwa kweli, moja linafikia shilingi bilioni na kuendelea. Shilingi bilioni moja, bilioni mbili, lakini bwawa likichimbwa, pengine *life span* yake ilikuwa iende miaka 50 na kuendelea, lakini haliwezi kufika muda huo pasipo kuwaelemisha wale wanufaika walioko pale, wana-*scheme* kwa sababu, baada ya muda bwawa linakuwa *salted,* halifai tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ninafikiri mnavyoenda kwenye kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji ni bora mkaingia mkataba na halmashauri au wale wanufaika wa *scheme*. Wakubaliane kuhusu utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji. Hata hivyo, kuna *schemes* nyingi sana ambazo Serikali imewekeza hela, lakini bado hazijamaliziwa, pengine ni bwawa tayari, ni *spillway* tayari, lakini miundombinu mingine bado *intake,* kuweka *line* kwenye mifereji pamoja na vitu vingine havijawekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, naiomba Serikali, kwa miradi ambayo Serikali imekwishawekeza hela na bado iko nusunusu haijakamilika, kwanza ingeikamilisha miradi hii ya umwagialiaji na ndipo ikaanza kujenga miundombinu mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Natany Malima, atafuatiwa na Mheshimiwa Aloyce John Kamamba na Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi ajiandae.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Wizara hii ya Kilimo. Kwanza naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye anaendelea kutulinda, kututunza na kutufanya tuendelee na shughuli zetu kama kawaida. Pili, nampongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi nyingi sana katika Wizara hii ya Kilimo. Sisi kule Mpwapwa tumepata bwawa kubwa sana la umwagiliaji lenye thamani ya shilingi bilioni 27.8 ambalo ujenzi wake unaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe. Yeye anajua jinsi nilivyofuatilia na hatimaye akakubali na sisi watu wa Mpwapwa tupate bwawa hili. Nakushukuru sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Silinde, nawapongeza kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuchangia bajeti ya Wizara hii. Mheshimiwa Waziri ameanza kueleza hali ya kilimo katika nchi yetu ya Tanzania. Ameeleza kwamba, kuna ukuaji wa Sekta hii ya Kilimo kwa 0.9% na kwamba, kulikuwa na ukuaji wa 3.3% mwaka 2022, lakini kwa ujumla mwaka 2023 kumekuwa na ukuaji wa 4.2%.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana kwa jitihada hizi, lakini naamini kabisa nchi yetu inaweza kukua zaidi ya hapa. Ukuaji huu ni mdogo ukilinganisha na maeneo ya kilimo tuliyonayo katika nchi yetu, tunaona kwamba tungeweza kufika katika asilimia kubwa kuliko hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niongelee kwenye eneo la umwagiliaji. Umwagiliaji ndicho kilimo cha uhakika kuliko kilimo kingine chochote na ripoti au bajeti imeeleza kwamba, mpaka sasa hivi nchi yetu ina hekta 727,000.3, ndilo eneo ambalo linafanyiwa kilimo cha umwagiliaji. Ukiangalia nchi yetu ni kubwa na pia maeneo ni mengi ambayo kama yangeweza kutambuliwa, kujengwa mabwawa na kuwekewa miundombinu ya umwagiliaji, ukuaji wa sekta hii ya kilimo ungeweza kuwa mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, hata ukiangalia mchango wa Sekta ya Kilimo kwenye pato la Taifa bado ni mdogo. Tofauti yake ni ndogo sana, kutoka mwaka 2022 mpaka mwaka 2023 imekua kwa asilimia 0.3, kwa hiyo, bado utaona mchango wake ni mdogo sana. Ni mdogo kwa sababu gani? Eneo tunalolitumia, kwa ajili ya umwagiliaji ni eneo dogo la hekta 727,000 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule Mpwapwa tuna maeneo mengi, lakini naamini hata sehemu nyingine za nchi yetu pia, kuna maeneo mengi ambayo yana sifa ya kufanya kilimo cha umwagiliaji. Kwa mfano, kule Mpwapwa, Kata ya Chitemo kuna eneo zuri, Mlembule kuna eneo zuri, Godegode, ukienda kule Pwaga, ukienda Kitati, ukienda Lumuma, haya maeneo yote kama yangeweza kufanyiwa utafiti na Serikali yakaweza kujengewa miundombinu, kilimo hiki kingeweza kuwa na tija na kingeongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda kuchangia ni ukosefu wa mbegu bora. Wakulima wengi wa Kitanzania wana juhudi sana ya kilimo, lakini shida ambayo wanakutana nayo ni kwamba, unapofika msimu wa kilimo wanapokwenda madukani kununua mbegu, wapo wafanyabiashara wengine ambao siyo waaminifu, wanauza mbegu ambazo ni *fake*. Mbegu ambazo hazijafanyiwa utafiti, hazina sifa ya kuitwa mbegu bora. Kwa hiyo, wakulima wanapokwenda kupanda zile mbegu, matokeo yake hawapati ile tija ambayo walikuwa wanaitarajia. Hili ni tatizo kubwa sana. Naishauri Wizara ya Kilimo, wakati msimu wa kilimo ukikaribia wafanye ufuatiliaji kwenye haya maduka yanayouza mbegu, watakutana na mbegu hizi *fake* ninazosema. Hii itatusaidia kupunguza athari hizi zinazotokea.

Mheshimiwa Spika, pia, nimeona wanasema wametenga fedha katika sekta hii kama shilingi bilioni 43 hivi. Fedha hizi wanasema kazi yake kubwa ni kujaribu kufanya utafiti ili kupata mbegu bora na kuzisambaza. Basi bajeti hii ingejikita sana kwenye utafiti ili tuwe na mbegu bora na lengo liwe ni kutosheleza nchi yetu yote ya Tanzania. Wananchi wetu wanaoshughulika sana na kilimo waweze kupata mbegu bora kwa wakati na kwa bei

ambayo ni *affordable* ili waweze kuongeza kilimo na ikifika mwakani au angalau hata baada ya miaka miwili tuweze kuona matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bashe anachakarika sana kujaribu ku-*transform* kilimo katika nchi yetu, nampongeza sana. Tunaona mikakati mingi anayoifanya, lakini kama hawezi kujikita kwenye upatikanaji wa mbegu bora, juhudi zake zote zinaweza kuwa hewani. Kwa hiyo, naomba sana nimshauri Mheshimiwa Waziri kwamba, mbegu ndiyo kitu muhimu sana katika kilimo. Ni lazima tupate mbegu zilizo bora ambazo watu wetu wanaweza kunufaika nazo. Kama tunavyosema, kilimo ndicho kinachangia asilimia kubwa ya ajira katika nchi yetu, lakini kwa miaka mitatu nimefuatilia hali ya asilimia ya ajira zinazotokana na kilimo iko katika *range* ya 65 mpaka 70, kwa nini haikui? Ni kwa sababu ya mambo kama haya madogomadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, hatuja-*utilize* eneo letu lote la umwagiliaji, lakini pili, hata wakulima wetu hawatumii mbegu zile ambazo tunadhani ni bora ambazo zinaweza kuleta tija. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ajaribu kuangalia sana suala la utafiti ili tuwe na mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo pia tunakutana nalo kwenye vijiji, ni wakulima wetu hawana elimu ya kilimo. Tunao Maafisa Ugani, lakini hawatoshelezi. Taarifa yake inasema mpaka sasa hivi tuna asilimia 35 tu ya Maafisa Ugani ambao wako kwenye maeneo yetu, lakini tuna upungufu wa Maafisa Ugani 20,000 na kuendelea, sasa hili ni tatizo. Kata moja inakuwa na Afisa Ugani mmoja, vijiji ni sita, anawezaje kufanya kazi katika mazingira hayo?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunadhani kwamba, Serikali ni lazima ichukue hatua muhimu na maamuzi magumu kuajiri Maafisa Ugani kwa wingi. Kama tunataka kupata matokeo, kama tunataka kuongeza pato la Taifa kupitia Sekta hii ya Kilimo ni lazima tuwe na wataalam wanaojua ambao watawasaidia wakulima wetu kulima kilimo cha kisasa. Pia, wawe wanaweza kutambua mbegu *fake* na mbegu bora kwa sababu ya utaalam

watakaokuwa nao. Bila hao, wakulima wetu wataendelea kulima kama kawaida, watalima kilimo walichokizoea na matokeo yake hakutakuwa na tija.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuchangia na pengine litakuwa la mwisho ni kuhusu uhakika wa masoko kwa mazao yetu ya kilimo. Sasa hivi ukienda vijijini mazao mengi yameiva na yamekomaa, lakini walanguzi wameshavamia kule wananunua kwa bei ya chini kabisa. Kwa hiyo, mkulima anapomaliza msimu wa kilimo anakuwa haoni kitu alichopata. Ameuza mazao yote kwa bei ndogo, wanaofaidi ni wale *middlemen* wanaokuja kulangua na kwenda kuuza mahali pengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali ingekuwa na mfumo wa kuwa na masoko rasmi ambayo mkulima anajua nikilima karanga, nikilima ufuta, nitakwenda kuuza mahali fulani na bei inaweza kuwa imetangazwa inajulikana. Hii itawasaidia kujikwamua kiuchumi, lakini pia, sekta itakuwa na itaongeza pato la Taifa.  Kwa hiyo, masoko ni jambo la muhimu. Hatujawa na soko kamili katika nchi hii, wakulima wetu hawajui. Tunajaribu kuhangaika kutumia vyama vya ushirika, lakini bado kuna maeneo mengi vyama hivi havifiki. Kwa mfano, Wilaya yetu ya Mpwapwa, sidhani kama kuna chama cha ushirika pale. Wakulima wetu wanajihangaikia wenyewe, wakishapata mazao walanguzi wanakuja wanachukua mazao yao kwa bei ya chini, wale wanabaki maskini mwaka baada ya mwaka. Kwa hiyo, naomba sana jambo hili lichukuliwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, miaka miwili mitatu huko nyuma Kanda ya Kati tulipiga kelele sana juu ya kilimo cha alizeti na zabibu, lakini kuanzia mwaka jana na mwaka huu sisikii kitu. Ni kama hiki kitu kilikuwa ni mbio za sakafuni. Sasa hivi hakuna tena *pressure* ya kuhimiza watu walime alizeti, walime zabibu. Hii inawezekana ni kwa sababu ya bei za mafuta ambazo hazieleweki, lakini pia soko la zabibu ambazo zinalimwa hapa Dodoma bado halijulikani.

Mheshimiwa Spika, watu wanatengeneza michuzi ya zabibu, lakini mahali pa kuuza hakuna, matokeo yake inaharibika. Kwa hiyo, watu wanaacha wanakata tamaa. Wakulima wanakata tamaa kuendelea na kilimo kwa sababu hakilipi na wala hakijawa na mfumo rasmi wa kuwasaidia wakulima. Kwa hiyo, tukitaka wakulima wetu wafanye vizuri, ni lazima tuwawekee mazingira mazuri kwa maana ya masoko, mbegu na wataalam wawepo, hapo ndipo tutaona kilimo hiki kinakua. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bashe naunga mkono hoja, lakini zingatia haya mambo. Kilimo chetu kitakua na wananchi wetu watafaidika. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Aloyce John Kamamba, atafuatiwa na Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi na Mheshimiwa Livingstone Lusinde ajiandae.

**MHE. ALOYCE J. KAMAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu, hoja ya Wizara ya Kilimo. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuongoza nchi yetu, lakini kwa fedha nyingi ambazo anazipeleka katika miradi ikiwemo Wilaya ya Kakonko. Ametuletea fedha nyingi kwenye miradi ya afya, elimu na hata kwenye kilimo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, ndugu yangu Mheshimiwa Bashe na wasaidizi wake ikiwemo pamoja na Katibu Mkuu na wataalam wote, wanafanya kazi nzuri, wameandika historia ya nchi hii kwenye Wizara ya Kilimo. Nawapongeza sana kwa kazi hiyo nzuri ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunafahamu Watanzania kwa asilimia kubwa ni wakulima, lakini wananchi wetu wanategemea kilimo. Serikali imefanya kazi kubwa kuboresha kilimo kwa hatua ambayo tunapongeza, lakini yapo maeneo kadhaa ambayo yanahitaji kuangaliwa. Kwangu mimi, moja ni upatikanaji wa wataalam wa kilimo. Wataalam wa kilimo kwenye maeneo yetu hawatoshelezi, naomba sana wataalam waajiriwe na wapelekwe katika

maeneo yetu na wakienda katika maeneo yetu ya kijijini ambako kilimo kinafanyika waende watoe elimu kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna uwezekano wataalam wakawepo, lakini hawafikishi elimu kwa wakulima, niombe wataalam waajiriwe, lakini waende kwa wananchi kutoa elimu juu ya kilimo bora ikiwa ni pamoja na wao wenyewe kuonesha mfano kwa kuwa na mashamba katika maeneo ya vijijini ili wananchi wetu waweze kujifunza kutoka kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utoshelevu wa pembejeo; kwangu kwenye utoshelevu wa pembejeo nitazungumzia mbegu ambazo wenzangu pia wamezungumza. Mbegu hazipatikani kwa wakati, mbegu hata zikipatikana hazitoshelezi, kwa nini? Kwa sababu uzalishaji wake ni mdogo sana na upatikanaji wake ni mdogo sana na hivyo hata bei inakuwa siyo rafiki. Niombe yaanzishwe mashamba ya kutosha ya kuzalisha mbegu kwa ajili ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwetu sisi Kakonko ardhi tunayo, Mheshimiwa Waziri aje Kakonko tutampatia ardhi kwa ajili ya kuweka mashamba ya kuzalisha mbegu katika mazao mbalimbali yakiwemo mahindi, alizeti na kadhalika. Nina hakika kwetu Kakonko tukija kupata wataalam hawa, wakaja katika maeneo yetu ule uzalishaji wa mbegu kwa sababu mashamba yapo, wataalam wapo nina hakika yatatusaidia wananchi wetu kuweza kuboresha kilimo chao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri aliyoitoa, ukurasa 30 anasema kwamba hadi Aprili mwaka huu upatikanaji wa mbegu ulikuwa ni tani 68,474.67 ambayo ni sawa na 54%. Maana yake ni kwamba wananchi wa nchi hii, wakulima wa nchi hii wanazalisha au wanafanya kilimo chao wakiwa na mbegu kwa 46% tu, maana yake nusu ya mbegu inayohitajika nchini haipo. Kwa nafasi hii niwapongeze wakulima wa nchi hii ambao wanazalisha na kulisha nchi hii, lakini wakiwa na upungufu wa 46%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wenzangu wamesifia Wizara kwa kupeleka mbolea katika maeneo yao. Kwetu sisi Kakonko ni tofauti, mbolea hatuipati kwa wakati, lakini hata ikipatikana inapatikana kwa kiwango kidogo sana na niombe, Mheshimiwa Waziri Bashe tulishaongea, shida tuliyonayo sisi hatuna wakala wa usambazaji wa mbolea katika Wilaya ya Kakonko. Anayetusaidia kusambaza mbolea katika Wilaya ya Kakonko ni yule anayetumika Wilaya ya Kibondo.

Mheshimiwa Spika, nitoe ombi maalumu, nafahamu zipo taratibu za kumpata huyo wakala ikiwa ni pamoja na uchumi wake, lakini kwa Wilaya yetu ya Kakonko fedha kwa wafanyabiashara wetu kuna uwezekano ikawa kidogo, kuna uwezekano wasiweze kufikia vile viwango vinavyotakiwa. Niombe Mheshimiwa Waziri aangalie na atupatie majibu atakapokuwa anatoa taarifa. Lini tutapata msambazaji wa mbolea katika Wilaya yetu ya Kakonko? Ili tuwe na uhakika wa kupata mbolea kwa wakati lakini kwa utoshelevu wake.

Mheshimiwa Spika, zao la muhogo; zao la muhogo ni zao ambalo ni la kutegemewa kwa biashara katika Wilaya yetu ya Kakonko, lakini na Mkoa wote wa Kigoma. Wilaya ya Kakonko tunategemea zao la muhogo kama zao la biashara. Muhogo kwa Wilaya ya Kibondo ni zao la biashara, hivyo hivyo Wilaya ya Kasulu, Buhigwe, Kigoma hadi Uvinza lakini zao hili halijaweza kupewa kipaumbele. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, tuliangalie zao hili la muhogo kwa Mkoa wetu wa Kigoma kama zao pekee kwa ajili ya kuongeza uchumi wa wananchi wa Mkoa wetu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo mambo kadhaa ambayo yanahitaji kufanyika katika eneo hilo. Zao hilo halina bei ya kutosheleza, zao hilo halina mbegu ya kutosheleza, kwa hiyo nashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali ihakikishe zao la muhogo kutoka Mkoa wa Kigoma linapewa kipaumbele kwa kutafutiwa soko la ndani na nje ya nchi;

(ii) Kuendelea kufanya utafiti ili tuweze kupata mbegu bora ambazo zitaongeza uzalishaji kwa lengo la wananchi kuzalisha kwa kiwango kikubwa zaidi; na

(iii) Serikali itengeneze mazingira kuwawezesha wafanyabiashara wadogo na wafanyabiashara wa kati kuweza kuanzisha viwanda ambavyo vitaongeza uzalishaji, lakini kuongeza thamani ya zao hilo katika mkoa wetu na kwa nchi yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo changamoto nyingine kwa upande wa kilimo, wakulima wanalima kwa uzoefu wa mazingira yao, udongo haupimwi. Niombe sana, imezungumzwa katika hotuba ziongezwe juhudi za ziada kuhakikisha kwamba udongo unapimwa. Mwaka jana mimi mwenyewe nilikuja hapa nikatoa taarifa kwamba nimetumia mbolea lakini haikutoa matunda kwenye eneo langu. Wataalam walivyokuja kupima kulinganisha mbolea niliyonunua na kutumia na udongo uliopo havikuwa sawa. Kwa hiyo maana yake nilitumia mbolea ambayo haifai kulingana na udongo ule, kwa nini? Udongo ule haukuwa umepimwa. Kwa hiyo niombe Wizara ichukue mawazo ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kwamba udongo unapimwa ili wananchi wajue udongo uliopo katika shamba unafaa kwa mbegu ipi na unafaa kwa mbolea ipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kuwapongeza Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kwa nchi nzima ikiwa ni pamoja na Mheshimiwa Rais. Tunazidi sisi kuwapa moyo kuhakikisha kwamba wanafanya kazi, wanaongeza bidii katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kingu.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimesimama kwa Kanuni ya 76 na kwa heshima kubwa ya mbele ya Kiti chako naomba nisiisome kwa sababu ya muda, lakini naomba Mwongozo wa Kiti chako kutokana na jinsi nilivyokuwa nimefuatilia michango ya Wabunge wengi toka asubuhi na hasa nilipofuatilia mchango wa Dkt. Ntara asubuhi wakati anachangia. Aliongea mambo ya msingi sana akihusisha namna gani benki zetu Tanzania zinaweza zikasaidia *vision* kubwa aliyonayo Mheshimiwa Waziri wetu na Naibu wake na Wizara yake katika ku-*transform* kilimo kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe tunaona juhudi za benki wanazozifanya katika kuwakopesha wakulima, lakini naomba nilipe Bunge lako taarifa kwamba, tarehe 19 mwaka 2023 Benki Kuu iliagiza *Tanzania Bankers Association* wafanye mapitio ya *regulations* na *legal framework* ili waweze ku-*accommodate* kitu kinaitwa *Islamic Banking* ili ziweze kusaidiana na benki zingine katika kutoa mikopo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu *Islamic Banking* kwa mujibu wa machapisho mbalimbali zinafanya kazi katika mataifa baadhi ya Nchi za Afrika. Zinafanya kazi kwa baadhi ya Mataifa ya Ulaya ya Mashariki na Magharibi. Je, ni lini Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kupitia maagizo haya ambayo *BOT* walikuwa wameyatoa na kuwapa *Association of Bankers,* italeta hapa sheria ya mabadiliko ili *Islamic Banking* ianze kufanya kazi Tanzania? Tuwasaidie wakulima kupata mikopo bila riba, Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge amesimama Mheshimiwa Kingu hapa akiomba mwongozo wa maelezo ambayo mmeyasikia akiyahusisha na michango ya waheshimiwa wabunge na sikusudi kuyarejea tena yale ambayo yeye ameyasema wote tumeyasikia. Sasa mwishoni hajataka mimi nitoe mwongozo ameuliza swali, ameulizwa swali na anaiuliza Serikali kwamba lini italeta hayo mabadiliko. Kwa hiyo ameingia

kwa Kanuni ya 76, lakini ameuliza swali akitaka Serikali lini italeta mabadiliko.

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu bado ninao Wabunge wachache hapa wa kuchangia, halafu hoja hii itaanza kuhitimishwa na namwona Mheshimiwa Waziri wa Fedha alikuwa ananyanyua kisemeo kuashiria kwamba pengine anayo majibu ya swali lako. Kwa hivyo Mheshimiwa Waziri kabla sijamwita Naibu Waziri wa Kilimo nitakupa nafasi ya kuchangia, utachangia kwenye hoja hii ambayo Mheshimiwa Kingu ameuliza swali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, atafuatiwa na Mheshimiwa Livingstone Lusinde na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hoja hii iliyopo mbele yetu ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Naungana pamoja na Wabunge wenzangu kuendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuruhusu kuendelea kuweka fedha nyingi katika hii Wizara ya Kilimo akitambua kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kumpongaza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri ambayo wanaendelea kuifanya katika hii sekta ya kilimo katika kuwasaidia Watanzania. Kama tunavyofahamu kwamba kilimo, kwanza kinachangia kwa nafasi kubwa katika uchumi wa nchi yetu, lakini kilimo vilevile kinachangia kwa nafasi kubwa katika ajira ya nchi yetu. Kwa hali hiyo tuna kila aina ya sababu ya kusaidia kilimo na ndiyo maana tunasema kilimo ndiyo uti wa mgongo wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia leo kati ya changamoto kubwa tuliyonayo katika nchi hii ni changamoto ya ajira, yaani vijana wengi wanamaliza shule za msingi wanaingia kwenye soko la ajira, wanamaliza vyuo wanaingia kwenye soko la ajira, lakini

kwa bahati mbaya sana kwa sababu ajira ni pungufu au ni chache wanahangaika katika namna ya kupata ajira. Hata leo unaangalia wapo vijana wengi wanaamua kutoka vijijini kuja mjini, hii si kwa sababu nyingine ni kwa sababu tu hatujawatengenezea mazingira hasa ya kilimo ya kuwawezesha waendelee kuishi kule vijijini.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme tu kwamba, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alionesha njia hasa kwa mwaka jana pale alipoanzisha ule Mpango wa *BBT*. Kusema ukweli mimi binafsi nilifarijika sana na niliona kwamba ule mpango ungeweza kusaidia ajira kubwa kwa vijana wetu, lakini ukiangalia katika bajeti ya mwaka huu ile nguvu aliyoiweka mwaka jana aliyoanza nayo, kwa hali halisi siyo nguvu aliyoiweka mwaka huu. Naamini kwamba hilo limetokea kwa sababu ya changamoto alizokumbana nazo katika ule mpango mzima wa *BBT*.

Mheshimiwa Spika, nimpongezee tu kwamba walau alithubutu na anaendelea kupambana. Ni vizuri tukaona namna nzuri zaidi tunavyoweza kuiboresha ile *BBT* kwa sababu tukifanya hivyo itawezesha vijana wengi zaidi kujiajiri hasa katika hii Sekta ya Kilimo. Niseme, mwaka jana kati ya changamoto ambazo zilitokea ni kwa sababu vijana wengi walichukuliwa kwa njia ya kupitia mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ulikuwa unamkuta kijana yupo Dar es Salaam aliona ombi aka-*apply* na akabahatika kupata nafasi, lakini hawakuwa wale walengwa halisi. Sasa kwa safari hii ambacho nimshauri Mheshimiwa Waziri kama kweli tunataka kupunguza tatizo la ajira na tunataka kuongeza tija ya kilimo hasa kwa hawa vijana wetu ambao wanamaliza vyuo, wanamaliza shule na hata wale wa darasa la saba ambao wanaingia mtaani kwa kuanza maisha, tuliboreshe kwa kuunganisha kilimo pamoja na watu wetu wa JKT (Jeshi la Kujenga Taifa). Wakitangaza tu kwamba leo kuna nafasi ya kuchukua wale vijana wanaotaka kuingia JKT, yaani nafasi labda 50 za wilaya, vijana wanaoenda pale ni zaidi ya vijana 1,000 wanaenda pale wanajipanga, kwa sababu wanahangaika ili waweze kupata nafasi ile. Hiyo

inaonesha kwamba ni kwa kiasi gani vijana wengi hawana ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nadhani Mheshimiwa Waziri wa Kilimo kama tunataka kuwasaidia hebu aingie mkataba na wale JKT, wao wafanye kazi ya kuwatambua wale vijana, kuwaweka kambini, kuwatunza na kuwasaidia katika yale mafunzo yote ya kilimo. Yeye huku atoe mtaji baada ya kutoa mtaji na aone namna ya kuwawezesha mtaji pamoja na utaalam. Tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo, basi ni rahisi kuchuja wale vijana ambao wapo tayari kwa ajili ya kilimo, wakapata mafunzo ya ukakamavu, wakapata mafunzo ya kilimo na wakasimamiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya hivyo baada ya ile miaka miwili, mitatu naamini kwamba, watakuwa wamezalisha kiasi kikubwa na kutokea hapo sasa ni rahisi wakapewa mitaji. Kwa sababu mafunzo wameyapata sasa wakapewa mitaji, tena mitaji ile kwa kiasi kikubwa watakuwa wameizalisha wao wenyewe. Tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo sasa, kwa sababu mahitaji ya chakula ni makubwa, leo ukiangalia mfano zao kama la mpunga nchi zote zinazotuzunguka ukienda Kenya, Uganda, Rwanda na kila mahali mchele una soko kubwa; kwa sababu mabonde tunayo makubwa yanayoweza kusaidia hiki kilimo, basi inakuwa ni rahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, niseme yaani Mheshimiwa Waziri leo akija pale Mara, tukaenda tukazungumza na wale watu wa JKT Rwamkoma; kwa sababu mabonde yapo mengi kwa nini tusifanye pale tu-*cite example*, ambacho mimi naamini kwamba mfano ule lazima tu utafaulu na ukishafaulu, basi tuone namna ya ku-*implement* katika nchi nzima, kuliko hivi ambavyo tunawaacha vijana kila leo ukipita mpaka saa nane za usiku hawana kazi wanacheza *pool*. Ukipita vijana wanasema Mheshimiwa hatujaamka, Mheshimiwa hatuna ajira na wakati kuna mahali ambako tunaweza tukawaficha wale vijana tukawaweka na maisha yao yakaweza kuendelea. Kwa hiyo kama Serikali au Mheshimiwa Waziri atalichukua hilo wazo basi tunaweza kuona

namna ya kuli-*implement* na likatusaidia kupunguza ajira kwa ajili ya vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, lipo hili suala la Ushirika. Tunatambua kwamba, ushirika una manufaa mengi na una faida nyingi, kwa sababu watu wengi leo hata pale anapolima, akitaka kwenda benki anajikuta hana dhamana ya kuwafanya waweze kupata mkopo. Kwa hiyo, watu wengi kila wanapojaribu kusimama hawawezi kusimama, si kwa sababu nyingine lakini ni kwa sababu hawana zile *security* za kuweza kupeleka benki kwa maana ya nyumba na *security* nyingine ili waweze kupewa mikopo, lakini kupitia ushirika maana yake ni kwamba, watu wengi itakuwa rahisi kupata mikopo na wakaendesha maisha.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika Ushirika wa Tanzania ule unaoendelea ni ule ushirika wa Vyama vya Wafanyakazi huo unaendelea. Huu ushirika mwingine kila unaposimama unaanguka. Sasa hili nataka tu kumwomba Mheshimiwa Waziri kwamba, wala tusiende mbali tuangalie tu kwa wenzetu wa Kenya hapa, ushirika karibu katika kila *angle* unakuta kama ni hawa watu wenye magari daladala, wapo katika ushirika wanaendelea vizuri, ukikuta watu wanauza maziwa, wapo katika ushirika, ushirika wao wa maziwa unaendelea vizuri. Ni vizuri na sisi hapa kwetu … *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Manyinyi, kengele ya pili ilishagonga.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika ni kengele ya kwanza, labda kama mmechanganya tu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mbili zimeshagonga.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, basi nimalizie tu kwamba, nadhani kuna haja ya kuona namna ambavyo tunajifunza hata kutoka kwa wenzetu, halafu tukauleta

huo ushirika na naamini kwamba, utawasaidia watu wetu na maisha yataendelea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Livingstone Lusinde, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe na Mheshimiwa Michael Kembaki, ajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nitoe mchango wangu kwa Wizara ya Kilimo. Awali ya yote, nataka nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, pamoja na timu yake nzima kwa kazi kubwa ambayo wanafanya. Vilevile nataka nimtahadharishe kwa sababu najua kuna wengine hawajamzoea sura aliyoingia nayo leo, watu wengi hawajaitafsiri.

Mheshimiwa Spika, chama kinachotawala nchi hii ni Chama cha Wakulima na Wafanyakazi, kwa hiyo *seriousness* yake kwa jioni ya leo inazingatia hilo kwamba, hii bajeti ya leo tunaijadili ni bajeti ya wananchi wa Tanzania karibu 90%. Kwa hiyo, wawe makini sana Mheshimiwa Waziri Bashe na Mheshimiwa Naibu Waziri Silinde, wanaweza wakapotea ghafla hapo kama hawatasikiliza kwa makini mambo yanayozungumzwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amepanga safu kwenye Wizara hii ambayo siyo tu imekuja kuchangamsha, bali imewafanya vijana wengi na Watanzania kutamani sasa kuingia kwenye kilimo. Imegeuza fikra kabisa kwamba, hata maeneo makavu kama Mkoa wa Dodoma, imeonekana wazi kwamba ukame wa Dodoma haukuwa ukame wa ardhi bali ulikuwa ukame kwenye vichwa, kwa maana kumbe tukiweza kuchimba maji chini ya ardhi tukapata mabwawa ya kutosha ukame itakuwa ni hadithi, hatutazungumzia habari ya ukame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumpongeze Mkuu wa Nchi kwa namna anavyoshusha pesa kwenye Wizara hii na *vision* yake. Tumeona

akitoa usafiri nchi nzima kwa ajili ya wataalam wetu mbalimbali waweze kufika shamba. Tumeona zikinunuliwa mashine mbalimbali za kupima udongo, lakini shida yangu kubwa ni namna Wizara itawezesha vile vyombo kuweza kutembea. Sijui *OC,* mafuta yanapatikanaje ili pikipiki ziweze kufika kwenye mashamba ya wakulima badala ya watu kurandaranda nazo pale Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa wa Dodoma sisi, naomba ku-*declare* na mimi sasa hivi ni mwekezaji mdogo wa Kiwanda cha Mchuzi wa Zabibu, tunatengeneza *wine*, kwa hiyo, tumejifunza mengi sana kutokana na zao la zabibu. Zao la zabibu ni zao la matunda na halitunziki kirahisi, ni lazima uchakate mchuzi na uweze kutunza ule mchuzi. Vyombo ya kutunzia mchuzi ni ghali sana. Kwa hiyo, tungemwomba Mheshimiwa Waziri, Serikali ijaribu kuwaangalia wasindikaji wadogo wadogo iwasaidie hata kupata vyombo vya kutunzia huo mchuzi kwa kipindi kirefu ili waweze kumudu, waweze kutunza mchuzi na baadaye wakulima waweze kupata tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni lazima kutambua ardhi, siyo Mkoa mzima wa Dodoma unalima zabibu, kuna maeneo zabibu hazikubali. Ardhi inayolima zabibu ni ndogo sana. Kwa hiyo, ni vyema Wizara ikaitambua hiyo ardhi ikapimwa wakulima wakapata hati na tukalinda eneo hilo, kwa sababu kuna uwezekano mkubwa eneo hilo likapangiwa matumizi mengine, basi itakuwa hadithi ya kusikia kwamba, Dodoma tunalima zabibu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni vema Serikali sasa ikajikita kwenye kutafuta masoko ya mazao. Masoko yamekuwa tatizo, wakati wa mavuno chakula kinakuwa kingi ndani ya nchi, kuna baadhi ya maeneo kinashuka sana bei na maeneo mengine kinakuwa kimepanda sana. Kwa hiyo, utakuta mkulima hanufaiki chochote isipokuwa mfanyabiashara wa mwisho ndiyo anayenufaika na mazao ya mkulima, hii sasa si sawa! Ni lazima tuangalie namna ya ku-*balance* ili mkulima aweze kuinuka pale alipo.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *BBT*, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, namna alivyotutengenezea kitu kizuri, Jimbo letu la Mvumi tumepata huu mradi zaidi ya hekari 11,000 zinalimwa pale, ni rai yangu kwa Mheshimiwa Waziri kututengenezea barabara, kwa sababu huku kote barabara tumeweza kuitengeneza, lakini kutoka Kijiji cha Ndogowe kupita kwenye ule mlima kuelekea Ihimbwa, kushuka Mlazo kwenda kwenye mradi, pale pamekuwa pana tatizo kubwa sana pale mlimani. Kwa hiyo, niiombe Serikali, kwa sababu ipo siku Mheshimiwa Rais, atatamani kwenda kule, hivi watampitisha na helikopta wakati barabara ipo? Kwa hiyo, ni vema wakatutengenezea kile kipande cha kilomita kama nane hivi au kilomita tano wakaweka *concrete* zege pale kwenye mlima. Hii itasaidia hata magari makubwa na mitambo kupita kuelekea kule kwenye mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru sana Wizara kwa namna ambavyo wanafanya kazi. Mkoa wa Dodoma hauna mito inayotiririka maji msimu mzima. Sasa hivi ukitembea huwezi kukuta mto unatiririka maji pamoja na mvua kubwa ambayo imenyesha mwaka huu. Kwa hiyo, ni rai yangu kuwaomba, hatuwezi kulima bila mabwawa. Sisi hapa ili tuweze kupata kilimo cha umwagiliaji ni rai yetu kwa Serikali ituchimbie mabwawa makubwa ambayo yatatunza maji, hayo maji tuyatumie kwa ajili ya mifugo na tuyatumie kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona *Eng*. Mndolwa, akitupatia *Eng*. Salehe, tumezunguka naye Jimbo zima, ameainisha baadhi ya maeneo ambayo yanafaa kuziba tu. Kuna baadhi ya maeneo ukiziba unapata bwawa kubwa. Ni vema wataalam wetu, ukipita hii barabara kubwa ya kwenda Dar es Salaam, ukifika Mtanana na Kibaigwa Waheshimiwa Wabunge, wakati mwingine unakuta kuna kibao pale kimeandikwa taratibu maji yanakata barabara. Lile eneo mimi huwa naona ni bwawa kubwa. Ni bwawa kubwa ambalo unaweza kuziba tu ile barabara ukaihamisha ikapita sehemu nyingine ukapata bwawa kubwa Kibaigwa na ukapata maji mengi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wataalam wetu wakati mwingine wajielekeza kugundua maeneo ambayo unaweza ukaziba kidogo halafu ukapata maji mengi ambayo yanaweza kufaa vitu vingi. Yanaweza kufaa kufuga samaki, yanaweza kufaa humo kwa umwagiliaji, yanaweza kufaa vitu vingi hata kuongeza nguvu katika uzalishaji wa umeme.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Serikali katika kuboresha kilimo, badala ya kuwatambua vijana kupitia JKT pekee yake, wapo vijana ambao hawapo JKT, lakini nao wanataka kulima, wanajibidiisha na kilimo, hawa nao tuwatambue, tuwape elimu, tuwape uzoefu na tuwape ujuzi ili waende wakafanye kazi na zaidi sana tuwape vitendea kazi. Tuwakopeshe watu matrekta ili wabadili kutoka kilimo cha mikono kwenda kwenye kilimo ambacho kinafaa. Kilimo cha treka kitatuleta mazao mengi kwa wakati mfupi, kuliko mkulima anashinda shamba anapambana kutwa nzima lakini tija ya uvunaji mazao inakuwa kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Kembaki na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, ajiandae.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana wewe kwa kunipa nafasi hii adhimu ili niweze kupata nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Mwenyezi Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi kuishukuru na kuipongeza sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, ambayo inaongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuonesha kwa vitendo na dhati wanawajali wakulima wa nchi hii, kwa kuwaongezea bajeti kufika shilingi trilioni 1.2. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme kuwa Mheshimiwa Rais ameonesha mapenzi makubwa sana kwa Watanzania kwa bajeti

hii ya mkulima, kwa bajeti hii ya Mtanzania, kwa nafasi yake amemaliza kazi yake imebaki kwa watu ambao wamepewa dhamana kwa ajili ya kwenda kuitekeleza bajeti hii iweze kuleta matunda. Niwashukuru timu nzima ya Wizara ya Kilimo wakiongozwa na Mheshimiwa Hussein Bashe, tunawashukuru sana kwa miradi yote ya maendeleo ambayo wametupatia ndani ya Jimbo la Momba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza hapa. Naunga mkono michango yote ya wenzangu ambao wamechangia. Naomba nijielekeze mahali hapa. Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe katika mchango wake akiwa anahitimisha kule mwishoni anakiri kwamba, yapo baadhi ya maeneo ambayo wakulima wa nchi hii wanapitia changamoto. Namnukuu Mheshimiwa Waziri anasema hivi; "Ninawashukuru sana Wakulima wa nchi hii kwa kuendelea kufanya kazi katika mazingira magumu na kuendelea kulinda uchumi wa nchi yetu na usalama wa nchi yetu." Kwa hiyo, anakiri kwamba, yapo baadhi ya mazingira magumu ambayo wakulima wa nchi hii wanapitia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri mwanzoni kabisa akiwa anamshukuru Mwenyezi Mungu na Mheshimiwa Rais, namnukuu Mheshimiwa Waziri Bashe anasema; "Ninamwahidi Mheshimiwa Rais na Watanzania kuwa, nitatumia uwezo wangu wote kwa uaminifu na uadilifu mkubwa kuhakikisha kuwa, kilimo kinachangia kikamilifu katika kuhakikisha usalama wa chakula na lishe nchini. Kulisha wengine kibiashara, kuongeza ajira na kuinua pato la mkulima ili kupunguza umaskini." Kwa hiyo, pia yapo baadhi ya maeneo Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba, bado kuna maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende mahali ambapo panawafanya wakulima wafanye kazi katika mazingira magumu na Mheshimiwa Waziri anakiri kwamba, ndiyo hayo maeneo yanafanya kuwepo umaskini, mikopo kwa wakulima. Pamoja na ukubwa wa bajeti hii ambayo tunaiona, lakini niseme wakulima wadogo wadogo wa nchi hii bado hawajanufaika kikamilifu na mikopo hii, kuna urasimu mkubwa changamoto nyingi ambazo mkulima wa kawaida wa nchi hii hawezi kupata mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mheshimiwa Mbunge ambaye natoka kijijini, niliamua kujipa jukumu mwenyewe kuunda vikundi vya wakulima kwenda nao mguu kwa mguu kwenda benki kupita Wizarani. Tumepitia changamoto nyingi, kadhia nyingi mpaka sasa hivi kuna vikundi havijapata mkopo. Kwa hiyo, nataka kumwambia nini Mheshimiwa Waziri? Naomba Mheshimiwa Waziri, anisikilize yeye ni Waziri wa wakulima na mimi ndiyo mchangiaji wa mwisho. Tunaomba bajeti hii kubwa ambayo ametuletea sisi hapa Bunge tumpitishie, tunaomba bajeti hii kwenye mikopo iwaguse wakulima wadogo wa chini, ndio ambao wanaumia katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, takwimu kubwa ambazo zinasomwa hapa Bungeni kuonesha kwamba wakulima wamepiga hatua ni wale wafanyabiashara wachache ambao wao wanajinasibu huko kwamba, wao ndiyo wakulima ilihali wao wamejisajili kama wakulima tu, lakini wao kazi yao kubwa ni kwenda kuchukua mazao vijijini kwa wakulima, ni kwenda kuchukua mazao kwa bibi zetu, babu zetu ambao mpaka sasa hivi wanalima kwa kutumia jembe la mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali hii haikubaliki, inaendelea kuwaumiza wakulima na watu wachache ndiyo ambao wanaendelea kunufaika ambao ni madalali wa kilimo. Ndiyo ambao wanaendelea kunufaika na ndiyo ambao wanasomwa kwenye hizi takwimu kubwa za Wizara ya Kilimo. Mimi Mheshimiwa Mbunge ambaye ninatoka kwa watu ambao ni wakulima nakiri kwa kusema zaidi ya 90% hakuna mwananchi ambaye amenufaika na mkopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mkopo uliwatangaza pale wadau wageni wake waliokuwa wamekuja *CRDB* na *NMB,* tunaomba wanapotoa mikopo kwa wakulima wetu watoe mikopo kwa wakati. *(Makofi)*

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Inatokea wapi Taarifa? Aah! Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara.

**TAARIFA**

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge anayeongea sasa hivi. Sasa hivi saa 11.05 nimepokea simu kuna wafanyabiashara wananunua mahindi kwa shilingi 300 pale Peramiho.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani mnajua taarifa inamaanisha nini wakati wa mchango wa Mheshimiwa Mbunge, haya Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, napokea taarifa. Naendelea kusisitiza kwamba, wakulima wadogo hawanufaiki, madalali ndiyo wananufaika na ndiyo ambao wanasomwa kwenye hizo takwimu za Wizara ya Kilimo kuonesha kwamba wakulima wanaendelea kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *CRDB* na *NMB* pamoja ni wadau wa maendeleo tunaomba wawape wakulima wetu mikopo kwa wakati. Wao ndiyo wanafanya wakulima waende wakakope kausha damu. Sisi katika nchi hii, msimu wa kilimo unaanza kuanzia mwezi wa Novemba, wanaenda kumpa mkulima mkopo mwezi Januari, anakuwa ameshakopa tayari kausha damu, anachukua pesa yao ndiyo anakwenda kulipa kule.

Mheshimiwa Spika, wahanga wakubwa wa kausha damu ni wananchi wa Jimbo la Momba, wanateseka sana. Mtu anakopa shilingi 100,000 anakuja kurudisha shilingi 500,000. Mheshimiwa Waziri kama ambavyo amesema amewaahidi Watanzania na Mheshimiwa Rais, kufanya kwa uaminifu na kwa uadilifu, tunaomba katika hili afanye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusiana na lumbesa na vipimo vikubwa ambavyo vinawanyonya wakulima. Tunaomba Mheshimiwa Waziri aziandikie waraka Halmashauri zetu nchini kwa kushirikiana na Wizara husika. Jambo hili mtu yeyote ambaye ananunua kipimo kikubwa kumnyonya mkulima, achukuliwe kama mhujumu uchumi kama watu wengine tu.

Mbona kuna vitu vidogo watu wanafanya wanachukuliwa hatua? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakulima wanaendelea kuumia, utakuta ni viazi, gunia linapaswa kuwa kilo 80 mtu anachukua kilo 200 na analipa shilingi 30,000. Kwa mfano, kule kwetu Momba gunia la mpunga linapaswa liwe kilo 100, anaenda kuchukua kilo 250, halafu analipa shilingi 40,000. Huu ni unyonyaji uliopitiliza, ni uuaji na ni wizi kama wezi wengine tu ambao wanaiba huko mtaani. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, uadilifu na uamini wake ambao amewaahidi Watanzania hapa, tunaomba kuuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbolea, mimi ni Mbunge ninayetoka Jimbo ambalo lipo mpakani. Kule Momba tuna Tarafa tatu, tuna Tarafa ya Ndalambo, tarafa hii ipo barabarani na ndiyo Tarafa ambayo inapakana na Zambia. Mawakala wake wote ambao anawatuma wanaishia kuuza mbolea pale kwa sababu wanataka kushirikiana na wafanyabiashara wezi ambao wanavusha mbolea kupeleka Zambia. Katika hili Mheshimiwa Waziri, Ofisi yake inajua vizuri sana namna ambavyo wapo watu wasiokuwa waaminifu wanauza mbolea Zambia. Mheshimiwa Naibu Waziri yupo hapo, analijua sana hili sitaki kuongelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi kile walijitahidi kwamba, sijui wamechukua hatua, hakuna lolote sasa hivi wamebadilisha mfumo, lakini mbolea kwenda Zambia inaenda. Takwimu zinakuja kubwa, watu wa Mkoa wa Songwe wameingia kwenye orodha kubwa ya kuonekana ni watu ambao wanalima sana kwa kutumia mbolea. Tarafa ya Kamsamba yenye Kata sita za Ivuna, Mkomba, Mkulwe na Chilulumo hawajawahi kupata mbolea. Tarafa nzima ya Msangano ambao ndiyo wanaongoza kwa kulima mpunga pamoja na Chitete kuna skimu ya umwagiliaji hawana mbolea. Mbolea inaenda wapi kwenye takwimu inaonekana ni kubwa, kwamba tumetumia mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba uendelee kuongeza ujuzi wa namna ya kumsaidia mkulima wa kawaida ambaye anaumia, mpaka sasa hivi anayeumia ni mkulima wa kawaida, naamini

hata majimbo mengine wenzangu wameongea hapa kwamba, mbolea zinaishia mijini hazifiki vijijini, mkulima wa kawaida na mdogo yupo kijijini hayupo mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na masoko Mheshimiwa Waziri bado Wizara yake haijalitendea kikamilifu Soko la *DRC - Congo*. Soko la *DRC Congo*, Nchi ya Tanzania hatujalitendea haki hata kidogo, Mheshimiwa Waziri anajua ni kwa kiasi gani ambavyo kuna maghala yalifunguliwa kule yameishia wapi? Huwezi kuwa unaenda kuuza mchele na unga *DRC,* unatoa unga Iringa, unatoa unga Mwanza katika uchumi, hizo ni biashara gani si utapata hasara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshaiambia Wizara na taasisi yake wanaohusika tumewapa eneo pale Kakozi, ambapo watapata malighafi kwa bei rahisi, mahindi ya kutosha kutoka kwa watu wa Rukwa, watapata mahindi ya kutosha ndani ya Jimbo la Momba lenyewe, kwamba watengeneze kiwanda pale wasindike unga, watengeneze mchele wakauze *DRC*. Wazambia wanaishia kuchukua mchele wetu wana-*brand* wanaenda kuuza *Congo*. Bado hatujaweza kumsaidia mkulima kwenye masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *as we are speaking now,* ndani ya Jimbo letu, mahindi sasa hivi yananunuliwa shilingi 35,000 mpaka shilingi 40,000, lakini kama kungekuwa kuna soko zuri, wamefungua kiwanda pale wanasindika, naamini wakulima wengi wangeenda kuuza mazao pale. Hata wale wachuuzi wanaoenda wangenunua vizuri, kwa sababu *demand* ingekuwa *high*, kwa vyovyote vile *price* ingeweza ku-*shoot*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la *BBT*. Mheshimiwa Waziri wazo lake lilikuwa ni jema, lakini jambo hili tunaomba akalifanye jambo hili la *BBT* kwenye maeneo yetu *locally*. Hata hayo mashamba ambayo anawatafutia vijana anawapa, mengine yangetumika mashamba yao wao wenyewe. Kwa hiyo, hata gharama za kuendesha hiyo programu ingekuwa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wapo kule vijana wanataka kuwezeshwa wapate mbegu na mbolea. Wangefanya hilo zoezi wangesaidia vijana wengi wa Kitanzania. Hatusemi vijana wa Kitanzania wabaguliwe kusaidiwa, la hasha! Vipo vipaumbele, kama hiyo mikoa wanaitambua kwamba inaongoza kwa kuzalisha chakula, tunataka nguvu itumike huko wazalishe ili waweze kuleta tija kwenye nchi hii. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Condester kengele ya pili imeshagonga. Sekunde 30 malizia.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Spika, sekunde 30. Mkoa mzima wa Songwe zaidi ya 70% tunatumia mbegu kutoka Zambia. Shida ipo wapi kwa watu wa Waziri wa utafiti wa *TARI* na watu wa mbegu? Kwa nini mbegu za kutoka kwenye nchi yetu zisifanywe kwenye Mkoa wa Songwe? Waziri ana kazi ya kufanya, *otherwise* naunga mkono hoja ya bajeti yake. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Michael Kembaki atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba na Mheshimiwa David Ernest Silinde ajiandae.

Mheshimiwa Kembaki hayupo, tuendelee.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mungu anayeendelea kunijalia afya na nguvu ya kuendelea kuwatumikia wananchi wangu.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Bashe pamoja na timu yake kwa kazi kubwa anayoifanya kwenye Wizara ya Kilimo, kwa muda mfupi tumeona mageuzi makubwa sana, Wizara ameitendea haki. Nazidi kumwombea neema na msaada wa Mungu ili Mungu aendelee kumpa maono makubwa kwa ajili ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze na kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wetu kwa kuendelea kuongeza bajeti ya kilimo na hii ni kutambua umuhimu wa Sekta ya Kilimo kuwa ndio uti wa mgongo wa Taifa, lakini pia Mheshimiwa Rais kutambua umakini na usimamizi mzuri unafanywa na Wizara ya Kilimo chini ya Mheshimiwa Bashe.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Kilimo ndio sekta inayotoa ajira nyingi kuliko sekta nyingine yoyote, hii ni sekta muhimu kwa Taifa, tukiendelea kuweka nguvu zaidi na kuiongezea bajeti chini ya Waziri makini Mheshimiwa Bashe tunakwenda kuliongezea Taifa fedha nyingi za kigeni ambazo tunazihitaji sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kuuza kahawa kwenye mnada ngazi ya *AMCOS;* nimpongeze sana Mheshimiwa Bashe kwa kuruhusu kahawa kuuzwa kwa njia ya mnada kupitia *AMCOS,* hii imekuwa na mafanikio makubwa sana, utaratibu huu wanachama wa *AMCOS* kukusanya kahawa yao pamoja na ushindani wa mnada kufanyika ngazi ya *AMCOS* inaleta uwazi, bei nzuri na inaondoa mambo mengine yaliyokuwa yamejificha katika utaratibu wa zamani.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu unampa nguvu mwananchi au wana *AMCOS* kuamua kuuza kahawa au kutouza akisubiria bei nzuri ya soko, lakini kupitia utaratibu huu tumeshuhudia bei ya kahawa kupanda mfano kwa Kyerwa mwaka 2021/2022 bei ilkuwa kati ya shilingi 1,100 mpaka shilingi 1,500. Baada ya mnada kufanyika ngazi ya *AMCOS* mwaka 2022/2023 bei imetoka shilingi 1,800 mpaka shilingi 2,800 na mwaka 2023, bei imefika shilingi 3,200. Haya ni mafanikio makubwa na ukombozi wa mkulima, Mheshimiwa Mama Samia na Mheshimiwa Bashe tunawashukuru sana kwa maamuzi hayo magumu yaliyokuwa yameshindikana miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, nashauri utaratibu huu kwa kuwa umeonesha ufanisi mkubwa na umeleta uwazi, nashauri utumike kwa mazao mengine ya kimkakati kwa sababu ndio mkombozi wa mkulima.

Mheshimiwa Spika, naomba nimtie moyo Mheshimiwa Bashe asirudi nyuma katika hili, tunamwombea na tuko pamoja na yeye, mafanikio yoyote lazima yawe na maumivu na kuna upande mmoja lazima uumie, najua Mheshimiwa Bashe kwa kuruhusu na kusimamia utaratibu huu wako waliokuwa wakinufaika na utaratibu wa minada ya mwanzo hawawezi kufurahi hata kidogo.

Mheshimiwa Spika, niipongeze sana Serikali kwa kuanzisha Benki ya Ushirika, nataka nitoe na nishauri benki isiishie kwa wakulima wakubwa au wanunuzi wakubwa, benki hii iangalie namna itakavyomsaidia mkulima wa hali ya chini ambao ni wanachama wa *AMCOS,* wasaidiwe pale anapohudumia mazao yake mpaka anapopeleka mazao yake sokoni.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu pamoja na mafanikio niliyoyataja hapo juu bado wananchi wanapata wakati mgumu na biashara ya butura na kangomba ambayo biashara hii inawaacha wakulima wakiwa maskini, kama mkulima amejisajili kwenye *AMCOS* na shamba lake linajulikana, ni kwa nini asikopeshwe akahudumia mazao yake ili kuepukana na biashara ya kangomba na butura.

Mheshimiwa Spika, ili tuwe na kilimo chenye tija tunawahitaji Maafisa Ugani wa kutosha, hapa Mheshimiwa Waziri Bashe lazima tumwombe sana aongeze nguvu kubwa sana, bado Maafisa Ugani waliopo hawajaweza kutimiza majukumu yao ipasavyo, Maafisa Ugani tunataka tuwaone pale mwanzo mkulima anapoanza kulima mpaka anapovuna, Maafisa Ugani wakimsaidia mkulima ipasanyo tutaongeza uzalishaji na mavuno yenye ubora na hapo ndipo tutakapoongeza mauzo ya nje na kuliingizia Taifa fedha nyingi za kigeni. Maafisa Ugani waliopo sasa baadhi yao walio wengi tunawaona pale mkulima anapoanza kuvuna, wakianza kuwasumbua wakulima na kuwakamata hovyo, kama wangeanza tangu mwanzo mkulima anapoanza kupanda, anapalilia mpaka anavuna itaondoa sintofahamu wakati wa mavuno kuanza kukimbizana na wananchi na kutengeneza mianya ya rushwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko ya kimkakati; Kyerwa tunayo masoko ya Nkwenda na Murongo, masoko haya ni ya miaka mingi yametelekezwa, nimpongeze Mheshimiwa Bashe kwa kuyachukua ili wayakamilishe, ni jambo jema kwa sababu ya umuhimu wake, masoko haya yakikamilika yanakwenda kumsaidia mkulima, lakini pia kuwavutia majirani zetu kuuza na kununua kwetu na yakaliingizia mapato ya kigeni. Nimwombe sana Mheshimiwa Bashe masoko haya yakamilike, maana tangu ameeleza kutangaza *tender* imepita karibu mwaka sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miche ya kahawa; Kyerwa ndio Wilaya inayozalisha kahawa nyingi, lakini pamoja na kuzalisha kahawa nyingi, mibuni mingi ni ya miaka mingi na mingine imeshambuliwa na ugonjwa wa mnyauko. Ombi langu nimwombe sana Mheshimiwa Bashe kutuongeza miche ya kahawa angalau iwe shilingi 10,000 kwa sababu mahitaji ni makubwa sana na kama ajuavyo kila kilo inayouzwa inakatwa pesa kwa ajili ya kuendeleza zao la kahawa na Kyerwa ni mzalishaji mkubwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niendelee kumwombea Waziri mafanikio na naunga mkono hoja.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Wizara ya Kilimo, kwanza kwa kumpongeza Waziri Mheshimiwa Bashe na Naibu Waziri pamoja na timu nzima kwa kazi nzuri na ubunifu katika kufanya majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ya kuharakisha maendeleo katika sekta zote, sisi Wanamtwara tuna mambo mengi sana ametufanyia, tunamshukuru sana kipekee kwa Sekta ya Kilimo naomba kutaja machache: -

(a) Upanuzi wa Bandari ya Mtwara ili kuwezesha korosho kusafirishwa;

(b) Upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima wote na hasa viatilifu vya korosho *(sulphur);* na

(c) Kupanda kwa bei ya mazao hasa ufuta na mbaazi. Kwa msimu uliopita mbaazi imeuzwa 4,000 kwa kilo jambo ambalo halijawahi kutokea tangu tupate uhuru, wananchi wa Mtwara walifurahi na kuishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia changamoto zifuatazo:-

(1) Upatikanaji wa viatilifu usimamiwe na Bodi ya Korosho;

(2) Wizara itafute masoko nje ya nchi hasa Vietnam kwa ajili ya korosho badala ya wanunuzi kutumia mawakala;

(3) Wizara isimamie kwa karibu sana mfumo mpya wa ununuzi wa korosho ambao Tume imependekeza yaani *TMX* badala ya boksi;

(4) Tozo nyingi za korosho zinapunguza bei kwa mkulima hivyo zipunguzwe hasa tozo ya *TARI* shilingi 25 na Bodi shilingi 25 zote kwa sasa zifutwe;

(5) *Export levy* 100% ipelekwe Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kuendeleza zao la korosho; na

(6) Mradi wa kongani ya korosho Maranje iendelee.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, naomba mapendekezo ya Tume Maalum yafanyiwe kazi yote ili kuboresha uzalishaji wa zao la korosho

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa,

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mawaziri na viongozi wote wa Wizara ya Kilimo, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Kilimo kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Serikali katika utekelezaji wa ustawi wa jamii na maendelo endelevu. Hii ni mojawapo ya nguzo kuu katika utayari wetu wa Ushindani wa Kimataifa *(National Competitiveness)*. Bajeti hii inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Spika, kulingana na taarifa ya Wizara ya Kilimo, Tanzania ina hekta milioni 44 zinazofaa kwa kilimo cha mazao, kwa wastani hekta milioni 10.8 tu sawa na 24% ndizo zinazolimwa kila mwaka. Sekta hii kwa mwaka 2022 imechangia asilimia 26.1 kwenye pato la Taifa, imetoa ajira kwa wananchi kwa wastani wa 65% na imechangia 65% ya upatikanaji wa malighafi za viwanda. Sekta ya Kilimo ni mhimili wa uchumi wa nchi na inachangia pato la mkulima mmoja mmoja, kaya na Taifa kwa ujumla. Sekta ya Kilimo na hususani sekta ndogo ya mazao imechangia 15% katika pato la Taifa na zaidi ya 100% ya upatikanaji wa chakula kinachozalishwa nchini na kupelekea utulivu wa mfumuko wa bei kwa takriban 59%.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko kubwa la mauzo ya mazao nje ya nchi kufikia dola za Marekani bilioni 2.3, nashauri Serikali ichukue hatua za kuhamasisha taasisi za fedha kuongeza utoaji mikopo kwenye Sekta ya Kilimo ili kuoanisha na mchango wa kilimo kwenye pato la Taifa, nashauri Serikali kuboresha mifumo ya TEHAMA ili isomane kati ya Taasisi za Kilimo, Wizara ya Kilimo, Benki Kuu, Wizara ya Fedha, *TRA* na hata Bandarini. Kwa

kuboresha mfumo mzuri wa TEHAMA unaosomana, Serikali itaweza kupata taarifa sahihi za uzalishaji, mauzo nje ya nchi, mapato ya fedha za kigeni na hata kuongeza mapato ya kodi. Kwa sasa mchango wa kilimo wa chini ya asilimia moja kwenye makusanyo ya kodi, ni mdogo sana kulingana na kilimo kuajiri zaidi ya 65% ya Watanzania. Pamoja na kushamiri kwa biashara ya mazao nje ya nchi, bado mapato ya fedha za kigeni kutokana na biashara hizo, hayajawa bayana kupunguza urari wa biashara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujitosheleza kwa chakula na kuchangia katika uchumi wa Taifa, takribani mazao yote yanazalishwa kwa tija ndogo katika eneo husika. Uzalishaji wa mahindi wa chini ya tani mbili kwa hekta moja ni asilimia 29 tu ya uzalishaji unaotegemewa wa tani sita kwa hekta moja. Uzalishaji huu wa chini kwa mazao yote kwa kiasi kikubwa unatokana na ukosefu wa ushauri wa watalaam wa kilimo ikiwemo matumizi yasiyo sahihi ya mbolea na pembejeo zingine. Katika hali hii, kilimo hakijamsaidia mkulima kwa kiasi kikubwa kujinasua kwenye umaskini na kimeendelea kutoa mchango mdogo kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa mbolea nchini hadi Aprili, 2024 ulikuwa tani 1,052,218.4 ambayo ilikuwa juu ikilinganishwa na tani 819,442 mwaka 2022/2023. Pamoja na bei za mbolea kwenye soko la dunia kuanza kupungua, bado zilikuwa ni za juu na tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kutoa ruzuku. Hatua hii muhimu ni mafanikio makubwa katika safari ya kuleta tija kwenye kilimo nchini na napendekeza kuendelea na ruzuku ya pembejeo pamoja na kuanzisha *Price Stabilization Fund* kwa pembejeo hasa mbolea ili kuongeza tija kwenye uzalishaji wa mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali iendelee kuimarisha usalama wa chakula nchini kwa kununua na kuhifadhi nafaka kupitia Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula. Kutokana na ukame maeneo mengi katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati na pia kuendelea kwa vita ya Urusi na Ukraine kunaashiria kuendelea kuwa na upungufu mkubwa wa nafaka katika maeneo yanayotuzunguka. Kwa kuzingatia gharama kubwa za

uzalishaji, Serikali ichukue hatua za makusudi kusaidia wakulima wapate bei nzuri ya *NFRA* badala ya kuuza kwa walanguzi na kutorosha chakula nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuongezeka kwa idadi ya watu, kufikia mwaka 2030 biashara ya mazao ya chakula inakadiriwa kufikia dola za Marekani trilioni moja. Serikali ichukue hatua za makusudi kuboresha uzalishaji wa mazao ya chakula kutosheleza soko la ndani na nje. Uzalishaji wenye tija kwenye kilimo utaongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na kupunguza pengo la urari wa biashara.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie fursa za Kiwanda cha Viuadudu cha Kibaha kuanza uzalishaji wa viatilifu inayotokana na pareto ambayo inazalishwa hapa nchini na imekuwa inauzwa nchi za nje kama *semi-finished product* kwa bei ndogo ya kutupa. Viatilifu kutokana na pareto ni suluhisho la soko la pareto na pia suluhisho kwa upotevu wa mazao kushambuliwa na wadudu *(post-harvest losses)*.

Mheshimiwa Spika, Serikali ianze mchakato wa kuanzishwa viwanda vya mbolea kwa kutumia madini *(calcium carbonate, agricultural lime, phosphates, natural gas etc)* yanayopatikana kwa wingi hapa Tanzania ili kuanza uzalishaji wa mbolea hapa nchini. Kutokana na athari za vita ya Urusi na Ukraine zinazoendelea, iwe fursa kwetu kwa kuanza kutumia rasilimali zinazopatikani nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali iendelee kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo hasa kwenye miundombinu ya umwagiliaji. Matumaini pekee ni hatua zilizooneshwa kwenye bajeti ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji na Serikali iweke mikakati madhubuti kuhakikisha ufanisi wa utekelezaji wa bajeti hii ya umwagiliaji. Serikali iangalie utelezaji wa miradi ya mabwawa kuunganisha uratibu kwa mahitaji ya jumla kama vile mahitaji ya Wizara ya Mifugo na hata Wizara ya Maji, kunaweza kuwa na tija kuwa na chombo kimoja chenye nguvu zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia mikakati hii iweke nyongeza za ujenzi wa mabwawa hasa maeneo yenye mafuriko makubwa ikiwa ni pamoja na kuzuia mafuriko, lakini pia napendekeza Serikali iweke msukumo mkubwa wa kuharakisha utekelezaji wa miradi iliyomo kwenye Mradi wa Bonde la Mto Songwe *(Songwe River Basin Development Programme - SRBDP),* wenye ofisi zake Kyela, Tanzania. Mradi huu unaotekelezwa kwa pamoja na Serikali za Tanzania na Malawi, ni muhimu sana kwa sasa kutokana hasa na ujenzi wa mabwawa ambayo pamoja na manufaa mengine, yatasaidia kupunguza mafuriko ya Bonde la Kyela. Mabwawa haya yamelenga kuzalisha umeme, kilimo cha umwagiliaji, shughuli za uvuvi na hata utalii ambao unahitajika sana katika Wilaya ya Mbeya na ukanda wote wa Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua za haraka kuleta Bungeni mapendekezo ya Sheria ya Kilimo ambayo pamoja na mambo mengine itawezesha usimamizi wa matumizi bora ya ardhi ya kilimo ambayo inaendelea kupotea kwa matumizi ya makazi. Pia kutokana na changamoto za tabia nchi, kumekuwepo na uharibifu mkubwa wa mazingira na ongezeko la upungufu wa vyanzo vya maji. Uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu umepelekea misitu mingi kuharibiwa na uchomaji moto, ukataji mkaa na hata kilimo kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, napendekeza Serikali iongeze msukumo kwa Wizara za Maji, Kilimo, Maliasili na Mazingira kufanya kazi kama timu moja ili kukabiliana na janga hili kubwa ikiwemo ujenzi wa mabwawa makubwa katika maeneo yanayokumbwa na mafuriko. Kama ilivyo kwa athari za mafuriko ya Kyela, hata Ziwa Rukwa linaathirika sana na kujaa mchanga na udongo unaosombwa na mito kutokana na mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAIMUNA S. MTANDA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambayo ameendelea kuipa fedha Wizara ya Kilimo ili kuongeza uzalishaji katika mazao mbalimbali yakiwemo ya chakula na biashara, lakini pia niwapongeze pia

viongozi wa Wizara ya Kilimo kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuisimamia Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao la korosho kwa upande wa viatilifu; tunaishukuru Serikali kwa kuendelea kutupatia pembejeo bure kwa wakulima wetu. Naomba Serikali isimamie ubora wa pembejeo zinazopelekwa kwa wakulima wetu. Zipo dosari chache za kiutendaji kutoka kwa wasambazaji wetu, kufuatia ripoti ya Tume iliyoundwa kuchunguza mwenendo mzima wa zao la korosho, yapo maelezo ya dawa isiyostahili kwenye zao la korosho ambayo msimu uliopita walipewa wakulima. Sumu ambayo ni kwa ajili ya maua ya *rose* na mbogamboga wamepewa wakulima wa korosho. Matokeo ya dawa za namna hii ni kuharibu mimea na kuathiri uzalishaji. Tunaomba dawa ile kwa mamlaka yenu wakulima waarifiwe wasiitumie na zoezi hili lifanyike mapema kwa kuwa huu ndio msimu wa maandalizi ya mashamba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu waatalam wetu tulionao *site* (Maafisa Ugani) wapewe mafunzo ili nao wajue namna ya kutumia viatilifu vinavyoletwa kwenye maeneo yao. Wengi hawajui, hali inayowafanya wakulima kulima kwa mazoea. Rejea maelezo ya taarifa ya Ripoti ya Tume iliyoundwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mfumo wa *TMX* niiombe Serikali isimamie vizuri mfumo huu ili ulete tija kwa wakulima. Tusiruhusu watu wenye maslahi binafsi kuuingilia mfumo huu, isije wakaja wale wanunuzi wahuni waliokuwa wanajimilikisha makampuni zaidi ya kumi kwenye mtindo wa kulaza sanduku wakijifanya ni watu tofauti kumbe ni mnunuzi mmoja yule yule ndiye anajifanya makampuni kumi. Tuwe makini tusije tukaharibiwa na wajanja wachache.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mjengeko wa bei ya korosho, naiomba Serikali ijitahidi kututafutia masoko ya uhakika ya kununua mazao yetu. Aidha, suala la tozo katika bei ya korosho liangaliwe upya kwa sababu tozo nyingi zinaathiri malipo ya mkulima moja kwa moja. Mfano tunaposema shilingi 110 ya gunia

analipia mnunuzi, sio sahihi kwa sababu mwisho wa siku kimsingi anayelipia ni mkulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uhakiki wa idadi ya miche ya mikorosho kwa wakulima; zoezi limegubikwa na sintofahamu nyingi. Wengi hawajakwenda mashambani wamekadiria tu, matokeo yake ni kutotosheleza kwa pembejeo tunayowapatia.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali ya Mama Samia kwa kuendelea kutenga fedha kwenye bajeti kwa ajili ya ununuzi wa korona tano tangu Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi kwenye bajeti hii ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na kukarabati korona iliyopo shamba la Kibaranga, Wilayani Muheza kwa ajili ya kuwasaidia wakulima wadogo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi hizi za Serikali kuwasaidia wakulima wadogo, nasikitika kuwa ukarabati wa korona ya Kibaranga umefikia 80% na kinachokwamisha kuanza kazi ni uunganishaji wa umeme wa *TANESCO* ambapo miundombinu yote ya umeme ipo tayari, lakini kuna urasimu wa kufanya maunganisho. Namwomba Mheshimiwa Waziri aingilie kati uunganishwaji wa umeme na ikiwezekana Mawaziri wa Kilimo na Nishati wasaidie kuwaondoa wakulima katika mkwamo huo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi kubwa za Serikali kuwasaidia wakulima wa mkonge nchini, kumekuwa na uanzishwaji wa tozo na kodi mbalimbali kwa wakulima bila kufuata taratibu na katika hali inayokinzana na sheria mama za fedha. Kumekuwa na tozo ambazo hazina tija moja kwa moja na uzalishaji wa mkonge, kwa mfano tozo ya zimamoto na kukitokea moto hawafiki kusaidia. Tozo ya *OSHA* ambayo hutozwa kiwango kikubwa kwa kupima kila mfanyakazi bila kujali wafanyakazi hao wamelipiwa bima ya afya au laa. Serikali ione namna ya kusawazisha au kuziondoa kabisa.

**MHE. SAMWELI X. HHAYUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze mchango wangu kwa kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuongeza fedha kwenye Sekta ya Kilimo kutoka wastani wa bilioni 294 mwaka wa fedha 2021/20221 mpaka bilioni 1,248.96 mwaka wa fedha 2024/2025. Ongezeko hili ni kubwa na inaenda kuimarisha na kupata mafanikio kwenye maeneo yafuatayo:-

(i) Kuchangia kwenye pato la Taifa kwa zaidi ya 26.2% ya sasa;

(ii) Kuendelea kutoa ajira ya uhakika kwa Watanzania kwani Sekta ya Kilimo inaajiri zaidi ya 65.6% ya Watanzania;

(iii) Kuchangia zaidi ya 65% ya sasa ya malighafi ya viwandani ikiwepo eneo la vinywaji vinavyotengezwa kwa kutumia shairi; na

(iv) Kuzalisha ziada ya chakula ambayo tutauza nje ya nchi ili itupatie fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizoongezwa zitawezesha kilimo cha uhakika kwa umwagiliaji, nimshukuru sana Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe kwa kupokea na kufanyia kazi sehemu ya maombi yangu niliyowasilisha Wizarani kwa Skimu ya Umwagiliaji ya Endagaw kuendelea kuimarishwa, lakini kufanyika kwa usanifu wa Skimu ya Endasiwold ikiwepo kuchimbwa kwa visima maeneo ya Getasam, Balangdalalu, Laghanga na Qutesh.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iendelee kusimamia kilimo cha ngano na shayiri kwa kuhakikisha isitolewe kibali cha kuingiza nchini ngano na shayiri kabla ya kuhakikisha kuwa watumiaji wa ngano na shayiri wameshiriki kikamilifu katika hatua za kusaidia wazalishaji wa ngano na shayiri na kununua baada ya kuzalishwa. Haiingii akilini vitu ambavyo tunaweza kuzalisha hapa nchini tuendelee kuagiza toka nje ya nchi. Serikali ije na mkakati

wa kina wa uzalishaji wa ngano na shayiri ili kupunguza utegemezi wa mazao haya nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mbegu za shayiri ni kizungumkuti, mwaka huu mbegu walizopewa wakulima hazikuota na imekuwa kilio kikubwa kwa wakulima wangu wa Hanang. Jambo la mbegu ya shayiri nimeshaifikisha Wizarani, naomba ufuatiliaji wa kina ufanyike na wakulima walioathirika wafidiwe ipasavyo na kampuni iliyoleta mbegu ambazo hazina kiwango.

Mheshimiwa Spika, naomba kumkumbusha Waziri kuhusu ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Gidahababieg, Skimu ya Umwagiliaji Bwawa la Bassotughang na kuona namna ya kuimarisha kilimo cha umwagiliaji Ziwa Bassotu.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nianze mchango kwa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Bashe kwa kazi nzuri sana ambayo ameifanya. Mheshimiwa Bashe amewatendea haki wakulima wa nchi hii na kwa sasa kilimo siyo cha mazoea tena, ni kilimo biashara. Niendelee kumpongeza Naibu Waziri wa Kilimo, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na Taasisi kwa kuleta mageuzi katika kilimo.

Mheshimiwa Spika, nitachangia mambo yafuatayo nikianza na Tume ya Umwagiliaji. Napongeza kazi nzuri inayofanywa na Tume hii na ongezeko la bajeti.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wetu wa Iringa tunayo miradi ya umwagiliaji ambayo ni ya muda mrefu sana. Ushauri wangu, Tume sasa ifanye upembuzi yakinifu ili kuweza kukamilisha miradi ya muda mrefu kabla ya miradi mipya haijaanza ili pia kupunguza gharama, sababu miradi ikichukua muda mrefu gharama zinaongezeka. Pia kuna miradi ambayo haifanyiwi ukarabati na kusababisha miradi hiyo ianze kujengwa upya. Naomba kujua vigezo vinavyotumika katika hii miradi ya

umwagiliaji kwa sababu kuna baadhi ya mikoa ina miradi mingi na mikoa mingine hakuna.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao la parachichi, naipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwa na mkakati maalum wa zao hili, tunaamini kuwa wananchi wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini tunakwenda kuwa dhahabu, naamini sasa mkakati uliowekwa kwa ajili ya kuondoa changamoto hizo itakwenda kuzimalizika kabisa hasa kuhusiana na miche bora ya ruzuku, masoko ya uhakika kwa wakulima hasa kwa maeneo yasiyo sehemu na ku-*pack* na kuhifadhi matunda haya ili kuyapeleka sokoni.

Mheshimiwa Spika, pia napongeza mpango mzuri unaofanywa na Serikali wa kuwa *block farm* kwa ajili ya kilimo cha parachichi, ni jambo jema japo lazima kuwepo na usimamizi na mpango mzuri wa uratibu kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao la pareto, zao hili linalimwa na wakulima wa Nyanda za Juu Kusini ukiwemo Mkoa wa Iringa na kuna wakulima wanalima kilimo cha mkataba. Naomba kujua mkakati wa kusaidia Kiwanda cha Pareto kilichopo Mafinga Wilaya ya Mufindi ili kuweza kuchakata zao hili ili kuweza kuleta manufaa kuliko kusafirisha maua ya pareto.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya wakulima kutofikisha mazao sokoni kwa kipindi cha mvua ya masika; hii ni changamoto kubwa sana hasa kwa wakulima wetu wa Mkoa wa Iringa, sababu barabara nyingi zinazotoka mashambani ni za *TARURA* hazipitiki kabisa na wakulima wetu wanalima mazao ya mbogamboga na matunda kama nyanya, vitunguu, njegere, kabichi na kadhalika. Mazao haya yanaoza mashambani kwa sababu hakuna magari yanapita kwenda kuchukua bidhaa hizo, sasa nini mpango mkakati wa kuwasaidia wakulima hawa sababu wengi wao wamechukua mikopo benki? Wanateseka sana.

Mheshimiwa Spika, napongeza mpango mzuri wa kuwawezesha vijana na akinamama kwa Mradi wa *BBT*, ni mradi mzuri sana na utasaidia kwa kiasi kikubwa kutoa ajira kwa vijana wengi na akinamama nchini. Tunaomba ikiwezekana halmashauri

zote wapatiwe mradi huu na pia kwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwezekana mikopo ile inayotolewa na halmashauri ya akinamama, vijana na watu wenye ulemavu iwe pia ya kilimo ili Wizara isaidie utaalam tu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nampongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia, mama yetu kipenzi kwa kuona umuhimu wa kuendelea kuongeza pesa kwa Wizara hii ili kuwatendea haki wakulima ambao ni zaidi ya 80%.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikianza na kilimo cha umwagiliaji kiwe ndiyo uti wa mgongo wa Wizara na Kilimo badala ya kutegemea mvua za kudra ya Mwenyezi Mungu. Kilimo kiwe cha kisasa kwa kukibadili kutoka jembe la mkono mpaka kilimo cha zana za kisasa mfano matrekta na zana nyingine. Pia kuwe na vituo vya zana za kulimia vijijini vinavyoweza kukodishwa na wakulima. Nashauri mbolea zifungwe katika mifuko ya kiasi cha kilo mbalimbali ili wakulima wanunue kiasi wanachohitaji na kumudu.

Mheshimiwa Spika, katika Kijiji cha Majengo, Kata ya Ikongolo Uyui kuna mradi wa kusanifu bwawa la umwagiliaji, tafadhali wananchi wana mategemeo makubwa na bwawa hili, mradi huu uendelezwe kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

**MHE. BENARDETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote katika Wizara hii, kwa kazi nzuri sana inayolenga kuleta mapinduzi ya kilimo nchini. Hongera sana wanastahili sifa.

Mheshimiwa Spika, wameweka nguvu nyingi sana kwenye kuboresha na kupanua kilimo cha umwagiliaji ili wakulima waweze kulima, kumwagilia na kuwawezesha kulima na kuvuna

mwaka mzima. Natambua juhudi zinazolenga kuboresha kilimo cha kahawa nchini, hususan Mkoa wa Kagera. Mkoani Kagera kahawa ni biashara na ni siasa. Niwaombe ziwepo juhudi za makusudi ili bei ya kahawa iendelee kupanda ili mkulima aweze kunufaishwa na kilimo chake.

Mheshimiwa Spika, Mkoani Kagera kilimo cha *vanila* kilianza kwenye miaka ya 80 hivi. Viongozi wa mkoa walihamasisha na watu wengi wakaingia kwenye kilimo cha *vanila*. Wananchi wamekuwa wakinufaika na kilimo hiki, wamesomesha watoto, wamenunua pikipiki, wamejenga nyumba kutokana na mauzo ya *vanila*.

Mheshimiwa Spika, huko nyuma Shirika la Mayawa ndio waliendeleza hiki kilimo kwa kutoa elimu, huduma za ugani na masoko. Miaka ya hivi karibuni Mayawa ilipata changamoto na kuacha kabisa kununua *vanila*. Wapo wakulima ambao yapata miaka mitatu au minne hawajalipwa fedha zao walizouza *vanila*. Mwaka jana alijitokeza mnunuzi mmoja, akaomba kununua, mkoa ukampa kibali, akanunua na akapotelea kusikojulikana bila kuwalipa wakulima hadi leo. Kuna kilio kikubwa sana cha wakulima wa *vanila.*

Mheshimiwa Spika, nimeshamfuata Mheshimiwa Waziri mara kadhaa kuhusu kilimo cha *vanila*, hata Wabunge wa Kagera wengine nao wameongelea *vanila*, lakini hatujui Serikali wana mpango gani wa kuwasaidia wakulima wa *vanila* ili waweze kupata soko la uhakika. Ni kweli bei ya *vanila* kidunia imeshuka, lakini hata kahawa kwa miaka kadhaa bei ya kahawa iliporomoka, lakini waliendelea kuwa na soko na hivyo kilimo kiliendelea.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana Waziri aliniahidi kuwa anakuja mnunuzi wa *vanila* na atajenga kiwanda pale Maruku, lakini Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, kwenye hotuba yake ya bajeti sikusikia neno hata moja kuhusu kilimo na mkulima wa *vanila*. Kwa mwaka huu wa 2024, msimu wa kuvuna *vanila* unaanza Juni – Julai, je, hawa wakulima maskini wa *vanila* watauza wapi? Je, sisi wawakilishi wa wananchi tukirudi mkoani tuwaeleze nini wakulima

hawa? Je, Serikali wanawasaidiaje wakulima wa *vanila* Kagera na wanawapa matumaini gani?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, natambua kazi kubwa inayofanywa na Wizara ya Kilimo kwa usimamizi wa Mheshimiwa Hussein Bashe kwa kushirikiana na wasaidizi wake wa Wizara ambapo wamekuwa mstari wa mbele katika kutafsiri maono ya Mheshimiwa Rais katika kuinua Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wangu napenda kuchangia kuhusiana na uwepo wa zao la viungo ambapo kwa upande wa Morogoro Kusini Mashariki limekuwa zao linalostawi vizuri na kutoa mazao yenye kuvutia soko, hivyo naomba mambo yafuatayo:-

(i) Tunaomba Wizara itambue na kusaidia kutambulisha mazao ya tangawizi, mdalasini na vitunguu;

(ii) Serikali itoe mbegu na pembejeo zingine ili kulipa uzito zao la viungo;

(iii) Kuendeleza mpango wa ugawaji miche katika maeneo yetu ili kulinda maendeleo ya kilimo cha viungo; na

(iv) Tunaomba kufanyiwa marekebisho ya Skimu ya Umwagiliaji ya Kiroka ambayo itakuwa mkombozi mkubwa wa kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Spika, Serikali itafute soko la uhakika la zao la mahindi Ludewa, pia Serikali ijenge maghala ya kuhifadhia mahindi Ludewa na mabwawa ya kilimo cha umwagiliaji yanayojengwa Ludewa yaweze kupandwa samaki. Pia Serikali iwekeze sana eneo la uzalishaji mbegu na isimamie ufungashaji ambao utaepusha utengenezaji wa mbegu *fake* hasa mbogamboga na mahindi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbegu ya mahindi ya *Pana 53* imefanya vizuri sana Ludewa na Ruvuma ila inazalishwa Zambia. Serikali ifanye utafiti wa mbegu hii, izalishwe na kuhakikisha inapatikana kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TFRA* wawe na ofisi ngazi ya mikoa, wananchi wanaipongeza sana Serikali kwa kufungasha mbolea kilo 25 na wanaomba iwepo ya kilo 10 na kilo tano.

**MHE. REGINA N. QWARAY:** Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kuendelea kuipa nguvu Wizara ya Kilimo kwa kuongeza bajeti. Hii inadhihirisha kuwa Serikali imedhamiria kuinua wananchi walio wengi kwani tunafahamu kilimo ni uti wa mgongo.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, upimaji wa usalama wa vyakula nchini katika masoko ya ndani kwa ajili ya mabaki ya sumu *(residuals)* inayotokana na mbolea, madawa na wanyama kutokana na matumizi holela ya viatilifu na madawa ya mifugo ndiyo inahatarisha afya za Watanzania. Napendekeza kuwekwe vifaa vya upimaji katika masoko yote nchini na utoaji wa elimu ya matumizi ya viatilifu na madawa ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu masoko, bado kuna haja ya Serikali kuangalia namna ya kusogeza karibu upatikanaji wa masoko kwa wakulima. Katika hili nishauri kuwepo na mawasiliano ya karibu na Wizara nyingine na Serikali iangalie suala ya miundombinu maana kama tunavyojua kwa sasa barabara ni mbovu, wananchi watashindwa kusafirisha mazao yao.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumpongeza Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe kwa hotuba yake ya bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Ni hotuba nzuri yenye taarifa na takwimu muhimu za kutuwezesha Waheshimiwa Wabunge kujadili na kushauri Serikali kuhusu sekta hii muhimu ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Tume ya Umwagiliaji; Tume na Wizara zimeanzisha miradi mingi kwa wakati mmoja na imeshindwa kukamilisha hata mradi mmoja tangu Mwaka wa Fedha 2022/2023. Hivi sasa Tume inatekeleza miradi 780 ambapo kati ya miradi hiyo 17% ni miradi ya tangu Mwaka wa Fedha 2022/2023.

(i) Mradi wa Ujenzi la Bwawa katika Kijiji cha Mwaukoli, Jimbo la Kisesa, Wilaya ya Meatu; ujenzi ulitarajiwa kuanza Juni Mosi, 2023 na kukakimilika Juni Mosi, 2024, lakini hadi sasa mradi huu uko katika hatua ya kumpata mshauri elekezi, miaka miwili iliyopita.

(ii) Skimu 25 za umwagiliaji zinazoendelea na ujenzi (Kiambatisho Na.1), wastani wa utekelezaji ni 30% na miradi mingine iko kwenye hatua za usanifu na mingine kutangazwa zabuni na hakuna mradi hata mmoja uliokamilika.

(iii) Miradi 30 ya skimu za umwagiliaji zinazoendelea na ukarabati (Kiambatisho Na.2), wastani wa utekelezaji wa miradi ni 32% na mradi mmoja uko kwenye hatua ya kumpata mkandarasi, hakuna mradi uliokamilika.

(iv) Mabwawa 14 ya umwagiliaji yanayoendelea na ujenzi (Kiambatisho Na.3) ambayo wastani wa utekelezaji ni 40% na hakuna mradi uliokamilika.

(v) Miradi 711 ya skimu na mabwawa ya umwagiliaji (Kiambatisho Na. 4, 5, 6, 7, 8, 9, 10) ambapo miradi hii iko kwenye upembuzi yakinifu na usanifu, manunuzi ya kumpata mshauri elekezi, hatua ya kusaini mikataba, hatua za manunuzi ya ujenzi na miradi michache ambayo ujenzi umeanza.

(vi) Fedha zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge katika kipindi cha miaka hiyo miwili ni shilingi bilioni 631.85 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya skimu na mabwawa ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, Waziri atuambie ukweli nini sababu ya kusuasua kwa miradi hii hadi leo miaka miwili hakuna mradi uliokamilika hata mmoja. Pia mwaka jana nilihoji hapa Bungeni sababu za kubadilishiwa matumizi fedha za umwagiliaji takribani shilingi bilioni 200 na bila ridhaa ya Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa mbolea ya ruzuku, wanufaika wa mbolea ya ruzuku; katika Mwaka wa Fedha 2022/2023 wananchi 3,389,951 walijiandikisha kupata mbolea ambapo kati yao wananchi 2,551, 239 hawakupata mbolea sawa na 75% pamoja na kwamba walikuwa na sifa zote za kupata mbolea ya ruzuku. Licha ya kuripotiwa kuwa na bakaa ya mbolea ya tani 326,344. Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 wakulima waliosajiliwa katika mpango wa mbolea ya ruzuku walifikia 3,910,556. Hotuba ya Waziri haijaeleza idadi ya wanufaika wa mpango wa mbolea ya ruzuku katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, Waziri atuambie sababu za kuwafikia wakulima 25% tu huku idadi kubwa ya wakulima wakikosa mbolea ya ruzuku, ruzuku ya mbolea inayotolewa na Serikali ni haki ya wananchi wote wenye mahitaji. Jambo hili tumelilalamikia hapa Bungeni mwaka jana lakini hatuoni hatua za Wizara za kuhakikisha wakulima wote wanapata mbolea. Hawa wananchi waliokosa mbolea wanaendeshaje shughuli zao za kilimo? Ruzuku ya mbolea ni kwa ajili ya kundi fulani la wakulima?

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa fedha kugharamia mpango wa mbolea ya ruzuku katika Mwaka wa Fedha 2022/2023, *TFRA* na Wizara ya Kilimo walinunua mbolea ya ruzuku yenye thamani ya shilingi bilioni 480 wakati bajeti iliyoruhusiwa na Bunge ilikuwa ni shilingi bilioni 150, hili ni sawa na ongezeko la 220%. Wizara ilipata wapi kibali cha kununua mbolea ya ruzuku zaidi ya shilingi bilioni 330 ya kiwango kilichoruhusiwa na Bunge. Waziri atoe maelezo ya kutosha kuhusu suala hili kwani hana mamlaka kisheria kubadilisha matumizi ya vifungu na bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa bei elekezi ya mbolea ya ruzuku, ili kupata tija katika utoaji wa mbolea ya

ruzuku, ni lazima bei zinazotangazwa ziwe halali, wakulima wamudu bei hizo na fedha za umma zitumike kihalali. Pasipo usimamizi imara na kuwepo bei elekezi *(indicative price)* ruzuku inayotolewa haiwezi kuwanufaisha wakulima kwani bei zitaendelea kuwa juu na kuwepo madai hewa ya waagizaji na wasambazaji wa mbolea.

Mheshimiwa Spika, kukosekana msingi wa mjengeko wa bei na hivyo kwa sehemu kubwa bei inatokana na matamko ya wafanyabiashara, *TFRA* na Wizara kuacha kutumia mfumo wa *BPS* katika kuagiza na kusambaza mbolea nchini na hivyo kuondoa ushindani na manufaa ya ununuzi wa pamoja *(economies of scale)*. Katika mwaka wa fedha 2022/2023 manunuzi ya kutumia mfumo wa *BPS* ulikuwa 6.3% tu.

Mheshimiwa Spika, *BPS* inataka kufanya uhakiki wa bei katika masoko mbalimbali *(due diligence)* ili kushindanisha wazabuni kwenye soko lenye bei nafuu na kuagiza kwa pamoja ili kupata bei nzuri. Hivyo kwa mazingira haya huwezi kushusha bei ya mbolea hata kama utatoa ruzuku.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi dhaifu wa bei elekezi, pamoja na kuwepo bei elekezi, lakini baadhi ya wauzaji na wasambazaji wa mbolea hawazingatii bei elekezi iliyotangazwa na *TFRA,* imethibitika kuwa wauzaji wengi wa mbolea *(Agro Dealers)* katika *LGA* zaidi ya 80% wanauza kwa bei kubwa tofauti na bei elekezi iliyowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala la ufuatiliaji wa dhaifu wa bei katika soko la dunia, karibu kila mwezi bei ya mbolea ilikuwa ikishuka, lakini bei ya mbolea hapa nchini ilibaki vilevile hadi Machi, 2023.

Mheshimiwa Spika, utoaji wa mbolea ya ruzuku una tija ndogo kwani unawafikia wakulima 25% tu, pia kuwepo kwa bei kubwa zisizo na uhalisia na matumizi makubwa ya fedha za umma unaopelekea kuharibu mipango mingine ya Serikali. Bado naamini kuwa kama kungekuwa na usimamizi makini wakulima wengi wangepata mbolea tena kwa bei nafuu na mzigo kwa Serikali ungekuwa mdogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu upatikanaji na usambazaji wa mbolea; mwaka jana nililalamikia juu ya matumizi ya mfumo wenye changamoto nyingi ikiwemo kukosa usalama *(security)* na kuruhusu kufanyika *multiple scanning,* pia kuwepo kwa mbolea *fake*/mbolea bandia, wakulima kuuziwa mchanga badala ya mbolea, kuuziwa mbolea iliyokwisha muda wa matumizi, utoroshaji nje ya nchi na kuliingiza Taifa kwenye hasara kubwa. Haya yote yanafanyika Waziri na *TFRA* wapo na hatujaona masahihisho yoyote kukabili changamoto hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uzalishaji wa mbolea ya ndani ya nchi; pamoja na nchi yetu kuwa na uzalishaji mkubwa wa mbolea ya samadi, mboji na uzalishaji wa viwanda vya ndani, lakini kwa sehemu kubwa tunaagiza mbolea kutoka nje ya nchi, Wizara haina mkazo wowote wa kuongeza matumizi ya mbolea za asili na pia viwanda vya ndani ikiwemo Kiwanda kipya cha *ITRACOM* ambapo umepelekea kuongeza uzalishaji wa mbolea na kufikia tani 114,224. Waziri atueleze ni kiasi gani cha mbolea ya ndani kimenunuliwa kupitia mfumo wa ruzuku ya mbolea? Nini mkazo wa Serikali wa kuongeza matumizi ya mbolea za asili?

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya madeni; Wizara imelipa madeni kwa mawakala wa pembejeo za kilimo na wazabuni wa pamba kiasi cha shilingi bilioni 64.5, madai ya mwaka wa fedha 2015/2016 ambayo yamehakikiwa na kukubaliwa mwaka wa fedha 2023/2024. Je, kwa nini madeni ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 yafanyiwe uhakiki na kukubaliwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 takribani miaka kumi iliyopita, kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani *(IAG),* amekuwa akifanya uhakiki wa madeni ya nyuma na kukamilisha kazi hiyo tangu mwaka 2017. Waziri atakapokuja kuhitimisha bajeti yake aweke wazi orodha ya watu waliolipwa fedha hizi ili kuweka uwazi wa matumizi wa fedha za umma. Awali tuliambiwa baada ya uhakiki yalibainika madeni mengi hewa ambayo yalifutwa na Serikali. Ni jambo linalofikirisha madeni ya miaka kumi kufanyiwa uhakiki leo na kukubaliwa kwa malipo ni lazima tujiridhishe Waheshimiwa Wabunge ili eneo la madeni lisije kutumika kama uchochoro wa kufuja fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu zao la pamba, bei ya pamba kuwepo makato makubwa ya fedha yasiyo na uhalali kwa kisingizio cha ununuzi wa pembejeo. Mfano, wakulima wa pamba katika msimu wa kilimo wa 2022 walikatwa kiasi cha shilingi 400 na mwaka 2023 walikatwa shilingi 300 kwa kila kilo waliyouza. Makato yanayokatwa kupitia Mfuko wa Wakfu wa Kuendeleza Zao la Pamba katika kununua mbegu, viuatilifu na vinyunyizi ni makubwa na kwa kiwango kikubwa yanaathiri bei ya mkulima na kumtia hasara kubwa, kwani gharama za kilimo ni nyingi, sio mbegu na viatilifu tu, bali kuna kupata shamba, kulima, kupanda, kupalilia zaidi ya mara nne, kupulizia dawa, kuvuna, kuuza, kusafirisha, kuhifadhi kwenye ghala na kadhalika ambako kote kunahitaji gharama.

Mheshimiwa Spika, bei ya kilo moja ya pamba ni shilingi 1,360 halafu mkulima anakatwa shilingi 300 kwa kila kilo moja sawa na 22% kulipia pembejeo. Kwa maelezo ya aina yoyote suala hili halikubaliki, badala ya kuwainua wakulima tunawatia umaskini. Pamoja na kikao cha wadau kilichokutana Machi, 2024 ambacho amekinukuu Waziri katika Ibara ya 339 ya hotuba yake, makato haya hayakubaliki na kuna haja ya kupanua mjadala kwa kuwashirikisha wakulima wenyewe kutoka kila wilaya na Mabaraza ya Madiwani, mfano Baraza la Madiwani la Meatu na Baraza la Madiwani la Bariadi walipinga makato hayo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa pamba kupitia kampuni moja usiruhusiwe kwa kuwa utaenda kuua ushindani ambao utapelekea kuporomoka kwa bei na usumbufu wa kuuza zao hilo. Kata 40 ambazo zilikusudiwa kupelekewa matrekta ya kulimia, matrekta hayo hayajapelekwa hadi sasa na hivyo hakuna sababu ya kupeleka kampuni moja katika maeneo hayo. Hata baada ya matrekta hayo kupelekwa, mwakani utafutwe utaratibu mzuri ambao hautaathiri biashara ya zao la pamba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bei za mbegu na viuatilifu na usimamizi wa bei za pembejeo kwa wakulima; pembejeo hizi za kilimo zimekuwa zikiuzwa kwa bei kubwa isiyo na uhalisia mfano mfuko wa kilo mbili za mbegu ya mahindi kuuzwa kati ya shilingi 16,000 hadi shilingi 24,000 wakati mahindi ya kawaida kuuzwa kwa

shilingi 1,200 kwa kilo mbili. Hakuna uthibitisho wa uhalali wa bei hizo za mbegu zinazoagizwa kutoka nje na zinazozalishwa ndani ya nchi. Kuna tishio kubwa la kupotea mbegu za asili na Taifa kuwa tegemezi kwa mbegu za kisasa ambazo zinalazimu kununua kila mwaka, mfano zaidi ya 45% za mbegu za mahindi tunaagiza kutoka nje ya nchi kila mwaka. Baadhi ya maeneo wananchi wanauziwa viatilifu *fake* vinavyonenepesha wadudu badala ya kuua, lakini pia viatilifu vimekuwa vikichelewa kuwafikia wakulima na hivyo kuwasababishia hasara kubwa. Inashangaza kuona mambo haya yameruhusiwa huku Waziri na mamlaka zipo zinazosimamia za *TPRI, TFRA, ASA, TARI* na *TOSCI.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mageuzi makubwa ya kilimo tunachokiendea hatuna sababu ya kutokuwa na Maafisa Ugani katika vijiji na kata zetu zote, Serikali imalize tatizo hili kwa haraka kwa kutoa ajira mpya.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimpongeze sana Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Bashe na Naibu wake Mheshimiwa David Silinde na wataalam wa Wizara na taasisi zote zinazosimamiwa na Wizara kwa kazi nzuri wanazofanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita kwenye zao la kahawa. Hapa duniani kahawa ni moja kati ya vinywaji maarufu vinavyopendwa na vinavyotumika. Baada ya maji ya kunywa, kahawa ni kinywaji cha pili kinachotumika zaidi duniani. Kahawa inapendwa kuliko vinywaji vingine kama chai na kakao, kutokana na uwepo wa *caffeine* kubwa.

Mheshimiwa Spika, wanasayansi wanasema kwamba unywaji wa kahawa mara kwa mara una faida nyingi kiafya kama vile kuzuia uwezekano wa kupata kisukari *type 2, alzheimer's disease,* msongo wa mawazo, ugonjwa wa moyo, kurefusha maisha, kupunguza maumivu mwilini na kuongeza hamu ya kula - *fiber intake*. Kutokana na umaarufu huu, kahawa ya kijani ni

bidhaa ya pili kibiashara duniani baada ya mafuta ya petroli na dizeli.

Mheshimiwa Spika, inakadiriwa kwamba wanywaji wa kahawa duniani hutumia wastani wa vikombe bilioni 2.6 kila siku. Huko Amerika na Australia kikombe cha kahawa kinauzwa dola 3.72 na dola 3.50 (shilingi 9,300 – 8,750). Aidha, kilo moja ya kahawa iliyokaangwa inaweza kuzalisha vikombe 120 - 140 Amerika 1,116,000 - 1,302,000) na Australia (1,050,000 - 1,225,000).

Mheshimiwa Spika, takwimu kutoka Bodi ya Kahawa Tanzania zimeonesha kwamba kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 bei ya kilo moja ya *Arabica* ilikuwa shilingi 3,000 na bei ya kilo moja ya *Robusta* iliuzwa shilingi 2,000. Bei hii haijafika hata bei ya nusu kikombe cha kahawa iliyoelezwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, ukilinganisha bei hii na na kazi ngumu za kuzalisha zao la kahawa, pesa anayopata mkulima ni ndogo sana na kilimo cha kahawa hakimlipi mkulima wa kahawa ya *Arabica*. Kwa ujumla uzalishaji wa kahawa ni mgumu.

Mheshimiwa Spika, kazi muhimu na zenye gharama kwenye kahawa ni pamoja na kukata matawi, kupalilia, kuweka mbolea, kupiga dawa, kuvuna, kupukuchua, kuchagua na kuondoa kahawa mbovu, kuikausha na kuisafirisha kuipeleka sokoni.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ugumu wa kuzalisha kahawa, bei wanayopewa wakulima wetu huwa ni ndogo sana. Kwenye mnyonyoro wa masoko mkulima huuza kwenye vyama vya ushirika, bodi ya kahawa na baadaye hupelekwa nje na kwenye mfumo huu mkulima hupata bei ndogo.

Mheshimiwa Spika, takwimu kutoka Bodi ya Kahawa zinaonesha kwamba tani 81,498 za kahawa ziliuzwa nje ya nchi kwa msimu wa 2022/2023 na kutupatia dola milioni 231 (shilingi bilioni 440.4) na kuweka rekodi ya mauzo toka tupate Uhuru, jambo hili ni jema. Ili nchi ifikie lengo la kuzalisha kahawa nyingi kama ilivyo kwenye mipango ya kitaifa na mkulima kupata bei

nzuri kwa kahawa wanayozalisha, naishauri Serikali ifanye haya yafuatayo:-

(i) Kwa kuwa kahawa inahitaji maji mengi muda wa msimu wote, ni vyema miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya wakulima wadogo ikarekebishwe (mifereji ya asili). Serikali itenge fedha za kutosha kuboresha mifereji ya asili kwenye maeneo yanayozalisha kahawa, kwani maji ni hitaji kubwa kwenye uzalishaji wa kahawa.

(ii) Serikali iendelee kutoa miche bora ya kahawa kwa njia ya ruzuku kwa wakulima. Miche 20,000,000 haitoshelezi mahitaji ya wakulima.

(iii) Serikali ihamasishe wawekezaji watakaofanya usindikaji wa bidhaa za kahawa hapa nchini. Serikali ishawishi makampuni makubwa ya kusindika kahawa wafungue viwanda hapa nchini. Ni vyema makampuni kama *Nestle, Starbucks Corporation, Matthew Algie & Company Limited, Kraft Foods Inc., Tata Consumer Products Limited, Strauss Group Limited, Jacobs Douwe Egberts* na *Tchibo Coffee International Limited* yakashawishiwa kuwekeza hapa nchini.

(iv) Serikali iimarishe uwezo wa makampuni ya ndani kuongeza thamani kwenye zao la kahawa kwa kuikaanga na kusindika kahawa hapa nchini. Tuwe na viwanda vingi kama kile cha *instant coffee* cha Bukoba.

(v) Pembejeo muhimu za kahawa kama vile mbolea na dawa za wadudu na magonjwa zitolewe kama ilivyo kwenye zao la korosho.

(vi) Serikali isaidie wakulima wa kahawa kupata soko la uhakika watakakouza kahawa yao kwa bei nzuri na ya kuridhisha. Ni vyema vyama vya ushirika vikapatiwa taarifa za uhakika za soko na vikaruhusiwa kushiriki kwenye kutafuta bei nzuri ya kahawa popote soko lilipo duniani.

(vii) Serikali isaidie wakulima kuzalisha kahawa yenye ubora ili kukidhi viwango vya soko la kimataifa.

(viii) Serikali isaidie kuwapatia wakulima wa kahawa hapa Tanzania huduma muhimu za ugani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama Mbunge wa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini naendelea kuishukuru Serikali kwa suala la mbolea ya ruzuku, tunaishukuru mno Serikali. Hatua hii imesaidia mambo kadhaa:-

(i) Kupunguza makali ya bei;

(ii) Kuhamasisha wananchi kuongeza mashamba kwa maana ya eneo la kulima; na

(iii) Kuongeza uzalishaji/mavuno kwa maana ya *high productivity.*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kuna changamoto kadhaa kwa mawakala, makampuni, *TRA* na namna ya usambazaji wa mbolea za kufika vijijini japo hadi ngazi ya kata.

Mheshimiwa Spika, mawakala wanakabiliana na changamoto ya kwanza kutoka kwa baadhi ya makampuni, kwa mfano kwa Kampuni ya Yara inamtaka wakala kulipa fedha yetu pamoja na ile ya ruzuku hali ambayo inamnyima wakala nguvu ya kimtaji kuweza kusambaza kwa haraka na kwa ukubwa. Baadhi ya makampuni hayana masharti magumu, wapo ambao wanataka tu *commitment* ya wakala kwa kutaka tu aweke *deposit* ya kiasi fulani cha fedha baada ya hapo wanaendelea kufanya kazi na wakala na mbolea inafika kwa mkulima kwa wakati. Kwa nini Yara wasiwe *flexible,* Yara ni *giant company,* ni matarajio yangu kuwa ingeunga mkono jitihada za Serikali kwa kuwa na masharti rafiki kwa mawakala. Binafsi nawaona Yara kama wahujumu wa jitihada za Serikali.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu Serikali iwape maelekezo Yara, wawe na masharti nafuu kwa mawakala, wao Yara ni wanufaika wa mfumo wa mbolea ya ruzuku, lakini pia ni wanufaika kibiashara ndani ya Tanzania, kwa nini wasiwe na moyo mwema wa kui-*support* Serikali katika suala hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *issue* ya *TRA,* wakati waingizaji wa mbolea kwa maana ya makampuni wanauza mbolea kwa bei ya soko na mawakala wa pembejeo wanauza kwa bei ya ruzuku, *TRA* imekuwa ikiwasumbua linapokuja suala la kodi. Hii inatokana na ukweli kwamba kunakuwa changamoto za kimahesabu baina ya mawakala na maafisa wa *TRA,* kwa maafisa wa *TRA* kutokutambua mfumo wa dijitali wa *TFRA Agro-dealer Tools* na hivyo mawakala kujikuta wakipigwa faini na *TRA* kwa kuonekana kuwa wana manunuzi makubwa kuliko mauzo.

Mheshimiwa Spika, shida ni kwamba Maafisa wa *TRA* hawatambui kwamba wafanyabiashara hao wananunua mbolea kwa bei ya juu kwa maana bei ya soko na kuuza kwa bei ya ruzuku ambayo ni bei ya chini, hali ambayo inasababisha kuonekana wana manunuzi makubwa na mauzo kuwa madogo. Kwa sababu hiyo kuna kila sababu Serikali kwa maana Wizara ya Kilimo kukaa na Wizara ya Fedha ili kuweza ku-*harmonize* suala hili. Wote tunamtumikia mwananchi mmoja, tuwe na uelewa wa pamoja. Tusiwaumize mawakala licha ya kuwa hii ni biashara, lakini kwa kiasi fulani ni huduma.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa mbolea inafika ngazi walau ya kata, kumekuwa na changamoto ya gharama za bei ya nauli ya mbolea kukosa uhalisia kwenye kufika ngazi ya kata, kwa mfano umbali wa kilometa 40 gharama za kusafirisha mfuko mmoja wa mbolea ya kilo 50 ni shilingi 300 hali inayosababisha mawakala kufanya kazi katika mazingira magumu na wakati mwingine kushidwa kupeleka mbolea vijijini na wakulima kulazimika kufuata mbolea maeneo ya mjini kwa umbali mrefu na hivyo kuongeza gharama. Nashauri wataalam watusaidie namna ya kukabiliana na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maghala, kutokana na uwepo wa mbolea ya ruzuku na kutokana na ukweli kwamba bado hatujawa na maghala makubwa na ya kisasa, nashauri ili kuongeza uwezo wa kuhifadhi chakula na hasa nafaka tutumie sekta binafsi katika kujenga maghala makubwa na ya kisasa, Serikali peke yake haitakaa iweze na kama itaweza basi itachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kilimo cha parachichi; Kata za Wambi, Rungemba, Bumilayinga, Sao Hill na Isalavanu wananchi wameitikia wito wa kulima parachichi na wenzetu wa Kibidula wamekuwa msaada sana ku-*support* huduma za ugani na kuwatafutia soko wakulima wa nje yaani *out growers.* Nashauri Serikali kuwaunga mkono wananchi na Kibidula hata kwa kuwasaidia kufanya kilimo cha mkataba ili kulinda haki za pande zote mbili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mara kadhaa suala la soko limekuwa changamoto, nashauri watu kama hawa wa Kibidula kupewa kila aina ya *support* na ushauri kwa sababu walau hawa ni mkombozi linapokuja suala la soko kuyumba.

Mheshimiwa Spika, pili, nafahamu kuwa kuna miradi ya *RISE* na *Agro-connect*, naomba awamu ijayo tuitazame barabara ya changarawe kupitia Skimu ya Umwagiliaji ya Mtula, Matanana, Kisada kutokezea Nyololo, eneo lote inakopita kuna shughuli za uzalishaji wa mazao ya mbogamboga na matunda kwa maana ya parachichi, itasaidia sana kufikisha mazao sokoni kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tatu, Mheshimiwa Waziri Bashe na timu yake wamekuwa wakifanya kazi kubwa kiasi wamefanya Watanzania kuona kuwa kilimo *is no longer a theory issue, but real.* Hata hivyo, yako maeneo ni kikwazo, kwa mfano wenzetu wa *TRA,* Bandari na *TANROADS*/mizani, hasa kwa mazao ya mbogamboga na matunda, pamekuwepo na ucheleweshaji wa mizigo kwa sababu zisizo za msingi, huwezi kumsimamisha mtu ambaye amebeba kontena la parachichi kisa tu sijui risiti ya *EFD* ya *transport,* sisemi kwamba sheria zivunjwe la hasha, bali kuna maeneo tutumie *common sense,* gari limesajiliwa, dereva ana

leseni, kwa nini usiache gari liwaishe mzigo sokoni na huyu dereva au mwenye gari umpige faini hata *online* kama ambavyo wamekuwa wakifanya Jeshi la Polisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bandari, nashauri pamoja na maboresho yanayoendelea katika kuimarisha bandari yetu, pawepo jitihada za makusudi kuwa na eneo maalum kwa ajili ya kusafirishia mazao ya mboga mboga. Hivi sasa wasafirishaji kwa mfano wa parachichi wanategemea Bandari ya Mombasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *BBT* na visima 67,000; jambo hili limekuwa na *mixed feelings* kwa sababu ya uelewa, nashauri Serikali isichoke kuelimisha kuwa hii ni *program up to 2030* maana kuna watu wanadhani hii ni *one year project,* nashauri Wabunge na Watanzania kwa ujumla waelimishwe kwa lugha rafiki, *in humble manner,* maana wapo watu wanaamini kuwa tayari Wizara ina mabilioni ya fedha kumbe *so far* ni *pledges.*

Mheshimiwa Spika, napongeza pia kupanua wigo wa *BBT* kupitia ile programu ya visima 67,000, nayo ni muhimu sana ifahamike kuwa ni programu ya kutoka sasa hadi 2030, vinginevyo ama kwa kutoelewa au kwa nia ya kupotosha watadhani kwamba programu hii ni kwa *this financial* hii ya 2024/2025. Kwa hiyo nashauri maelezo yajitosheleze na Serikali wasichoke kufafanua.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru sana kwa Mradi wa Umwagiliaji wa Mtula.

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kusema kilimo chetu, maisha yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, atafuatiwa na Mheshimiwa David Ernest Silinde na mtoa hoja ajiandae.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia hoja hii iliyopo mezani. Awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu

Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuleta mageuzi katika Sekta hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiki kinachofanyika kwenye sekta ya kilimo ni maono sahihi ya Mheshimiwa Dkt. Samia katika kushughulikia matatizo ya Watanzania ambayo yamekuwa yakiikabili nchi yetu kwa muda mrefu. Hili ndiyo jawabu sahihi la kushughulikia matatizo ya ajira kwa vijana wa Kitanzania. Mageuzi katika sekta ya kilimo ni jawabu sahihi la kushughulikia upungufu wa fedha za kigeni ambalo limekuwa likizikumba nchi nyingi za Afrika kwa sababu tutaongeza mauzo ya nje na tutaongeza fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuwekeza kwenye sekta ya kilimo cha kisasa ni jawabu sahihi la kuongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja kwa sababu kilimo ndiyo sekta inayoajiri Watanzania walio wengi. Kwa hiyo huu ni uelekeo sahihi na sisi kama Wizara ya Fedha tutafanya kila jitihada kuhakikisha kwamba fedha ambazo zinatengwa na Bunge lako Tukufu zinawafikia wenzetu wa Wizara ya Kilimo ili waweze kutekeleza miradi hii ambayo itaenda kuleta mageuzi kwenye maisha ya Watanzania hasa vijana ambao sasa wamekwenda kwenye shughuli hizo za kilimo.

Mheshimiwa Spika, tunaendelea kufanya mawasiliano na taasisi nyingine kwa sababu kilimo ni jambo ambalo linafanywa kwa kiwango kikubwa na Sekta Binafsi. Tunazialika na sekta nyingine na taasisi nyingine na nyingi zimeshaonesha utayari wa kuja kushirikiana na sekta yetu ya kilimo ili kuweza kuhakikisha kwamba kuanzia kwenye uzalishaji mpaka kwenye toleo la mwisho, vyote vinakuwa vinafanywa kwa njia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, kwa maslahi ya muda, niguse pia jambo ambalo ulinipa nafasi ya kuchangia pale mwanzoni. Jambo hili tumelipokea na kama ambavyo Mbunge ameongelea kwamba Benki Kuu walishatoa maelekezo kwa Umoja wa Taasisi za Kifedha. Mpaka imeenda Benki Kuu tayari huo ulikuwa ni mchakato ambao ulikuwa unahusisha kufanyia kazi jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unajua utaratibu wa utungaji wa sheria ya aina yoyote ile una mchakato wake, una mchakato wa kushirikisha wadau ili iweze kufika mpaka hatua ya mwisho ya kuitunga sheria. Sasa katika hatua hiyo ambayo imeshafika ni hatua nzuri. Kitu kitakachosalia tulipokee sisi kama Serikali. Litapita mikono ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na baada ya hapo kama yatakuwa yameshashughulikiwa maoni yote ambayo yametolewa na wadau ambapo tayari tumeshapata mojawapo ni lile linalohusisha Benki Kuu pamoja na Umoja wa Mabenki yaani ile *association* ya mabenki. Baada ya hapo Serikali itatoa jawabu lake kuhusu utaratibu wa hatua za kisheria ambazo huwa unakuja Bungeni. Kwa hiyo naomba Bunge lako liridhie kwamba tumelichukua, tutamaliza *consultation* ya ndani ya Serikali, tutamaliza *consultation* ya wadau na baada ya hapo taratibu za kiutungaji wa sheria zitaweza kufuatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie, kuna baadhi ya michango iliyokuwa imetolewa inayohusu *BBT*. Ukienda nchi ambazo zimeendelea, nchi ambazo tulikuwa sawa huwa tunatolea mfano, Vietnam pamoja na nchi nyingine ambazo wamepiga hatua kubwa sana kwenye masuala ya kilimo. Sehemu walipoanzia ilikuwa ni kuipeleka nguvu kazi iende kwenye kufanya kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, kilimo hakiwezi kikawa ni shughuli ya wazee, hakiwezi kikawa ni shughuli ya wastaafu kwamba mtu akishastaafu ndiyo anasema anataka kwenda kulima. Hatuwezi tukapiga hatua kwa kufanya hivyo. Ni lazima tufanye *orientation* na hivi tulivyofanya ndiyo njia sahihi. Hatuwezi tukaanza mara moja kwa kila kitongoji, hatuwezi tukaanza hivyo. *(Makofi)*

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, tunaanza kwa miradi na tutapiga hatua. Baada ya muda hiyo ndiyo itakuwa *standard* ya utaratibu tunaolima hapa nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mafuwe.

**TAARIFA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nataka kumpa kaka yangu kwa mchango wake mzuri taarifa kwamba ni kweli tunapaswa kuwekeza kwenye kilimo, lakini bajeti hii inayopita imekwenda kwa 53% tu. Maana yake tulipaswa hasa Wizara yake ingetusaidia, fedha zingeenda ili kilimo sasa kiwe ni kilimo cha vijana, waweze kufanya kazi na miradi iweze kutekelezwa, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mwigulu, Taarifa hiyo unaipokea?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa yake kwa sababu inahamasisha fedha ziende kwenye miradi, lakini naomba tu nitoe taarifa kwa Watanzania kwamba mwaka huu tumeathiriwa sana na mafuriko. Kwa kweli mradi usingeweza kuendelea eneo kama Rufiji. Usingeweza kuendelea maeneo kama Manyara, kusingeweza kuendelea na maeneo mengine ya aina hiyo. Sipingani naye na sisi kama Wizara na Mheshimiwa Rais mara zote anatuambia tusikae na fedha Wizarani, anatuelekeza fedha ziende kwenye miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sipingani naye isipokuwa kwa kweli si mradi ule tu, tumeathiriwa sana na masuala ya mafuriko na sio tu kwamba miradi imesimama, miradi imeathiri pia miundombinu mingine. Ukiambiwa uchague kati ya kupeleka mradi uendelee au ukawafukue watu waliofukiwa na nyumba zao, utapeleka fedha kufukua watu kwanza. Kwa sababu lazima ufukue watu kwanza na uwape makazi ndiyo upeleke fedha kwenye miradi ya maendeleo. Kwa hiyo hiki ni kipaumbele wala hakitabadilishwa na mafuriko, la mafuriko ni la dharura tu, tutaendelea na utekelezaji kama kawaida, ndiyo maana tumeiongeza bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilichokuwa namalizia naona na kengele imeshagonga. Nilichokuwa namalizia ni kwamba, Watanzania tunatakiwa tuvuke, huwa tuna bidhaa nzuri sana kwenye maonesho, ukioneshwa mazao yaliyopo kwenye sherehe za maonesho zile yanakuwa bora sana. Hivyo hivyo na kwenye

mifugo, yanakuwa bora sana. Anachokifanya Mheshimiwa Rais anataka vile ambavyo huwa tunavionesha kwenye Maonyesho ya Nanenane na Sabasaba, iwe ndiyo *standard* ya *production* ya nchi. Hapo ukishakuwa na mazao ya aina hiyo unaweza ukauza popote kule na nchi ikawa *the world largest producer* na *exporter* wa zao hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii itaanza na miradi kama hii ambayo Wizara ya Kilimo inafanya. Kwa hiyo Wizara ya Kilimo wapo kwenye njia sahihi na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo tumekutengea na ofisi pale Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuhakikisha hii miradi haikwami, mara zote tunashirikiana ili tuweze kuhakikisha mambo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Ernest Silinde atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, mtoa hoja.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii kuchangia hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo. Kabla sijakwenda katika mchango wangu, niungane na Wabunge wenzangu wote kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambazo amekuwa akizifanya hususan katika Wizara ya Kilimo, kwa kweli tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais amewatendea haki wakulima wa nchi hii kwa kipindi cha miaka mitatu tangu ameingia madarakani. Mheshimiwa Rais ameyatenda haya kwa vitendo na kila Mbunge hapa ni shahidi. Tunayoyasema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu moja, karibu kila jambo ambalo Mheshimiwa Rais alilisema amelitekeleza kwa kiwango kikubwa sana. Kwa hiyo hili linatupasa sisi sote tuendelee kumuunga mkono na kumpa moyo ili aendelee kuwatumikia Watanzania kwa miaka mingine mitano inayokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mtu wa pili wa kumshukuru ni Waziri wangu *Comrade* Hussein Bashe. Mheshimiwa Bashe ni kiongozi, ni mzalendo, ni mchapakazi na ni moja ya Mawaziri wanaotaka kuona matokeo. Mimi binafsi ukiacha kwamba ni kiongozi wangu ni *role model* wangu katika mambo mengi sana hususan ya kiuongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote unayoona leo Waheshimiwa Wabunge wanayashuhudia, msukumo wa Mheshimiwa Hussein Bashe kwa kiwango kikubwa, mimi huwa namwambia yeye ni Waziri Mtendaji, anafanya kwa moyo mkubwa sana. Niwaambie Watanzania, tuna mtu sahihi na mwelekeo anaotupeleka ni sahihi kabisa. Ndiyo maana leo kilimo tunaiona kabisa ni *game changer* katika uchumi wa nchi yetu; kila mmoja anaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, timu nzima ya Wizara ya Kilimo na Menejimenti. Kama kuna Wizara inafanya kazi vizuri *as a team work*, Wizara ya Kilimo inaongoza. Nayasema haya hata Waheshimiwa Wabunge ni mashuhuda, kama kuna Wizara tunafanya kama *team work*, kila mmoja anashirikishwa kwenye kila hatua Wizara ya Kilimo tunafanya. Tunawashauri wengine waje kujifunza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutaendelea kumshukuru zaidi Mheshimiwa Rais kwa ongezeko la bajeti. Tangu anaingia madarakani kutoka shilingi bilioni 294 katika mwaka wa fedha 2020/2021 mpaka leo tunapozungumzia, bajeti ya shilingi trilioni 1.248 mwaka wa fedha 2024/2025. Mheshimiwa Rais ana maono, anataka kubadilisha uchumi wa kawaida wa mwananchi wa Tanzania kupitia Sekta ya Kilimo. Katika fedha hii ambayo leo Wizara ya Kilimo tunaiomba, shilingi trilioni 1.06 inakwenda katika miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unaona kabisa kwamba tunataka kufanya kilimo chenye kumnufaisha mkulima wa kawaida, ndiyo maana tunasema hivi, ukiangalia hata kwenye bajeti ya umwagiliaji, ongezeko la bajeti wakati Mheshimiwa Rais anaingia madarakani mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo

ilikuwa shilingi bilioni 45, leo tunazungumzia zaidi ya shilingi bilioni 410.

Mheshimiwa Spika, lengo la Mheshimiwa Rais anataka Tanzania tupeleke kilimo kinachotegemea maji na wala si kilimo kinachotegemea mvua. Mheshimiwa Rais anataka Mtanzania wa kawaida anayejishughulisha na shughuli za kilimo alime mwaka mzima, yaani awe na vipindi zaidi ya viwili vitatu ambavyo anaweza kukaa shambani akajiongezea kipato cha kawaida. Hii itatuletea faida kubwa sana katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matarajio yetu ni kwamba miradi yetu ya kilimo itakapokuwa imekamilika, tunaamini tuta-*double export value* ya mazao yetu, tutaongeza kipato cha mkulima mmoja mmoja na *contribution* katika *GDP* ya Taifa itaongezeka mara dufu kwa sababu matokeo ya kilimo huwa yanalipa moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wizara ya Kilimo tunaamini katika tafiti. Ndiyo maana unaona leo Wizara ya Kilimo tumeongeza fedha katika taasisi zetu zinazofanya tafiti na malengo yetu makubwa ni kuongeza uzalishaji wa mbegu nchini na sio kuagiza kutoka nje ya nchi. Ndiyo maana leo moja ya kazi kubwa wanayofanya *TARI* ni kufanya tafiti ya mbegu mbalimbali nchini na hiyo kazi inaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Spika, sisi Wizara ya Kilimo tunaamini kilimo ni biashara kama biashara nyingine, ndiyo maana sasa hivi ukiona hata katika ajenda yetu ya 2030 tumeandika moja kwa moja kilimo ni biashara. Mkulima yeye anapolima asiwe tu ni yule mtu ambaye anategemea kilimo kama sehemu ya kujipatia chakula cha kawaida, lakini iwe ni sehemu ya kujipatia fedha zake zitakazomsaidia katika shughuli nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tunaamini katika kilimo kinachotegemea maji na wala sio mvua. Ndiyo maana wataona ukipitia katika Kitabu chetu cha Bajeti, tunapitia mabonde yote, tunayafanyia usanifu wa kina ili Watanzania wanaoishi katika

maeneo hayo waweze kufanya shughuli za kilimo katika mwaka mzima ambao utakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, tunaamini katika kuongeza tija katika kilimo, ndiyo maana sasa hivi unaona moja ya jukumu kubwa tulilonalo Wizara ni kuhamasisha wakulima wetu waongeze tija katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu, tunaamini katika kilimo cha kisasa. Ndiyo maana Wabunge wanaona tunafanya mambo makubwa yakiwemo *modernization of agriculture* hususan katika *mechanization.* Kuleta vifaa vipya vya kisasa, kilimo cha kidijiti ambacho kitakwenda kumsaidia mkulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na vipaumbele vingi kama Wizara ikiwemo utafiti na uzalishaji wa mbegu. Tumeongeza usambazaji wa mbolea, hata Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo langu la zamani la Momba Mheshimiwa Condester, alipokuwa anazungumzia, sisi kama Wizara tunakiri kwamba zipo changamoto ndogondogo ambazo tutaendelea kukabiliana maana yake mnapokuwa katika kutengeneza *road map* lazima panatokea changamoto.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo changamoto kama alizozieleza Mheshimiwa Mbunge zipo, lakini sio kwa kiwango kikubwa. Ndiyo maana vingine nitamshauri tu Mheshimiwa Mbunge apitie bajeti yetu pale. Masuala ya *BBT* asome aone mipango ambayo Wizara ya Kilimo tumejaribu kuiainisha pale ili kuweza kuwasaidia Watanzania wa kawaida.

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu tumewekeza nguvu sasa hivi katika kutoa huduma za ugani. Hili tunalifanya kwa sababu tunaamini kilimo kinahitaji wataalam watakaokwenda kuwasaidia wakulima wa chini. Sisi lengo letu tunataka tumsaidie mkulima wa chini, tunataka kumsaidia mkulima wa Katikati, lakini hatuwezi kumuacha mkulima mkubwa katika nchi hii ilimradi ni Mtanzania. Hata mwekezaji yeyote anayekuja, sisi kama Wizara ilimradi anaongeza tija katika Sekta ya Kilimo, Wizara tupo tayari

kumsaidia wakati wowote. Hayo ndiyo malengo makubwa ambayo sisi tupo nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara tuna jukumu kubwa la kuongeza wigo wa masoko kwa wakulima wetu kwa sababu ukiongeza tija bila kuhakikisha unakuwa na masoko ya uhakika, maana yake wakulima watafanya kazi kubwa na mwisho wa siku mazao yao yanaweza kuharibika kwa kiwango kikubwa. Kwa mfano, ukiacha ya kwamba watu wanaozalisha mazao ya nafaka kama mahindi na mpunga, hawa soko lao la kwanza litakuwa ni *NFRA*. Jukumu moja la Wizara tulilonalo sasa hivi ni kuongeza wigo wa uhifadhi wa chakula kufikia tani 500,000, lakini malengo yetu tunataka tufikie tani 3,000,000 kwa mwaka, *NFRA* awe na uwezo wa kuhifadhi chakula hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni malengo makubwa, yanahitaji wenye *vision* kubwa, wenye msimamo wanaoweza kutekeleza. Hili jukumu sisi tunaliweza, haliwezi kutushinda na tukafikia malengo ya Mheshimiwa Rais ambayo anataka Tanzania ya baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbolea, changamoto ndiyo zimekuwepo, lakini kwenye mbolea ninyi nyote ni mashuhuda katika mwaka uliopita. Sasa hivi sisi kama Wizara kupitia kampuni yetu ya *TFC* tunataka kuanzisha *blending facilities* kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ili sehemu ya uzalishaji wa mbolea uwe unafanyika hapa nchini. Hili linafanyika kwa sababu ni maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na sisi tunalitekeleza kwa sababu lipo katika mpango. Sasa hivi tunavyozungumza tupo katika mchakato wa kupata mzabuni ili sasa kutengeneza *blending facilities* ambazo zitaweza kusaidia uzalishaji wa mbolea hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hayo ni malengo ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyaweka kwa Watanzania ili kuhakikisha Sekta ya Kilimo tunaweza kufanikiwa kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la utafiti wa jumla tumeendelea kufanya hivyo, kuhakikisha mazao yote yakiwemo mazao ya kimkakati na yale mazao mengine, kwa sababu Wizara ya Kilimo tunasimamia mazao 89 na kati ya hayo 89 kuna mazao ya kimkakati yakiwemo mazao ya kibiashara; sasa jukumu letu sisi kama Wizara ni kuhakikisha kwamba tunakwenda na mazao yote, ikiwemo kuyapa kipaumbele mazao yale yanayoiingizia Serikali fedha nyingi za kigeni.

Mheshimiwa Spika, jukumu hilo tunalifanya kwa uaminifu mkubwa na Watanzania wakiendelea kutuamini Serikali ya Chama Cha Mapinduzi chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ana *passion* ya moja kwa moja kwenye kilimo. Ninyi wote ni mashahidi, hakuna uwekezaji mkubwa kwenye kilimo uliowahi kutokea katika vipindi vyote vya uongozi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya. Kwa hiyo tunawaomba Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono, wapitishe bajeti yetu ili sisi kama Wizara twende tukatekeleze yale yote yaliyopo kwenye Ilani ya Chama Cha Mapindizi na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ambayo amekuwa akiyatoa kwa sisi watendaji na kwa Watanzania wote, pamoja na Bunge lako Tukufu ili haya tunayoyasema yaweze kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, niwaondoe shaka Waheshimiwa Wabunge, kwamba miradi yote ambayo tumeahidi itatekelezeka kwa sababu tuna mahusiano ya karibu na Wizara ya Fedha na wamekuwa wakituahidi kuleta fedha na wanafanya hivyo, isipokuwa pale zinapotokea changamoto za kawaida.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nakushukuru kwa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge sasa nimwite Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo, aje ahitimishe hoja yake.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kukushukuru wewe kwa dhati kwa kunipa fursa ya kuja kuhitimisha hoja. Pili, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote

kwa michango yao. Hoja yetu imechangiwa na jumla ya Waheshimiwa Wabunge 48. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, ndugu yangu Silinde. Namshukuru sana kwa *support* anayonipa na ushirikiano anaonipa Wizarani. Namshukuru sana na namuahidi kuendelea kufanya naye kazi kwa karibu, kwa sababu ya historia yetu mimi na yeye. Namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kila wakati kunipa Naibu Waziri ambao tuna historia ya pamoja ya muda mrefu. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, natumia nafasi hii kukishukuru chama changu, Chama Cha Mapinduzi. Nakishukuru sana chama na jana walikuja hapa baadhi ya viongozi wa Sekretarieti ya Chama Taifa na baadhi ya Wajumbe wa Kamati Kuu, kuangalia na kusikiliza mwenendo wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Nawashukuru sana na nitaendelea kuhakikisha kwamba Ilani ya Uchaguzi inatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Katibu Mkuu na Menejimenti ya Wizara ya Kilimo, ahsante sana kwa *support* wanayonipa kama Waziri na kuendelea kuwatumikia Watanzania. Nawashukuru Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa. Waziri wa Kilimo hana wakulima ofisini, hana wakulima Dodoma. Nawashukuru sana wakuu wa wilaya walioko katika maeneo mbalimbali, wanaosimamia shughuli zetu za kilimo kila siku. Nataka niwaahidi, tarehe 7 na 8 tutakuwa na semina ya pamoja ya wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya. Sisi Wizara ya Kilimo katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha za kusimamia shughuli za kilimo ambazo tutazipeleka moja kwa moja kwenye ofisi ya mkuu wa wilaya ili asimamie shughuli za kilimo katika ngazi ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna Mradi wa *P4R*, nataka niwahakikishie wakuu wa wilaya wote wa nchi hii na wakuu wa mikoa, kwamba Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Ofisi ya Wizara ya Kilimo itawapa *support* zote wanazohitaji ili kuhakikisha

wanasimamia miradi na shughuli tunazopeleka katika ngazi ya wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie Bunge lako Tukufu kumshukuru sana Mkuu wa Mkoa wa Tabora. Sijui kama yupo hapa, ndugu yangu Chacha, namshukuru sana. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Spika, Mkuu wa Mkoa wa Tabora hivi ninavyoongea amekamata Maafisa Ushirika wa Halmashauri watatu, kawaweka ndani. Amekamata watendaji na amekamata Madiwani wa Chama Cha Mapinduzi. Naendelea kuwapa moyo wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya, kwamba yeyote anayehujumu shughuli, miradi na efforts za wakulima katika ngazi ya wilaya katika nchi hii wana mamlaka waliyopewa na Mheshimiwa Rais, watumie mamlaka waliyopewa. Hatutaruhusu nguvu zinazopelekwa na Serikali na Bunge lako Tukufu kuidhinisha pesa halafu watu wachache wakafaidike na jasho la wakulima.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

*Mheshimiwa Spika, hawa wamekamatwa kwa kufanya ukangomba wa tumbaku. Namshukuru sana Chacha na Wizara ya Kilimo iko pamoja naye. Aliyebaki ni Meya wa Jiji la Tabora ambaye aliiba mbolea za wakulima, yuko mtaani. Kiongozi yeyote hana immunity, hata kama ni ndugu yangu atakayehujumu rasilimali za Serikali zinazopelekwa katika Sekta ya Kilimo, Serikali iwachukulie hatua na isiwe mambo ya kukamata watu wadogo. Tumekubaliana kwamba hili ni jambo la kufa na kupona. (Makofi)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu ambalo nataka niseme, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, namshukuru kwa dhati. aliponiteua kuwa Waziri wa Kilimo, aliniuliza swali dogo tu, kwamba unadhani matatizo ya kilimo ya nchi hii ni nini? Nikamwambia Mheshimiwa Rais, ni *public investments*; fedha ya umma kuwekeza kwenye maeneo ya msingi, wakulima si wavivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha ya umma inapowekezwa na tunapojenga mazingira mazuri ya sekta binafsi kufanya kilimo, kwa sababu wakulima ni sekta binafsi; hii dhana ya sekta binafsi kusubiri kudhani ni mtu mwenye suti na *briefcase* na anaongea Kiingereza siyo sahihi. Sekta binafsi ya nchi yetu inaongezwa na wakulima wadogo wadogo wa nchi hii, hawa ndio *drivers* wa sekta binafsi ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili uweze kutathmini fedha za umma zinazowekezwa unatakiwa uangalie mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kitu cha kwanza, je, ukuaji wa sekta hiyo mnayopeleka fedha za umma kuna ukuaji wa aina yeyote? Kitu cha pili mnatakiwa mjiangalie, je, kuna ajira zinatengenezwa? Kitu cha tatu, *efforts* zenu mnazozifanya zina mahusiano na tumbo na mifuko ya hao watu mnaowapelekea hizo fedha?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2021, Bajeti ya Wizara ya Kilimo ilikuwa ni shilingi bilioni 294. *Export* yetu kwa wastani ilikuwa kati ya dola milioni 800 mpaka dola bilioni 1.2. Kwa maamuzi ya kufungua mipaka, kuondoa ukiritimba, kupeleka mbolea ya ruzuku na kufanya *efforts* mapato yetu ya *forex* yameongezeka kutoka dola bilioni 1.2 mpaka dola bilioni 2.3. Wala siyo maeneo ya kutisha, ni maeneo yale yale ambayo wakulima wetu wadogo wamekuwa wakifanya *efforts* na sisi tunafanya jitihada za kuwasaidia kufungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mauzo ya mazao yanayoitwa *oil seeds* yameongezeka mpaka kufika dola milioni 743 katika msimu wa kilimo uliopita. *Horticulture* imefikia dola milioni 265, *legumes* zimefikia dola milioni 338 na *traditional crops* zimefikia dola milioni 509. *Serials,* kwa mara ya kwanza tumeruhusu tu-*export* mahindi na mchele katika nchi hii, imefikia dola milioni 448. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili la kujiuliza, hizi dola zipo kwa wakulima? Hawa wakulima wadogo wanazipata? Hii ndiyo kazi tunayotakiwa kuifanya sisi waliotupa dhamana. Jambo la kwanza tunalolifanya na naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge

wa korosho, ahsanteni sana kwa *support* wanayotupa katika mabadiliko tunayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nitoe mfano mdogo wa zao la korosho na mwone namna ambavyo kama hatutoamua pamoja, juhudi za Mheshimiwa Rais zitaishia hewani, kama hatutaamua pamoja kufanya haya mabadiliko. Nataka nitoe mfano, mkulima wa korosho akivuna korosho na kuipeleka mnadani, kwa mwaka jana, natumia msimu uliokwisha, halmashauri zinapata kati ya tani 310,000 tulizozalisha kutoka tani 180,000 ya miaka miwili iliyopita. Hii ni kwa sababu Mheshimiwa Rais alitoa ruzuku ya pembejeo bure na kuwapa wakulima wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka wakati tunachukua hii hatua ilionekana ni muujiza, tukawa tunalaumiana sana, tukawa tunapiga kelele na sasa leo ile kelele haipo kwa watu wa korosho. Tunajadili namna ya kuujenga mfumo wa ruzuku ili mkulima aweze kufaidika. Halmashauri zimepata shilingi ngapi? Mwaka jana halmashauri zimepata bilioni 14 kama *cess*. Ushuru kwa Bodi ya Korosho ni bilioni sita, ushuru kwa *TARI* ni bilioni sita, tozo za ushirika ni bilioni 24, tozo za maendeleo kwa ajili ya zao ni bilioni 26, tozo za taasisi zingine za umma zinazopata kutokana na kilo moja ya mkulima, ni bilioni 12, *export levy* ni bilioni 96. Jumla ni bilioni 186. Hizi ni fedha zimechukuliwa kutoka kwa mkulima, tumechukua sisi. Ni lazima tufanye *reform*. Tumemwomba Mheshimiwa Rais ruzuku ametupatia na kwa hiyo ni lazima tufanye *reform*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu ni kuhusu *cartel.* Nataka niwape, wao ndio Waheshimiwa Wabunge, mnaona hizi fomu mbili? Hizi karatasi mbili na hii nimechukua karatasi ya Kampuni inaitwa *Harmony Agro Limited*. Wanapoweka lile dude la kulala usiku lile, debe; mnunuzi anaingiza karatasi mbili kwenye ile bahasha. Karatasi moja anaandika bei kabisa, karatasi nyingine inakuwa *empty*. Usiku ufunguo mmoja anao afisa ushirika, ufunguo mwingine anao kiongozi wa ushirika. Wanaitana usiku, wanakaa wanafungua sanduku. Wakimaliza kufungua sanduku wanampigia simu Hussein, katani ameandika 2,000 ndiyo bei ya juu, na wewe umeandika 1,980. Unaonaje uandike 2,010 halafu sisi utatupa shilingi 30?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa amejaza hizi katarasi mbili; na *we have enough evidence,* Bunge hili likiwa tayari nitawawekea, ninazo video, tume-*record* vikao vya siri. Sasa kinachofanyika, kwa kuwa tumeshakubaliana tunaitoa ile karatasi ya bei halali uliyoweka tunaweka sasa ile bei tuliyokubaliana saa nane usiku. Halafu na sisi tumepeana shilingi 30, 40, 50. Kwa uchunguzi wa Kamati, sijui ile Kamati yangu kama iko hapa, hata mmoja; nawashukuru sana; wamefanya hii kazi kwa miezi mitatu, wamekutana na *resistance* kubwa sana katika ngazi za wilaya. Nilijua kwa sababu kuna ajali za kisiasa, niliwaambia kila wanakofanya mkutano, wahakikishe wana-*record* kwa siri na kwa dhahiri. *Average* waliyochukua watu wa *cartel* ni kati ya shilingi 40 mpaka shilingi 60. *Over 20 billion shillings* wamegawana hawa watu. Hatuwezi kuruhusu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru Mkuu wa Mkoa wa Songwe na Mheshimiwa Mulugo, sijui kama yupo; tumezuia mnada wa ufuta uliokuwa ufanyike siku tatu zilizopita huko Songwe. Eti wamekubaliana mnada au debe liwekwe leo halafu lifunguliwe baada ya siku tatu. Nimemwambia Mheshimiwa Chongolo na *RAS* wake, tumekubaliana *TMX* inakwenda.

Mheshimiwa Spika, wakulima wa nchi hii siyo wajinga, wanajua bei ikianguka na bei ikipanda. Yule pale Mheshimiwa Kinanasi, yule pale, amepiga kelele kuhusu *cocoa* kwa muda mrefu. Sauti yake ikabaki ya kwake peke yake. Leo cocoa imefika shilingi 30,000 katika Wilaya ya Tukuyu na Kyela. *Cartel* ya wizi ya *cocoa* ilihusisha watumishi wa umma, *politician and every leader.* Hatuwezi kuruhusu hili. Aidha, ni afadhali tumwambie Mheshimiwa Rais asilete fedha kwenye kilimo na apeleke kwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu hapa Mheshimiwa Waziri Mkuu, tumekwenda naye Kagera tukaenda kufanya mkutano wa kahawa; Waheshimiwa wabunge wa Karagwe na kwingine wako hapa; leo kahawa iliyokuwa inanunuliwa shilingi 700, *its almost 3,000 shillings* kwenye *open market*. Tumeenda kufanya nini? Tumeenda kubadili mfumo, tumebadili mfumo. Tatizo siyo mfumo wa ushirika, tatizo lilikuwa ili kiongozi wa ushirika aibe ni lazima Afisa Ushirika wa Wilaya ashiriki kwenye wizi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nimwambie Mheshimiwa Katani na wenzake, Serikali iko *determined*. Tutakwenda ku-*confront the big elephant in the house*. Nimemwambia Mkurugenzi wa *TMX*, yuko hapa, yuko ndani ya Bunge hili; Ofisi ya *TMX* na mfumo wa *TMX* wanahamishia Mtwara na Lindi. Nimemwambia Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho atoe jengo, tutaweka kompyuta, tutaanza *bidding* pale *openly* na tutaanzisha mfumo wa kuweka *minimum price*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaanza na ufuta, tunakwenda mbaazi na baadaye tunakwenda kwenye korosho. Wakulima hawa kama bei wanaiona wamekaa hivi, wanaona washindani wanashindana, wana haki ya kukataa bei kwa sababu zao litakaa ghalani, halili wali wala halitaki chai. Tunakwenda ku-*confront*, najua na tunafahamu kuna shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili, nimeongelea kuhusu tozo. Cha kwanza, mbele ya Bunge lako Tukufu, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mkurugenzi wa *COPRA* mwenye mamlaka kwa mujibu wa sheria kusimamia mazao yasiyokuwa na bodi, ameanza kazi. Nataka niseme hivi, mmeona hii kwenye korosho nimetaja zaidi ya shilingi bilioni ngapi, zinazorudi kwa mkulima, Mheshimiwa Rais mwaka jana alivyoruhusu *export levy 50 percent* irudi. Mwaka huu tumeshakubaliana na Mheshimiwa Mwigulu, yule pale kwamba *export levy 100%* inarudi kwenye korosho, yote ni hela ya wakulima na Mheshimiwa Rais ameshaidhinisha hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili ni hivi, halmashauri zinapokea *cess* halafu kule chini kuna watu wanaitwa watu wa kwenye kata wanamkata tena mkulima shilingi 20 ya kata kila kilo, jumlisheni. Acha hizi nilizozitaja, kuna shilingi 20 tena kila kilo ya kata, shilingi 20 ya wilaya jumla ni 40 na ya mkoa shilingi 10, hivyo jumla hamsini. Ukipiga hesabu kwa tani laki tatu ni *15 billion shillings* wanachukua tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halmashauri imeshachukua *cess* inatosha. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia anapeleka madarasa, maji, umeme na barabara. Kupitia Bunge lako Tukufu na

Mkurugenzi wa Bodi ya Korosho, yuko hapa, Mrajisi wa Vyama vya Ushirika yuko hapa na Mkurugenzi Mkuu wa *COPRA* yuko hapa; ni marufuku kuchukua tozo tofauti na tozo zilizowekwa kwa mujibu wa sheria, marufuku. Ni mwisho kwenye ufuta, mbaazi, korosho kuchukua shilingi 20 ya kata, shilingi 20 ya wilaya na shilingi 10 ya mkoa, hakuna. Tutapunguza shilingi 10 kutoka kwenye Bodi ya Korosho na tutapunguza shilingi 10 kutoka kwenye Bodi ya *TARI*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wameongelea *Stabilisation Fund*, namshukuru Mheshimiwa Rais, tulivyompelekea wazo la kwenda kuanzisha *Agricultural Development Fund*, akaidhinisha, *Agricultural Development Fund* tumeipitisha kwenye sheria ya mwaka jana na ina *function* kubwa tatu: -

*(i)* *Stabilisation*;

*(ii)* *Infrastructure Development*; na

*(iii)* Kusaidia mifumo ya *Irrigation* na *Digitalisation*.

Mheshimiwa Spika, ilivyoidhinishwa na Mheshimiwa Rais, tukatakiwa tuanzishe vyanzo vya mapato ambavyo tutachukua kutengeneza kwenye *Agricultural Development Fund*. Namshukuru Mheshimiwa Waziri wa Fedha amesaini kanuni kama miezi miwili iliyopita. Tunaenda kuanzisha Mfuko wa Kuendeleza Kilimo katika nchi hii, mfuko huu utakuwa na jukumu la *stabilisation*. Moja ya kazi ya *stabilisation* ni pale ambapo bei labda zimeanguka katika Soko la Dunia na mkulima anatakiwa kulindwa kutokana na bei hiyo.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wameshauri tutengeneze Mifumo ya Mjengeko wa Bei, tunayo mifumo kwenye tumbaku, tunao mfumo mzuri kwenye pamba, tutaenda kutengeneza kwenye korosho na mazao mengine ili tuwalinde wakulima. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge waturuhusu kama Serikali, watupe nafasi tutakapokuja kusoma bajeti ya mwaka kesho, kutakuwa kuna tengo lililo wazi la Mfuko wa Kuwalinda Wakulima katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeshaweka *legal framework,* tunatengeneza vyanzo ili mfuko huu uwe *sustainable,* tunauanza, hiyo safari itatuchukua muda lakini lazima tuijenge na ni jambo la kisera. Nataka niwaambie wakati tunaanza ruzuku ya mbolea, Taasisi za Kimataifa zote zilitupinga zikatuambia *it's not sustainable*, leo ukienda Europe wana-*subsides* wakulima wao. Wanawa-*subsides* kwenye *equipment*, wanawa-*subsides* kwenye *inputs* wanawa-*subsides* kwenye *price, why not us*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua ya kuwapunguzia wakulima gharama za uzalishaji na hii ni sehemu mojawapo ya *stabilisation*. Kwa sababu, *stabilisation* ni aidha uifanye kwenye *price* ama uifanye kwenye *cost of production*, Rais kafanya nini? Tumeanza ruzuku ya mbolea hapa, ilikuwa tunaona kama ni jambo gumu, lakini namshukuru Mwenyezi Mungu naamini zipo changamoto, changamoto haziwezi kwisha, zitakuwepo tu. Tutaendelea kukabiliana na hizi changamoto moja baada ya nyingine ili tuweze kuzipunguza na tuweze kumlinda mkulima kama inavyotakiwa. Niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, mawazo yao tunayapa thamani na tunayasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka niseme ni kwenye zao la pamba, Wabunge wameongelea hoja ya mbegu, wameongelea suala la bei ya pamba na kuongeza thamani. Tulivyoanzisha maranja ya korosho tulisema 2026/2027, nchi hii hatutaki ku-*export raw cashew nuts*, tunataka korosho ibanguliwe. Serikali imepeleka fedha *cross to ten billion* mwaka huu na tutaendelea kupeleka mpaka tukamilishe ile *infrastructure,* lakini *priority* tutawapa *local,* hakuna dhambi, Serikali kutumia kodi ya nchi yake kumwezesha *Private Sector Local* wa kwake na Sekta hii ya Kilimo tunafanya, tunaanza maranje na hiyohiyo *model* tunaipeleka kwenye pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi tumeshachukua hekari 156 ambazo tunazifanya Mkoa wa Simiyu, Serikali inaenda kupeleka umeme, tunapeleka maji, tunapeleka barabara, lakini vilevile tunaenda kujenga *shades* na kujenga *warehouses*. Niwaombe *Ginners,* wao watakuwa *priority* ya kwanza, nitumie Bunge lako

Tukufu hili kuwaambia, yeyote atakayekuja kwenye hicho kituo na kuweka Kiwanda cha *Cotton Twine* ambazo ni kamba tutakazozitumia kwa ajili ya kufungia zao la tumbaku, tuta-*save importation* ya *seven million dollar*, sisi tutampa *off taking agreement* ya miaka mitano kulinda uwekezaji wake pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe tuache ku-*export ma-robot* tuanze kuongeza thamani, tumekubaliana na Bodi ya Pamba tunachukua hii hatua na tutaanza kuifanya na tutawekeza.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka niliseme ni kuhusu mazao ya *horticultural* (ndizi na parachichi). Tumefanya tathmini Nyanda za Juu Kusini na Kaskazini kuangalia uwezekano wa kulitumia zao la ndizi, Kigoma na Kagera kuweza kuondoa watu kwenye umaskini. Jambo kubwa ambalo tumegundua sisi tumekuwa kila siku tunataja magonjwa mnyauko, sijui nini, tunamfundisha mkulima ng'oa miche, halafu Serikali inachukua hatua gani?

Mheshimiwa Spika, cha kwanza tunajenga maabara mbili kubwa za *tissue cultural*. Moja tunaiweka Maruku nyingine tunaiweka Kaskazini katika Kituo chetu cha Utafiti cha Arusha na pale ndiyo itakuwa *Centre of Excellency* kwa ajili ya *multiplication* ya miche ya ndizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha pili tunachokifanya, tumeamua kuichukua Wilaya ya Rombo, tunaifunga Wilaya ya Rombo, tutang'oa migomba, tutapanda *variety* moja kwa ajili ya *export* na tutaweka miundombinu ya umwagiliaji kwa hao wakulima, linawezekana. Tumeshaanza na namshukuru *boss* wangu wa zamani, Waziri amekubali ku-*take the risk* ili tuanze hiyo safari ya pamoja ni lazima tuwekeze, matokeo hayawezi kutokea kesho, yatatuchukua tu muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua matamanio ya Watanzania wote, wakulima wa nchi hii na Waheshimiwa Wabunge ni kuona matatizo yote yanaisha leo. Niwaombe *patience,* hizi hatua

tutakwenda nazo polepole, tutatatua tatizo mojamoja na tutavuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni parachichi, parachichi na *Horticultural* ndiyo Sekta inayokua haraka katika Sekta zote za kilimo. Inakua kwa wastani wa asilimia saba. Tuliwaacha wakulima wameenda. Serikali inafanya nini kuanzia mwaka ujao wa fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, tunawapelekea vifaa kwa ajili ya kufanya *irrigation* kwenye mashamba yao. Tunaenda kuwa-*support* wale wenye eneo ambalo kuna mito midogomidogo, tutaweka mabwawa madogo, tutawapa *pump*, tutaweka *pipes* ili waweze kumwagilia kwenye miti yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha pili tunachokifanya, tunajenga *common use facility*, ukienda Wilaya ya Rungwe mazao yanapotea, tumeshaanza, tunajenga mbili, moja Iringa nyingine Rungwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, cha tatu tunachokifanya, namshukuru Waziri Dkt. Mwigulu, tumeenda kuongea na *African Development Bank*. Tunaweka kitu kinaitwa *Agricultural Special Processing Zone* (Vituo vya Kuchakata Mazao ya *Horticultural*) tunaanzia Nyanda za Juu Kusini, Kaskazini lakini tuna-*link* na bandari. Tunalalamika hapa kila siku parachichi yetu inasafirishwa na Wakenya, ni kwa sababu bandari zao zina miundombinu. Rais Dkt. Samia katuruhusu, tunachukua dola milioni 100 kuanzia mwaka ujao na sasa hivi tumeshatoa *one million dollar* kwa ajili ya *feasibility study.*

Sasa hivi namsubiri kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu ndani ya miezi miwili, mitatu atasaini huo mkataba ili hizo fedha tuanze kujenga *common use facility* ambayo itatumika kwa ajili ya *sorting, grading, packing* na *processing*. Halafu tunaweka *core chain facility* kwenye eneo la Dar es Salaam pale Kurasini. Haya hayawezi kutokea *over night* yatachukua muda, lakini niwatie moyo wakulima wa parachichi, tumeweka fedha mwaka huu, tunawapa ruzuku ya madawa bure ili waweze kupambana na vidudu vinavyoathiri parachichi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine nililotaka niliongelee kidogo katika mkutano wako, nimpe dada yangu Mbunge wa Mbarali uhakika, tukimalizana na *Highland Estate*, shamba lile ni la wakulima wadogo, tutawagawia wakulima wadogo, tutahakikisha wanapata haki yao wale ambao wanafanyishwa kazi za kuwa vibarua katika ardhi yao, tutahakikisha *Mbarali Highland Estate Farm* tutakubaliana naye na kumlipa haki zake zote, hatutamdhulumu tutahakikisha linakuwa shamba la wakulima wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la nne, *mechanisation*, siku zote tumekuwa tukisema wakulima wanunue matrekta, ni mzigo kwa mkulima wa heka moja kumwambia nenda kakope milioni 70 benki kwa riba ya asilimia hizo zinazofahamika halafu alime kwa trekta? Rais Dkt. Samia tulivyoenda India akaagiza tutengeneze mpango wa Serikali kununua jumla ya trekta 10,000 kwa kipindi cha miaka mitano. Tunaanza sasa hivi, mwaka huu tunaanza kujenga *mechanisation centre*, sisi tunapeleka trekta na vifaa vyote wakulima watakodi pale kwa bei ambayo Serikali itaiweka ya ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaanza na *mechanisation centre* 10 katika maeneo ya uzalishaji na Mbarali ni mojawapo ambapo tutaweka, kwingine ni Mkoa wa Rukwa, Mkoa wa Ruvuma tutaziweka hizi *mechanisation centre*. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tutafanya hivi kwa mikoa yote ya uzalishaji kasoro Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge wameongelea *issue* ya upimaji wa afya ya udongo. Wakisoma Hotuba ya Wizara ya Kilimo tumesema tumeshapima mikoa 17, imebaki mikoa nane. Sasa hivi, kwenye bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kumalizia mikoa nane, maana yake mikoa yetu 25 ya Tanzania Bara yote itakuwa imepimwa na kupata *soil profile* ya mikoa yote. Hatua itakayofuata ni kuzalisha ramani za kila mkoa kuonyesha namna ambavyo udongo wake ulivyo.

Mheshimiwa Spika, tumeshachukua hatua sasa hivi Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, tumeshaleta vifaa vya

kupimia afya ya udongo katika halmashauri 142 na hii ni huduma ya bure. Ombi langu kwao wanapoenda kukaa kwenye Mabaraza ya Madiwani wamuulize Afisa Kilimo na Mkurugenzi mwaka huu umepimia wakulima wangapi, afya ya udongo na kuwapa *certificate*? Zile *certificate* zina lugha mbili, Kiswahili na Kiingereza. Inaeleza kuhusu zao unalofaa kulima, mapungufu ya *nutrients* kwenye eneo lako na unatakiwa utumie virutubisho gani na baada ya hapo kama Serikali tutapiga marufuku aina za mbolea ambazo hazikidhi mahitaji ya udongo wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa ni kuhusu Vituo vya Utafiti na Vituo vya Kufundishia. Hili naomba niliongee polepole wanielewe, ni hivi Mwalimu Nyerere alivyoanzisha Vituo vya Utafiti pembeni alijenga Vituo vya Kufundishia na Mwalimu alijua anaowafundisha ni wakulima, baadaye tulibadili Sera, tukaamua kuvigeuza ni sawasawa na *Sokoine University* na *CBE*, tukawa tunasomesha watu *Diploma*, *Certificate*, *Advance Diploma* wanaondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeamua jukumu la kusomesha *Certificate*, *Diploma*, *Advance Diploma* atabaki nalo kaka yangu Profesa Mkenda. Wizara ya Kilimo, sisi tunaenda kufanya *retraining* ya *Extension Officer* walioko kwenye halmashauri, tutawarudisha madarasani mle ndani, tunawa-*train* kama yeye yuko Kusini anaenda Naliendele, atafundishwa kuhusu korosho, atafundishwa kuhusu mbaazi, atafundishwa kuhusu ufuta na mahitaji ya ikolojia iliyoko Naliendele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, tutaanza kuwafundisha wakulima ili tuwapatie elimu kuhusiana na ikolojia zao na warudi vijijini. Wakulima hawataki kufundishwa mambo makubwa na kizungu kingi, wanataka waambiwe mbegu ya mahindi bora ni hii, unapanda hivi, mbolea unaweka kwenye *stage* hii, *simple language* kazi hiyo itafanywa na Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, nimalizie tu jambo moja. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tumeanza safari hii ya

mabadiliko, tunawekeza kwenye *irrigation*. Matokeo ya *irrigation* yanaweza yasitokee kesho yatatokea muda ujao. Naamini mwelekeo tuliochukua kama nchi ni mwelekeo sahihi sana. Hakuna hata siku moja kwenye kilimo mahali popote ambapo matokeo ya kilimo yametokea kwa urahisi ni uwekezaji wa muda mrefu na Serikali hii imechukua hatua hiyo. Wakulima wa mahindi, *NFRA* anakuja kununua mahindi wasiwe na hofu, tutaanza kununua mahindi siyo muda mrefu kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani ni kengele ya mwisho hiyo. Ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, naomba iidhinishiwe kukusanya Maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 10.6 kupitia Fungu 43 na Fungu Na.5. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 7.0 zitakusanywa katika Fungu 43 na shilingi bilioni 3.6 kupitia Fungu Na.5.

Katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 1,248,961,680,000 kupitia Fungu 43, Fungu Na.5 na Fungu 24 kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 43; shilingi 824,069,158,000, kati ya fedha hizo shilingi 700,318,469,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo na shilingi 123,000,750,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi 69,894,933,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 53,000,000,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara, Bodi na Taasisi.

Mheshimiwa Spika, Fungu Na.5; shilingi 403,783,833,000, kati ya fedha hizo shilingi 331,899,223,000 ni fedha za maendeleo na shilingi 71,000,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida; kati ya hizo shilingi 64,000,000,000 ni kwa ajili ya *OC* na shilingi 7,000,000,000 kwa ajili ya *payee*.

Mheshimiwa Spika, Fungu 24; shilingi 21,108,000,000, kati ya fedha hizo shilingi 20,000,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi 11,954,614,000 ni mishahara ya watumishi na shilingi 8,325,459,000 ni matumizi ya *OC*. Aidha,

fedha za ndani kiasi cha shilingi 828,626,000 zinaombwa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hamjaunga mkono hoja msimame hivyohivyo. Mheshimiwa Waziri, nilikuwa natazama ukurasa wa 193 na 194 wa Kitabu chako cha Hotuba, tuchukue takwimu hizi zilizoko humu kwa maana ulikuwa humalizii ukisema laki inabidi utaje laki kama ukisema laki tunajua ni mia zile ulizotaja badala ya maelfu. Kwa hiyo, tuchukue takwimu hizi ama nikurejeshe usome tena?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba uchukue takwimu zilizopo kwenye kitabu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hoja hii kuungwa mkono tunaendelea na utaratibu wetu.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI - MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.............Sh. 6,668,597,096

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kifungu hiki kina Mshahara wa Mheshimiwa Waziri na kuna majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge ambao wangependa kupata ufafanuzi juu ya mambo ambayo yanaruhusiwa kutumia Kanuni yetu ya 122. Kuna jina hapa la Mheshimiwa Twaha Mpembenwe.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini kwanza naomba nimtoe shaka tu ndugu yangu Mheshimiwa Bashe sikusudii kuushika mshahara wake isipokuwa, nataka tupate maelezo ya kina kwa maslahi mapana ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ya kilimo ni sekta muhimu sana. Takwimu zinatuambia kwamba inaajiri takribani 80% ya Watanzania. Sambamba na hilo tunaambiwa kwamba *GDP* inayochangiwa na kilimo ndiyo kubwa kwa 26%, lakini takwimu za kikodi zinaonyesha kuwa kuanzia Julai, 2018 mpaka Machi, 2024 mchango wa kikodi ambao unakusanywa kupelekwa kwenye kikapu kikubwa kinachoenda kwa ndugu yangu pale Mheshimiwa Mwigulu ambacho kinaweza kutusaidia kwenda kufanya shughuli za kimaendeleo ni 0.75%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kusikitisha zaidi siyo tu Wizara ya Kilimo ni *combination* ya Wizara kama tatu, kuna uvuvi, kuna misitu na kilimo. Sasa nataka kujua ni nini hasa mkakati wa Serikali kwa Wizara hii katika kuhakikisha wanasaidia kwenda ku-*widen* ile *tax base,* ili sasa fedha zinazopatikana katika makusanyo ya kodi kwenye eneo la kilimo ziende kuchangia katika Mfuko mkubwa wa Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ufafanuzi.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa hoja ya Mheshimiwa Twaha. Kwanza ukiichukua sekta ya kilimo kwa maana ya kutazama *tax base* au *tax collected* kutoka kwa mkulima wa mahindi itakuwa ni *very wrong interpretation* ya *tax system* kwa sababu, mkulima wa mahindi ama wa korosho akivuna korosho zake anakuja kufanya suala la *value addition*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni *argument* ambayo nimekuwa na majadiliano hata na wakusanya kodi, kwamba, ni wapi unautafsiri mchango wa sekta ya kilimo kwenye kapu la kodi? Kama unataka kwenda ku-*tax* mahindi, uwele au choroko, maana yake ni kwamba, unakwenda ku-*tax raw materials*. Kwa hiyo hili ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili. Ni lazima kama nchi tukubaliane tuna-*formalize informal sector* ili tuweze kupata kodi ya kutosha na hawa ni akina nani? Ni *traders* wa mazao, ni wale wanaonunua mazao ya wakulima wasajiliwe, wapate leseni, wafanye nini? Hii hatua tumeianza toka mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeamua kama Serikali hakuna mtu yoyote atakayeruhusiwa ku-*export* mazao kama hana *business license*. Hakuna mtu yeyote atakayeruhusiwa ku-*trade* mazao kama hana *tin number*. Hii itatusaidia kuongeza wigo wetu wa walipakodi ili tuweze kupata mapato mengi ya kodi. Nakubaliana naye kwamba, ukitazama dhana ya ukusanyaji wa kodi kwa mkulima shambani unaweza usimwone, lakini ukimtazama mkulima anayevuna mazao na kuwapa viwanda, kuwapa *transporter,* kuwapa *exporter* na kodi tunayoikusanya kutokana na hao, mchango wa sekta za uzalishaji kwenye kodi ni mkubwa sana katika uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka tu nimwombe Mheshimiwa Twaha aelewe kwamba, wakulima wale wa korosho na ufuta kule kwake na pwani yote wanachangia sana kwenye kodi, lakini tukitafsiri kwa lugha hiyo tutakuwa tunafanya tafsiri isiyo

sahihi ya ku-*define tax base* kwenye nchi yetu. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Twaha nakuona umesimama, lakini kwa maelezo uliyokuwa umetoa awali mimi hayanipi nafasi ya kutoa tena fursa kwako kuzungumza, kwa sababu, ulizungumza kwa sura kwamba, unataka tu ufafanuzi halafu basi. Sasa ukisimama maana yake sijajua sasa umeghairi lile la kwamba, huna mpango wa kushika shilingi na kama ndivyo ulipaswa useme mwanzoni kama hujaridhika.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uniwie radhi, lakini kutokana na maelezo haya sasa kuna uwezekano mkubwa wa 100% kushika shilingi. Nataka kuweka rekodi vizuri kidogo. *(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Sasa Mheshimiwa Twaha kwa sababu ya ule mguu ulioingilia inakuwa ngumu sana kukufungulia mlango. Sawa Waheshimiwa Wabunge ndiyo Kanuni zetu zinataka hivyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ninalo jina lingine hapa. Jina la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Hivi karibuni Serikali kupitia mamlaka ya ukusanyaji kodi nchini *(TRA)* wametoa waraka wa kuvitaka vyama vyote vya msingi nchini vianze kutumia mashine za *EFD (Electronic Fiscal Device)*. Hivi vyama vya msingi kwanza havina leseni ya biashara, ni wakulima walioungana ambao *transaction* yao ni mara moja tu kwa mwaka na wanapeleka mazao yao mnadani, wakishafanya mnada wanapata hela wanarudi nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nataka Mheshimiwa Waziri aniambie huu waraka kwanza unawaongezea mzigo wakulima kwa sababu, *implication* yake mwishoni mwa mwaka watalazimika wa-*file tax return.* Kwa kila anayetumia hii mashine

ya *fiscal device* analazimika ku-*file tax return* na hii ni kuviongezea mzigo hivi vyama vya msingi vya ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nipate majibu ya uhakika ni *logic* ipi iliyotumika kuvilazimisha hivi vyama vya msingi vya ushirika nchini vianze kutumia hizi mashine wakati sio wafanyabiashara na wala hawana hata leseni ya kufanya biashara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge umesema huo waraka umetolewa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kuelekea kwa wakulima. Sasa mkulima anaweza kuwa hana majibu ya hilo jambo kwa sababu, limetoka sehemu nyingine. Hii Wizara ni ya Kilimo na hilo jambo naona limetoka upande wa Wizara ya Fedha.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu anayewajibika kwa wakulima ni Waziri wa Kilimo.

**MWENYEKITI:** Yeye hana majibu kwa sababu siyo mtoa waraka, mwenye majibu atakuwa ni yule wa fedha. Maana yake ni nini? Hii hoja yako Mheshimiwa uitunze kwa sababu, Waziri wa Fedha atakuja hapa kusimama. Leo ni hoja ya kilimo, hoja zinazohusu mambo yaliyotoka Wizara ya Fedha kuja Kilimo huyu wa Kilimo atatoa wapi majibu, maana siyo yeye ambaye ametoa huo waraka?

Waheshimiwa Wabunge, hapa kazi yangu ni kulinda Kanuni. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na kwamba, namwona hapa, lakini kwa sababu hoja hii siyo ya kwake, akijibu namna isivyofaa halafu ukashika shilingi ni shilingi ya Wizara ya Kilimo sio ya Fedha, Waheshimiwa Wabunge mmenielewa? *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge hiyo hoja yako uishikilie, itakapokuja hoja ya Waziri ambaye waraka umetoka kwake, siku hiyo yeye atasikiliza habari za kilimo kwa sababu, waraka ule unaenda kwa kilimo kutokea kwake. Mheshimiwa Mbunge umenielewa?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Hayo ndiyo yalikuwa majina mawili yaliyokuwa yanataka ufafanuzi na nimewauliza hapa. Ndiyo shida ya walimu kama mmenielewa, ili mtu asije akaona hoja kama imepotelea hivi, hapana. Kwa sababu, ni hoja ya kushika shilingi, sasa ikishikwa shilingi kwa maelezo atakayoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na ni shilingi ya Waziri wa Kilimo itakuwa kidogo haijakaa sawa, nadhani mmenielewa.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea. Kifungu kinaafikiwa?

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1002 – *Finance and Account Unit*...............Sh. 2,102,122,000

**MWENYEKITI:** Ukitaja laki hutaji elfu kule mbele kwa sababu, maana yake ni hela zinaongezeka. Haya, soma tena.

Kifungu 1002 – *Finance and Account Unit*...............Sh. 2,102,122,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...................Sh. 2,805,451,237
Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute*………..Sh. 41,365,038,000
Kifungu 1005 – *Internal Audit Unit*……….....................Sh. 668,080,000
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*........Sh. 960,663,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*.......................................................Sh. 635,757,000
Kifungu 1008 – *Legal Service Unit*…....…......…………..…Sh. 703,068,000
Kifungu 1009 – *Management Information System Unit*………………...……...…………..Sh. 760,913,000
Kifungu 1010 – *Environment Management Unit*.........Sh. 488,937,000
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*.......Sh. 1,154,644,000
Kifungu 2001 – *Crop Development*……….……...Sh. 46,844,051,000
Kifungu 2002 – *Agricultural Mechanization*…..……Sh. 6,170,133,000

Kifungu 2003 – *Agriculture Land Use Planning and Management*...............................Sh. 967,172,000
Kifungu 2004 – *Plant Breeders' Unit*…….....….......…......Sh. 390,405,667
Kifungu 5001 – *National Food Security*……...........….Sh. 11,065,657,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kifungu *1001 – Administration and Human Resources Management*..................Sh. 2,167,839,000
Kifungu *1002 – Finance and Accounts Unit*.................Sh. 397,654,000
Kifungu *1003 – Planning, Monitoring and Evaluation Unit*…...............................…..….Sh. 513,833,000
Kifungu *1004 – Government Communication Unit*........................................................Sh. 160,798,000
Kifungu *1005 – Procurement Management Unit*........Sh. 532,556,000
Kifungu *1006 – Internal Audit Unit*………....………...…Sh. 252,569,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge kwa muda uliobaki Kanuni zinatutaka tusome kwa mafungu tupitishe bajeti kwa mafungu kwa dakika zilizobaki.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit*…...............……………Sh. 110,340,000
Kifungu 1008 – *Legal Service Unit*...………..…...............Sh. 141,182,000
Kifungu 1009 – *Environment and Social Management*.......................................Sh. 116,640,000
Kifungu 2001 – *Design and Research Division*........Sh. 51,705,289,000

Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development*..................................Sh. 13,920,088,500
Kifungu 2004 – *Operations Division*..........................Sh. 1,614,191,500
Kifungu 2005 – *Compliance and Quality Assurance*............................................Sh. 251,630,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*.................Sh. 2,017,070,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 307,281,130
Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation Unit*......................................Sh. 427,591,130
Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*..................................................Sh. 296,784,310
Kifungu 1005 – *Legal Service Unit*................................Sh. 183,529,745
Kifungu 1006 – *Procurement Management Unit*........Sh. 237,381,745
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit*..................................Sh. 799,067,745
Kifungu 1008 – *Internal Audit Unit*.................................Sh. 233,146,745
Kifungu 1009 – *Research and Training Unit*..................Sh. 305,228,310
Kifungu 4001 – *Cooperative Promotion and Coordination Section*..........................Sh. 355,893,900
Kifungu 4002 – *Cooperative Microfinance Section*..................................................Sh. 435,205,900
Kifungu 4003 – *Regional Cooperative Offices*.........Sh. 6,738,746,000
Kifungu 4004 – *Cooperate Marketing and Investment Section*.............................Sh. 268,347,720
Kifungu 4005 – *Registration Service Section*................Sh. 271,298,720
Kifungu 4006 – *Inspection and Supervision Services Section*................................Sh. 7,403,489,900

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 43 – Wizara ya Kilimo**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*……...............................….Sh. 0
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*...............Sh. 466,576,974,740
Kifungu 1004 – *Agriculture Training Institute*...........Sh. 32,122,900,000
Kifungu 1007 – *Government Communication Unit*…..................................................Sh. 300,000,000
Kifungu 1009 – *Management Information Systems Unit*...............Sh. 0
Kifungu 1010 – *Environmental Management Unit*......Sh. 203,135,000
Kifungu 1012 – *Monitoring and Evaluation Unit*.......Sh. 2,300,000,000
Kifungu 2001 – *Crop Development*……...…...……Sh. 99,600,000,000
Kifungu 2002 – *Agricultural Mechanization*..........…Sh. 21,314,027,260
Kifungu 2003 – *Agriculture Land Use Planning and Management*….........................…Sh. 3,669,600,000
Kifungu 5001 – *National Food Security*....................Sh. 74,231,832,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji**

Kifungu 1003 – *Planning, Monitoring and Evaluation*……......................................…Sh. 860,840,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*…...……..................Sh. 86,304,0000
Kifungu 1007 – *Information Communication Technology Unit*...................................…Sh. 671,520,000
Kifungu 1009 – *Environment and Social Management Unit*……........................…...Sh. 1,123,864,000
Kifungu 2001 – *Design and Research Division*............................................Sh. 19,014,288,000
Kifungu 2002 – *Irrigation Infrastructure Development*…...........................Sh. 307,555,787,500

Kifungu 2004 – *Operations Division*……....…………....Sh. 2,018,319,500
Kifungu 2005 – *Compliance and Quality Assurance Section*…...........….….....Sh. 568,300,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika**

Kifungu 4001 – *Cooperative Promotion and Coordination Section*…..........................................….Sh. 500,000,000
Kifungu 4004 – *Cooperative Marketing and Investment Section*…......................................……Sh. 0
Kifungu 4006 – *Inspection and Supervision Services Section*……..........................................…Sh. 328,626,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mtoa Hoja Taarifa. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imeyapitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wizara ya Kilimo, Fungu 43, 24 na 05 kwa mwaka wa fedha 2024/2025, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo basi, naomba sasa Bunge lako Tukufu iyakubali makadirio hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsanteni sana. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Wote wameafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ahsanteni sana wote mmeafiki, kwa hiyo Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 yamepitishwa rasmi na Bunge. Kwa kusema hivyo, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na viongozi wote chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kushirikiana vizuri na Kamati yetu mpaka wamefikia hapa ambapo Bunge zima limeweza kuafikiana na yale ambayo wameyaleta mbele ya Bunge.

Kwa hiyo, tunawapongeza sana na kwa kusema hivyo tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa yale yote mliyoyaahidi katika hotuba hii ya Wizara. Pia yale ambayo Waheshimiwa Wabunge walipata nafasi ya kuchangia na hapa katika kujibu kwenu mmeonesha kwamba mmeyasikia na mtayafanyia kazi, basi hapa na pale ambapo Waheshimiwa Wabunge wamependekeza marekebisho mkayatazame na hayo katika utekelezaji wa bajeti hii na tunawatakia kila la kheri.

Waheshimiwa Wabunge, pia niishukuru sana Kamati yetu ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuisimamia Wizara hii. Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote tunawashukuru sana kwa sababu mmefanya kazi

nzuri sana kwa niaba yetu sote. Wabunge ambao mmepata nafasi ya kuchangia nanyi tunawashukuru kwa sababu yale mliyoyasema yanawasaidia Wizara kufanya maboresho hapa na pale, kwa sababu mpaka kufikia hapa Wizara ya Kilimo, kupokea pongezi nyingi kutoka kwenu ni dhahiri kwamba mawazo yenu ambayo mmekuwa mkiyatoa kila tunapokutana hapa yamefanyiwa kazi. Kwa hiyo, ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano wenu wote. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaahirisha shughuli za Bunge, kuna mambo matatu:-

Jambo la kwanza, wakati Mheshimiwa Waziri akihitimisha hoja yake hapa alizungumza kuhusu Meya wa Jiji la Tabora na yale ambayo yametokea huko Tabora. Kwa ajili ya kuheshimu utawala wa sheria basi na kwa kuwa hapa ni Bungeni tungependa utawala wa sheria uheshimiwe. Kwa hivyo kumtaja hapa kwa sura ile aliyomtaja hapa Mheshimiwa Waziri, kama atakuwa amekamatwa atakuwa ni mtuhumiwa. Maana yake ni tuhuma, kwa hiyo inabidi apelekwe kwenye vyombo vingine vya haki ili aweze kusikilizwa na huko watafanya maamuzi sasa ya yeye kama amehukumiwa ama vinginevyo. Kwa hiyo, kwa muktadha huo maneno aliyoyasema hapa Waziri sikuwa nimetaka kumkatiza kwa sababu nilitaka amalize mchango wake. *(Makofi)*

Pia wale wengine aliowataja kwamba wamekamatwa kwa uongozi wa Mkuu wa Mkoa, vivyo hivyo na wao tunatarajia kwamba sheria itachukua mkondo wake kwa sababu nchi hii inafuata utawala wa sheria. Kwa hivyo, mhimili mwingine utakapopelekewa hayo mambo isije ikaonekana kwamba humu Bungeni tayari tulikuwa tumeshatoa hukumu. Kwa hiyo, kwa muktadha huo yale aliyokuwa ameyasema Mheshimiwa Waziri ambayo si kwa maana ya kuyafuta lakini kwa ile sura ya kwamba wale watu ni kama vile wamehukumiwa tayari yale yanaondoka lakini kwa maana ya kwamba kuna watu pengine wamefanya mambo yasiyofaa kwenye sekta ya kilimo huo mchango wake utabaki kwa sura hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, liko tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kesho tarehe 4 Mei, 2024 kutakuwa na semina kuhusu hatua zilizofikiwa katika ujenzi wa Reli ya Kisasa *(SGR)* itakayotolewa na Wizara ya Uchukuzi. Semina hii itafanyika saa nne asubuhi katika Ukumbi wa Msekwa. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kuja kusikiliza maendeleo haya na tumefikia wapi katika uwekezaji huu mkubwa unaofanywa na Serikali yetu. Naamini kwamba tutajifunza mambo mengi ikiwa ni pamoja na hatua ambayo imefikiwa mpaka sasa hasa ukizingatia kwamba kuna maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais alikuwa ameshayatoa, kwamba kufikia kipindi fulani, basi tuanze kusafiria hivi vyombo vya usafiri na vianze kutoa huduma hiyo na sisi Wabunge tutakuwa ni sehemu ya watu ambao tutakuwa tukitumia vyombo hivyo. Kwa hiyo, ni muhimu kuja kwenye semina hiyo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, liko tangazo lingine na hili ni refu kidogo, nitaomba mnivumilie kidogo. Hili tangazo linahusu wageni.

Waheshimiwa Wabunge kama mnavyofahamu Bunge hili ni la wananchi, kwa hiyo wananchi wanaruhusiwa kuja hapa kwa ajili ya kutembelea Bunge, pia kuja kutazama shughuli za Bunge na wengine huwa wanakuja kwa ajili ya mafunzo, kuna wanafunzi huwa wanakuja hapa.

Tumekuwa tukipata idadi kubwa sana ya wageni na kwa sababu hiyo hatuwezi kuendelea na utaratibu huu tulionao, pia hatuwezi kuzuia wageni kuja kwenye chombo chao cha uwakilishi. Kwa hiyo tutaweka masharti ya muda kwamba watu wanaokuja kutembelea hapa Bunge wanaweza kukaa kwa muda gani ili wapishe wengine waweze kuja. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaposema hivi ni kwa maana ya hapa ndani na huko nje pia, kwa nini? Kwa sababu pamoja na mambo mengine eneo letu hili limefungwa. Kwa hiyo, lazima tuzingatie masharti ya usalama wa Wabunge, lakini pia wa wageni wetu. Kwa hiyo, zipo siku ambazo wageni wanakuwa

wengi sana, kama jana tulipata wageni zaidi ya 1,000. Sasa sisi sote tukiwa hapa na kila mtu akaja akakaa tangu asubuhi mpaka jioni, kidogo inaleta changamoto kwa maana ya usalama.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na ili tuweze kuwahudumia wageni wote wanaokuja hapa kwa ajili ya kututembelea sisi kama wawakilishi wao, lakini pia kutembelea chombo hiki kama mhimili unaowahusu, basi masharti yafuatayo ndiyo yatakayotumika:-

Wageni watakaokuja kwa ajili ya mafunzo, wageni hawa watafika katika muda ambao wamepangiwa, siyo kwamba watu watakuwa wanakuja asubuhi halafu wakae kwenye foleni mahali. Kwa hiyo, watapangiwa muda ambao watatakiwa kufika kwenye geti na muda gani wataingia humu ndani. Kwa hiyo hayo yote watakuwa wameambiwa na watatakiwa kufuata muda huo ambao wameambiwa. Kwa hivyo, baada ya utambulisho pia watapangiwa muda ambao wanatakiwa kukaa kwenye viwanja vya Bunge.

Sasa wageni watakaokuwa wanakuja kwa ajili ya mafunzo, watakaokuwa wanatangazwa kwenye kile kipindi cha mara baada ya maswali, wataingia hapa Bungeni saa 2.00 asubuhi na baada ya kutambulishwa wakatolewa hapa ndani na kupelekwa Msekwa kwa ajili ya mafunzo ama elimu kwa umma, wataondoka katika viwanja vya Bunge saa 6.00 mchana.

Wageni watakaotangazwa kati ya saa 6.00 hadi saa 7.00 mchana hao watafika saa 4.00 asubuhi hapa maeneo ya Bunge. Baada ya kutambulishwa na kupewa elimu kwa umma wataondoka maeneo ya Bunge saa 9.00 mchana.

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge watakuwa ni kama wageni wetu ambao wanakuja kwa makundi ama mmoja mmoja, masharti yale niliyotaja kwa ajili ya wale wageni wanaokuja kwa ajili ya mafunzo ndiyo yatakayotumika.

Watumishi wa Serikali; watumishi wanaotoka Serikalini kwa ajili ya kuchukua hoja za Wizara Bungeni wasizidi 30 na watakaa

katika ukumbi ulioandaliwa na siyo kuzunguka kwenye maeneo ya Bunge. Hii ni kama nilivyosema, kwa sababu ya usalama, wageni wanakuwa wengi, sasa ukikutwa unazunguka huko unaweza kutolewa na wewe, wakidhani muda wenu wa kutoka umefika, kumbe wewe ulikuja hapa kwa ajili ya kusikiliza hoja. Kwa hiyo, eneo mtakalokuwa mmeambiwa make, mnaosikiliza hoja, tafadhali mkaa pale ili msije mkabebwa na wale wageni wengine kutoka nje ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, watumishi wanaohusika na Maonyesho ya Wizara, Taasisi na Sekta Binafsi wanaokuja hapa Bungeni; watumishi wanaokuja kwa ajili ya maonesho watafika katika Viwanja vya Bunge saa 2.30 asubuhi na wataondoka katika Viwanja vya Bunge kabla ya saa 1.00 usiku. Aidha, watumishi wanaokuja kwa ajili ya maonesho mbalimbali, watapaswa kuzingatia usafi wa maeneo wanayopangiwa kutumia wakati wote wanapokuwepo na wanapoondoka. Vilevile, idadi ya watumishi wanaokuja kwa ajili ya maonesho itakuwa kama ifuatavyo -

(i) Maonesho binafsi, watu wasizidi watano; na

(ii) Maonesho ya Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma hawatazidi 50.

Matumizi ya Mgahawa; Waheshimiwa Wabunge ambao wana wageni wanaozidi 10 watapaswa kutumia Mgahawa ulioko Jengo la Utawala *Annex*, kutoa nafasi kwa ajili ya Wabunge kwa sababu mgahawa huu ulio karibu hapa, Wabunge wanapata nafasi ya kwenda na kurejea kwa haraka. Kwa hivyo wageni wakiwa wengi sana hapo Wabunge wanakosa nafasi na kwa hiyo watachelewa wakienda eneo la mbali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, aidha, Wabunge wenye wageni zaidi ya 50 watapaswa kutoa taarifa mapema ili waandaliwe chakula katika mgahawa wa *Dodoma Carnival* ambao kwa sasa ni sehemu ya Bunge. Hii itatusaidia kwa sababu kwa huu muda tuliopangiana wa kukaa hapa, tusije kuwaambia wale ambao

watakuwa wanasubiri muda wao wa kuingia ufike, kwamba, wengine bado hawajatoka hapa ndani. *(Makofi)*

Maegesho ya magari; Waheshimiwa Wabunge kipindi hiki tunapata changamoto kidogo kwa sababu Wizara na Taasisi mbalimbali zinafanya maonesho katika Viwanja hivi vya Bunge ambayo kwa kweli ni ya muhimu sana, yanatupa nafasi sisi kama Wabunge kujifunza kwenye mambo mbalimbali, lakini Bunge sasa limesitisha utaratibu wa kuegesha magari kwa Wabunge hapa ndani kwa sababu lile eneo ndilo linalotumika kwa ajili ya maonyesho.

Waheshimiwa Wabunge, kwa sasa kwa kuwa Serikali imetuongezea maeneo ambayo yanazunguka hili eneo la Bunge, basi Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote kipindi hiki ambacho hawawezi kutumia lile eneo la maegesho wanashauriwa ku-*park* ama kuegesha magari yao katika maegesho yaliyoko karibu na Bohari na mkabala na Bodi ya Nafaka badala ya kuegesha magari kando ya Barabara Kuu ya Dar es Salaam.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge muegeshe magari upande huu kwa sababu sasa hivi hilo ni eneo la Bunge na yatakuwa salama kabisa, msiwe na wasiwasi kuliko lile eneo ambalo mnaegesha kule. Huko nyuma tuliwahi kupata changamoto ya Mheshimiwa Mbunge mmoja kugongwa na gari huko wakati akivuka. Sasa ili tuepuke hayo, basi tuegeshe magari upande huu mwingine ambao hakutakuwa na magari mengi yanapita kwa sababu sasa ni eneo la Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mengine haya hata kama hamkuyashika myashike yale yanayohusu wageni wenu, hayo mengine yote mtaendelea kukumbushwa taratibu na pia tangazo hili mtawekewa kwenye vishikwambi ili na ninyi mwendelee kuweka vizuri mapokezi ya wageni wenu na wale ambao ni wakarimu sana, wanapenda wawape chai wageni wao, basi uwe umejua kwamba kwa idadi ya wageni wako, wataenda kunywa wapi chai. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.53 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 6 Mei, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*